

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 7 Novemba, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Hawa Wanyamwezi sijui wamefanyaje meza yangu hapa, inaelekea Wanyamwezi wanaroga. Katibu!

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mhe. Janeth Maurice Massaburi

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Nane wa Bunge, Bunge lilipitisha miswada mitatu ya sheria kama ifuatavyo; kwanza Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 3, Bill 2017*).

Pili, Muswada wa Sheria ya Reli wa mwaka 2017 (*The Railways Bill, 2017*) na tatu Muswada wa Sheria ya Madaktari wa Meno na Wataalam wa Afya Shirikishi wa mwaka 2016 (*The Medical Dental Allied Health Professionals Bill, 2016*).

Kwa taarifa hii, ningependa kiliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari miswada hiyo imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi zifuatazo:-

(i) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 ya mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 3 Act. No. 9 of 2017*);

(ii) Sheria ya Reli No. 10 ya mwaka 2017 (*The Railways Act. No. 10 of 2017*); na

(iii) Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalam wa Afya Shirikishi No. 11 ya mwaka 2016 (*The Medical Dental and Allied Health Professionals Act. No. 11 of 2017*).

Baada ya hayo Waheshimiwa Wabunge ningeomba tupunguze sauti kidogo, tumesharudi tena. Tukumbushane wale wote ambao tunaongea ongea, tafadhalii.

Ningependa kuchukua nafasi hii kuwatambulisha au kumtambulisha rasmi Katibu wa Bunge mpya Ndugu Stephen Kagaigai. (*Makofii*)

Ahsante sana na kwa niaba yenu nimkaribishe sana Bungeni. Ningewaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote tumpe Katibu wetu mpya kila aina ya ushirikiano. Lakini pili niwajulishe kwamba ndugu yetu tuliyekuwa naye kama Katibu wa Bunge Dkt. Kashililah yeye ameteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo. (*Makofii*)

Kwa maana hiyo hiyo, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Dkt. Thomas Kashililah kwa kazi nzuri sana ambayo

tulifanya kwa pamoja katika Bunge hili, amefanya kazi kwa karibu miaka 30 katika taasisi hii na tumtakie kila la heri huko kilimo ambako ameenda na ninajua bado tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, basi baada ya taarifa hizo nitumie nafasi hii kuwakaribisha tena Dodoma kwa mara nyingine, Dodoma ni njema. Safari hii tumehakikisha Dodoma ni salama zaidi kuliko wakati mwingine wowote, msiwe na wasiwasi na Dodoma. Kwa hiyo, karibuni sana, hizo ndiyo taarifa rasmi.

Taarifa zisizo rasmi ni mambo madogo madogo tu, wakati hampo hapa haya mambo Waziri wa Mambo ya Ndani anayajua vizuri zaidi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ule uwanja wa shamba la bibi kule Dar es Salaam kulikuwa na mechi moja hivi, Mheshimiwa Nchemba alikuwepo, nilimuona na Mheshimiwa Nape nadhani. Wale jamaa, aah! Wakachomoa lile goli kwa taabu sana. Yaani kwa shida basi ikawa *draw!* Nikamuona Mheshimiwa Nchemba anacheka meno nje, anashangilia *draw*. Basi yote mema, hayo ndiyo yaliyotokea katikati wakati hampo jamani. (*Makof/ Kicheko*)

Basi baada ya hapo, Katibu tunaendelea!

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, kwa niaba yake tafadhalii.

**MHE. FLATEY G. MASSAY (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango juu ya Mpendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

#### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 1

**Ajira kwa Vijana Wanaomaliza Shule Nchini**

**MHE. AIDA J. KHENAN** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kwa vijana wanaomaliza shule za msingi, sekondari na vyuo kwa kuwawezesha kujajiri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mikakati mbalimbali ambayo inawezesha vijana wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mikakati inayotekelawa mahsus kwa ajili ya vijana wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari ni kama ifuatavyo:-

(i) Ni kutekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi nchini, ambapo kupitia programu hii tumeanzisha utaratibu maalum wa kutambua ujuzi uliopatikana kupitia mfumo usio rasmi na kuurasimisha kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wale walio tayari kuhitaji na kuwapa vyeti vinavyotambulika. Utaratibu huu unawapa fursa vijana wetu kuendelea na mfumo rasmi wa mafunzo na pia kutambulika na waajiri au watoa kazi.

(ii) Ni kuhamasisha vijana wanaomaliza shule za msingi na sekondari kuijunga katika vikundi vya kuzalisha mali na kusajiliwa rasmi kupitia Sheria ya Usajili wa *NGO's*. Hadi sasa jumla ya vikundi vya vijana vya uzalishaji mali 10,200 vimekwishakusajiliwa.

Aidha, ipo mikakati ya kuwawezesha wahitimu wa vyuo kujiajiri na kuajiriwa ambayo ni pamoja na:-

(i) Ni kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi nchini ambayo inawezesha vijana wahitimu wa vyuo kupata ujuzi wa kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Programu hii inatoa mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu (*internship*) ili kuwapatia uzoefu wa kazi.

(ii) Serikali imerahisisha utaratibu wa uundai wa makampuni kupitia BRELA hivyo vijana wengi wanaomaliza vyuo kuweza kuanzisha makampuni na biashara zinazoweza kuajiri vijana wengine.

Mheshimiwa Spika, pia ipo mikakati inayowawezesha wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu kujajiri ambayo ni:-

(i) Serikali imeendelea kuimarisha utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao unalenga kuwasaidia vijana wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu kuweza kujajiri kwa kuwapa mikopo ya mashati nafuu na mafunzo ya ujasiriamali. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 hadi mwaka 2016/2017 Serikali kupitia Mfuko wa Mendeleo ya Vijana imetoa mikopo ya masharti nafuu ya shilingi bilioni 5.8 kwa vikundi vya vijana 6,076 vyenye wanachama 30,380 katika Halmashauri za Wilaya 157 kupitia *SACCOS* za vijana.

(ii) Serikali kupitia Halmashauri zinatenga maeneo kwa ajili a vijana wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu kufanya shughuli za uzalishaji mali ili kujipatia ajira. Katika mwaka 2016, jumla ya hekta 271,882 zilitengwa kwa ajili ya shughuli za vijana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Serikali ya Awamu ya Tano imepunguza wafanyakazi kwenye kada mbalimbali kwa kigezo cha kutokuwa na sifa, ni lini sasa Serikali itatoa ajira kwa kuwapa kipaumbele vijana wa nchi hii ambao kwa sasa ni wengi wamerundikana mtaani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kwa kuwa mikopo hiyo anayoizungumza Waziri, Halmashauri inatenga asilimia tano ambayo kwa sasa haiwezi kukidhi haja kulingana na idadai au wimbi kubwa la vijana walipo mtaani. Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuwa na mpango mkakati wa kuwapa mafunzo maalum au kuanzisha vyuo kwenye mikoa yote ili kuwapa ufanisi vijana waweze kujajiri? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili ya nyongeza, Mheshimiwa Antony Mavunde, Mbunge wa hapa tulipo.

## **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA**

**NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma ya kutengeneza nafasi nyingi za ajira hasa kwa kundi kubwa hili la vijana, Serikali imekuja na mipango mikakati mbalimbali, si kweli kwamba tunaweza tukawa tuna nafasi za kuwaajiri vijana wote kwenye sekta ya umma, ndiyo maana kupitulia program nilizozisema Serikali imeona ni vyema kuendelea kuishirikisha sekta binafsi, lakini vilevile na kwenda na falsafa ya uchumi wetu wa viwanda, lakini vilevile na kuwahimiza vijana kushiriki katika sekta za uzalishaji mali ikiwemo kilimo, ufugaji na biashara ili kwa pamoja tuwe tumetengeneza nafasi nyingi za ajira kwa vijana kuliko kuendelea kuwafanya vijana wengi wa Kitanzania kuamini kwamba nafasi za kazi ni lazima ziwe za maofisini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Ajira, imezungumza vyema kabisa tafsiri ya neno ajira maana yake ni shughuli yoyote halali inayompatia mtu kipato. Kwa hiyo, Serikali tunachokifanya ni kuendelea kutengeneza nafasi nyingi zaidi za ajira ili vijana wengi zaidi waweze kupata nafasi ya kujajiri na kuajiri vijana wengine.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la nyongeza amesema ni lini tutaanzisha mkakati wa kuanzisha vyuo ili kuwajengea vijana hawa uwezo. Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, tunavyo vyuo vya maendeleo ya vijana ambayo lengo lake ni kuwapa vijana mafunzo, kuwajengea ujasiri na kuwasaidia pia katika kuweza kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, pia kupitia programu hizi katika Ofisi ya Waziri Mkuu tunao Mpango Maalum wa Ukuzaji Ujuzi nchini ambaa lengo lake ni kumfanya kijana wa kitanzania apate ujuzi ambaa utamsaidia kujajiri na kuajiri vijana wengine.

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza hivi sasa kupitia mpango huu tayari tunao vijana takribani 2,000 ambaa wanapata mafunzo ya kutengeneza nguo na kukata vitambaa katika Kiwanda cha *Tooku Garment* pale Mabibo,

tunao vijana 1,000 ambao wako tayari *Mazava Fabrics*, Morogoro ambao wanajifunza kutengeneza *t-shirts* za michezo na wataajiriwa wote.

Mheshimiwa Spika, pia tunao vijana 1,000 ambao wako *D/T- Mwanza* wanajifunza kutengeneza viatu na bidhaa za ngozi. Tunao vijana 3,445 ambao wako katika sehemu mbalimbali za *Don Bosco* ambao wao wanapata mafunzo katika TEHAMA, kutengeneza vitanda kwa maana ya *carpentry, masonry*, ambao wote hao kupitia programu hii tunaamini kabisa watakwenda kusimama na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, ni hayo, naomba kuwasilisha.  
(*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu hayo mazuri. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Amina Makilagi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 2

#### **Hitaji la Maji Safi na Salama Halmashauri ya Wilaya ya Musoma**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE (K.n.y. MHE. AMINA N. MAKILAGI)** Aliuliza:-

Wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma katika Kata za Etaro, Ifulifu, Nyegina na Nyakatende wanakabiliwa na taizo la maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi wa kata hizo maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Amina Makilagi naomba kwanza nitoe shukrani zangu za

dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyoionyesha kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais , TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma katika Kata za Itaro, Ifulifu, Nyegina na Nyakatende wanakabiliwa na tatizo la maji kwa sababu mahitaji halisi ya maji katika kata hizo ni lita 953,550 wakati uzalishaji wa maji katika vyanzo vilivyopo ambavyo ni visima sita katika Vijiji vya Keimba na Kabegi kwenye Kata ya Ifulifu, Kijiji cha Mkikira katika Kata ya Nyegina na Vijiji vya Kigera, Nyegina na Kamguruki katika Kata ya Nyakatende vinazalisha lita 5,100 kwa siku pamoja na mradi wa maji ya bomba katika Kata ya Nyegina unazalisha lita 50,000 kwa siku na hivyo kufanya jumla ya lita zinazozalishwa kwa sasa kuwa 55,100 tu ambazo ni asilimia sita ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kuboresha huduma za maji kwenye eneo hilo, Serikali inakamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa maji utakaohudumia wakazi wa Manispaa ya Musoma pamoja na wakati wa Kata za Nyamkanga, Bukabwa na Busimwa katika halmashauri ya Wilaya ya Butiama na wakazi kwenye Kata za Etaro, Nyegina na Nyakatende katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma. Hadi sasa Serikali imeshapeleka shilingi milioni 900 kwenye Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma, ambayo inasimamia utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kazi ambazo zimeshatekelezwa hadi sasa ni kupima njia ya bomba, kuchonga barabara kuelekea Mlima Balima kutakakojengwa tenki lenye ujazo wa lita milioni mbili ambalo litasambaza maji kwa mtiririko kupeleka huduma za maji safi na salama katika kata nilizotaja. Aidha, taratibu za ununuzi wa mabomba yenye urefu wa kilometra 35 zimekamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini hili tatizo la hizi kata limekuwa la muda mrefu na hasa ukizingatia kwamba kata zenyewe ziko pembezoni mwa Mji wa Musoma. Nataka kuuliza ni lini haya maji yatawafikia hizo kata kwa sababu wamekuwa na usumbufu wa muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na matatizo ya mji wa Musoma pia kuna matatizo makubwa ya Mji wa Bunda na hasa Jimbo la Bunda ninakotoka mimi. Kuna kata saba zina matatizo makubwa ya uhaba wa maji ambazo ni Unyali, Kitale, Mgeta, Mihingo, Nyamaghunta na Salama; nilitaka kumuomba tu Waziri ni lini atafika? Nimuombe tu afike kwenye hizo kata saba za Jimbo langu ili aweze kujiona hali halisi ya uhaba wa maji katika jimbo hilo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu mafupi kwa sababu ni ombi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ni kweli kwamba, ni muda mrefu, lakini nimuhidi kwamba, mara mradi huu ambao umeanza kutekelezwa utakapokamilika wakazi hawa watafaidika na maji hayo. Swali la pili kuhusu Bunda; naomba nimuhidi Mheshimiwa Mwita Getere kwamba mara baada ya Mkutano huu wa Bunge nitatembelea Mkoa wa Mara na nitafika Bunda. Ahsante sana.

Na. 3

#### **Kufanya Vibaya kwa Shule za Sekondari za Umma Nchini**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani mahususi katika kuboresha mazingira ya kujifunza katika shule za umma za sekondari nchi nzima ikiwa ni pamoja na ukarabati wa majengo, madarasa, mabweni na maabara?

(b) Je, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuifuta kazi Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Elimu Tanzania na kuiunda upya kwa sababu imeshindwa kusimamia ubora wa elimu nchini?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifufua shule zilizokuwa za watoto wenyewe vipaji maalum?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), refu sana, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya juhudii mbalimbali za kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za umma za sekondari nchini. Kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II) ulianza kutekelezwa mwaka 2004 hadi mwezi Disemba 2016, jumla ya shule za sekondari 792 zimejengwa na kukarabatiwa miundombinu yake na kuwa shule kamili kwa gharama za shilingi bilioni 123.8.

Aidha, katika kipindi hicho jumla ya maabara 6,287 sawa na asilimia 60.52 ya lengo zimekamilika kati ya maabara 10,387 zilizohitajika. Kupitia Mpango wa Lipa kwa Matokeo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi bilioni 21.9 zimeidhinishwa kwa ajili ya upanuzi wa shule 85 za sekondari na shule 19 za msingi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya vyumba vya madarasa 320, mabweni 155 yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 80 kila moja na matundu ya vyoo 829 yatajengwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania huchangia katika kukuza ubora wa elimu nchini kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi chuo kikuu. Changamoto iliyopo ni upatikanaji wa fedha za kutosha

kuwezesha kutekeleza miradi mingi zaidi kama inavyotarajiwa na wananchi katika maeneo mengi nchini.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuzikarabati shule kongwe 89 zikiwemo shule nane za wanafunzi wenye vipaji maalum kuititia Mamlaka ya Elimu Tanzania na Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (*EP4R*). Mradi huu utakaogharimu jumla ya shilingi bilioni 89 hadi kukamilika unatekelezwa kwa awamu. Hadi kufikia Julai, 2017 jumla ya shule kongwe 43 zimekarabatiwa na shule 20 zitakarabatiwa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**SPIKA:** Mheshimiwa Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na niseme ninatambua jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano katika kuboresha elimu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati gani katika mabweni haya 155 ambayo inatarajia kuyajenga katika mwaka wa fedha 2017/2018 kuhakikisha kwamba, inazingatia kipaumbele katika ujenzi wa mabweni katika shule zetu za kata?

La pili, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Mamlaka ya Elimu ya Juu Tanzania ambayo inaonekana inapata changamoto kutokana na kutokuwa na fedha za kutosha, inatengewa fedha za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa kujenga mabweni kwa kushirikiana na Halmashuri na wananchi, kama ambavyo tumekuwa tukifanya na hivi natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote kule kwenye maeneo yao ambako kuna ujenzi wa mabweni, basi wasaidie

kuwahamasisha wananchi washiriki kikamilifu kwenye mkakati huu, lengo ni kuhakikisha kwamba, tunakamilisha ifikapo mwezi Juni mwakani, kama ambavyo tumejipanga.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tutaweka fungu maalum kwenye bajeti kwa ajili ya kuisaidia taasisi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja pamoja na taasisi nyingine ambazo zinasaidia maendeleo ya elimu nchini. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hatujaendelea, Mheshimiwa Katimba swali lako lilikuwa refu mno, ukiangalia pale ni maswali matatu ndani ya swali moja. Sasa maswali ya namna hii kwa kweli na tulishaeleza hapa Bungeni namna ya kuandika maswali, Katibu naelekeza kabisa maswali ya namna hii yasipangwe tena katika orodha, ukishalionia maswali yako lundo zima, msiyaweke yanatulia muda.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea.

Na. 4

### **Mradi wa REA /// Wilayani Nachingwea**

**MHE. HASSAN E. MASALA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali kupitia *REA* /// ina mpango gani wa kusambaza umeme katika kata zilizobaki Wilayani Nachingwea?

(b) Je, nini mpango wa Serikali kutatua tatizo la kukatikakatika kwa umeme Wilayani Nachingwea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa imani yake na nikushukuru wewe pia Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa vijiji vyote visivyo na umeme vinapata umeme kuititia mradi kabambe wa kupeleka umeme vijiji Awamu ya Tatu (*REA III*) unaotegemewa kukamilika mwaka 2020/2021. Mradi huu utajumuisha vipengele vitatu vya *Densification, Grid Extension na Off-Grid Renewables*. Mkoa wa Lindi chini ya Mradi wa Uendelezaji wa Gridi mzunguko wa Kwanza unatekelezwa kwa muda wa miezi 24 na Kampuni ya *State Grid & Technical Works Ltd*. Katika Wilaya ya Nachingwea Mpango wa Awamu ya Tatu utavipatia umeme vijiji 30. Kazi za utekelezaji wa mradi zilianza mwezi Julai, 2017 na zitakamilika Juni 30, 2019. Aidha, vijiji vilivyobakia vitapatiwa umeme katika mzunguko wa pili wa *REA III* utakaoanza Aprili, 2019 hadi Disemba 2021.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme mzunguko wa kwanza itajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 380, ufungaji wa transfoma 180, ujenzi wa njia za msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometra 360 na uunganishaji wa wateja wapatao 5,710 katika Mkoa mzima wa Lindi. Aidha, kwa Wilaya ya Nachingwea jumla ya wateja wapatao 1,200 wataunganishwa. Mkandarasi anaendelea na upimaji wa njia za umeme ambapo amefikia asilimia 30 na kazi za upimaji zitakamilika mwishoni mwa Novemba, 2017. Gharama za miradi hiyo ni jumla ya shilingi 24,636,112,764.82 na dola za Kimarekani 5,657,471.30 pamoja na VAT.

(b) Mheshimiwa Spika, umeme unaotumika katika Wilaya ya Nachingwe unatoka katika kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia kilichopo Mtwara Mjini ambapo njia ya kusafirisha umeme kutoka Mtwara ina urefu wa kilometra 210 na pia hugawa umeme katika maeneo ya Mkoa wa Mtwara kabla ya kufika Nchingwea. Hivyo, pakitokea tatizo lolote mwanzoni au katikati ya njia basi,

umeme hukatika katika maeneo mengi ya Mkoa wa Lindi, ikiwemo Nachingwea. Ili kukabiliana na tatizo hilo Serikali kuititia TANESCO imejenga njia mpya ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 kutoka Mtwara hadi Mnazi Mmoja, Lindi na kujenga kituo cha kupoza umeme chenye uwezo wa MVA 20, 132/33kV ambapo ujenzi wake umekamilika na mradi mzima umegharimu jumla ya shilingi bilioni 16.

Mheshimiwa Spika, umeme utapozwa katika msongo wa kilovoti 33 na kusafirishwa kwenda katika Wilaya za Ruangwa, Nachingwea na badae Liwale. Ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 ya Wilaya ya Ruangwa unategemewa kuanza Januari, 2018 baada ya kupatikana kwa fedha za utekelezaji. Pamoja na ujenzi huo, ukarabati wa miundombinu iliyopo unaendelea ili kuboresha mfumo mzima wa usambazaji katika Wilaya ya nachingwea na Lindi kwa ujumla.

**SPIKA:** Duh! Maswali ya nyongeza mengi kweli kweli. Mheshimiwa Masala, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa naomba kupata ufanuzi katika maeneo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni takribani miezi minne sasa imepita toka Mkataba wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu usainiwe pale Chinongwe, lakini mpaka leo nazungumza, pamoja na majibu aliyoyatoa, kazi kubwa iliyofanyika ni kuweka tu vijiti. Sasa nilikuwa nataka kujua Serikali imekwama wapi kutoa fedha mpaka sasa hivi kwa ajili ya kuanza kazi hii ya kusambaza umeme vijijini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, nilikuwa naomba nimuulize Naibu Waziri, pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme pale Mahumbika ambacho tuliamini kingekuwa ni tiba kwa tatizo la kukatika umeme kwa Mkoa wa Lindi na Mtwara. Ni jitihada gani za makusudi au za

dharura ambazo Serikali itakwenda kuchukua, ili kuwaondoa wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara gizani, ukizingatia maagizo ya kufunga mashine yalishatolewa na Mheshimiwa Waziri alipofanya ziara Mkoani Mtwara na aliwapa siku kumi, mpaka leo bado hakuna kilichotekelawa, naomba kufahamu nini kinaendelea?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri kwa ujumla wanaauliza *REA* /// mbona inasuasua kuna nini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ni kweli wakandarasi wa *REA* walishaanza kazi kama anavyosema miezi minne iliyopita na ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge pamoja n Bunge lako Mamlaka ya Umeme Vijiji (*REA*) wameshalipa kiasi cha takribani bilioni 28 kwa wakandarasi wote kama *advance*. Nimeongea pia na Mkandarasi wa Mkoa wa Lindi ambaye ni *State Grid*, yupo anafanya kazi na alikuwa katika Wilaya ya Ruangwa na kati ya vijiji 34 alikuwa ameviflikia vijiji 19 mpaka jana na akitoka Ruangwa ataaelekeea Wilaya ya Nachingwea. Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli Serikali imedhamiria kabisa kwamba vijiji vyote vilivyosalia na kwa awamu hii ya kwanza ni vijiji 3,559 mpaka 2019 umeme vitakuwa vimepetia.

Mheshimiwa Spika, swalı lake la pili aliuliza namna gani Serikali inachukua jitihada kumaliza tatizo la umeme Mikoa ya Mtwara na Lindi. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, mkandarasi anayefanya matengenezo ya mashine tisa za kuzalisha umeme Mkoa wa Mtwara ameanza hizo kazi. Vipuri vimewasili kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alielekeza na kazi inaendelea. Na mpaka jana mashine sita zenye uwezo wa kuzalisha megawati 12 zilikuwa zinafanya kazi, lakini pia Serikali imechukua hatua imeagiza mashine mbili mpya kwa ajili ya kuzalisha megawati nne kwa thamani ya bilioni nane ambazo zitafika mwakani mwezi wa tatu na zitakuwa zimefungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pia Serikali kupitia *TANESCO* inafanya matengenezo ya mtambo wa kuzalisha umeme Somangafungu ambao unazalisha

megawati 7.5. Tuna uhakika, naomba niwathibitishie wakazi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi itakapofika Disemba, 31 hali ya upatikanaji umeme Mtwara na Lindi itaboreka. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Jamani mnaiona bunduki hiyo? (*Makof*)

Kwa majibu hayo siruhusu swali la nyongeza, tunaendelea. Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala. Karibu Mheshimiwa Issa Ali Mangungu. (*Kicheko*)

Na. 5

**Miradi ya Umeme Jimbo la Mbagala**

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y MHE. ISSA A. MANGUNGU)** aliuliza:-

Je, ni lini miradi ya umeme yenyе zabuni Na. PA/001/2015/DZN/W/12 maeneo ya Chamazi Dovya, Kwa Mzala 1 – 3, Mbande kwa Masista na Chamazi Vigoa itakamilika ili wananchi wa maeneo hayo wapate umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi tajwa hapo juu katika maeneo yaliyotaja Mheshimiwa Mbunge ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chamazi Dovya kulikuwa na miradi mitatu na yote imekamilika. Kazi ya kupeleka umeme ilijumuisha ujenzi wa kilometra 3.297 za ujenzi ya njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 11, kilometra 1.4 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 na ufungaji wa transfoma nne za KVA 100 na transfoma mbili za ukubwa wa KVA 200 kila moja. Miradi hiyo mitatu iligharimu jumla ya shilingi 585,271,539 na

ilikamilika kati ya Juni, 2016 na Januari, 2017 na kwa sasa wananchi wa maeneo hayo wanapata umeme.

Mheshimiwa Spika, Mbande kwa Masista kuna miradi mitatu; Masista Magogo Na. 1, Masista Magogo Na. 2 na Masista Magogo Na. 3 na kazi ya kupeleka umeme ilijumuisha ujenzi wa kilometra 3.5 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 11, kilometra 15.8 za njia umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 na ufungaji wa transfoma tatu zenyenye ukubwa wa KVA 100 na transfoma tatu za ukubwa wa KVA 200 kila moja.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo ka ujumla ina thamani ya shilingi 726,075,289.40. Mradi wa Masista Magogo Na. 1 ulikamilika tarehe 17 Juni, 2017 na wateja wanapata umeme. Aidha, miradi ya Masista Magogo Na. 2 na Na. 3 itakamilika mwishoni mwa mwezi Disemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, Chamazi Vigoa kazi ya kupeleka umeme ilihuisha ujenzi wa kilometra 0.99 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 11; kilometra 3.92 za njia ya umeme wa kilovoti 0.4 na ufungaji wa transfoma tatu za ukubwa wa KVA 100 kila moja. Mradi huu wenye thamani ya shilingi 178,584,000 ulikamilika tarehe 9 Juni 2016 na wateja wanapata umeme.

**SPIKA:** Swali la nyongeza endelea Mheshimiwa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwanza nionyeshe masikitiko yangu makubwa kwa majibu ya Serikali, lakini natambua ugeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri na nimhakikishie kwamba hayo majibu ambayo umeandaliwa yana mapungufu makubwa.

Je, utakuwa tayari kwenda *field* kutembelea ukajioneed halii halisi iliyopo katika mradi huu kwa sababu sio kweli kwamba umekamilika?

Mheshimiwa Spika, la pili, kumekuwa na matatizo makubwa ya kukatikakatika kwa umeme na hasa

kunapokuwa na dalili za mvua au mvua inaponyesha. Je, tatizo hili la kukatikakatika kwa umeme litakwisha lini katika Halmashauri ya Temeke?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri amekutuhumu, majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi mwenyewe binafsi Jumapili nilifanya ziara ya kutembelea miradi hii na nilipita pamoja na *TANESCO*. Tulikuwa na Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Umeme (*TANESCO*) na Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Temeke tulitembelea. Katika majibu yangu ya msingi nimeainisha miradi ambayo haijakamilika na mradi ambaao haujakamilika ulikuwa Masista Magogo Na. 2 na Na. 3 ambaao utakamilika Disemba 2017.

Mheshimiwa Spika, kwahiyoo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba miradi hiyo kwa kweli nimeiona lakini changamoto kubwa iliyopo ni kwamba wakati miradi inakuwa *designed scope* yake na tunatambua maeneo ya Mbagala na Wilaya ya Temeke na Kigamboni ujenzi wa makazi unaongezeka kwa kasi, kuna maeneo yameongezeka wananchi wengi wamejenga. Kwa hiyo, *scope* ile imewaacha nje kwa hiyo unaona kwamba mahitaji yameongezeka kuliko ambavyo *scope* ilizingatiwa. Kwa hiyo, nimthibitishie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza tatizo la kukatikakatika kwa umeme kwa Wilaya ya Temeke litaisha lini. Ni kweli kuna tatizo la kukatikakatika kwa umeme maeneo ya Temeke, Mbagala, Yombo Dovya, Buza na Kigamboni. Serikali kuitia *TANESCO* imekuwaikitekeleza miradi mbalimbali, hata mwaka huu wa fedha imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.2.

Mheshimiwa Spika, sambaba na hilo kuna ujenzi wa miradi inayoendelea chini ya Mradi wa *TEDAP* (*Tanzania Energy Development and Access Expansion Project*). Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa msongo wa KVA 232 unaotoka

Gongolamboto mpaka Mbagala na ujenzi wa kituo kikubwa cha kupoozea umeme chenye MVA 50.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pia kuna ujenzi wa msongo wa umeme wa kilovoti 132 ambaa unatoka Mbagala unaelekea Kigamboni, ujenzi wa msongo wa umeme unaotoka Kurasini kuelekea Kigamboni. Kwa hiyo, jitihada zote hizo na tatizo linasababishwa na kuongezeka kwa mahitaji ya umeme Mbagala na ndio maana unakatikakatika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kutokana na kazi zitakamilika Desemba 2017 na kuanzia Disemba, 2017 nakuthibitishia kwamba tatizo la kukatikakatika kwa umeme kwa Wilaya ya Temeke litakuwa limepungua na litaisha kabisa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, umeona majibu hayo Mheshimiwa Mtolea, umemuita Mheshimiwa Waziri muongo, aende akatembelee, mwenzio keshafika *site*. Kwa hiyo, muongo unakuwa ni wewe sasa. Tuwe makini kidogo na maneno yetu, yana athari kwa umma kuitana waongo wakati kumbe watu wana heshima zao. (*Makofi*)

Tunaendelea na swali linalofuata la Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kwa niaba yake Mheshimiwa Kakoso nilikuona.

Na. 6

### **Usindikaji wa Mazao ya Kilimo**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO (K.n.y MHE. SULEIMAN J. ZEDI)**  
aliuliza:-

Serikali imejitahidi sana kupeleka umeme vijijini jambo ambalo litaongeza ajira kutokana na uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ya kilimo maeneo ya vijijini kama vile usindikaji wa mafuta ya alizeti,

kukoboa na kupaki mpunga na kusaga na kupaki unga wa mahindi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa vijiji kupata elimu, mitaji na masoko ili shughuli za kuanzisha usindikaji wa mazao ya kilimo kiwe tija?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Suleimani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Zedi kwa kutambua juhudii za Serikali za kupeleka umeme vijiji ambao ni kichocleo muhimu katika uanzishwaji wa viwanda vidogo vyaa usindikaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa viwanda katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi, Wizara yangu kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) inatekeleza mkakati wa Wilaya moja, bidhaa moja (*One District, One Product – ODOP*) ambao *SIDO* kwa kushirikiana na wadau katika Halmashauri walichagua bidhaa moja katika Wilaya kwa lengo la kuiendeleza. Kwa upande wa Bukene wao walichagua zao la mpunga.

Mheshimiwa Spika, hivyo, *SIDO* ina jukumu la kutoa huduma mbalimbali ikiwemo mafunzo juu ya usindikaji mazao ya kilimo, kuendeleza teknolojia rahisi za uongezaji thamani mazao ya kilimo na kuandaa maonesho ya kikanda ili kuwasaidia wajasiriamali waweze kupata masoko ya bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Ujasiriamali (*National Entrepreneurship Development Fund*) wananchi wa vijiji wamekuwa

wakikopeshwa fedha kwa masharti nafuu ili waweze kuanzisha miradi midogo na ya katika lengo la kujipatia ajira na kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, tunatambua tatizo la *SIDO* kutowafikia wananchi walio wengi zaidi vijijini kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa rasilimali fedha na mtandao wa shirika kuishia ngazi ya Mkoa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Hivi sasa changamoto hizo zitatazamwa kwa kina katika hatua ya kupitia upya sheria ilioanzisha shirika hilo kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa shirika katika kuhudumia jasiriamali ndogo na za katika nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa majibu ya Serikali, kwa kuwa wananchi wa Bukene wamepata fursa nzuri ya kupata umeme na wananchi wa Bukene wamejipanga katika shughuli nzima ya ujasiriamali na tatizo kubwa wao wana ukosefu wa mitaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wananchi wa Bukene ili waweze kupata mitaji na waweze kuanza shughuli za ujasiriamali?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Katavi una fursa nyingi za uwekezaji na vivutio vya kutosha hasa kwenye sekta ya kilimo, uvuvi na eneo la maliasili. Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara wana mpango upi wa kusaidia Mkoa huu ili kuweza kupatiwa wawekezaji waje kuwekeza katika maeneo hayo? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza katika suala la mitaji, nipende tu kuwashamasisha wananchi wote

wakiwemo wananchi wa Bukene kwamba mtaji wa kwanza ni mtu kuamua kufanya shughuli ya uzalishaji, mtaji wa pili ni huo wa kupata taarifa na mafunzo, lakini vilevile kufuatilia taasisi kama za benki na kwa upande wetu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupitia *SIDO* kama nilivyosema awali, tunao mfuko ambao unawezesha wajasiriamali pale ambapo wapo *serious* katika kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Katavi niwaombe kupitia Serikali ya Mkoa na Halmashauri na wananchi kwa ujumla kuendelea kuhamasisha fursa zilizopo katika Mkoa wa Katavi ili wawekezaji wengi wa ndani na wan je waweze kupenda kuwekeza katika Mkoa huo. Kwa siku za nyuma mmekuwa mkifanya makongamano mbalimbali ya kukaribisha wawekezaji, nashauri muendelee kufanya hivyo.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa *SIDO* ndio wanaohusika kutoa elimu kwa wajasiriamali wadogo lakini imeonekana wanachaji pesa kubwa sana hasa mafunzo ya vifungashio. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie ni jinsi gani *SIDO* itapunguza bei na kusaldia hao wajasiriamali wadogo waweze kufanikiwa katika biashara zao? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi la nyongeza *SIDO* wapunguze bei.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kimsingi bei iliyokuwa inakuwa-*charged* ilikuwa inategemeana na gharama halisi za upatikanaji wa vifungashio hivyo. Jambo ambalo tunaweza tukafanya ni kuendelea kuangalia uwezekano wa kuipatia *SIDO* ruzuku ya kutosha lakini pia kuwakaribisha watu binafsi katika kutengeneza vifungashio hivyo kwa kadri itakavyowezekana.

**SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri, kabla hatujaendelea kwa kuwa tupo kwenye viwanda, biashara na uwekezaji; niwajulishe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji baada ya Mheshimiwa Stanslaus Nyongo kupata wadhifa alionao sasa wa kuwa Naibu Waziri wa Madini ambaye ndio alikuwa kiongozi wa Kamati hiyo, Kamati imekutana na kuchagua Mwenyekiti mpya ambaye ni Mheshimiwa Suleiman Saddiq Murad na Mheshimiwa Murad ameshaanza kazi mara moja na leo hii anaambatana na msafara wa Mheshimiwa Rais katika kukagua Kiwanda cha Sukari cha Kagera. (*Makofi/Vigelegele*)

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali linaulizwa na Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli, Mbunge wa Lupembe.

Na. 7

#### ***MSD Kuchelewesha Dawa Kwenye Halmashauri***

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Dawa zinazotolewa na *MSD* zimekuwa zikichelewa sana kupelekwa kwenye Halmashauri na hivyo kusababisha baadhi ya dawa kupelekwa zikiwa zimekaribia kuisha muda wake wa matumizi hali inayozisababishia Halmashauri gharama kubwa za utekelezaji.

Je, ni kwa nini gharama za uteketezaji wa dawa hizo zigharamiwe na Halmashauri badala ya *MSD* ambayo inachelewa kuzipeleka?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO** aliibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu wa usambazaji wa moja kwa moja wa dawa kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya umma (*direct delivery*) unaofanywa na Bohari ya Dawa (*MSD*). Kwa mujibu wa utaratibu huu, Kamati za Afya za vituo husika kupokea na kuhakiki kila dawa iliyopokelewa kituoni hapo kama inavyoonyeshwa kwenye hati ya madai. Hati hiyo huonyesha ghamama za dawa pamoja na muda wa dawa kuisha matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, endapo Kamati ya afya ya kituo haitaridhika na kupokea dawa kwa sababu yejote ile muhimu ikiwa ni pamoja na kuharibika au dawa kuwa na muda mfupi kwa matumizi, kituo hutakiwa kujaza fomu namba saba ili kurudisha bidhaa iliyokataliwa moja kwa moja Bohari ya Dawa ambapo ghamama ya dawa husika hurejeshwa kwenye akaunti ya kituo husika.

Mheshimiwa Spika, taarifa za usambazaji wa dawa na vifaa tiba kutoka *MSD* katika Halmashauri ya Njombe kwa mwaka 2016/2017 hazionyeshi uwepo wa dawa zilizosambazwa zikiwa na muda mfupi wa matumizi. Hivyo, *MSD* haipaswi kugharamia uteketezaji wa dawa zilizokwisha muda wa matumizi katika Halmashauri ya Njombe kwa kuwa jukumu la uteketezaji ni la Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nitumie Bunge lako Tukufu kuzitaka Halmashauri zote nchini kuzingatia vyema taratibu za kupokea, kuhifadhi na matumizi ya dawa.

**SPIKA:** Swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa swali la nyongeza, ninalo moja tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe haina Hospitali ya Wilaya na ina kituo kimoja kikubwa sana cha afya ambacho wananchi wengi wanatibiwa pale na kituo hiki kipo umbali wa takribani kilometra 80 kutoka Njombe mjini mpaka kule Lupembe.

Je, Serikali haioni kama inaweza ikatoa au ikafungua duka la dawa pale Lupembe ili iwe rahisi kwa wananchi kupata dawa kuliko kusafiri umbali mrefu pale dawa zinapokosekana kwenda Kibena ambapo inatarajiwa kufunguliwa duka la dawa lakini bado halijafunguliwa? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la nyongeza Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, suala la kufungua maduka ya dawa, tumelirudisha kwa Halmashauri husika kwa sababu moja ya vyanzo vikubwa vyta mapato katika hospitali ni kutoka mauzo ya dawa. Kwa hiyo, suala hili ni Halmashauri yenye we ya Njombe kuweka fedha kidogo kwa ajili ya kufungua au kuanzisha duka la dawa.

Mheshimiwa Spika, sisi tupo tayari kumsaidia kuitia *MSD* endapo wataweka miundombinu ya kuanzisha duka la dawa tupo tayari kuwakopesha dawa zenye thamani mpaka ya shilingi milioni 50 ili wananchi wa Halmashauri ya Njombe waweze kupata dawa bila changamoto zozote, ahsante.

**SPIKA:** Nakuona Waziri Kivuli Afya, kuna swali lolote la nyongeza Dkt. Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante, hapa tunachokisema ni katika nchi ambayo kuna upungufu mkubwa wa dawa, lakini vilevile unaona kuna dawa ambazo zinaharibika na tunatumia mabilioni ya fedha kuteketeza hizo dawa. Mheshimiwa Waziri wa Afya hawezi akafikiri kwamba kuna umuhimu wa kutizama kwamba inawezekana kuna ujisadi kati ya *MSD* na viwanda vikubwa vyta dawa kugeuza nchi yetu kama *dumping space* ya dawa, atuletee kuja kututhibitishia hapa Bungeni kwamba hakuna ujisadi kati ya wanaonunua dawa katika nchi hii na viwanda vikubwa? Nikwambie Waziri sikurupuki, hebu tufanye hiyo kazi uone kama hujakuta kuna shida hapo. (*Makof!*)

**SPIKA:** Majibu ya wasiwasi huo Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka kumsahihisha Waziri Kivuli jambo moja, hakuna upungufu mkubwa wa dawa Tanzania na katika jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli amelifanya ikiwemo katika Jimbo lako ni kuongeza bajeti ya dawa.

Mheshimiwa Spika, na dawa muhimu zaidi na Mheshimiwa Dkt. Mollel unajua, tunaposema upatikanaji wa dawa tunapima dawa 135 na katika Halmashauri yako ya Siha zipo. Nataka kuonesha mfano kwa sababu swali hili lilikuwa ni la Njombe, Njombe walikuwa na bajeti ya dawa shilingi milioni 43 kwa sababu ya jitihada za Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, bajeti ya dawa ya Njombe ni zaidi ya shilingi milioni 150 kutoka shilingi milioni 43. Kwa hiyo, tusikariri taarifa zilizopitwa na wakati. Kama mnataka kumtendea haki Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, mtendeeni haki kwa kumpima ni kiasi gani amewekeza katika upatikanaji wa dawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; Mheshimiwa Dkt. Mollel wewe ni mtaalam, kuna *international standard* za dawa kuchina, dawa ambazo zinaruhusiwa ku-expire. Kama umenunua dawa za milioni 100 zisifike asilimia tano ya kiasi cha milioni 100. Tanzania dawa zinazochina ni asilimia 1.8, tupo chini ya kiwango cha kimataifa cha asilimia tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini dawa zinachina Tanzania? Tunazo changamoto na namshukuru sana Mheshimiwa Jafo, kuna tatizo kubwa la maoteo. Watu hawaleti mahitaji halisi ya dawa lakini Mheshimiwa Jafo amechukua hatua na sasa hivi TAMISEMI wanajipanga kuleta maoteo halisi ya dawa.

Mheshimiwa Spika, hatua kubwa ambayo tumechukua, kwa nini dawa zinachina ni dawa za misaada.

Unakuta sisi tumenunua dawa kwa ajili ya kutibu malaria unaletewa tena dawa za misaada. Tumechukua mwongozo, sasa hivi hatupokei dawa ya msaada ambayo *either* imekaribia kuharibika muda au dawa hiyo tayari tunayo katika bohari ya dawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliona nimpe shule Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa sababu yeye ni mtaalam. (*Makofi/Vigelegele*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, inaonekana Waziri Kivuli hayupo *informed* kabisa na kinachoendelea. (*Makofi*)

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, changamoto kwa Mawaziri Kivuli jamani muwe mna..., Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi tafadhalii. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 8

### **Utekelezaji wa Mpango wa Kilimo Kwanza**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Katika Mpango wa Kilimo Kwanza Serikali ilihamasisha Watanzania kuongeza uzalishaji katika kilimo ili Serikali itoe mikopo ya matrekta kwa wingi.

(a) Je, kumekuwa na mafanikio kiasi gani kwa mazao ya biashara na chakula?

(b) Kama kumekuwa na mafanikio, je, kuna utaratibu gani wa kuendeleza mpango huo kwa wananchi wanaohitaji kukopeshwa matrekta wakiwemo wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru sana Mungu. Vilevile ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa dhamana hii. Ninakushukuru sana wewe binafsi kwa kunilea vyema na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Kilimo Kwanza umekuwa na mafanikio katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara nchini ambapo uzalishaji wa jumla wa mazao ya biashara katika msimu wa 2016/2017 umeongezeka kufikia tani 881,583 ikilinganishwa na tani 796,562 mwaka 2015/2016. Aidha, uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka hadi kufikia tani 16,172,841 kwa msimu wa 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula kwa Mkoa wa Singida umeongezeka kutoka tani 453,097 mwaka 2013/2014 hadi tani 481,452 kwa mwaka 2015/2016. Aidha, uzalishaji wa mazao ya biashara umeongezeka kutoka tani 184,066 mwaka 2012/2013 hadi tani 293,873 kwa mwaka 2015/2016. Uzalishaji wa mazao ya chakula katika Wilaya ya Manyoni umeongezeka hadi kufikia tani 42,554 kwa mwaka 2015/2016 ambapo uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka tani 1,342 mwaka 2011/2012 hadi kufikia tani 6,212 mwaka 2015/2016. Alizeti uzalishaji umeongezeka kutoka tani 4,464 mwaka 2010/2011 hadi tani 21,871 mwaka 2016/2017, na ufuta umeongezeka kutoka tani 2,285 mwaka 2010/2011 hadi kufikia tani 8,874 kwa mwaka 2015/2016.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya matrekta 18,774 yanafanya kazi nchini ambapo kati ya matrekta hayo, matrekta makubwa ni 11,500 na matrekta madogo ya mkono ni 7,274. Aidha, Wilaya ya Manyoni ina matrekta makubwa 32, matrekta madogo ya mkono 39 na wanyamakazi 14,782 ambapo kilimo cha kutumia maksai ni maarufu katika Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali Kuu katika kuhakikisha wakulima wanapata zana bora za kilimo, halmashauri za wilaya pia zimeelekezwa kuhamasisha wakulima kujunga au kuanzisha vyama vya akiba na mikopo (*SACCOS*) ambavyo vitakopesha wanachama wake au kuwadhamini kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya kununua matrekta na zana zake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Massare, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake haya mazuri, majibu yenye kutia moyo, majibu ambayo yanaonyesha dhamira ya kweli ya Serikali katika kuondokana na dhana hii ya upungufu mkubwa wa chakula, hasa katika mikoa kame, mikoa ya katikati.

Mheshimiwa Spika, majibu yake haya yameonyesha kwamba wanakopesha vyama vya akiba na mikopo kama *SACCOS*. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje juu ya wananchi wa Jimbo langu ambao wengi wao hawajajiunga na *SACCOS*, wataweza kupatiwa mikopo hii ya matrekta?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali imeanza kuonesha nia na wanawekeza katika kuunganisha matrekta hapa nchini, ikiwemo pale *TAMCO* Kibaha.

Je, katika kuwahi msimu huu wa kilimo anaweza akatutengea matrekta hata matano tu ambayo tuko tayari kuyalipia kwa awamu ya kwanza katika Jimbo la Manyoni Magharibi, Halmashauri ya Itigi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Kilimo kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba katika majibu yangu ya msingi nikianzia na lile swali lake la pili nimejibu kwamba wananchi wanaweza wakajiunga katika vikundi ili waweze kukopeshwa kupitia katika Mfuko wa *SACCOS*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nikija katika swali lake la kwanza, ameuliza kama wananchi wanaweza wakakopeshwa mmojammoja. Na mimi naomba nimwambie kabisa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi kwamba Wizara ya Kilimo imefanya utaratibu kupitia Mfuko wake wa Taifa wa Pembejeo na Kilimo, kwamba tunaruhusu mkulima yejote mmojammoja kuweza kukopa jinsi anavyotaka.

Mheshimiwa Spika, kubwa la msingi aweze kwenda kwenye halmashauri zetu kule atakutana na maafisa wa kilimo na mkurugenzi, atajaza fomu atapeleka katika mfuko wetu wa pembejeo akiwa na *proforma invoice* yake na sisi kupitia mfuko huo tuko tayari hata kutoa mifuko kwa wakulima na mikopo kwa wakulima wadogo wadogo. Ahsante. (*Makofii*)

Na. 9

### **Kukamilika kwa Mradi wa Umwagiliaji**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Mwaka 2013 Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, aliahidi kutoa shilingi 295,000,000 kwa ajili ya kusaidia ukamilishaji wa mradi wa umwagiliaji uliopo katika Kijiji cha Nundwe, Kata ya Ihalimba.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hii ya Waziri Mkuu Mstaafu ili vijana walio wengi wapate ajira?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso tafadhali. (*Makofii/Vigelegele*)

## **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu. Lakini la pili, nimshukuru sana Rais wangu, Dkt. John Pombe Magufuli, lakini pamoja na wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushirikiano wote mnaonipa kipindi ambacho nipo Bungeni hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, ilianza kutekelezwa mwaka 2014 kwa Serikali kutoa kiasi cha shillingi milioni 101 ikiwa ni sehemu ya ahadi ambapo fedha fedha hizo zilitumika kujenga banio la Skimu ya Umwagiliaji ya Nundwe. Wakulima wa skimu hiyo waliweza kuchangia nguvukazi kwa kuchimba mfereji mkuu wenye urefu wa mita 1,500. Hata hivyo, usakafiaji wa mfereji mkuu kwa lengo la kudhibiti upotevu wa maji haujafanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa mradi huu, Wizara yangu hivi sasa inafanya mapitio ya mpango kabambe wa umwagiliaji wa mwaka 2002 ambapo miradi yote iliyoanzishwa na haijakamilika na ile inayohitaji ukarabati imepewa kipaumbele katika utekelezaji. Hivyo basi, mradi huu utaingizwa katika bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa hatua zaidi ya utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa swali la nyongeza.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Serikali, nina swali moja na ombi moja.

Ombi, namuomba Mheshimiwa Naibu Waziri mara baada ya Bunge hili aje pale kwenye Kijiji cha Nundwe atembelee mradi huu aweze kujiona hali halisi na mahitaji ya mradi huu ambao unatarajia kuajiri vijana wasiopungua takribani 5,000.

Mheshimiwa Spika, swalilangu, mradi huu ni miongoni mwa miradi ya *FP* / ambao ulikuwa na thamani ya milioni 660. Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu alipokuja kufungua mradi huu, tayari shilingi milioni 101 zilikuwa zimeshatumika lakini ilionekana kulikuwa kuna mahitaji ya shilingi milioni 295 ili mradi uweze ku-*take off*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kwamba baada ya miezi mitatu shilingi milioni 295 zingekuwa zimefika, maana zingekuwa zimefika Juni, 2015, lakini mpaka leo hizi hela hazijafika. Sasa nataka Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie, lini watatuletea hizi hela, shilingi milioni 295, ili vijana waweze kupata ajira?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya nyongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, moja, kuhusu ombi la mimi kwenda katika Kijiji cha Nundwe, nataka nimhakikishie, kwa kuwa anayelala na mgonjwa ndio anayejua mihemo ya mgonjwa, nipo tayari kwenda kuukagua mradi ule ili usikwame, ili uweze kuleta uvezeshaji wa kiuchumi na chakula cha kutosha kwa kijiji kile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu swalilangu la pili; lengo la Serikali ni kukamilisha miradi yote ili iwe endelevu katika suala zima la utekelezaji. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutatafuta fedha katika vyombo mbalimbali ili kuhakikisha fedha zile zinapatikana ili mradi usikwame uende kutekelezwa mara moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

Na. 10

**Kipande cha Barabara (Mugumu – Nata) Mara – Arusha**

**MHE. MARWA R. CHACHA** aliuliza:-

Katika bajeti ya 2016/2017 kipande cha barabara (Mugumu – Nata), ni barabara pekee inayounganisha Mkoa wa Mara na Arusha, kilitengewa fedha shilingi bilioni 12; tangazo la zabuni ya barabara lilitoka mara tatu na mwishoni mkandarasi wa kujenga barabara hiyo akapatikana, lakini Serikali ilikataa kusaini mkataba kwa maelezo kwamba Serikali haina fedha wakati fedha zilitengwa kwenye bajeti.

(a) Je, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa barabara hii ambayo iko kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM?

(b) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Mkoa wa Mara kuhusu ujenzi wa barabara hii?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba uniruhusu nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake, na nimshukuru kipekee Mheshimiwa Raís kwa kunitfea ili niweze kutumika kama Naibu Waziri wa Ujenzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii tayari imeshaiweka kwenye mpango wa ujenzi kwa kiwango cha lami barabara hii ya Mugumu – Nata yenye urefu wa kilimotea 41.725 na barabara ya kuunganisha Mji wa Mugumu zenye urefu wa kilometra 1.575 kwa kukamilisha usanifu wa kina na nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uhakiki wa fidia ya mali za wananchi zitakazoathiriwa na ujenzi wa barabara ya Mugumu – Nata na tathmini hiyo imeshapelekwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa mapitio na kuidhinishwa ili hatimaye malipo ya fidia kwa wananchi yafanyike.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaanza taratibu za ununuzi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo, hivyo, baada ya malipo ya fidia kufanyika, taratibu za kumpata mkandarasi zitakamilishwa ili ujenzi kwa kiwango cha lami uanze. Aidha, kwa sasa Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) inaendelea kuifanya matengenezo barabara ya Mugumu – Nata ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Mbunge wa Serengeti.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ambayo inaunganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha imetengewa fedha mwaka 2016/2017, shilingi bilioni 12. *Tender* ikatangazwa kuanzia mwezi wa Disemba, 2016, hivi ninavyoongea ni mwaka mwingine wa fedha bado mkandarasi hajapatikana. Wananchi wa Jimbo la Serengeti, wananchi wa Mkoa wa Mara na Arusha wanataka kusikia, ni lini *compensation* na ujenzi wa barabara hii utanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa sasa kipande cha Barabara Nata – Mugumu hakipitiki, kimesababisha mfuko wa *cement* sasa hivi ni shilingi 22,000. Mna mpango gani wa kutengeneza kipande hiki kwa kiwango cha changarawe kwa wakati huo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Naibu Waziri tafadhalil.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kuwa Serikali inafanya juhudhi ya kufanya barabara hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja ambayo inatoka maunganiko

ya barabara kwenda Sanzate - Mugumu - Nata mpaka Arusha kama alivyotaja ina urefu wa kilometra 472.

Kwa hiyo, kwenye Awamu ya Kwanza barabara hiyo ya maunganisho imeshakamilika lakini sasa kwa eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge anataja ni kweli kuna fedha zilitengwa katika mwaka 2016/2017, shilingi billioni 20, hii ilikuwa ni sehemu ya barabara nzima, lakini kwa mwaka huu wa fedha pia kuna shilingi billioni 17.397 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, hatua za ujenzi ni *process*, ni hatua ya tathmini na kulipa fidia ni hatua ya ujenzi wa barabara hii. Kwahiylo, baada ya tathmini ambayo imeshapelekwa, kiasi cha kama shillingi billioni 4.1 ambazo zinahakikiwa kwa sababu zoezi la kuhakiki ni kujihakikishia kwamba malipo yanafanyika kwa uhalali, kumekuwa na matatizo kwenye utathmini, saa nyingine kumekuwa na rekodi ambazo sio sahihi, kwahiylo baada ya kukamilisha zoezi hili, *process* ya manunuzi itakuwa inakamilishwa na ujenzi utakuwa unaendelea kwenye awamu hii ya pili.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu agizo kwa upande wa *TANROADS*, kama eneo hili halipitiki basi *TANROADS* Mkoa wa Mara waende waliangalie eno hili ili warekebishe maeneo wananchi waendelee kupita wakati hatua za ujenzi zinaendelea. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu mazuri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Naibu Waziri. Sijui kwa nini Mheshimiwa Mbunge wa Serengeti, inajengwa Nata – Mugumu badala ya Nata – *Fort Ikoma* – Mugumu, sijui kwa nini.

Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 11

## **Hitaji la Meli kwa Wananchi wa Mkoa wa Kagera**

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI** aliuliza:-

Wananchi wa Mkoa wa Kagera wanakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa usafiri wa meli, jambo ambalo linawasababishia usumbufu mkubwa na usafiri wa mabasi umekuwa na gharama na hatari zaidi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia usafiri wa meli wananchi hao ili kuwapunguzia gharama pamoja na ajali za mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, vilevile nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu. Nimshukuru na Raís wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuweza kumsaidia. Lakini vilevile nikushukuru kwa ushirikiano pamoja na Wabunge wote, ambao mmeendelea kunipa katika kipindi ambacho nilitumika kama Mwenyekiti wa Kamati na Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri katika Ziwa Victoria kati ya Mwanza na Bukoba zilisimama mwezi Machi, 2017 baada ya meli ya *MV Serengeti* kupata hitilafu katika *engine* na mfumo wa shafti. Serikali imeipatia Kampuni ya Huduma za Meli (*MSCL*) kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya ukarabati wa meli nne za Ziwa Victoria ikiwemo meli ya *MV Serengeti*. Matengenezo ya meli hii yamekwishaaza baada ya vifaa vyake kupatikana na yanatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Januari, 2018.

Mheshimiwa Spika, mbali na ukarabati wa *MV Serengeti*, Serikali kuitia *MSCL* inatekeleza mradi wa ukarabati mkubwa wa Meli ya *MV Victoria*. Mzabuni kwa ajili ya kutekeleza kazi hii amekwishapatikana ambaye ni *KTM Company Limited* kutoka nchini Korea Kusini. Taratibu za uhakiki (*due diligence*) wa kampuni hii zinaendelea na mkataba unatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Novemba, 2017. Matengenezo haya yanatarajiwa kutumia muda wa miezi kumi tangu kusainiwa kwa mkataba.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imekamilisha utaratibu wa kumpata mkandarasi atakayetekeliza mradi wa ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria yenye uwezo wa kubebe abiria 1,200 na tani 400 za mizigo. Mkandarasi aliyepatikana ni Kampuni ya *STX Shipbuilding and Chipyard Company Limited* kutoka nchini Korea Kusini. Utaratibu wa uhakiki wa kampuni hii unaendelea na mkataba wa utekelezaji wa kazi unatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Novemba, 2017. Utekelezaji wa ujenzi huu utachukua takribani miezi 24 tangu kusainiwa kwa mkataba.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Serikali kuwa kukamilika kwa miradi hii mitatu itasaidia kuwaondolea adha ya usafiri wananchi wote watakaokuwa wanasafiri kwa njia ya maji katika Kanda ya Ziwa Victoria wakiwemo wakazi wa Mkoa wa Kagera. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Alfredina swali la nyongeza tafadhalii.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniamsha mara ya pili. Swali langu la nyongeza, je, Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha kwamba huduma hii haijurudii baada ya kupata usafiri endelevu, ili kadhia hii isiweze kujirudia tena? Ahsante (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Alfredina, siku zijazo ukumbuke Kanuni leo nimekumezea. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali inafanya miradi mitatu ya kuhakikisha kwamba meli tatu katika Ziwa Victoria zinafanya kazi kwa pamoja. Kwa hiyo, tuna uhakika kabisa kwamba hata itakapotokea meli moja imepata hitilafu kutakuwa na meli mbili ambazo zinaendelea kufanya kazi kwa pamoja. Ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata la Wizara hii hii la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Rhoda tafadhalii.

Na. 12

**Fidia kwa Wananchi Wanaopisha Ujenzi wa Reli**

**MHE. RHODA E. KUNCHELA** aliuliza:-

Ujenzi wa reli ya kati ni hatua inayochukuliwa kuboresha miundombinu katika nchi hii.

Je, Serikali inawasaidiaje wananchi wanaokumbwa na bomoabomoa kupata fidia zao kwa wakati hasa ukizingatia kuwa wananchi wengi ni maskini na hawawezi kumudu gharama za kujenga makazi upya?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuendeleza mtandao mzima wa reli kwa kiwango cha kimataifa (*standard gauge*) ukiwa na jumla ya urefu wa kilometra 4,886. Mtandao huu wa reli unajumuisha

Ukanda wa Kati ambaao una kilometra 2,561 amabao unajumuisha reli ya kutoka Dar es Salam - Isaka - Mwanza (kilometra 1,219), Tabora – Uvinza – Kigoma (kilometra 411), Kaliua – Mpanda – Karema (kilometra 321), Isaka – Rusumo (kilometra 371), Keza – Ruvubu (kilometra 36) na Uvinza – Kalelema kuelekea Msongati (kilometra 203). Ukanda wa Kusini ambaao unajumuisha reli ya kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay na matawi yake ya kuelekea Liganga kwa ajili ya chuma na Mchuchuma kwa ajili ya makaa ya mawe yenye jumla ya urefu wa (kilometra 1,092) na Ukanda wa Kaskazini ambaao unajumuisha reli kutoka Tanga – Arusha – Musoma yenye jumla ya urefu wa kilometra 1,233.

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kuwa asilimia 75 ya njia ya reli mpya itapita katika hifadhi ya reli iliyopo. Wananchi waliopo katika hifadhi ya reli wanapaswa kuondolewa bila kulipwa fidia kwani wamevamia maeneo ya reli. Aidha, zoezi la ubomoaji linaloendelea sasa linalenga kuwaondoa wavamizi wa hifadhi ya reli na maeneo ya uendeshaji yaliyotengwa tangu reli ya kwanza ilipoanza kujengwa kati ya mwaka 1904 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hakuna mgogoro wala athari zilizojitokeza katika utwaaji ardhi mpya ili kupisha mradi wa reli ya kisasa kwa sababu usanifu utakaonyesha wananchi watakaopitiwa unakamilishwa.

Aidha, Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (*RAHCO*) imeajiri Mshauri Mwelekezi kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi kwa ajili ya kufanya kazi ya utwaaji wa ardhi na tathmini kwa wananchi watakaolazimika kupisha reli hiyo. Ushirikishwaji wananchi, sheria na taratibu zote za nchi zitafuatwa ipasavyo katika kutekeleza zoezi la fidia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda Kunchela, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba wananchi hawa watabomolewa nyumba zao na Serikali haitalipa fidia na tafsiri yake ni kwamba wananchi hawa wamevunja sheria.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Oktoba, 2017 Rais alipokuwa Mwanza, alizua wananchi wa Mwanza kubomolewa makazi yao. Je, kauli hii ililenga Ukanda wa Mwanza peke yake au ni Tanzania nzima? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, imekuwa ni kawaida kwa Serikali hii ya CCM kuendelea kupeleka huduma za kijamii katika maeneo hayo ambayo wananchi wanabomolewa ikiwepo kata ya Tambukareli, Msasani pamoja na Illemo, huduma za maji, umeme pamoja na vituo vya kupigia kura lakini leo hii mnakwenda kuwabomolea. Je, ni kwa nini Serikali haina mkakati wa kuhakikisha sasa inazuia huduma hizo katika maeneo hayo kwa sababu hayajapimwa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Atashasta Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, wakati mwingine ni lazima Waheshimiwa Wabunge tushirikiane na Serikali na tufuatilie taarifa rasmi zinazotolewa na Serikali. Mheshimiwa Rais kauli yake haikumaanisha waliovamia hifadhi ya reli.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, wale ambao wamevamia hifadhi nya reli ambapo vipimo vyake viro kabla ya mwaka 1904 wataondolewa bila kulipwa fidia yoyote na wale ambao reli itawafuata kwenye maeneo yao utaratibu wa fidia unaendelea kupangwa na watalipwa kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linauliza kuhusu huduma zinazoendelea kupelekwa. Kiukweli ni kwamba sehemu nyingi sana ambazo ni maeneo ya hifadhi ya reli baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu wameendelea kuwapimia viwanja wananchi. Wale tulikwishaongea na kwamba Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na TAMISEMI watawachukuliwa hatua watumishi wasiokuwa waaminifu lakini bado nina hakika wananchi walikuwa wanajua kwamba wanapimiwa maeneo ambayo si sahihi kwao kwenda kujenga kwa sababu yanaeleweka wazi.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe mfano kidogo, maeneo yaliyopita umeme mkubwa wa Gridi ya Taifa yako wazi na wananchi hawaendi kujenga kule, lakini wao hawalalamikiwi isipokuwa sehemu ya reli ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu watu wanaivamia na hawaulizwi. Kwa hiyo, ukweli kwamba huduma zillizopelekwa zitaondolewa uko palepale kwa sababu hata waliojenga mabondeni nao huduma zinaondolewa ili kupisha huduma za kijamii, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, tafadhali.

Na. 13

**Kulipa Pesheni Wafanyakazi wa *TTCL* Waliokuwa  
Chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA** aliuliza:-

Wafanyakazi wa *TTCL* wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki waliolipwa pesheni ni wale waliofungua kesi mahakamani na kushinda. Aidha, wapo ambao wanastahili malipo lakini hawakuwa na uwezo wa kumlipa Wakili katika kuendesha kesi hiyo.

Je, ni lini Serikali itawalipa wafanyakazi wa *TTCL* wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki madai ya pesheni zao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wiziri ya Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba wafanyakazi wa *TTCL* wa iliyokuwa Jumuiya ya Mashariki waliolipwa pesheni ni wale tu waliofungua kesi mahakamani. Kumbukumbu zinaonyesha kwamba tarehe 31 Disemba, 1990 Serikali ilisitisha mfuko wa ujulikanao kama *East Africa Non Contributory Pension Scheme* baada ya kushauriana na kukubaliana na Menejimenti pamoja na Chama cha Wafanyakazi wa *TTCL* wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya kusitishwa kwa mfuko huo kila mfanyakazi alilipwa asilimia 50 ya michango yake na asilimia 50 iliyobaki illipelekwa *NSSF* kwa ajili ya pesheni ya kila mwezi pindi watakapostaaifu. Ni vema ikafahamika kwamba, wafanyakazi wote wa *TTCL* wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanalipwa pesheni zao na *NSSF* baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya malipo ya asilimia 50 kwa 50 kukamilika, wafanyakazi 254 hawakuridhika na maamuzi ya Serikali ya kusitisha mfuko wa *East African Non Contributory Pension Scheme* na kufungua kesi Na. 69/ 2005 Mahakama Kuu kupinga maamuzi ya Serikali. Katika shauri hilo, Mahakama Kuu illiamua kuwa uamuzi wa Serikali kusitisha mfuko huo haukuwa sahihi kisheria na hivyo wafanyakazi 254 walikuwa katika shauri hilo walipwe madai yao ambayo yalijumuisha malipo ya mkupuo, riba pamoja na pensheni ya kila mwezi ya wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Spika, baada ya uamuzi huo wa Mahakama Kuu, Hati ya Makubaliano (*Deed of Settlement*) yenye tuzo ya shilingi 13,685,450,397.82 ilisainiwa mnamo tarehe 27 Agosti, 2013 na kusajiliwa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam mnamo tarehe 2 Agosti, 2013 ikiwa ni tuzo kwa wafanyakazi wote waliofungua shauri husika. Aidha, mahakama ilielekeza kuwa wadai katika kesi hiyo ambaao bado wako kazini malipo yao yatafanyika mara

baada ya kustaafu. Kwa mujibu wa Hati ya Makubaliano malipo yaligawanywa katika awamu tatu ambapo hadi kufikia Julai 2017 awamu zote tatu zimelipwa jumla ya shilingi 12,665,994,447.92.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa wastaafu 245 wameshalipwa madai yao yote ya fedha za mkupuo ambapo kati yao wastaafu 54 wamefariki dunia na fedha zao walilipwa warithi na wastaafu 198 wanaendelea kulipwa malipo ya nyongeza ya pensheni ya kila mwezi. Kwa upande wa wadai ambao bado wapo kazini amebaki mmoja na wengine wawili wamestaafu hivi karibuni na tunatarajia kuwaombea fedha zao mwezi huu wa Novemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mahakama Kuu kutoa uamuzi huo, lilitokeza kundi lingine la wastaafu wa *7TCL* walliokuwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Ilkiongozwa na Bwana L. Mwayela na wenzake 324 na kuomba kuunganishwa katika *Deed of Settlement* ya kesi Na 69/2005 kati ya Bwana Berekia G. Mkwama na wenzake 254 dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa kuwa Mahakama Kuu iliamua pamoja na mambo mengine kuwa wafanyakazi waliofungua kesi hiyo ndiyo walipwe madai yao na kwamba *Deed of Settlement* iliyosajiliwa Mahakamani ilihusisha wafanyakazi waliofungua kesi hiyo tu, wafanyakazi wengine ambao hawakuwa sehemu ya kesi hiyo hawawezi kulipwa kwa kutumia hukumu na tuzo ya kesi ambayo hawakuwa sehemu yake. Kwa msingi huo, Serikali haiwezi kulipa madai mengine ambayo hayajathibitika kisheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ukiparipata kuangalia suala hilo jinsi lilivyo, hawa wote walikuwa wanastahili kulipwa lakini kilichotokea ni kwamba wenza walikuwa na uwezo wakaajiri *advocate* na kwenda mahakamani.

Je, Serikali haioni busara kwa sababu kesi hiyo ni kama inawahuisha wote isipokuwa tu hawa wengine

hawakuwa na uwezo wa kumpata *advocate* kwamba hata hawa wakienda mahakamani watalipwa sawa na kama ambavyo wenzao wamelipwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi la nyongeza, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tafadhali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngalawa kwamba majibu ya Naibu Waziri katika swali lake la msingi amesema msingi wa malipo yale na hawawezi wakalipa kwa madai ambayo hayajathibitishwa kisheria. Natambua pia kwamba hawa wafanyakazi wamemuomba Waziri wa Katiba na Sheria kusudi wapate fursa ya kufungua mashauri. Kama wanataka kufanya ambavyo wenzao walifanya basi wafungue kesi, lakini Serikali haiwezi kulipa tu madai ambayo hayajathibitishwa kisheria.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata la Wizara ya Katiba na Sheria la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha.

Na. 14

**Mpango wa Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo/Wilaya Nchini**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Katika bajeti ya 2016/2017 Serikali ilipanga kujenga baadhi ya Mahakama za Wilaya na za Mwanzo katika maeneo mbalimbali nchini.

(a) Je, ni hatua ipi imefikiwa katika ujenzi wa Mahakama hizo?

(b) Kwa kuwa Mahakama ya Mwanzo Mtowisa katika Wilaya ya Sumbawanga Vijijini ni mionganoni mwa Mahakama iliyopangiwa bajeti ya ujenzi kutokana na uchakavu mkubwa na hatarishi kwa wananchi, je, ni lini ujenzi utaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU - KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijilibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mahakama imepanga kujenga na kukarabati majengo yake katika maeneo mbalimbali nchini. Mahakama imejewekea mpango wa kujenga na kukarabati majengo hayo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Utekelezaji wa mpango huu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mahakama imepanga kujenga Mahakama Kuu Kigoma na Mara na kufanya ukarabati mkubwa wa Jengo la Mahakama Kuu Sumbawanga. Aidha, kwa upande wa Mahakama za Hakimu Mkazi, kipaumbele kimetolewa katika Mikoa ya Simiyu, Njombe, Katavi, Manyara, Lindi na Geita.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imepanga kujenga Mahakama za Wilaya na za Mwanzo katika maeneo mbalimbali nchini. Mahakama ya Mwanzo Mtowisa ni moja ya maeneo yaliyopangwa kujengwa na ujenzi utaanza mara moja baada ya upatikanaji wa fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Mahakama wa kujenga majengo kwenye Mikoa mbalimbali, kikwazo kimekuwa ni upatikanaji wa viwanja pamoja na hati miliki za viwanja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malocha swali la nyongeza kama lipo.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Mahakama ya Mwanzo Mtowisa ni mahakama iliyojengwa toka enzi za

mkoloni na kutokana na hali hiyo imechakaa na inahatarisha maisha ya wananchi. Ndiyo maana Serikali katika bajeti ya mwaka 2015/2016 ni mionganini mwa mahakama iliyopangwa kujengwa upya. Je, Serikali haionti umuhimu wa kuipa kipaumbele cha pekee kunusuru hali inayoweza kutokea kwa wananchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa vile vikwazo uliviyovieleza vyta upatikanaji wa kiwanja na hati miliki vyote vilishakamilika na uongozi wa Mahakama ya Wilaya ya Sumbawanga ulishathibitisha. Je, ni lini sasa Mahakama hiyo itaanza kujengwa? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi la ujenzi wa Mahakama ya Mtowisa, lini itaanza kujengwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU - KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi kwamba katika mipango ambayo Wizara tumejiwekeea ni kuhakikisha tunatimiza ukarabati wa ujenzi wa Mahakama kadri ya upatikanaji wa fedha za maendeleo. Hivyo kwa sababu katika mwaka huu wa 2017/2018, Mahakama ya Mwanzo Mtowisa ni kati ya Mahakama za Mwanzo ambazo zimewekwa katika mkakati huu, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi fedha zitakapopatikana jambo hili litatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa sasa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ardhi na Baraza la Ujenzi la Taifa, baada ya utafiti kufanyika kuititia teknolojia mpya ya ujenzi wa Mahakama kuititia Moladi ambapo imeokoa takribani asilimia 50 ya gharama za kawaida naamini kabisa fedha hizi zikipatikana Mahakama ya Mwanzo wa Mtowisa na yenewe itaguswa pia.

**SPIKA:** Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Wakati wa maswali sasa umeisha, tunaendelea na shughuli nyingine.

Kwanza nitambulisse wageni, kipekee tunae Mama Tunu Pinda, karibu sana mama yetu, karibu sana mjengoni kwa mara nyingine tena. Mama Tunu Pinda ni mgeni wa Mheshimiwa Mbunge Janeth Maurice Massaburi pamoja na wageni wengine hamsini ambao wamekuja kushuhudia kuapishwa kwake. Wageni wa Mama Massaburi naomba msimame, ahsanteni sana sana na karibuni sana hapa Dodoma. Mheshimiwa Massaburi tumeshampokea, tulishakuwa naye, kwa hiyo, ye ye ni mzoefu hapa mjengoni. (*Makof*)

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Nchimbi. Wanamaombi karibuni sana, msisahau kutuombea. (*Makof*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Zacharia Issaay ambaye ni Mwenyekiti Mstaafu wa Halmashauri ya Mbulu, Ndugu Herman Inna kutoka kule Mbulu. Karibu sana Ndugu Herman. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, napenda kumtambulisha kipekee mchezaji wetu wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Anna Gidarya sijui anakaa wapi, naomba usimame. Mheshimiwa Anna Gidarya katika uchaguzi uliopita wa CHANETA-Taifa amechanguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti Taifa, CHANETA. Ahsante sana, hongera sana, natumaini pia mchezo wa *netball* ndani ya *Bunge Sports Club* utaimarika zaidi kuititia nafasi yako. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho, niwatangazie kwamba Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) wataendesha zoezi la upimaji wa afya kwa Waheshimiwa Wabunge katika kipindi chote cha Mkutano huu wa Bunge la Kumi na Moja. Zoezi linaanza leo hadi mwisho wa Mkutano huu katika kituo chetu cha afya, wataalam kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili

wakishirikiana na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (*The Jakaya Kikwete Cardiac Institute*) watakuwepo. Zoezi linalenga uchunguzi wa magonjwa ya moyo na macho. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote mtumie fursa hii kuweza kufanya vipimo na uchunguzi wa afya zenu na huduma hiyo ni bure. Kwa hiyo, tunaombwa tupite pale kituoni siku yoyote kati ya leo na mwisho wa Mkutano huu lakini kuwahi ni muhimu

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Haya Katibu niandikie majina. Tunaendelea na miongozo, tunaanza na Mheshimiwa Mwambalaswa

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nimesimama kwa Kanuni ya 47.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya imegawanyika zimekuwa Wilaya mbili (Wilaya ya Songwe na Wilaya ya Chunya), sasa hivi nchi nzima kuna *operationya* kuwaondoa watu kwenye hifadhi hasa za misitu. Kwa hiyo, Wilaya ya Chunya na Songwe ambazo zina misitu mingi sana zinafanya *operation* hizo Wakuu wa Wilaya wakiongoza .

Mheshimiwa Spika, katika *operation* hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya bila kujua ali-*trespass* kwenye Wilaya ya Songwe eneo la Ngwala akawaondoa watu kwenye hifadhi. Kitendo hicho kilimuudhi sana Mkuu wa Wilaya ya Songwe akaamua kulipa kisasi kwa kuingia ndani ya Wilaya ya Chunya akiwa na askari, akanyang'anya ng'ombe 90 za wafugaji na akawapeleka kwenye Wilaya yake ya Songwe.

Mheshimiwa Spika, kKesho yake Mkuu wa Wilaya hiyo akaandamana na Meneja wa Kanda wa *TFS* kuja Chunya bila kuzijulisha mamlaka na Halmashauri ya Chunya wakaenda sehemu hiyo walikonyang'anya ng'ombe, wakachoma *crusher* nne za wachimbaji wadogo wadogo

na *crusher* moja ni karibu shilingi milioni 15, wakabeba na makinikia ya wachimbaji wadogo wadogo sijui wameyapeleka wapi.

Mheshimiwa Spika, siku inayofuata, huyu Meneja wa *TFS* wa Kanda, Mheshimiwa Maghembe alipokuwa Waziri wa Maliasili nimemlalamikia sana, akaingia tena kwenye Wilaya ya Chunya bila kuhusisha mamlaka wala Halmashauri akaleta askari kutoka Wilaya ya Songwe kulinda sehemu hiyo. Sasa wananchi wa sehemu hiyo walitaka kuchukua sheria mkononi, tumefanya *effort* kubwa sana kuwapooza. Sasa hivi ng'ombe hao wengine wameanza kufa, karibu ng'ombe sita wamekufa.

Mheshimiwa Spika, sasa hii tabia ya viongozi wa Serikali kutunishiana misuli imenikera sana. Naomba Bunge lako liahirishe shughuli zake tuweze kujadili Jambo hili ambalo linahatarisha usalama katika Wilaya ya Chunya na Songwe.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwambalaswa, bahati mbaya hukutoa hoja, kwa hiyo, Serikali imesikia.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jenista maelezo kuhusu jambo hilo, tafadhalli.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, Serikali tumelisikia jambo hili na linavyoonekana ni jambo mtambuka linakwenda katika Wizara kadhaa na sisi kama Serikali ni lazima tujiridhishe kwanza mawanda ya jambo lenyewe kabla hatujasema chochote mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tutalichukua na tutakwenda kulifuatilia kwa taratibu za kiserikali ambazo tumekuwa tukizitumia na Mheshimiwa Mbunge aendeelee kuwasiliana na Mawaziri ambao wako ndani ya mawanda aliyooyazungumza ili tuweze kujua nini cha kufanya. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ulivyo sikiia hilo tunakuachieni, ma-*DC* wamefika mahali wanapambana wao kwa wao sasa. Imeshavuka kote huko imekuwa wao kwa wao sasa. Kwa hiyo, hili jambo lisipoangaliwa, ningeomba sana Mheshimiwa Mwambalaswa apewe ushirikiano kwa sababu linaathiri sana wananchi na tumesikia mpaka ng'ombe wanakufa hovyo kwa ubabe, kwa hiyo liangaliwe kidogo. Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwamba udahili wa wanafunzi wa vyuo vikuu umeongezeka sana, wanaomaliza kidato cha sita kwenda vyuo vikuu wamekuwa wengi. Hata hivyo, wanafunzi wengi wallodahilliwa kuingla vyuo vikuu wengine wamekosa nafasi pamoja na kwamba bado wana sifa, sasa hapo ni mwongozo wangu wa kwanza kwamba nitakuja na mwongozo.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ni kwamba katika wale waliopata nafasi za kuingia vyuo vikuu wengine wanastahili kupata mkopo, lakini wengi pia hawakupata mkopo pamoja na kwamba asilimia kubwa ya kupewa mkopo imeongezeka.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, pamoja na kwamba kuna wanafunzi ambao wamepata mkopo wale wanaostahili ambao ni wengi sana bado kuna tatizo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais alishalitolea maelekezo kwamba wanafunzi hawa waliopata mkopo wanapofika vyuoni wasisumbuliwe, wapokelewe ili waweze kuanza masomo yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa wanafunzi hawa wakifika vyuoni, wanafunzi wa maskini, wanafunzi yatima bado wanakutwa na tatizo la kwamba waweze kulipa fedha ya kusajiliwa pale chuoni. Tatizo hili limekuwa ni kubwa, wanafunzi wengi wako nje na sisi

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Wabunge tumeombwa sana na wanafunzi hawa ili tuwalipie fedha za kusajiliwa waweze kuwa wanafunzi pamoja na kwamba wana mkopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa katika mambo haya matatu, naomba mwongozo wako ili Serikali iseme ni kitu gani inaweza ikafanya kuondoa tatizo hili. Ahsante.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu Mwongozo huo wa Mheshimiwa Martha Mlata, jambo hili ni *serious* kabisa wala siyo wa mwaka wa kwanza peke yake na wa miaka mingine, wawe wa mwaka wa pili, mwaka wa tatu, yaani mtu ana mkopo anatakiwa akifika chuoni alipe kwanza fedha za kuwa-*registered*pale chuo halafu akishasajiliwa na chuo ndiyo sasa apate ile haki yake ya mkopo. Watoto hawa ni wa maskini wanazagaa nchi nzima ni matatizo makubwa.

Kwa hiyo, tunaomba kesho baada tu ya kipindi cha Maswali Serikali itoe tamko au taarifa kamili kuhusu nini kinachoendelea kuhusu jambo hili ambapo mtu ana haki yake hapewi mpaka pawe na utaratibu ambao unataka tena hela na ndiyo maana alipata mkopo kwa sababu hana kitu halafu tena anatakiwa atoe hela ili apate haki yake. Kwa hiyo, kesho Serikali ituambie lipi ni lipi katika jambo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Kunchela.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama kwa Kanuani ya 68(7) sambamba na Kanuni ya 46(1).

Mheshimiwa Spika, katika swali langu la msingi linalohusiana na masuala ya bomoabomoa inalolikumba Taifa kwa sasa, Mheshimiwa Waziri hakunijibu kikamilifu kwa sababu swali langu lililenga namna gani Serikali itawalipa fidia wahanga wa bomoabomoa lakini ni kwa nini kauli ya Rais aliyoitamka tarehe 30/10/2017 kwamba wakazi wa

Mwanza wasibomolewe na ilhali wananchi wa Mwanza pia wapo waliopo katika hizo mita za reli ambao wanapaswa kubomolewa.

Mheshimiwa Spika, sasa nilitaka kufahamu na kupata majibu ya Serikali ya uhakika kwamba kauli hii ya kubomolewa inalenga watu wa Mwanza peke yake au pia watu wa Katavi na maeneo mengi yanayokumbwa na bomoabomoa katika Taifa hili? Nilitaka nipate majibu ya Waziri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda wote tulikuwepo tatizo mnaongeaongea mno huko, hamuwasikilizi Mawaziri wanapojobu...

**WABUNGE FULANI:** Aha, aha.

**SPIKA:** Usibishe, Waziri amejibu hivi, kauli ya Rais haihusu eneo la reli, aliyoko ndani ya eneo la reli Tanzania nzima atabomolewa ndivyo alivyojibu hapa, kama uko ndani ya eneo kwa sheria ile ya wakati ule reli ilipoanza 1900 utabomolewa, hilo kasema hapa.

Aidha, kasema endapo kutakuwa na watu ambao wako katika eneo la reli lakini reli imewakuta watalipwa, kasema hayo yote mawili. Sasa kwa majibu hayo ni jibu lipi ambalo halijajibowi la kumtaka tena Waziri aanze kujibu upya hapa? Kwa hiyo, majibu yametolewa, tuwe tunasikilizana tu vizuri, wakati mwingine unapouliza unakuwa kidogo una-expect majibu fulani halafu hukuyapata basi inakupa tabu. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, miongozo hiyo mitatu inatosha kwa leo, tunaendelea na shughuli nyingine. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Najma Giga ili aweze kuendelea na shughuli zingine za leo.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu tuendeleee.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa lengo la Kuondoa Upungufu ambao umebainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hiyo (*A Bill for an Act to Amend The Drug Control and Enforcement Act in order to Keep the Law updated with challenges observed in its implementation.*)

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huo sasa utapelekwa kwenye Kamati husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Katibu tuendelee.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**MWENYEKITI:** Hoja za Serikali, Waziri wa Fedha na Mipango, karibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya. Aidha, tunamshukuru sana kwa kuendelea kulijalia Taifa letu amani na utulivu na kutuwezesha kukutana katika

Mkutano huu wa Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango kufuatia mabadiliko aliyoafanya hivi karibuni katika Baraza lake la Mawaziri, lakini pia safu ya uongozi wa Mikoa.

Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wakuu wa Mikoa waliobakia katika nafasi zao na wale waliobadilishwa vituo vyta kazi. Vilevile nawapongeza kwa dhati wote walioteuliwa kuwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wakuu wa Mikoa wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii adhimu kutambua na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na makini katika kusimamia rasilimali za Taifa, kupambana na rushwa, kuimarisha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma na zaidi ya yote kwa moyo wake adili katika kuzipatia majibu kero za wanyonge. Nina hakika uongozi wake umezidi kuijengea heshima kubwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mbunge aliyeeteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu hivi karibuni kutoka Chama Tawala (CCM). (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawiwa pia kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge wa Kondoa na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Doto Mgosha James kwa ushirikiano wanaonipa katika maandalizi ya hotuba hii na vitabu vyta Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo. Aidha, nawashukuru sana Wizara, Taasisi, Idara za Serikali,

Sekta Binafsi na wadau mbalimbali waliota maoni na michango yao katika kukamilisha Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ninayoiwasilisha hapa imetayarishwa kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji mpana wa jamii. Kwa ujumla tumepeata mawazo na ushauri kutoka makundi mbalimbali na siwezi kuwataja mmoja mmoja wale wote waliochangia hoja hii hadi kufika hapa. Hata hivyo, kwa namna ya kipekee, napenda kuishukuru na kutambua mchango mkubwa wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini katika kuboresha rasimu za Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/2019 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019.

Maoni na ushauri mahsusni wa Kamati ulijikita katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kujumuisha matumizi ya gesi asilia kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na kama malighafi katika viwanda ikiwemo viwanda vya mbolea.

(ii) Kuzingatia maeneo yanayogusa wananchi walio wengi kwa ajili ya kukuza kipato na kupunguza umaskini hususan kilimo, uvuvi, upatikanaji wa pembejeo na mitaji.

(iii) Kuweka msukumo mkubwa katika kuboresha mazingira kwa ajili ya ushiriki wa sekta binafsi katika kugharamia na kutekeleza miradi ya maendeleo inayolenga kutimiza azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu.

(iv) Kuendelea kuboresha mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuibua vyanzo vipyaa.

(v) Kuendelea kulipa madeni yaliyohakikiwa na kuzuia uzalishaji wa madeni mapya.

(vi) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 hadi mwaka 2020/2021 kwa kipindi cha miaka miwili ya awali.

Mheshimiwa Spika, hoja ninayowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu ni hatua ya awali katika mchakato wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha. Madhumuni ya mawasilisho haya ni kuomba maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wakiwa ndio wawakilishi wa sauti za wananchi kuhusu masuala yanayostahili kupewa kipaumbele na msisitizo katika Mpango na Bajeti kwa mwaka ujao. Hivyo, napenda kuahidi kuwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Bajeti na yote yatakayotokana na Bunge lako Tukufu linapokaa sasa kama Kamati ya Mipango tutayazingatia kwa dhati wakati wa kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa yamezingatia llani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2015, Sera na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kisekta, kikanda na kimataifa na maelekezo mengine ya Serikali. Aidha, vyote vimezingatia hali halisi ya mwenendo wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2016 na nusu ya kwanza ya mwaka 2017. Pia vimezingatia mahitaji ya msingi katika kuimarisha kasi ya utekelezaji wa Mpango na kujenga mazingira yatakayowezesha kufikiwa kwa azma ya Taifa ya kujenga uchumi wa viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ninayoiwasilisha ina vitabu viwili, kitabu cha kwanza kinahusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/2019 na kitabu cha pili kinawasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019. Vitabu vyote viwili vinapaswa kusomwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kueleza kwa ufupi mapitio ya viashiria vyta uchumi kwa nusu ya kwanza

ya mwaka 2017. Viashiria vya mwenendo wa uchumi kwa ujumla wake vinaonesha kuwa uchumi wa Taifa ni imara. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017, uchumi wa Taifa ulikua kwa asilimia 6.8, ukichangiwa zaidi na kuimarika kwa sekta za mawasiliano, usafirishaji na ujenzi. Ukuaji wa sekta ya kilimo uliongezeka kutoka wastani wa asilimia 2.7 nusu ya kwanza ya mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 3.1 nusu ya kwanza ya mwaka 2017 kutokana na hali nzuri ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mfumuko wa bei bado umeendelea kubakia katika wigo wa tarakimu moja kutokana na kuongezeka kwa ugavi wa chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani, kutoyumba kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia pamoja na utekelezaji wa sera za bajeti za kupunguza matumizi yasiyo na tija. Mfumuko wa bei mwezi Julai ulikuwa asilimia 5.2, Agosti asilimia 5.0 na Septemba asilimia 5.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 5 hadi 8 kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani kwa ujumla mwenendo uliendelea kuwa imara katika kipindi chote cha mwaka 2016/2017 na robo ya kwanza ya 2017/2018. Thamani ya shilingi ya Tanzania ilibadilika kutoka shilingi 2,177.26 kwa dola moja ya Marekani mwezi Januari, 2016 hadi shilingi 2,221.96 mwezi Januari, 2017. Kasi ya shilingi kupungua thamani iliongezeka na kudumu kwa muda mfupi mwezi Januari 2017 hali iliyosababishwa na Benki Kuu ya Marekani kupandisha riba yake na hivyo kuongeza mahitaji ya dola ya Marekani duniani kwa ajili ya kuwekeza. Aidha, baada ya mwezi Januari, 2017 thamani ya shilingi iliendelea kuwa tulivu na kufikia shilingi 2,237.78 mwezi Oktoba, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Deni la Taifa liliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 26,115.2 mwezi Juni 2017, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 17.0, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 22,320.76 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ongezeko hilo lilichangiwa na mikopo mipya iliyochukuliwa kugharamia miradi ya

maendeleo na hususani mradi wetu wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* lakini pia mradi wa *Strategic Cities* na mradi wa Usafirishaji Dar es Salaam (*DART*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017 tumetoa maelezo wa kirefu katika aya ya 17, 18, 19, 20, mpaka aya ya 21 ya hotuba yangu na naomba yote ipokelewe kwenye rekodi Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Kwa kifupi mapato yaliyopatikana yalikuwa shilingi trilioni 23.6 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi trilioni 29.5 na jumla ya hizo shilingi trilioni 23.6 zote zilitolewa ikiwa ni asilimia 80 ya makadirio ya mwaka 2016/2017. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 17.1 zilitumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 96.7 ya lengo na shilingi trilioni 6.4 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 55.0 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali napenda kuwapongeza Watanzania walioitikia wito wa Serikali wa kulipa kodi kwa hiari hususani ongezeko la mwitikio wa kutumia mashine za kieletroniki (*EFD*). Mwaka 2016/2017 tulishuhudia mwitikio na hamasa ya kipekee kwa wananchi kulipa kodi ya majengo. Haya kwa ujumla wake yanaonesha uelewa wa Watanzania kuhusu wajibu wa kulipa kodi ili kuchangia maendeleo yao. Nawaomba Watanzania waendelee na moyo huo wa kizalendo kwa kuwa ni njia pekee ambayo tutaweza kujenga msingi endelevu wa uchumi na ustawi wa jamii na kulinda heshima ya uhuru wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo tumeepata mafanikio mengi ambayo yako katika aya ya 20 na 21 pia tumeeleza hatua za utekelezaji wa baadhi ya miradi ambayo ilitekelezwa na Serikali, lakini pia sekta binafsi. Kwa upande wa miradi ya sekta binafsi na hasa ile ya viwanda pamekuwepo na mwenendo mzuri ambapo viwanda mbalimbali vilianza uzalishaji ikiwa ni pamoja na viwanda vya kuzalisha

vifungashio vya *Global Packaging (T) Ltd.* na *Madoweka Co. Ltd*; viwanda vya kuzalisha bidhaa za ujenzi vya *Goodwil Ceramics Ltd.* na *Waja General Co. Ltd*; viwanda vya kuzalisha vinywaji baridi vya *Saini Food Products Co. Ltd.*; *Sayona Drinks Ltd.* na kiwanda cha kusindika nyama cha *Mitoboto Farmers Co. Ltd.*, viwanda vyote nilivyotaja vipo Mkoa wa Pwani. Aidha, kuna kiwanda cha kusindika nyama cha Paul Kisivani kule Arusha na viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula vya *Jielong Mills Ltd* kilichopo Shinyanga, *Mkongori Oil Mills na Nkupa Oil Mills* vilivyopo Singida, *Super Cooking Oil* kilichopo Mwanza na *Mount Meru Millers* kilichopo Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi mingi ambayo imetekelizwa na Serikali katika Halmashauri kwa upande wa afya lakini pia kwa upande wa utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji, ujenzi wa bwawa hususani Bwawa la Kidunda, uchimbaji wa visima virefu pia mtandao usafirishaji wa maji safi Jijini Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na ujenzi wa matanki saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 13 tunaeleza utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika robo ya kwanza ya mwaka 2017/2018. Niseme tu kwa kifupi kwa upande wa ujenzi wa bwawa na mitambo ya kuzalisha umeme *Stiegler's Gorge*, Serikali ilitangaza zabuni na amepatikana mkandarasi wa mradi. Kwa upande wa ujenzi wa reli ya katii, kipande cha Dar es Salaam - Morogoro kazi imeendelea, ambapo ujenzi wa kambi za llala, Soga na Ngerengere unaendelea na mkandarasi wa ujenzi wa reli hiyo kwa kipande cha kutoka Morogoro - Makutupora amepatikana na mkataba ulisainiwa Septemba, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa shamba la miwa na kiwanda cha sukari cha Mkulazi, ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometra saba kwa kiwango cha changarawe umekamilika pia yalinunuliwa matrektta takribani matatu na kukamilisha usafishaji wa shamba kubwa lenye (ekari 1000) ambapo ekari 320 tayari zimepandwa miwa. Pia kazi ya ujenzi wa majengo ya kiwanda cha sukari hivi sasa unaendelea. Pia zimezinduliwa meli mbili za mizigo katika

Ziwa Nyasa na ujenzi wa kivuko kikubwa kati ya Kigongo na Busisi unaendelea. Tumeendelea na kazi ya kujenga *flyovers* pale Ubungo, lakini pia TAZARA na barabara ya KIA – Mererani kilometra 26 imekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uwezeshaji wa sekta binafsi, naomba kutambua mchango wa sekta binafsi kwa kuiunga mkono Serikali katika juhudzi za kuendeleza viwanda na hivyo kuinua maisha ya Watanzania. Katika mwaka 2016/2017, Kituo cha Taifa cha Uwekezaji ilisajili miradi 345 na kati ya hiyo, miradi 103 ni ya wawekezaji wa ndani, 137 ya wageni na 105 ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wageni. Thamani ya miradi iliyosajiliwa katika mwaka 2016 ilikuwa ni dola za Marekani bilioni 5.92. Mgawanyiko wa miradi kisekta unaonesha kuwa sekta ya nishati ilisajili miradi yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 2.46; majengo na biashara bilioni 1.13; uzalishaji viwandani bilioni 0.62; kilimo bilioni 0.5; usafirishaji mizigo bilioni 0.38; mawasiliano bilioni 0.28; maliasili bilioni 0.26 na bilioni 0.29 katika sekta zingine.

Aidha, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa kuvutia wawekezaji wengi ambapo mwaka 2016 ilisajili miradi 178 ikifuaatiwa na majengo ya biashara iliyosajili miradi 48, utalii miradi 33 na kilimo miradi 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palikuwepo changamoto katika utekelezaji wa mpango na bajeti na vilevile Serikali ilichukua hatua kukabiliana nazo. Kwa upande wa changamoto zilizokuwa kubwa ni uvujaji wa mapato ya Serikali, udhaifu katika ukusanyaji wa mapato, lakini pia kutokupatikana kwa wakati kwa mikopo yenye masharti nafuu na ile ya kibashara. Serikali ilichukua hatua mbalimbali ambazo tumeziorodhesha katika aya ya 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nieleze shabaha na malengo ya uchumi jumla yanayopendekezwa kipindi cha muda wa kati kuanzia mwaka kesho (2018/2019 – 2020/2021). Shabaha na malengo uchumi jumla itakuwa kama ifuatavyo:-

- (i) Ukuaji wa Pato halisi la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 7.0 mwaka 2017;
  - (ii) Kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei kutoka wastani wa asilimia 5.3 Juni 2017 hadi asilimia tano ifikapo Juni 2018;
  - (iii) Mapato ya kodi yafikie asilimia 14.2 ya Pato la Taifa mwaka 2018/2019 sawa na ilivyokuwa mwaka 2017/2018;
  - (iv) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 24.5 ya Pato la Taifa mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na asilimia 26.2 mwaka 2017/2018;
  - (v) Kupunguza nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada kutoka asilimia 3.8 mwaka 2017/2018 hadi asilimia 2.5 mwaka 2018/2019; na
  - (vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.
- Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi ya Mpango na Bajeti (*assumptions*) ni kama ifuatavyo:-
- (i) Kuendelea kuimarishwa na kudumishwa kwa amani, usalama, utulivu na umaja nchini na katika nchi jirani;
  - (ii) Kuimarika kwa viashiria vyta uchumi jumla na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama vile Pato la Taifa, ukusanyaji wa mapato ya ndani na mfumuko wa bei;
  - (iii) Kuendelea kuimarika na kutengemaa kwa uchumi wa dunia;
  - (iv) Kuendelea kuwa na utulivu wa bei za mafuta katika soko la dunia; na
  - (v) Kuwa na hali ya hewa nzuri ndani ya nchi na katika nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoteo ya awali ya ukomo wa bajeti 2018/2019; kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na sera za bajeti ambazo nimezieleza, maoteo ya awali yanaonesha kuwa jumla ya shilingi trillioni 32.4 zinatarajiwa kukusanya na kutumika katika kipindi hicho. Maoteo haya yatathibitishwa baada ya kufanya uchambuzi wa mwenendo wa utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017/2018. Mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trillioni 22.08, sawa na asilimia 68 ya mahitaji yote. Kati ya hayo, maoteo ya mapato ya kodi yatakuwa shilingi trillioni 18.8 sawa na asilimia 85.2 ya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mapato yasiyo ya kodi yatakuwa shilingi trillioni 2.4 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri yatakuwa shilingi bilioni 847.7. Serikali inategemea kukopa kiasi cha dola za Marekani millioni 600 sawa na shilingi trillioni 1.3 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibashara na shilingi trillioni 4.0 ni mikopo ya ndani kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zilizoiva.

Aidha, shilingi trillioni 1.3 sawa na asilimia moja ya Pato la Taifa, itakuwa ni mikopo mipya ya ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Katika maoteo hayo, washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia Shilingi trillioni 3.6 ambapo shilingi billioni 946 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, shilingi trillioni 2.1 ni misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi billioni 558.9 ni misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trillioni 32.4 ambapo matumizi ya kawaida yatakuwa shilingi trillioni 20.2 na maendeleo itakuwa shilingi trillioni 12.2. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi trillioni 7.6 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi za Umma na shilingi trillioni 9.7 ni kwa ajili ya deni la Taifa. Aidha, kwa upande wa matumizi ya maendeleo kiasi cha shilingi trillioni 9.5 au asilimia 76.6 ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 ni mwongozo katika uandaaji wa miradi na programu za maendeleo itakayojumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka kesho na kitabu cha bajeti ya maendeleo 2018/2019 nitakayowasilisha mwezi Juni hapa Bungeni. Hivyo, ni matarajio ya Serikali kuwa Waheshimiwa Wabunge watatumia fursa hii kutoa maoni yao yatakayojumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka kesho utakuwa wa ni wa tatu katika mwendelezo wa kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mapendekezo haya yamezingatia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, hasa kuendeleza kasi ya ukuaji wa uchumi; kuimarisha kasi ya utekelezaji wa Mpango hasa kwa kutanzua changamoto za upatikanaji wa fedha na mitaji; upatikanaji wa ardhi na maeneo ya uwekezaji na kuimarisha mipango miji na maendeleo ya makazi; kuongeza uzalishaji wa bidhaa za viwandani; kuongeza uwezo wa kupambana na umaskini; kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii kwa kutoa huduma bora za afya, elimu, maji na kinga kwa jamii; kuongeza matumizi ya teknolojia, ubunifu, ujuzi na utoshelevu wa mahitaji ya rasilimali watu yenye weledi unaohitajika kwa ustawi wa uchumi wa viwanda na pia kuhakikisha usalama wa chakula na mahitaji ya lishe bora nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nieleze vipaumbele vya Mpango na miradi itakayopewa msukumo wa kipekee katika mwaka ujao wa fedha. Vipaumbele vya mwaka ujao wa fedha vitazingatia maeneo manne ya kipaumbele ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano. Aidha, katika maeneo hayo yamejumuishwa miradi ya kielelezo ambayo utekelezaji wake utapewa msukumo wa kipekee kama ifuatavyo:-

(i) Kwa upande wa viwanda vya kukuza uchumi wa ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, lengo ni kuendelea

kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini na hususan za kilimo, madini na gesi asilia. Katika eneo hili, miradi itakayopewa msukumo wa kipekee ni pamoja na mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma; Kiwanda cha Kufua Chuma cha Liganga; Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi; ujenzi wa mtambo wa kusindika gesi kimiminika; uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi na Kituo cha Viwanda Kurasini.

Aidha, Serikali itaendelea kupanua na kuimarisha shughuli za Shirika la Viwanda Vidogo (*SIDO*) ili kulifanya kuwa chombo cha kuleta mageuzi ya viwanda nchini; (*Makofi*)

(ii) Kwa eneo la kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu; eneo hili linalenga kuendeleza mafanikio ya ustawi wa maisha ya Watanzania na hasa wa vijijini. Msukumo utakuwa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya na hususan huduma za kibingwa, elimu na ujuzi, huduma za ustawi wa jamii; upatikanaji wa uhakika wa chakula na lishe bora; na kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama vijijini na mijini;

(iii) Ujenzi wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na

(iv) Kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 37 mpaka 41 tumeelekeza maelekezo mahsus kwa ajili ya uandaaji wa mipango na bajeti kwa mwaka 2018/2019 na maelekezo hayo yanahusu ukusanyaji wa mapato ya ndani. Eneo la pili ni kudhibiti matumizi na kupunguza gharama. Eneo la tatu ni kulipa na kuzuia ongezeko la madeni ya Serikali, lakini pia yako maelekezo mengine ambayo yako katika aya ya 41.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwa kusema kwamba Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma zinaelekezwa kuzingatia Mwongozo katika kuandaa mipango na bajeti zao lakini pia

zinaelekeza kuzingatia maeneo ya kipaumbele ambayo nimemaliza kuyaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau na wananchi wote kwa juhudini wanazoendelea kufanya katika utekelezaji wa mipango na bajeti na natoa rai kwa sekta binafsi na wananchi wote kuendelea kuunga mkono juhudini za Serikali na hasa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuwekeza na kutekeleza wajibu wao wa msingi wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii pamoja na vitabu vya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka ujao wa fedha na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa vitapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili, litoe maoni na kuishauri Serikali kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO,  
MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO (MB), AKIWASILISHA  
BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA  
TAIFA KWA MWAKA 2018/19 NA MWONGOZO WA  
MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA  
MWAKA 2018/19 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## **UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya. Aidha, tunamshukuru sana kwa kuendelea kulijalia Taifa letu amani na utulivu na kutuwezesha kukutana katika mukutano huu wa tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.
3. **Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango kufuatia mabadiliko aliyoafanya hivi karibuni katika Baraza lake la Mawaziri na safu ya uongozi wa Mikoa. Aidha, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wakuu wa Mikoa waliobakia katika nafsi zao na wale waliobadilishwa vituo vya kazi. Vile vile, ninawapongeza kwa dhati wote walioteuliwa kuwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wakuu wa Mikoa wapya.
4. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitumie fursa hii adhimu kutambua na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri na makini katika kusimamia rasilimali za Taifa, kupambana na rushwa, kuimarisha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma na zaidi ya yote, kwa moyo wake adili katika kupatia majibu kero za wanyonge. Hakika uongozi wake umezidi kuijengea heshima kubwa nchi yetu.
5. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Janeth Masaburi (Mb) aliyeoteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu hivi karibuni kutoka Chama Tawala cha CCM. Aidha, nawapongeza kwa pamoja Waheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Kiza Hussein Mayeye, Nuru Awadh Bafadhili, Rukia Ahmed Kassim, Shamsia Aziz Mtamba, Sonia Jumaa Magogo, Rehema Juma Migilla na Zainab Mndolwa Amir walioteuliwa na Chama cha Wananchi - CUF kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninapenda

kuwakaribisha na kuwashauri watumie jukwaa hili kikamilifu katika kuishauri Serikali na kuwatumikia wananchi. Napenda pia kumpongeza Bw. Stephen Kagaigai kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**6. Mheshimiwa Spika**, ninawiwa pia kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb) na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bw. Doto Mgosa James kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya hotuba hii na vitabu vyta Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo. Aidha, ninawashukuru sana Wizara, Taasisi, Idara za Serikali, Sekta Binafsi na wadau mbalimbali waliotoa maoni na michango yao katika kukamilisha Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo.

**7. Mheshimiwa Spika**, hoja ninayoiwasilisha hapa imetayarishwa kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji mpana wa jamii. Kwa ujumla tumeposta maoni na ushauri kutoka katika makundi mbalimbali ya jamii na Taasisi za Serikali. Siwezi kuwataja mmoja mmoja wale wote waliochangia hoja hii hadi kufikia hapa. Hata hivyo, kwa namna ya kipekee, napenda kuishukuru na kutambua mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini katika kuboresha rasimu za Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19. Maoni na ushauri mahsuswa Kamati ulijikita katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

(i) Kujumuisha matumizi ya gesi asilia kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na kama malighafi katika viwanda ikiwemo viwanda vyta mbolea;

(ii) Kuzingatia maeneo yanayogusa wananchi walio wengi kwa ajili ya kukuza kipato na kupunguza umaskini hususan kilimo, uvuvi, upatikanaji wa pembejeo na mitaji;

- (iii) Kuweka msukumo mkubwa katika kuboresha mazingira kwa ajili ya ushiriki wa Sekta Binafsi katika kugharamia na kutekeleza miradi ya maendeleo inayolenga kutimiza azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu;
- (iv) Kuendelea kuboresha mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuibua vyanzo vipyta;
- (v) Kuendelea kulipa madeni yaliyohakikiwa na kuzuia uzalishaji wa madeni mapya; na
- (vi) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) kwa kipindi cha miaka miwili ya awali.

**8. Mheshimiwa Spika**, hoja ninayowasilisha leo mbele ya Bunge lako Tukufu ni hatua ya awali katika mchakato wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/19. Madhumuni ya wasilisho hili ni kuomba maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wakiwa ndiyo wawakilishi wa sauti za wananchi kuhusu masuala yanayostahili kupewa Kipaumbele na msisitizo katika Mpango na Bajeti kwa mwaka ujao. Hivyo, napenda kuahidi kuwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Bajeti na yote yatakayotokana na Bunge lako Tukufu linapokaa sasa kama Kamati ya Mpango tutayazingatia kwa dhati wakati wa kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/19.

**9. Mheshimiwa Spika**, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/19 na Mapendekazo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19 yamezingatia llani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2015; Sera na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kisekta, kikanda na kimataifa; na Maelekezo mengine ya Serikali. Aidha, vyote vimezingatia hali halisi ya mwenendo wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2016 na nusu ya kwanza ya mwaka 2017. Pia, vimezingatia mahitaji ya msingi katika

kuimarisha kasi ya utekelezaji wa Mpango na kujenga mazingira yatakayowezesha kufikiwa kwa azma ya Taifa ya kujenga uchumi wa viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

**10. Mheshimiwa Spika**, hoja ninayoiwasilisha ina vitabu viwili. Kitabu cha kwanza kinahusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19. Kitabu cha pili kinawasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19. Vitabu vyote viwili vinapaswa kusomwa kwa pamoja.

#### **MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/19**

**11. Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kuwasilisha Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19. Mwongozo huu unaainisha maelekezo mahsus yanayopaswa kuzingatiwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19.

**12. Mheshimiwa Spika**, lengo la Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19 ni kuwaelekeza Maafisa Masuuli kuhusu maeneo ya kipaumbele na masuala mahsus yanayopaswa kupewa msukumo wa kipekee katika uandaaji wa mipango na bajeti za mafungu husika. Maelekezo haya yanatokana na Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni zake; maboresho yaliyofanyika katika mifumo ya kibajeti, ukusanyaji wa mapato, usimamizi na udhibiti wa matumizi; usimamizi wa mashirika na taasisi za umma; na usimamizi wa madeni ya Serikali. Mwongozo pia umeainisha mfumo wa bajeti ya mwaka 2018/19, ikiwa ni pamoja na mapendekezo ya awali ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/19 na mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji.

## **Mapitio ya Viashiria vya Uchumi kwa Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2017**

**13.** **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuwasilisha vipengele muhimu vya Mwongozo, naomba nianze kueleza kwa kifupi mapitio ya viashiria vya uchumi kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017 na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/17.

**14.** **Mheshimiwa Spika**, viashiria vya mwenendo wa uchumi kwa ujumla wake vinaonesha kuwa uchumi wa Taifa ni imara. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017, **Uchumi wa Taifa** ulikua kwa asilimia 6.8, ukichangiwa zaidi na kuimarika kwa sekta za mawasiliano, usafirishaji na ujenzi. Ukuaji wa sekta ya kilimo uliongezeka kutoka wastani wa asilimia 2.7 nusu ya kwanza ya mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 3.1 nusu ya kwanza ya mwaka 2017 kutokana na hali nzuri ya hewa.

**15.** **Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa Bei** bado umeendelea kubakia katika wigo wa tarakimu moja kutokana na kuongezeka kwa ugavi wa chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani; kutoyumba kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia; na utekelezaji wa sera za bajeti za kupunguza matumizi yasiyo na tija. Mfumuko wa bei mwezi Julai ulikuwa asilimia 5.2, Agosti asilimia 5.0 na Septemba asilimia 5.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 5 hadi 8 kwa kipindi husika. Mwenendo wa **Thamani ya Shilingi** ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ultiendelea kuwa imara katika kipindi chote cha mwaka 2016/17 narobo ya kwanza ya 2017/18. Thamani ya shilingi ya Tanzania imebadilika kutoka shilingi 2,177.26 kwa dola moja ya Marekani mwezi Januari 2016, hadi shilingi 2,221.96 mwezi Januari 2017. Kasi ya shilingi kupungua thamani iliongezeka na kudumu kwa muda mfupi mwezi Januari 2017 hali iliyo sababishwa na Benki Kuu ya Marekani kupandisha riba yake na hivyo kuongeza mahitaji ya dola ya Marekani duniani kwa ajili ya kuwekeza. Aidha, baada ya mwezi Januari 2017, thamani ya shilingi iliendelea kuwa tulivu na kufikia shilingi 2,237.78 mwezi Oktoba 2017.

**16. Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa** liliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 26,115.2 mwezi Juni 2017, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 17.0, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 22,320.76 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ongezeko hilo lilichangiwa na mikopo mipya iliyochukuliwa ili kugharamia miradi ya maendeleo kama vile: *Standard Gauge Railway; Strategic Cities*; mradi wa usafirishaji Dar es Salaam (DART) na kupanua upatikanaji wa maji safi Dar es Salaam. Deni hili la Taifa linajumuisha deni la Serikali liliolifika dola za Marekani milioni 22,443.70 na deni la sekta binafsi la dola za Marekani milioni 3,671.50. Pamoja na ongezeko hili, viashiria vyote bado vinaonesha kuwa deni la Taifa ni himilivu kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Uwiano kati ya deni na Pato la Taifa umefikia asilimia 31.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 56.

### **Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti 2016/17**

**17. Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitekeleza bajeti kulingana na upatikanaji wa mapato. Mapato yaliyopatikana kutoka vyanzo vyote kwa mwaka 2016/17 yalikuwa Shilingi bilioni 23,634.55, ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi bilioni 29,539.60. Mapato ya ndani yalikuwa Shilingi bilioni 16,639.97, sawa na asilimia 90.2 ya makadirio lakini yakiwa na ongezeko la asilimia 17.7 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2015/16. Aidha, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilifikia Shilingi bilioni 2,474 sawa na asilimia 68.7 ya ahadi. Mikopo ya ndani ilikuwa Shilingi bilioni 4,504.8 sawa na asilimia 83.8 ya lengo la kukopa Shilingi bilioni 5,374.3. Kwa upande wa mikopo ya nje ya kibiashara, Shilingi bilioni 1,226.8 zilipatikana, ikiwa ni asilimia 58.4 ya malengo. Kiasi cha Shilingi bilioni 1,211.0 kati ya mikopo yenye masharti ya kibiashara hakikuweza kutumika kwa mwaka 2016/17 kwa kuwa kilipokelewa mwishoni mwa mwaka. Kiasi hiki cha fedha kitatumika kugharamia miradi ya maendeleo iliyokusudiwa katika mwaka 2017/18.

**18. Mheshimiwa Spika**, jumla ya Shilingi bilioni 23,634.55 zilitolewa, ikiwa ni asilimia 80.0 ya makadirio ya mwaka 2016/17. Kiasi hiki kilikuwa ni zaidi ya matumizi halisi ya mwaka

2015/16 ya Shilingi bilioni 22,099.1 kwa asilimia 6.5. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 17,136.2 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 96.7 ya lengo na Shilingi bilioni 6,498.3, kwa matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 55.0 ya lengo la mwaka.

**19. Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Serikali napenda kuwapongeza Watanzania walioitikia wito wa Serikali wa kulipa kodi kwa hiari hususan ongezeko la mwitikio wa kutumia mashine za kieletroniki (EFD). Mwaka 2016/17 tulishuhudia pia mwitikio na hamasa ya kipekee kwa wananchi kulipa kodi ya majengo. Haya kwa ujumla wake yanaonesha uelewa wa Watanzania kuhusu wajibu wa kulipa kodi ili kuchangia maendeleo yao. Nawaomba Watanzania waendelee na moyo huo wa kizalendo na kuwashimiza wale ambao hawajapata mwamko kuanza kulipa kodi kwa hiari. Ni kwa njia hii pekee ndipo tutaweza kujenga msingi endelevu wa uchumi na ustawi wa jamii na kulinda heshima ya uhuru wetu.

#### **Mapitio ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2016/17**

**20. Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/17 ni pamoja na:- kugharamia ujenzi wa awamu ya kwanza wa reli ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (Shilingi bilioni 1,000.0); ujenzi na ukarabati wa barabara kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara (Shilingi bilioni 807.4); mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu (Shilingi bilioni 495.4); elimumsingi bila malipo (Shilingi bilioni 206.9); upanuzi wa miundombinu ya umeme vijijini (Shilingi bilioni 361.5); uboreshaji wa usafiri wa anga kwa ununuzi wa ndege mpya mbili (Shilingi bilioni 103.4) na malipo ya awali ya ndege mpya nne (Shilingi bilioni 320.1); uwekezaji kwenye miundombinu ya umeme (Shilingi bilioni 176.5); ununuzi wa dawa na vifaa tiba (Shilingi bilioni 165); uwekezaji katika miundombinu ya usambazaji maji mijini na vijijini (Shilingi bilioni 137.4); na upatikanaji wa pembejeo za kilimo (Shilingi bilioni 21).

**21. Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na: kupata mradi mkubwa wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda hadi Chongoleani-Tanga (dola za Marekani bilioni 3.5) ambapo kupitia mradi huu Taifa litanufaika na ajira, utaalamu na fursa za kibashara. Miradi mingine ni pamoja na:- upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam (dola za Marekani milioni 345); ununuzi wa asilimia 35 ya hisa za ZANTEL katika Shirika la Simu Tanzania (TTCL) na hivyo kuiwezesha Serikali kumiliki TTCL kwa asilimia 100 (Shilingi bilioni 14.9); kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na rasilimali za Taifa.

**22. Mheshimiwa Spika**, hatua za utekelezaji wa baadhi ya miradi inayotekelizwa na Serikali na Sekta Binafsi ni kama ifutavyo:

(i) Miradi ya sekta binafsi, hususan, ya viwanda imekuwa na mwenendo mzuri, ambapo viwanda mbalimbali vilianza uzalishaji, ikiwa ni pamoja na viwanda vya kuzalisha vifungashio vya *Global Packaging (T) Ltd* na *Madoweka Co. Ltd*; viwanda vya kuzalisha bidhaa za ujenzi vya *Goodwil Ceramics Ltd* na *Waja General Co. Ltd*; viwanda vya kuzalisha vinywaji baridi vya *Saini Food Products Co. Ltd*; *Sayona Drinks Ltd* na kiwanda cha kusindika nyama cha *Mitoboto Farmers Co. Ltd*. viwanda vyote nilivyotaja vipo mkoa wa Pwani. Aidha, kuna kiwanda cha kusindika nyama cha Paul Kisivani – Arusha; na viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula vya *Jielong Mills Ltd* kilichopo Shinyanga, *Mkongori Oil Mills* na *Nkupa Oil Mills* - vilivyopo Singida, *Super Cooking Oil* - kilichopo Mwanza na *Mount Meru Millers* - kilichopo Mara;

(ii) Miradi mipya 1,160 ya maji katika vijiji 1,206 katika Halmashauri 148; uchimbaji visima 11 mkoani Tabora; upanuzi wa huduma ya maji safi katika manispaa ya Dodoma na Singida;

(iii) Hospitali ya Taifa Muhimbili: kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa vyumba 7 vya upasuaji na kuongeza idadi ya

vyumba kufikia 20 katika jengo kuu la upasuaji; kukamilika kwa ukarabati wa vyumba vinne (4) vya upasuaji katika jengo la watoto pamoja na kuweka mfumo wa hewa *medical gas piping*; kununuliwa kwa mashine 1 ya kisasa ya *CT-Scan*, mashine 14 za upasuaji (*diathermy machines*), mashine 2 kubwa za usafishaji vifaa (*auto clave machines*), vifaa vya usikivu (*cochlear implants*), mashine za kutolea huduma ya kupandikiza vifaa vya usikivu (*audiometer and ABR machine*) na lifti 2 kwa ajili ya majengo ya Kibasila na Sewahaji;

(iv) Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto: kukamilika kwa ukarabati mkubwa na ujenzi wa vituo vya afya 8 vilivyopo Kanda ya Ziwa ambapo hadi sasa vituo 171 vinatoa huduma ya upasuaji wa matatizo yatokanayo na uzazi pingamizi pamoja na upatikanaji wa damu salama; na ununuzi wa magari 67 ya kubebea wagonjwa;

(v) Utunzaji na Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji ambapo mipaka ya vyanzo vya maji kumi (10) imewekwa katika mabonde ya Rufiji; Ruvuma na Pwani ya Kusini; Ziwa Rukwa na Wami/Ruvu;

(vi) Ujenzi wa Bwawa la Kidunda: hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa usanifu wa bwawa na barabara ya Ngerengere – Kidunda (km 76) pamoja na sehemu ya malipo ya fidia kwa wananchi 2,603 waliohamishwa kupisha ujenzi wa bwawa na barabara;

(vii) Mradi wa Uchimbaji wa Visima Virefu Kimbiji na Mpera ambapo visima 15 kati ya 20 vilivyokuwa vimepangwa vimekamilika; na

(viii) Mtando wa Majisafi Jijini Dar es Salaam ambapo shughuli za ujenzi wa matanki saba (7), ulazaji wa mabomba makubwa yenye urefu wa kilometra 69 na madogo ya usambazaji maji kwa urefu wa kilomita 361 umekamilika na kuanza kuunganishiwa maji kwa wateja katika maeneo ya Mbezi, Kiluvya, Tegeta na Bagamoyo.

## **Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Robo ya Kwanza ya Mwaka 2017/18**

**23. Mheshimiwa Spika**, hatua za utekelezaji zilizofikiwa kwa baadhi ya miradi ya maendeleo katika robo ya kwanza ya mwaka 2017/18 ni pamoja na:

- (i) *Ujenzi wa bwawa na mitambo ya kuzalisha umeme - Stiegler's Gorge*: zabuni ilitangazwa ili kumpata mkandarasi wa mradi;
- (ii) *Ujenzi wa Reli ya Kati*: ujenzi wa kipande cha Dar - Morogoro uliendelea, ambapo ujenzi wa kambi za llala, Soga na Ngerengere unaendelea; na mkandarasi wa ujenzi wa reli hiyo kwa kipande cha Morogoro – Makutupora amepatikana, ambapo mkataba ulisainiwa Septemba, 2017;
- (iii) *Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi*: Ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 7 kwa kiwango cha changarawe kutoka barabara kuu ya Dodoma – Morogoro inayoingia katika kiwanda cha kuzalisha sukari cha Mbigiri; kununuliwa kwa matrekti 3; na kukamilika kwa usafishajji wa shamba kubwa (ekari 1000) ambapo ekari 320 zimepandwa miwa. Aidha, ujenzi wa majengo ya kiwanda cha sukari unaendelea;
- (iv) Kuzinduliwa kwa meli mbili (2) za mizigo katika ziwa Nyasa na ujenzi wa kivuko kikubwa kati ya Kigongo na Busisi unaendelea;
- (v) Ujenzi wa barabara zikiwemo *flyovers* unaendelea na barabara ya KIA – Mererani (km 26) imekamilika na kuzinduliwa;
- (vi) Hifadhi ya Mazingira na Vyanzo vya Maji: kuvitambua, kuviwekea mipaka na kuvitangaza vyanzo vya maji 78 kuwa maeneo tengefu;
- (vii) Huduma ya Maji Vijijini: kukamilika kwa ujenzi wa miradi 90 ya maji vijijini na hivyo kufanya jumla ya miradi

iliyokamilika kufikia 1,423; ujenzi wa jumla ya vituo vya maji 117,190;

(viii) Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe: kukamilika kwa asilimia 26.3 ya mradi ikiwemo ujenzi wa chanzo; mtambo wa kusafisha maji; na tanki la kuhifadhi maji;

(ix) Mradi wa Maji kwa Vijiji 100 Vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria, ambapo miradi ya vijiji 14 na upimaji na usanifu wa miradi ya vijiji 32 umekamilika; na

(x) Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi Dar es Salaam: ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 77 umekamilika katika maeneo ya Mbezi na Kiluvya.

#### **Uwekezaji wa Sekta Binafsi**

24. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba kutambua mchango wa Sekta Binafsi kwa kuiunga mkono Serikali katika juhudzi za kuendeleza viwanda na hivyo kuinua maisha ya watanzania. Katika Mwaka 2016, Kituo cha Taifa cha Uwekezaji kilisajili miradi 345 na kati ya hiyo, miradi 103 ni ya wawekezaji wa ndani, 137 ya wageni na 105 ya Ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wageni. Thamani ya miradi iliyosajiliwa mwaka 2016 ilikuwa ni dola za Marekani bilioni 5.92. Mgawanyiko wa miradi kisekta unaonesha kuwa sekta ya nishati ilisajili miradi yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 2.46 majengo na biashara bilioni 1.13; uzalishaji viwandani bilioni 0.62; kilimo bilioni 0.5; usafirishaji mizigo bilioni 0.38; mawasiliano bilioni 0.28; maliasili bilioni 0.26; na bilioni 0.29 katika sekta zingine. Aidha, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa kuvutia wawekezaji wengi ambapo mwaka 2016 ilisajili miradi 178 ikifuatiwa na majengo ya biashara iliyosajili miradi 48; utalii miradi 33 na kilimo miradi 24.

#### **Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti na Hatua za kukabiliana Nazo**

25. **Mheshimiwa Spika**, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na: uvujaji wa mapato; mwamko mdogo wa kulipa

kodi kwa hiari; udhaifu katika ukusanyaji wa mapato kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma; kutopatikana kwa wakati kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiashara kutoka nje; kuongezeka kwa ulimbikizaji wa madai; Wafadhili kupendelea zaidi kufadhili miradi moja kwa moja badala ya utaratibu wa kupitia bajeti ya Serikali unaoiwezesha Serikali kupanga matumizi kulingana na vipaumbele vyake: maandalizi ya miradi mingi kutokuwa kamili kuruhusu hatua za utekelezaji kuanza katika muda uliopangwa; na mwenendo wa kupungua kwa misaada na mikopo nafuu.

**26. Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali inaendelea kuchukua hatua zifuatazo: kuimarisha mifumo na taasisi za ukusanyaji wa mapato; kuimarisha mifumo na taasisi za udhibiti wa mapato na ulinzi wa rasilimali za Taifa; kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kodi; kuendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa walipa kodi kwenye kanzidata ya walipa kodi; kuhuisha mifumo ya kielektroniki ya kumtambua milipa kodi; kuendelea kuboresha makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi hasa yale yanayotokana na michango ya mashirika na wakala za Serikali; kuzitaka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma kutumia mifumo ya kielektroniki katika kukusanya maduhuli; na kutekeleza makubaliano kati Serikali na Washirika wa Maendeleo juu ya mfumo ulioboreshwa wa ushirikiano utakaoanza kutumika mwaka 2018/19. Hatua nyingine ni pamoja na: kuimarisha benki za maendeleo ili zichangie katika upatikanaji wa rasilimali fedha, hususan mikopo ya kibiashara ya muda mrefu; kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara kwa ajili ya kuchochea ushiriki wa Sekta Binafsi; kutoa mafunzo kwa wataalam wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Taasisi za Serikali juu ya uandaaji wa miradi ya maendeleo; kupitia Sheria ya uwekezaji kwa ubia (PPP); na uandaaji wa Mkakati wa Utekelezaji, Ufutiliaji na Tathmini ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

## **SHABAHA NA MALENGO YA UCHUMI JUMLA 2018/19 – 2020/21**

**27.** **Mheshimiwa Spika**, shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha muda wa kati (2018/19 – 2020/21) ni kama ifuatavyo:-

- (i) Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 7.0 mwaka 2017;
- (ii) Kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei kutoka wastani wa asilimia 5.3 Juni 2017 hadi asilimia 5.0 ifikapo Juni 2018;
- (iii) Mapato ya kodi kuwa asilimia 14.2 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 sawa na iliyokuwa mwaka 2017/18;
- (iv) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 24.5 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 ikilinganishwa na asilimia 26.2 mwaka 2017/18;
- (v) Kupunguza nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kutoka asilimia 3.8 mwaka 2017/18 hadi asilimia 2.5 mwaka 2018/19; na
- (vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

### **MISINGI YA MPANGO NA BAJETI (ASSUMPTIONS)**

**28.** **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha muda wa kati (2018/19 – 2020/21), misingi ya mpango na bajeti ni pamoja na:

- (i) Kuendelea kuimarishwa na kudumishwa kwa amani, usalama, utulivu na umoja nchini na nchi jirani;
- (ii) Kuimarika kwa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama vile Pato la Taifa, ukusanyaji wa mapato ya ndani na mfumuko wa bei;

- (iii) Kuendelea kuimarika na kutengemaa kwa uchumi wa dunia;
- (iv) Kuendela kuwa na utulivu wa bei za mafuta katika soko la dunia; na
- (v) Kuwa na hali ya hewa nzuri ndani ya nchi na katika nchi jirani.

### **MAOTEO YA AWALI YA UKOMO WA BAJETI 2018/19**

**29. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na sera za bajeti kwa mwaka 2018/19, maoteo ya awali yanaonesha kuwa jumla ya Shilingi bilioni 32,476 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Maoteo haya yatathibitishwa baada ya kufanya uchambuzi wa mwenendo wa utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017/18. Mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Shilingi bilioni 22,088.2, sawa na asilimia 68 ya mahitaji yote. Kati ya hayo, maoteo ya mapato ya kodi yatakuwa Shilingi bilioni 18,817.0 sawa na asilimia 85.2 ya mapato ya ndani. Vile vile, mapato yasiyo ya kodi yatakuwa Shilingi bilioni 2,423.5 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri yatakuwa Shilingi bilioni 847.7. Serikali inategemea kukopa kiasi cha dola za Marekani milioni 600 sawa na Shilingi bilioni 1,374.0 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibashara na Shilingi bilioni 4,028.6 ni mikopo ya ndani kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva. Aidha, Shilingi bilioni 1,327 sawa na asilimia 1 ya Pato la Taifa, itakuwa ni mikopo mipy ya ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**30. Mheshimiwa Spika**, katika maoteo hayo, Washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia Shilingi bilioni 3,658.2 ambapo Shilingi bilioni 946.0 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, Shilingi bilioni 2,153.3 ni misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi bilioni 558.9 ni misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kisekta.

**31. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi, Serikali itatumia jumla ya Shilingi bilioni 32,476.0 ambapo matumizi ya kawaida ni Shilingi bilioni 20,227.6 na maendeleo ni Shilingi bilioni 12,248.3. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, Shilingi bilioni 7,627.7 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi za Umma na Shilingi bilioni 9,705.2 kwa ajili ya Deni la Taifa. Aidha, kwa upande wa matumizi ya maendeleo kiasi cha Shilingi bilioni 9,536.2 au asilimia 76.6 ni fedha za ndani.

#### **MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2018/19**

**32. Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19 ni mwongozo katika uandaaji wa miradi na programu za maendeleo itakayojumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2018/19 na kitabu cha bajeti ya Maendeleo 2018/19 nitakavyowasilisha mwezi Juni hapa Bungeni. Hivyo, ni matarajio ya Serikali kuwa Waheshimiwa Wabunge watatumia fursa hii kutoa maoni yao yatakayojumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2018/19.

**33. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19 utakuwa wa tatu katika mwendelezo wa kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mapendekezo haya yamezingatia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21, hususan:- (a) Kuendeleza kasi ya ukuaji wa uchumi; (b) Kuimarisha kasi ya utekelezaji wa Mpango, hasa kwa kutanzua changamoto za upatikanaji wa fedha na mitaji, upatikanaji wa ardhi na maeneo ya uwekezaji, na kuimarisha mipango miji na maendeleo ya makazi; (c) Kuongeza uzalishaji wa bidhaa za viwandani; (d) Kuongeza uwezo wa kupambana na umaskini; (e) Kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii kwa kutoa huduma bora za afya, elimu, maji na kinga kwa jamii; (f) Kuongeza matumizi ya teknolojia, ubunifu, ujuzi na utoshelevu wa mahitaji ya rasilimali watu yenye weledi unaohitajika kwa ustawi wa

uchumi wa viwanda; na (g) kuhakikisha usalama wa chakula na mahitaji ya lishe bora nchini.

**Vipaumbele vya Mpango na Miradi Itakayopewa Msukumo wa Kipekee Mwaka 2018/19**

**34. Mheshimiwa Spika**, vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19 vitazingatia maeneo manne ya kipaumbele ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Aidha, maeneo hayo yamejumuisha miradi ya kielelezo ambayo utekelezaji wake utapewa msukumo wa kipekee:-

**(i) Viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda:**

Lengo ni kuendelea kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini, hususan za kilimo, madini na gesi asilia. Katika eneo hili, miradi itakayopewa msukumo wa kipekee ni pamoja na: **Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma; Kiwanda cha Kufua Chuma cha Liganga; Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi; Ujenzi wa mtambo wa kusindika Gesi Kimiminika; uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi; na Kituo cha Viwanda Kurasini.** Aidha, Serikali itaendelea kupanua na kuimarisha shughuli za Shirika la Viwanda Vidogo – SIDO ili kulifanya kuwa chombo cha kuleta mageuzi ya viwanda nchini.

**(ii) Kufungamanisha Uchumi na Maendeleo Watu:**

Eneo hili linalenga kuendeleza mafanikio ya ustawi wa maisha ya watanzania hasa wa vijijini. Msukumo utakuwa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya hususan huduma za kibingwa, elimu na ujuzi, huduma za ustawi wa jamii; upatikanaji wa uhakika wa chakula na lishe bora; kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama vijijini na mijini; kusimamia rasilimali za maji nchini; na kuimarisha usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa

utawala bora ikiwa pamoja na kukamilisha azma ya kuhamishia shughuli za Serikali Kuu Dodoma.

**(iii) Ujenzi wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji:**

Eneo hili linalenga kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu, ikijumuisha miundombinu ya nishati, usafirishaji (reli, barabara, madaraja na bandari), usafiri wa anga (viwanja vya ndege) na usafiri wa majini (meli na vivuko). Miradi itakayopewa msukumo wa kipekee katika eneo hili ni pamoja na: **ujenzi wa bwawa na mitambo ya kufua umeme wa Stiegler's Gorge; ujenzi wa Reli ya Kati; na kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**. Vile vile, Serikali inaendelea kuboresha mfumo wa ugawaji na usimamizi wa ardhi; kuboresha mazingira ya kibashara ili kuvutia uwekezaji na kupanua masoko; na kuendeleza ushirikiano wa kikanda na kimataifa hususan kwa njia ya diplomasia ya kiuchumi.

**(iv) Kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Mpango:** hatua zinazopendekezwa zinalenga kuboresha ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa Mpango, ikiwa ni pamoja na: kuimarisha mifumo na taasisi za utekelezaji wa Mpango; kuweka mfumo utakaowezesha upatikanaji wa uhakika wa rasilimali fedha kwa maandalizi na utekelezaji wa miradi; na kuweka vigezo vya upimaji wa mafanikio ya utekelezaji.

**Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

**35. Mheshimiwa Spika**, Mpango umebainisha miradi mikubwa ya maendeleo inayotarajiwu kutekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na mradi wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam; kiwanda cha kuzalisha madawa muhimu na vifaa tiba; na mradi wa Dar es Salaam – Chalinze *Toll Road*. Msukumo utawekwa kuongeza idadi ya miradi itakayotekelzwa kwa mfumo wa PPP.

## **Mikakati ya Kushirikisha Sekta Binafsi kwa mwaka 2018/19**

**36. Mheshimiwa Spika**, Sekta Binafsi ndio mtekelezaji mkuu wa Mpango kadri ya dhana ya kujenga uchumi wa viwanda. Serikali imeweka mikakati inayolenga kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa mpango, ikiwa ni pamoja na kuimarisha mikakati ya kubainisha maeneo yatakayowezesha kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi na kuainisha vivutio kwa wawekezaji katika maeneo ya kipaumbele; kuboresha zaidi mfumo rekebu na jukwaa la majadiliano kati ya Serikali na sekta binafsi kuhusu uwekezaji (*Investors round-table*); kufanya mapitio ya sheria ya uwekezaji wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; kuendeleza maboresho ya kimifumo na kitaasisi kuhusiana na ufumbuzi wa mahitaji ya sekta binafsi. Aidha, Serikali itaendelea kuziimarisha benki za ndani za maendeleo ili ziweze kukidhi ongezeko la mahitaji ya mikopo na udhamini kwa sekta binafsi.

## **MAELEKEZO MAHSUSI KATIKA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/19**

**37. Mheshimiwa Spika**, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni zake ikiwa ni pamoja na kuunda Kamati za Mipango na Bajeti na kuhakikisha Kamati hizo zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kifungu cha 17(3) cha Kanuni za Bajeti za mwaka 2015. Masuala muhimu ambayo Maafisa Masuuli wote wanapaswa kuzingatia wakati wa uandaaji na utekelezaji wa bajeti kama ifuatavyo:

### **Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani**

**38. Mheshimiwa Spika**, Maafisa masuuli wanaelekezwa: kuhakikisha kuwa makusanyo yote yanawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali; kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato; kuhakikisha zabuni za watoa huduma na makandarasi zinatolewa kwa wanaotumia mashine za kielektroniki; kukusanya mapato kutoka vyanzo bunifu vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango

wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano pamoja na vyanzo vingine; kutoingia mikataba yenyе vifungu vya sheria vinavyohusiana na misamaha ya kodi bila kupata ridhaa ya Waziri wa Fedha na Mipango; na kuhakikisha kuwa kampuni zote ambazo Serikali ina hisa zinaendeshwa kwa ufanisi na hivyo kutoa gawio stahiki kwa Serikali.

### **Kudhibiti Matumizi na Kupunguza Gharama**

**39. Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha Serikali inadhibiti na kupunguza gharama za uendeshaji, Wizara, Idara Zinazojitegema, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa: kuendelea kufanya uhakiki wa watumishi ili kuhakikisha kuwa mishahara inalipwa kwa watumishi wanaostahili; kuendelea kupunguza matumizi ya Serikali kwa kutumia Taasisi za Serikali zenyе gharama nafuu na huduma bora; kuhakikisha kuwa mikataba yote inayoingiwa na Serikali na Taasisi zake inakuwa katika Shilingi ya Tanzania isipokuwa kwa mikataba inayohusisha biashara za kimataifa; kufanya tathmini ya gharama za uendeshaji wa Taasisi za Serikali ili kuchukua hatua stahiki; na kuhakikisha kuwa Taasisi za Serikali zinazojiedesha kibiashara zinapata faida na kuacha kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu.

### **Kulipa na Kuzuia Ongezeko la Madeni ya Serikali**

**40. Mheshimiwa Spika**, katika kulipa na kudhibiti ongezeko la madeni ya Serikali, Maafisa Masuuli wanaagizwa: kuhakikisha madai yote yamehakikiwa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na kuingizwa kwenye hesabu za Fungu husika (Financial Statement); kutenga fedha za kulipa madeni yaliyohakikiwa; kutekeleza maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Serikali kuhusu ununuzi wa bidhaa na huduma; kutoingia mikataba ya miradi mipyä bila kuwa na uhakika wa upatikanaji fedha; na kuzingatia matumizi ya Hati ya ununuzi (LPO) zinazotolewa kwenye Mfumo wa Malipo (IFMS) ili kudhibiti ulimbikizaji wa madai.

## Maelekezo Mengine

41. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelekezo hayo mahsus, Maafisa Masuuli pia wanaelekezwa: kutoa taarifa za utekelezaji kwa kuzingatia muundo wa utoaji taarifa uliobainishwa katika Mwongozo; kuhakikisha mipango na bajeti inawekewa viashiria, vigezo na shabaha bayana ambavyo usimamizi wa utekelezaji utavizingatia; na kutekeleza Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa kuhakikisha kuwa fedha zinatengwa kwenye Halmashauri husika badala ya kutengwa kwenye bajeti za Wizara.

## HITIMISHO

42. **Mheshimiwa Spika**, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19 yaliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu yanalenga kujenga uelewa wa pamoja juu ya: hali ya uchumi na utekelezaji wa bajeti na miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha uliopita; maeneo ya kiupaumbele na bajeti yanayopendekezwa kwa mwaka 2018/19 katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini; hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na Serikali katika kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi hususan katika sekta ya viwanda; na kwamba juhudzi za makusudi zinahitajika katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ya kujenga uchumi wenye hadhi ya kipato cha kati. Msukumo mkubwa wa Serikali utawekwa katika mikakati ya kuongeza mapato, kupunguza gharama na matumizi ya uendeshaji wa Serikali na kudhibiti ulimbikizaji wa madeni.

43. **Mheshimiwa Spika**, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma zinaelekezwa kuzingatia Mwongozo katika kuandaa mipango na bajeti zao. Vile vile, zinaelekezwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19.

- 44.** **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu napenda kutoa shukurani za dhati kwa wadau na wananchi wote kwa juhudzi wanazoendelea kufanya katika utekelezaji wa mipango na bajeti. Natoa rai kwa Sekta Binafsi na wananchi wote kuendelea kuunga mkono juhudzi za Serikali hususan katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuwekeza na kutekeleza wajibu wa kulipa kodi.
- 45.** **Mheshimiwa Spika**, hotuba hii pamoja na vitabu vya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/19 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19 vitapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Fedha na Mipango ([www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz) na [www.mipango.go.tz](http://www.mipango.go.tz)).
- 46.** **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili, kutoa maoni na kuishauri Serikali kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/19 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19.
- 47.** **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, hoja imeungwa mkono. Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili na yeze aweze kuwasilisha maoni ya Kamati.

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza na taarifa yangu, napenda niwapongeze wale wote ambao wamepata uteuzi kutoka kwa Mheshimiwa Rais. Kamati yangu inapenda kuwaahidi kwamba wote tutawapa ushirikiano wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imepitia na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Taarifa hizi mbili zinatoa mwelekeo wa namna gani Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 utakavyoteklezwa katika kuimarisha uchumi wa viwanda na kupunguza umaskini. Kwa upande wa Mwelekeo wa Mpango, Serikali imepanga kujikita katika vipaumbele vyatkuendeleza viwanda vya kukuza uchumi ambavyo vitaimarisha kasi kubwa ya ukuaaji wa uchumi; miradi mikubwa ya kielelezo ya kuwezesha uchumi kukua na maeneo yanayolenga kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu; kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji pamoja na usimamizi wa utekelezaji. Aidha, Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti unatoa taswira ya uandaaji wa mipango na bajeti itakayotumika katika kugharamia maeneo ya vipaumbele vilivyoainishwa na vitakavyoteklezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mwongozo umeainisha ukuaaji wa baadhi ya sekta, pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka wa fedha 2018/2019, unaopendekezwa. Kwa pamoja imebainisha maelekezo mahsus yanayopaswa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonesha kwamba katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 (Januari hadi Juni) Pato Halisi la Taifa lilikuwa

shilingi triliuni 25.54 ikilinganishwa na shilingi triliuni 23.92 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Hii ni sawa na ukuaji wa Uchumi kwa asilimia 6.8 ikilinganishwa na asilimia 7.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu wa uchumi kwa mwaka 2017, umechangiwa na sekta zilizoongoza kwa ukuaji mkubwa ambazo ni pamoja na uchimbaji madini na mawe ambayo ni asilimia 26.1; habari na mawasiliano (asilimia 13.0); usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 11.3) na ujenzi (asilimia 8.6). Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 kulichangiwa zaidi na ukuaji mdogo katika shughuli za utawala, zilizopungua kwa ukuaji hasi asilimia 3.8. Hali hii ilichangiwa na hatua za kubana matumizi na kupungua kwa ankara za mishahara za watumishi hewa. Hata hivyo, katika kipindi hicho shughuli za fedha na bima zilipungua kwa (asilimia 8.1), sekta ya usafirishaji ilipungua kwa asilimia 11.3 na elimu asilimia 5.2. Aidha, ukuaji wa sekta ya kilimo na maji ulikua katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2016 kama ifuatavyo; sekta ya kilimo ilikuwa kutoka asilimia 2.7 hadi kufikia asilimia 3.1 na sekta ya maji ilikuwa kutoka asilimia 0.9 hadi kufikia asilimia 2.1 katika kipindi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Mwongozo haujatoa takwimu za mchango wa sekta za utalii na maliasili, ufugaji na uvuvi, ni maoni ya Kamati kuwa sekta hizi zinaweza kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu na hivyo Serikali itambue mchango wake na kuwekea mikakati mahsusini wa kuziendeleza sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei kwa mwaka 2017 uliongezeka kutoka asilimia 5.2 Januari, 2017 hadi kufikia asilimia 6.4 mwezi Machi na Aprili, 2017 na kisha kushuka kufikia asilimia 5.0 mwezi Agosti na kuongezeka kidogo kufikia asilimia 5.3 Septemba, 2017. Kuendelea kuimarika kwa mwenendo wa mfumuko wa bei nchini kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na mwenendo wa bei za mafuta ya petroli kushuka katika soko la dunia na ndani ya nchi; kuimarika kwa bei ya vyakula nchini na kuwepo kwa usimamizi bora wa sera za bajeti na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato la wastani kwa kila Mtanzania limeongezeka kutoka dola za Kimarekani 979.1 mwaka 2016 hadi dola za Kimarekani 1,025.7 mwaka 2017. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuweka mikakati ya kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ya wastani wa pato la Mtanzania kufikia dola 3,000. Kamati pia inaishauri Serikali kuongeza kasi na mikakati itakayowezesha kufungamanisha ukuaji wa uchumi wa nchi na ukuaji wa pato la kila Mtanzania. Kamati inatambua juhudini na jithada za Serikali ya Awamu ya Tano katika kukuza Pato la Taifa, usimamizi wa rasilimali na kuongeza ukusanyaji wa mapato. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuendelea kudhibiti ukuaji wa Deni la Taifa kwa kuangalia vyanzo vingine vyaa mapato hasa ushuru wa forodha, mapato yasio ya kodi pamoja na kuendelea kuangalia upatikanaji wa misaada yenye masharti nafuu na mikopo nafuu kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepitia Mwongozo wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019 na kwa kiasi kikubwa inaipongeza Serikali katika maboresho ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato, shabaha za uchumi jumla na misingi iliyowekwa kwa ajili ya bajeti. Hata hivyo, Kamati ina ushauri ufuatao katika Mwongozo huo wa Bajeti. Sura ya bajeti inaonesha kuwa jumla ya Shilingi trillioni 32.476 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho cha mwaka wa fedha 2018/2019. Hii ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 2.4 ya bajeti ya mwaka 2017/2018. Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuwa shilingi trillioni 22.08 sawa na asilimia 68. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi ni shilingi trillioni 18.81, mapato yasiyo na kodi ni shilingi trillioni 2.42 na shilingi bilioni 847.6 ni mapato ya Halmashauri. Serikali inategemea kupata kiasi cha shilingi trillioni 3.658 ikiwa ni misaada na mikopo kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019. Vilevile Serikali inatarajia kukopa kiasi cha shilingi trillioni 1.374 kama mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara. Aidha, Serikali inategemea kukopa kiasi cha shilingi trillioni 4.028 kutoka katika vyanzo vyake vyaa ndani kwa ajili ya kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva na shilingi

triliuni 1.327 sawa na asilimia moja ya Pato la Taifa ikiwa ni mikopo mipy ya ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa hapo juu, Serikali inategemea kutumia kiasi cha shilingi triliuni 32.47 kwa mwaka 2018/2019 hii ni sawa na ongezeko la asilimia 2.4 kwa bajeti ya mwaka 2017/2018. Aidha, Serikali imeeleza kwamba mapato yake ya yatafikia kiasi cha shilingi triliuni 22.088 tu, hivyo ili kukamilisha bajeti yake kiasi cha shilingi triliuni 10.388 kitapatikana kutoka katika mikopo ya masharti nafuu na mikopo yenye masharti ya kibashara kutoka ndani na nje ya nchi. Kamati inapongeza nia njema ya Serikali kuhakikisha kuwa inapata fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia bajeti yake hasa kwa upande wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwa mwongozo huu ujielekeze zaidi kuondoa changamoto zinazoikabili sekta ya fedha katika kutatua tatizo la uhaba mkubwa wa mtaji unaohitajika kusaidia kukuza uchumi wa Tanzania hasa katika kujenga uchumi wa viwanda. Hivi sasa tunazo benki takriban 45 na taasisi nyngi za kifedha, pamoja na wingi wake wananchi wengi hawajapata fursa ya kupata mikopo kwa ajili shughuli zao za kujipatia kipato na kujiajiri. Hali hii inatokana na ama masharti ya benki au kodi zisizo rafiki wakati wa uanzishwaji wa biashara. Serikali ione umuhimu wa kuimarisha utekelezaji wa *Credit Reference Bureau* ili kupunguza tatizo hili. Utaratibu huo utasaidia kupunguza viwango vya riba ambavyo hivi sasa viko juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi ndizo zinazoajiri Watanzania wengi na ndio sekta inayoweza kulihakikishia Taifa usalama wa chakula na malighafi za viwandani. Kamati inaishauri Serikali kuwa sekta hizi zipewe kipaumbele katika mpango wa bajeti ili mchango wa sekta hii uonekane katika harakati za kuelekea uchumi wa viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka

2018/2019 umekisia ukusanyaji wa mapato ya ndani kukua kwa asilimia 16.6 kwa uwiano wa Pato la Taifa. Hata hivyo, makisio hayo hayakuambatana na mipango thabiti na bayana inayoonyesha namna ya kufikia ukuaji huo na ikiwezekana hata zaidi ya asilimia tajwa. Kamati inaishauri Serikali kupanua ukusanyaji wa mapato kwa sekta ambazo bado hazijawa na mchango mkubwa katika mapato ya ndani, sekta hizo ni kama uvuvi, mifugo, misitu na maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kulipa madeni yaliyohakikiwa. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuonesha bayana kiasi cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya ndani ambayo tayari yamehakikiwa. Ushauri huu unaendana na msisitizo wa kusimamia malimbikizo ya madeni uliotolewa na Serikali kupitia Waraka wa Hazina Na. 4 wa mwaka 2014/2015 na utaratibu ambao Serikali imejiwekea wa kulipa madeni mara tu yanapohakikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti umezingatia Sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015 na Kanuni zake. Misingi ya ukuaji wa uchumi, maoteo pamoja na usimamizi wa mipango ya maendeleo umeanishwa katika kifungu cha 4, 5 na 6 cha Sheria ya Bajeti. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali wakati wa utekelezaji wa Mwongozo huu kufanya tathmini ni kwa kiasi gani imeweza kutekeleza misingi iliyojiwekea sawa na matakwa ya Sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono utaratibu wa Wizara, Taasisi na Mashirika yote ya Umma kutakiwa kuwasilisha Benki Kuu mapato yao yote yanayokusanya. Lengo la utaratibu huu ni kuiwezesha Serikali kuwa na udhibiti wa fedha za umma pamoja na kujua kiasi cha fedha kinachopatikana kila siku. Hata hivyo, Kamati inaisitizia Serikali kuhakikisha fedha za matumizi ya Wizara, Taasisi na Mashirika hayo zinapelekwa haraka kulingana na mipango kazi yao na kama Bunge lilivyopitisha katika bajeti zao ili kuepuka shughuli za utekelezaji wa bajeti kukwama au kutokutekeleza kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo huu pia haujaweza kuainisha namna sekta binafsi zitakavyoweza kushirikiana na Serikali katika kugharamia miradi ya maendeleo kupitia Sheria ya *PPP*. Suala hili limekuwa ni changamoto ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kushirikisha sekta binafsi katika kutekeleza miradi mikubwa ya kielelezo ili kupunguza mzigo mkubwa wa bajeti ya Serikali katika kugharamia miradi inayoweza kutekelezwa kwa mfumo wa ubia. Vilevile Mwongozo uainishe gharama zitakazotumiwa na sekta binafsi katika kutekeleza miradi iliyoinishwa kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 umezingatia maeneo makuu manne ya Kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambayo ni:-

- (i) Ukuaji wa uchumi na ujenzi wa uchumi wa viwanda.
- (ii) Kufungamanisha uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu.
- (iii) Kujenga mazingira wezeshi kwa uwekezaji na uendeshaji biashara.
- (iv) Kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa Mpango na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2018/2019 na inapenda kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ipo katika mpango wa kuwa nchi ya uchumi wa viwanda wenye kuwesha watu wake kufikia katika kipato cha kati ifikapo mwaka 2020/2025. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua hilo

na kuweka mikakati thabiti itakayowezesha nchi yetu kufanya mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeelezea kwamba imelenga kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu na kuweka mazingira mazuri ya ustawi kwa Watanzania hasa wa vijijini kwa kuboresha huduma za jamii kama vile afya bora, elimu, ujuzi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi zake katika kuimarisha sekta ya afya mijini na vijijini ikiwa ni kuendeleza ujenzi wa majengo ya hospitali, ununuzi wa vifaa tiba na kuongeza vyumba vya upasuaji katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya mkakati wake wa kufanya tathmini ya kina ili kujua mahitaji halisi pamoja na gherama za ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na vifaa tiba nchini, pamoja na kushughulikia upungufu wa wataalam wa sekta ya afya ili mahitaji hayo yaweze kutengwa katika bajeti ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maji ni muhimu sana kwa maendeleo, kijamii na kiuchumi. Maji ni uhai, nchi yetu bado inayo changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji hasa katika maeneo ya vijijini. Wakati umefika sasa wa Serikali kuweka mkakati mahsus kama ilivyofanya katika sekta ya umeme na barabara ili kuweza kutatua changamoto hii kwa ufanisi na kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya kweli ni lazima yawe endelevu. Sote tunafahamu hatuwezi kuwa na maendeleo endelevu kama mazingira yetu hayatakuwa endelevu. Hivyo ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa tunatunza mazingira kwa manufaa yetu na kwa manufaa ya kizazi kijacho. Aidha, Serikali ina kazi kubwa ya kufanya ili kuhakikisha mazingira yetu yanakuwa bora na endelevu. Iko haja sasa kwa Serikali kuweka mkakati wa kuwajibisha kila Sekta, Idara, Halmashauri na Sekta Binafsi kusimamia ipasavyo

kanuni na mikakati ya utunzaji wa mazingira katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua nzuri ilizochukua katika kufufua Shirika la Ndege la Taifa kwa kuimarisha mnejimenti yake na pia kununua ndege mpya. Vilevile Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuanza ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Dar es salaam hadi Morogoro na maandalizi ya ujenzi wa reli hiyo kuanzia Morogoro hadi Dodoma, ambapo tayari mkandarasi amepatikana na kazi imeanza. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa dhamira yake ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme ya *Stiegler's Gorge*, mradi utazalisha umeme MW 2100 kutokana na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo umeainisha miradi ya kielelezo itakayotekelawa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni mwendelezo wa utekelezaji wa miradi ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika utekelezaji wa Miradi ya Liganga na Mchuchuma. Maeneo maalum ya kiuchumi ya EPZ na SEZ, Kituo cha Viwanda cha Kurasini, Kiwanda cha Kusindika Gesi Kimiminika cha Lindi, Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi, Kiwanda cha Mbolea cha Mtwara na Kilwa kwa kutumia gesi asilia. Kamati ina imani kubwa sana kwamba miradi hii ikitekelezwala kwa kasi kubwa itasaidia sana kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia, inaipongeza Serikali kwa kufanikiwa kuingia mkataba na nchi ya Uganda katika ujenzi wa bomba la mafuta litakalotoka Hoima Uganda hadi Chongoleani, Tanga - Tanzania. Ujenzi wa Bomba hili utachochaea sana maendeleo kwa kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja wakati wa ujenzi wake na Serikali kupata kodi mara mradi utakapokamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa mradi huu muhimu, ikiwa ni pamoja na kujenga *Marine Export Terminal* katika Bandari ya Tanga na kuwajengea uwezo wataalam wa ndani ili waweze kusimamia mapato kutoka katika bandari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ingependa kurudia mapendekezo yake ambayo imekuwa ikiyatoa miaka iliyopita ya kuiandaa vyta kutosha sekta binafsi kwa kuweka mazingira wezeshi na kuainisha miradi ambayo sekta binafsi inaweza kushirikiana na Serikali katika kipindi husika. Aidha, Kamati inasistiza kwamba katika bajeti ya 2018/2019 itakayowasilishwa Bungeni iainishe wazi mchango wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mengine ni kama yanavyoonekana katika kitabu cha hotuba yangu. Pamoja na maoni na ushauri pamoja na maoni na ushauri huo uliojikita katika maeneo mahsus, Kamati ingependa kutoa maoni ya jumla yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ielekeze nguvu zaidi katika kutumia vema rasilimali yake ya gesi asilia katika kuendesha shughuli zake za kiuchumi hasa viwanda na upatikanaji wa umeme nchini. Hii itasaidia sana kupunguza *Import Bill* ya uagizaji wa mafuta kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inapongeza Serikali kwa usimamizi na ufanisi katika sekta ya madini katika kuhakikisha inapata mapato stahiki. Kamati inashauri Serikali kuimarisha usimamizi kwenye sekta hiyo kuititia uwezeshaji wa wachimbaji wadogo, ili wawe na mchango katika sekta hiyo na kusaidia kuongeza mapato ya kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia iweke mikakati ya makusudi katika kusimamia mwongozo wa kupunguza ukuaji na ulipaji wa Deni la Taifa linaloongezeka mwaka hadi mwaka pamoja na kwamba deni hilo kwa sasa linaonekana kuwa himilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mikakati madhubuti ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati ili kuweza kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizotolewa na UNICEF zinaonesha kwamba ifikapo mwaka 2050 Tanzania itakuwa na watoto wenyewe umri chini ya miaka 18 wapatao 58,000,000 hivyo kuleta jumla ya watu 108,000,000. Kamati inaishauri Serikali kuleta mkakati wa kitaifa utakaosaidia kukuza uchumi uutakaoendana na ongezeko hilo la watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo kama tulivyosema ishirikiane na sekta binafsi. Kamati inaishauri Serikali kuweka mpango wa usimamizi na uvunaji wa rasilimali misitu na bahari kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuongeza pato la nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaishauri Serikali iandae Sera itakayopunguza utumiaji wa fedha taslimu, ili kuongeza mapato ya Serikali kwa kutumia Vitambulisho vya Taifa katika kila eneo. Serikali pia iharakishe kuweka utaratibu utakaowezesha matumizi ya kadi (*cashless payment system*) na kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika miamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia, iboreshe mifumo ya ukusanyaji wa kodi, na Serikali iendeleze kasi ya zoezi la utoaji wa hati miliki za kimila ili tuweze kupunguza sekta isiyokuwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Benki Kuu ya Tanzania kuchukua hatua za kupunguza riba ya mikopo inayotolewa na Benki za Biashara na pia kupunguza kiwango cha amana ambacho benki za biashara hutakiwa kuhifadhi Benki Kuu kama amana, Kamati inaishauri Serikali kuitia Benki Kuu kufanya utafiti na hatua za ziada za kuchukua ili kuchochaea ujazi wa fedha katika mzunguko wa sarafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mengine ni kama yanavyoonekana katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuhitimisha kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyevit wa Kamati wa Bunge, pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wake pamoja na wataalam wote kwani mapendekezo mengi na ushauri ambao umetolewa na Kamati ya Bajeti imezingatiwa katika kuandaa Mwongozo pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa ushauri na ushirikiano mkubwa wanaonipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri. Pamoja na kwamba ni mgeni, lakini kwa kweli, ameonesha kwamba kwa kweli atatoa mchango mkubwa katika Bunge hili, hasa kwa vile alivyoisaidia Kamati ya Bajeti kuweza kutekeleza majukumu yake katika kipindi hiki kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda nimalizie kwa kukupongeza wewe na kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU  
MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA KUTAYARISHA  
MPANGO NA BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO WA  
TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti Kuhusu

Mapendekezo ya Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imepitia na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19. Taarifa hizi mbili zinatoa mwelekeo wa namna gani Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/19 utakavyotekelawa katika kuimarisha uchumi wa viwanda na kupunguza umasikini. Kwa upande wa mwelekeo wa mpango, Serikali imepanga kujikita katika vipaumbele vya kuendeleza viwanda vya kukuza uchumi ambavyo vitaimarisha kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi; miradi mikubwa ya kielelezo ya kuwezesha uchumi kukua (*Flagship projects*) na maeneo yanayolenga kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu, kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji pamoja na usimamizi wa utekelezaji. Aidha, mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti unatoa taswira ya uandaaji wa mipango na bajeti itakayotumika katika kugharamia maeneo ya vipaumbele vilivyoainishwa na vitakavyotekelawa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Mwongozo umeanisha ukuaji wa baadhi ya sekta, pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2018/19 unaopendekezwa kwa pamoja imebainisha maelekezo mahsus yanayopaswa kuzingatiwa na maafisa masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/19

## **2.0. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2017**

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonesha kwamba, katika nusu ya kwanza ya

mwaka 2017 (Januari hadi Juni) Pato Halisi la Taifa lilikuwa shilingi triliioni 25.54 ikilinganishwa na shilingi triliioni 23.92 katika kipindi kama hicho mwaka 2016; hii ni sawa na ukuaji wa Uchumi kwa asilimia 6.8 ikilinganishwa na asilimia 7.7 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2016. Ukuaji huu wa Uchumi wa mwaka 2017 umechangiwa na sekta zilizoongoza kwa ukuaji mkubwa ambazo ni pamoja na uchimbaji madini na mawe (asilimia 26.1); habari na mawasiliano (asilimia 13.0); usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 11.3) na ujenzi (asilimia 8.6).

**Mheshimiwa Spika**, kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika nusu ya kwanza ya Mwaka 2017 kulichangiwa zaidi na ukuaji mdogo katika shughuli za utawala, zilizopungua kwa ukuaji hasi asilimia 3.8. Hali hii ilichangiwa na hatua za kubana matumizi na kupungua kwa ankara za mishahara za watumishi hewa. Hata hivyo katika kipindi hicho shughuli za fedha na bima zilipungua kwa (asilimia 8.1), sekta za usafirishaji ilipungua kwa (asilimia 11.3) na elimu (asilimia 5.2). Aidha, ukuaji wa sekta ya kilimo na maji ulikua katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2016. Kama ifuatavyo; Sekta kilimo ilikuwa kutoka asilimia 2.7 hadi kufikia asilimia 3.1 na sekta ya maji ilikua kutoka asilimia 0.9 hadi kufikia asilimia 2.1 katika kipindi husika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa Mwongozo haujatoa takwimu za mchango wa sekta za utalii na maliasili, ufugaji na uvuvi, Ni maoni ya Kamati kuwa sekta hizi zinaweza kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu na kwa hivyo Serikali itambue mchango wake na kuweka mikakati mahsuswi wa kuziendeleza.

**Mheshimiwa Spika**, mfumuko wa bei kwa mwaka 2017 ulationezeka kutoka asilimia 5.2 Januari 2017 hadi kufikia asilimia 6.4 kwa mwezi Machi na Aprili, 2017 na kisha kushuka kufikia asilimia 5.0 mwezi Agosti, 2017 na kuongezeka kidogo kufikia asilimia 5.3 Septemba, 2017. Kuendelea kuimarkika kwa mwenendo wa Mfumuko wa bei nchini kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na: Mwenendo wa bei za mafuta ya petroli

kushuka katika soko la Dunia na ndani ya nchi; kuimarika kwa bei ya vyakula nchini na kuwepo na usimamizi bora wa sera za bajeti na sera za fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Pato la wastani kwa kila mtanzania (per capita income) limeongezeka kutoka Dola za Kimarekani 979.1 mwaka 2016 hadi Dola za Kimarekani 1,025.7 mwaka 2017, Hata hivyo Kamati inashauri Serikali kuweka mikakati yakuongeza kasi ya kukua kwa uchumi ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ya wastani wa Pato la kila mtanzania la Dola za Marekani 3,000. Kamati pia inaishauri Serikali kuongeza kasi na mikakati itakayowezesha kufungamanisha ukuaji wa uchumi wa nchi na ukuaji wa pato la kila mtu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudhi na jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano katika kukuza pato la Taifa, usimamizi wa rasilimali na kuongeza ukusanyaji wa mapato. Aidha, Kamati inaendelea kusitiza Serikali kuendelea kudhibiti ukuaji wa Deni la Taifa kwa kuagalia vyanzo vingine vya mapato hasa ya kodi katika ushuru wa forodha, mapato yasio ya kodi pamoja na kuendelea kuangalia upatikanaji wa misaada yenye masharti nafuu na mikopo nafuu kutoka nje.

### **3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MWONGOZO WA KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/19**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia Mwongozo wa Bajeti kwa mwaka 2018/19 na kwa kiasi kikubwa inaipongeza Serikali katika Maboresho ya Mfumo wa ukusanyaji wa mapato, Shabaha za uchumi jumla na misingi iliyowekwa kwa ajili ya Bajeti. Hata, hivyo Kamati ina ushauri ufuatao katika Mwongozo huo wa Bajeti:-

**Mheshimiwa Spika**, Sura ya Bajeti inaonyesha kuwa jumla ya Shilingi trilioni 32.476 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 hii ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 2.4 ya bajeti ya Mwaka

2017/18 (triliioni 31.71). Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuwa Shilingi triliioni 22.08 sawa na asilimia 68. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodii ni Shilingi triliioni 18.81, mapato yasiyo ya kodii ni Shilingi triliioni 2.42 na Shilingi bilioni 847.6 ni mapato ya Halmashauri. Serikali inategemea kupata kiasi cha Shilingi triliioni 3.658 ikiwa ni misaada na mikopo kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2018/19. Vile vile, Serikali inatarajia kukopa kiasi cha shilingi triliioni 1.374 kama mikopo ya nje yenye masharti ya kibashara. Aidha, Serikali inategemea kukopa kiasi cha shilingi Triliioni 4.028 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva na shilingi triliioni 1.327 sawa na asilimia moja ya pato la Taifa itakuwa ni mikopo mipyaa ya ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**3.1. Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa hapo juu, Serikali inategemea kutumia kiasi cha shilingi triliioni 32.47 kwa mwaka 2018/19 hii ni sawa na ongezeko la asilimia 2.4 ya Bajeti ya Mwaka 2017/18 (Triliioni 31.712). Aidha, Serikali imeeleza kwamba kwa kuwa mapato yake ya ndani (Mapato ya kodii, mapato yasiyo ya kodii pamoja na mapato ya Halmashauri) yatafikia kiasi cha Shilingi Triliioni 22.088 tu, hivyo ili kukamilisha Bajeti yake kiasi cha shilingi triliioni 10.388 kitapatikana kutoka katika mikopo ya masharti nafuu na mikopo yenye masharti ya kibashara kutoka ndani na nje ya nchi. Kamati inapongeza nia njema ya Serikali ya kuhakikisha kuwa inapata fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia bajeti yake hasa katika upande wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa mwongozo huu haujaweza kutoa ufumbuzi wa kutatua changamoto ya upatikanaji wa fedha kutoka kwa wafadhili ambazo kiasi kikubwa huelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Takwimu zinaonyesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha bajeti ya mwaka 2016/17 ulikuwa sio wa kuridhisha, hali iliyopelekea Serikali kutumia baadhi ya fedha zake za ndani ambazo zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kugharamia miradi hiyo. Hatua hii itasababisha Serikali kuzalisha madeni ya wakandarasi wa

ndani hasa kwa matumizi ya kawaida ambayo ni lazima yafanyike. Kamati inatoa angalizo kuwa fedha zinazokopwa zielekezwe katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya kimkakati itakayoleta matokeo chanya na ya haraka kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa Serikali kukopa zaidi katika vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kuziba nakisi ya bajeti unaathiri zaidi ukuaji wa sekta binafsi nchini, Mwongozo huu bado haujatoa ufanuzi wa kutosha kuhusu uimarishaji na ukuaji wa sekta binafsi kuititia upatikanaji wa mitaji katika vyombo vya fedha vya ndani. Njia yenye uhakika ni kwa Serikali kujielekeza kukopa vyanzo vya nje vyenye masharti nafuu ili kuwezesha sekta Binafsi ya ndani kupata mikopo ya ndani kwa gharama nafuu.

**3.2. Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuwa mwongozo huu ujielekeze zaidi kuondoa changamoto zinazoikabili sekta ya fedha katika kutatua tatizo la uhaba mkubwa wa mitaji unaohitajika kusaidia kukuza uchumi wa Tanzania hasa katika kujenga uchumi wa viwanda. Hivi sasa tunazo Benki takriban 45 na Taasisi nyingi za kifedha, pamoja na wingi wake wananchi wengi hawajapata fursa ya kupata mikopo kwa ajili shughuli zao za kujipatia kipato na kujiajiri. Hali hii inatokana na ama masharti ya Benki au kodi zisizo rafiki wakati wa uanzishwaji wa biashara. Takwimu zinaonyesha kuwa Mikopo chechefu imeongezeka na kuflikia asilimia 10.6 (2017) kutoka asilimia 8.9 (2016) hali hii inaathiri rasilimali za mabenki hivyo kupunguza kiwango chake cha ukopeshaji. Serikali ione umuhimu wa kusimamia utekelezaji wa *Credit Reference Bureau* ili kupunguza tatizo hili. Utaratibu huo utasaidia kupunguza viwango vya riba ambavyo hivi sasa viko juu.

**3.3. Mheshimiwa Spika**, Sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi ndiyo inaajiri Watanzania Wengi na ndio sekta inayoweza kulihakikishia taifa usalama wa chakula na malighafi za viwandani. Kamati inashauri sekta hii ipewe kipaumbele katika mpango wa bajeti ili mchango wa sekta hii uonekane katika harakati za kuelekea uchumi wa

viwanda. Aidha, Serikali ijiandae mapema kuhakikisha kuwa Wakala wa Hifadhi ya Chakula Nchini (NFRA) inapewa bajeti ya kutosha kununua akiba ya kutosha ya chakula.

**3.4. Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo ya muongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19 umekisia ukusanyaji wa mapato ya ndani kukua kwa asilimia 16.6 kwa uwiano wa Pato la Taifa. Hata hivyo makisio hayo hayakuambatana na mipango thabiti na bayana inayoonyeha namna ya kufikia ukuaji huo na ikiwezekana hata zaidi ya asilimia tajwa. Kamati inaishauri Serikali kupanua ukusanyaji wa mapato kwa sekta ambazo bado hazijawa na mchango mkubwa katika mapato ya ndani, Sekta hizo ni pamoja na uvuvi, mifugo, misitu na maliasili.

**3.5. Mheshimiwa Spika**, yapo maeneo ambayo yamekuwa yakiongelewa mara kwa mara kwamba yanaongeza gharama za uendeshaji wa biashara nchini (*cost of doing business*). Maeneo hayo ni; ukosefu wa Nishati ya Umeme wa uhakika, upatikanaji wa mitaji, upatikanaji wa vibali, usajili wa biashara, utekelezaji wa mikataba, upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji na kulinda wawekezaji. Kamati inaona bado Serikali inahitaji kufanya kazi zaidi maeneo haya ili kuweza kuleta tija katika biashara na katika kukuza uchumi wa viwanda. Mwongozo huu ujielekeze katika kutatua changamoto hizi.

**3.6. Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kulipa madeni yaliyohakikiwa. Aidha Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuonesha bayana kiasi fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya ndani ambayo yamehakikiwa. Ushauri huu unaendana na msisitizo wa kusimamia malimbikizo ya madeni uliotolewa na Serikali kuititia waraka wa Hazina na 4 wa mwaka 2014/15, na utaratibu ambao umewekwa wa kulipa madeni hayo.

**3.7. Mheshimiwa Spika**, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti umezingatia Sheria ya Bajeti Na 11 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake. Misingi ya Ukuaji wa Uchumi,

maoteo pamoja na usimamizi wa mipango ya maendeleo umeanishwa katika kifungu cha 4, 5 na 6 cha Sheria ya Bajeti, hata hivyo Kamati inaishauri Serikali wakati wa utekelezaji wa Mwongozo huu kufanya tathmini ni kwa kiasi gani imeweza kutekeleza misingi iliyojiwekea kupitia matakwa ya Sheria ya Bajeti Na 11 ya Mwaka 2015.

**3.8. Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono utaratibu wa Wizara, Taasisi na Mashirika yote ya Umma kutakiwa kuwasilisha Benki Kuu mapato yao yote wanayoyakusanya. Lengo la utaratibu huu ni kuiweseha Serikali kuwa na udhibiti wa fedha za umma pamoja na kujua kiasi cha fedha kinachopatikana kila siku. Hata hivyo, Kamati inaisisitizia Serikali kuhakikisha fedha za matumizi ya Wizara, Taasisi na Mashirika hayo zinapelekwa haraka kulingana na mipango kazi yao na kama Bunge lilivyopitisha katika bajeti zao ili kuepuka shughuli zao za utekelezaji wa bajeti kukwama au kutotekeliza kwa wakati.

**3.9. Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kufanya uthamini wa majengo ili kupata thamani itakayowezesha viwango stahiki vyta kodi ya majengo kutozwa kwa kila jengo nchini. Utaratibu wa uthamini wa ujumla yaani *mass valuation* umekuwa ukilikosesha Serikali mapato yake halali kwa kuwa thamani ya nyumba haizingatiwi. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali pamoja na utaratibu uliowekwa kisheria mwaka 2016, ni vyema kuwe na utaratibu maalum utakao onesha namna Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wanavyo kukusanya kodi hiyo katika maeneo yote (Majiji, Manispaa, Miji na Halmashauri).

**3.10. Mheshimiwa Spika**, Mwongozo huu bado haujaweza kuainisha namna Sekta binafsi itakavyoweza kushirikiana na Serikali katika kugharamia miradi ya maendeleo kupitia PPP. Sualia hili limekuwa ni changamoto ya muda mrefu, aidha miradi inayoainishwa kutekelezwa kwa njia ya PPP imekuwa ni ile ile kila mwaka kama vile miradi ya mabasi yaendayo kwa kasi na ujenzi wa barabara ya DSM-chalinze. Kamati haijaweza kuona ubunifu wa miradi

mingine mipyä itakayoweza kutekelezwa kwa njia ya ubia. Kamati inashauri Serikali kushirikisha sekta binafsi katika kutekeleza miradi mikubwa ya klelelezo ili kupunguza mzigo mkubwa wa bajeti ya Serikali katika kugharamia miradi inayoweza kutekelezwa kwa mfumo wa ubia. Vilevile, mwongozo uainishe gharama zitakazotumiwa na sekta binafsi katika kutekeleza miradi iliyoainishwa kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19.

#### **4.0. MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2018/19**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19 umezingatia maeneo makuu manne ya Kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21 ambayo ni;

- i. Ukuzaji wa Uchumi na Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda
- ii. Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu
- iii. Kujenga Mazingira wezeshi kwa Uwekezaji na Uendeshaji Biashara
- iv. Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mpango na Miradi ya Maendeleo

#### **4.1. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2018/19**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Mpango wa maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2018/19 na ingependa kutoa maoni na ushauri ufuatao;

## **4.2. Maoni Kuhusu Maeneo Makuu yaliyozingatiwa katika kuandaa Mapendekezo ya Mpango**

### **4.2.1. Ukuzaji wa Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda**

**Mheshimiwa Spika**, Nchi yetu ipo katika mpango wa kuwa nchi ya uchumi wa viwanda wenyewe kuwezesha watu wake kufika katika kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua hilo na kuweka mikakati thabiti itakayowezesha nchi yetu kufanya mapinduzi ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeeleza kuwa ili kufikia lengo la kuwa na viwanda vyta kukuza uchumi na ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda Vidogo nchini, imedhamiria kupanua na kuimarisha Shirika la kusimamia viwanda vidogo SIDO ili kulifanya kuwa ni chombo cha kuleta mageuzi ya viwanda nchini. Kamati inaunga mkono dhamira hii njema na inapaswa kuungwa mkono.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mkakati wa kuleta mageuzi ya viwanda kwa kuimarisha na kuzitumia Taasisi za Umma, kama vile Shirika la Maendeleo la NDC, STAMICO, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), TIRDO, CARMATEC, TEMDO, COSTECH, Nyumbu na Mzinga ili ziweze kuleta mchango katika kuendeleza viwanda nchini. Ili mkakati huu ufanikiwe ni lazima Mashirika na Taasisi hizi zikajengewa uwezo wa Kitaasisi, Kisheria na Kifedha ili yaweze kujihendesha kibashara na kupunguzia Serikali mzigo wa kuyapa ruzuku, na hatimaye yaweze kutoa mchango unaostahiki katika maendeleo ya nchi yetu.

### **4.2.2. Kufungamanisha Uchumi na Maendeleo ya Watu**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeeleza kuwa eneo hili linalenga kuweka mazingira mazuri ya ustawi kwa watanzania hasa wa vijijini kwa kuboresha huduma za jamii kama vile afya bora, elimu na ujuzi na kuondoa umaskini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudzi zake katika kuimarisha sekta ya Afya mijini na vijijini ikiwa ni kuendeleza ujenzi wa majengo ya hospitali, ununuzi wa vifaa tiba na kuongezeka kwa vyumba vyia upasuaji katika hospitali ya Taifa Muhimbili. Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi changamoto za sekta ya afya hasa zilizopo katika maeneo ya vijijini kama vile upungufu wa watumishi wa sekta hiyo. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya mkakati wake wa kufanya tathmini ya kina ili kujua mahitaji halisi pamoja na gharama ya ujenzi wa Zahanati, Vituo vyia Afya na Vifaa tiba nchini, pamoja na kushughulikia upungufu wa Wataalam wa Sekta ya Afya ili mahitaji hayo yaweze kutengewa bajeti ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya maji ni muhimu sana kwa maendeleo, kijamii na kiuchumi. “**MAJI NI UHAI**”. Nchi yetu bado ina changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji hasa katika maeneo ya vijijini. Wakati umefika sasa wa Serikali kuweka mkakati mahsus kama ule uliofanyika katika sekta ya umeme na barabara ili kuweza kutatua changamoto hii kwa ufanisi na haraka.

**Mheshimiwa Spika**, maendeleo ya kweli ni lazima yawe endelevu. Sote tunafahamu hakuwezi kuwa na maendeleo endelevu kama mazingira yetu hayatakuwa endelevu. Hivyo ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa tunatunza mazingira kwa manufaa yetu na manufaa ya kizazi kijacho. Aidha, Serikali ina kazi kubwa ya kufanya ili kuhakikisha mazingira yetu yanakuwa bora na endelevu. Iko haja sasa kwa Serikali kuweka mkakati wa kuwajibisha kila sekta, Idara, Halmashauri na Sekta Binafsi kusimamia ipasavyo kanuni na mikakati ya utunzaji wa mazingira katika maeneo yao.

#### **4.2.3. Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji na Ushiriki wa Sekta Binafsi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudzi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuweka mazingira bora yatakayoiwezesha Sekta binafsi kuwekeza

pamoja na kufanya biashara kwa urahisi. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji (barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege); kuboresha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika; kuanzisha na kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji; kuweka sheria za fedha na kodi zinazotabirika (zisizobadilika mara kwa mara); kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa mali ghafi kwa ajili ya viwanda na kunakuwa na Sheria bora za ajira.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa bado Serikali hajjaweka mazingira wezeshi yatakayowezesha na kurahisisha sekta hiyo kuwekeza kwa urahisi. Mfano katika Ripoti ya UNCTAD ya Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji ya mwaka 2016 (Doing Business Report 2016) inaonyesha Tanzania inashika nafasi ya 154 kati ya nchi 189 duniani, kwa urahisi wa ulipaji kodi. Hali hii inaonesha kuwa bado kuna jitihada za ziada zinatakiwa kuweka mifumo rahisi na rafiki ya ulipaji wa kodi kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

#### **4.3. Maoni Kuhusu Miradi Mikubwa ya Kielelezo (*Flagship Projects*)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua nzuri iliyochukua katika kufufua Shirika la ndege la Taifa (ATCL) kwa kuimarisha menejimenti yake, lakini pia kwa kununua ndege mpya. Vile vile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Dar es salaam hadi Morogoro na maandalizi ya ujenzi wa reli hiyo kuanzia Morogoro hadi Dodoma. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa dhamira yake ya kutekeleza Mradi wa ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme wa Stiegler's Gorge, mradi utakaozalisha umeme MW 2,100 kutokana na maji.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo umeainisha Miradi ya kielelezo itakayotekelawa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19, ambayo ni muendelezo wa utekelezaji wa Miradi ya mwaka 2017/18, Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

#### **4.3.1. Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma na Kiwanda cha kufua chuma cha Liganga**

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchumana na kiwanda cha kufua chuma cha Liganga umesuasua kwa muda mrefu. Moja ya sababu iliyokuwa ikisababisha kutotekelezwa kwa mradi huu ilikuwa ni kukosekana kwa makubaliano ya bei ya kuuziana umeme utakaozalishwa (MW 350) baina ya Serikali na mwekezaji. Kamati inaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuondoa changamoto hii kwa kuruhusu mwekezaji kuzalisha MW 250 kwanza ili zitumike kwenye kiwanda cha kuzalisha chuma cha Liganga na kuachana na mpango wa awali wa Serikali kununua MW 350, hii itasaidia sasa, mradi kuanza kutekelezwa katika mwaka 2018/19.

#### **4.3.2. Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi (EPZ/SEZ)**

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kuanzishwa kwa Kanda Maalum za Uchumi ni kurahisisha upatikanaji wa maeneo ya uzalishaji na uendeshaji biashara, ambapo kwa mwaka 2018/19 kipaumbele kimewekwa katika kuharakisha utekelezaji wa kanda zilizoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (5) (2016/17 – 2020/21), kanda hizo ni zifuatazo; eneo maalum la uwekezaji la Bagamoyo; Maeneo Maalum ya uwekezaji Kigoma Mtwara na Ruvuma pamoja na kituo cha Viwanda cha Kurasini (*Industrial Park*). Taarifa ya Serikali inaeleza kuwa, kanda hizi bado ziko kwenye hatua ya ukamilishaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi watakao pisha miradi hiyo, upatikanaji wa hati miliki za maeneo husika na ujenzi wa miundombinu wezeshi. Ni maoni ya Kamati kuwa, kukamilika kwa miradi hii muhimu kutaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na hasa kwa kipindi hiki ambacho nchi yetu ipo kwenye mageuzi ya kuelekea katika uchumi wa viwanda.

#### **4.3.3. Kituo cha Viwanda cha Kurasini**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulianzishwa kwa lengo la kuimarisha ushirikano wa kibashara kati ya Tanzania na

Mataifa mengine, kuititia uwekezaji katika miundombini ya biashara na ujenzi wa viwanda. Mapendekezo ya Mpango yanaonyesha kuwa, awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu itahusisha ujenzi wa kituo cha biashara cha kisasa kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi na awamu ya pili itahusisha ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona Serikali haijaweka mikakati thabiti ya utekelezaji wa mradi huu. Hii inajidhihirisha wazi kwakuwa hadi sasa bado ulipaji wa fidia haujakamilika. Pamoja na changamoto hiyo ya ulipaji fidia, ni matumaini ya Kamati kuwa Mradi huu utaanza kutekelezwa katika mwaka 2018/19 na ujenzi wa viwanda vitakavyotumia malighafi za nchini utaanza mapema iwezekanavyo.

#### **4.3.4. Bomba la Mafuta (Hoima Uganda – Chongoleani – Tanga, Tanzania)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanikiwa kuingia mkataba na nchi ya Uganda katika ujenzi wa bomba la mafuta litakalotoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani Tanga, Tanzania. Ujenzi wa Bomba hili utachochaea sana maendeleo kwa kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja wakati wa ujenzi wake na Serikali itapata kodi mara litakapokamilika na kuanza kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa mradi huu muhimu, hii ikiwa ni pamoja na kujenga ‘marine export terminal’ katika Bandari ya Tanga, na kuwajengea uwezo wataalam wa ndani ili waweze kusimamia mapato kutoka Bandari hiyo.

#### **4.3.5. Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kudhamiria kutekeleza mradi huu ambaou upo katika Mpango wa SAGCOT. Lengo la mradi huu ni

kuzalisha tani 230,000 kwa mwaka ambapo mpaka sasa ekari 320 zimeshapandwa miwa na ujenzi wa majengo ya kiwanda cha sukari unaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu utakuwa mkombozi mkubwa kwa nchi yetu na utasaidia sana kupunguza na ikiwezekana kumaliza changamoto ya upatikanaji wa sukari nchini. Ni matumaini ya Kamati kuwa mradi huu utazalisha pia sukari ya viwandani ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa sukari ya viwandani, na kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza sukari nje ya nchi na kudhibiti upotevu wa mapato.

#### **4.3.6. Kiwanda cha Mbolea**

**Mheshimiwa Spika**, Kumekuwepo na mazungumzo ya muda mrefu kuhusu ujenzi wa kiwanda cha Mbolea, Mtwara kutohakana na umuhimu wa kiwanda hichi ambacho kitakuwa soko la gesi inayozalishwa nchini na mkombozi wa wakulima, Kamati inaishauri Serikali ione umuhimu wa kukiweka kiwanda hiki katika mpango wa maendeleo wa Taifa ujao.

#### **4.4. Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha za kutosha za kutekeleza miradi ya maendeleo kama inavyokuwa imeainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Serikali imeainisha kuwa itagharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/19 kwa kushirikisha washirika wa maendeleo na sekta binafsi kwa utaratibu wa ushirikiano wa mfumo wa '*Public Private Partnership*' (PPP). Kamati ingependa kurudia mapendekezo yake ambayo imekuwa ikiyatoa miaka iliyopita ya kuiandaa vya kutosha Sekta Binafsi kwa kuweka mazingira wezeshi na kuainisha miradi ambayo Sekta Binafsi inaweza kushirikiana na Serikali katika kipindi husika. Aidha, Kamati inasisitiza kwamba bajeti ya 2018/19

itakayowasilishwa Bungeni iainishe wazi mchango wa Sekta Binafsi katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

#### **4.5. Maoni ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maoni na ushauri huu uliojikita katika maeneo mahsus, Kamati ingependa kutoa maoni ya jumla yafuatayo;

**4.5.1.** Serikali ielekeze nguvu zaidi katika kutumia vema rasilimali yake ya gesi asilia katika kuendesha shughuli zake za kiuchumi hasa viwanda na upatikanaji wa umeme nchini. Hii itasaidia sana kupunguza “Import Bill” ya uagizaji wa mafuta kutoka nje.

**4.5.2.** Kamati inapongeza Serikali kwa usimamizi na ufanisi katika Sekta ya madini katika kuhakikisha inapata mapato stahiki. Kamati inashauri Serikali kuimarisha usimamizi kwenye sekta hiyo kuitia kuwawezesha wachimbaji wadogo ili wawe na mchango katika sekta hiyo na kusaidia kuongeza mapato ya kigeni.

**4.5.3.** Serikali iweke mikakati ya makusudi katika kusimamia mwongozo wa kupunguza ukuaji na ulipaji wa Deni la Taifa linaloongezekwa mwaka hadi mwaka pamoja na kwamba Deni hilo kwa sasa linaonekana kuwa ni himili;

**4.5.4.** Serikali iweke mkakati madhubuti wa upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati ili kusaidia wakulima kupata mazao yanayostahiki. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa ruzuku za pembejeo zinazotolewa ziwe za kitaifa ili kuwepo na urahisi wa upatikanaji wa pembejeo hizo katika maduka mbalimbali kwa bei elekezi;

**4.5.5.** Kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Serikali itafute masoko mbadala ya zao la Mbaazi ambalo bei imeshuka kutokana na nchi ya India ambayo ilikuwa mnunuzi mkubwa kusitisha ununuzi wa bidhaa hiyo kutoka nje, isipokuwa kwa nchi zenyenye mkataba na taifa hilo tu.

**4.5.6.** Kamati inashauri Serikali kuleta mkakati wa kitaifa utakaosaidia kupunguza ongezeko la watu nchini ili ongezeko hilo liendane na ukuaji wa uchumi na maendeleo ya huduma za jamii. Takwimu za Shirika la UNICEF zinaonesha kuwa ifikapo mwaka 2050 Tanzania itakuwa na watoto wenye umri chini ya miaka 18 wapatao milioni 58 hivyo kuleta jumla ya watu million 108;

**4.5.7.** Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ishirikiane na Sekta binafsi kuanzisha minada ya mazao ya biashara kama vile Chai ili kurahisisha upatikanaji wa soko kwa wakulima wetu. Aidha, Serikali iwashawishi wafanyabiashara binafsi kuwekeza katika sekta ya kilimo kwa madhumuni ya kuanzisha mashamba ya kibiashara (commercial farming);

**4.5.8.** Kamati inatambua umuhimu wa kuwa na takwimu sahihi katika kuwasaidia wananchi kujua masuala mbalimbali yanayoendelea nchini. Kutokana na kutokuwepo kwa takwimu sahihi Kamati inashauri kwamba ni wakati muafaka kwa Serikali kuwa na takwimu zinazoshabihiana tofauti na hali ilivyo hivi sasa;

**4.5.9.** Kamati inashauri Serikali kuweka mpango wa usimamizi na uvunaji wa rasilimali misitu (*forest harvesting*) na bahari (*Deep Sea Fishing*) kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kwa lengo la kuongeza mapato ya nchi;

**4.5.10.** Pamoja na jitihada za Serikali za kununua ndege ili kuimarisha utalii, bado Kamati inashauri Serikali kuendelea kuvutia watalii zaidi kwa njia mbalimbali ikiwemo matangazo ili kuongeza pato la kigeni kutoka sekta hiyo;

**4.5.11.** Serikali ikamilishe haraka Mpango wake wa Kurasimisha Biashara na Mali (MKURABITA) za watu wenye kipato cha chini ili kuziongezea thamani, kuwawezesha waweze kukopa katika taasisi za kifedha hatimaye kusaidia Serikali kukusanya mapato stahiki. Aidha, Serikali za Mitaa zishirikishwe kwa karibu kuwatambua.

**4.5.12.** Serikali iandae Sera itakayopunguza utumiaji wa fedha taslim ili kuongeza mapato ya Serikali kwa kutumia vitambulisho veya Taifa katika kila eneo. Serikali iharakishe kuweka utaratibu utakaowezesha matumizi ya kadi (*cashless payment system*) na kupunguza matumizi ya fedha taslim katika miamala. Hii itapunguza ulazima wa watu kukaa na fedha nyingi kwa wakati mmoja na kuboresha mzunguko wa fedha katika uchumi.

**4.5.13.** Serikali iboreshe ufanisi wa mashirika ya umma, kwani ni dhahiri kuwa Serikali imekuwa ikipoteza Mapato yake inayokusanya kwa kugharamia mashirika yanayojiendesha kwa hasara; Pale inapowezekana sekta binafsi iingie ubia na mashirika haya ili yaweze kuijendesha kwa faida.

**4.5.14.** Serikali iboreshe mfumo wa ukusanyaji wa kodi na tozo kwa kuimarisha mfumo wa matumizi kwa njia za kielektroniki ili kurahisisha ukusanyaji wa tozo na kodi mbalimbali, pamoja na kuboresha ubadilishanaji wa taarifa kati ya taasisi za umma ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato;

**4.5.15.** Serikali iendeleteze kwa kasi zoezi la utoaji wa hati miliki za kimila na kukusanya kodi ya ardhi;

**4.5.16.** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza ufanisi katika bandari ya Dar es salaam, Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuendeleza ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo haraka iwezekanavyo ili meli kubwa Zaidi za kisasa ili ziweze kutia nanga katika hiyo.

**4.5.17.** Serikali izitake Benki za Biashara kupunguza mikopo chechefu kwa kuwachukulia hatua za Kisheria wadaiwa sugu ili waweze kurejesha mikopo hiyo kwa haraka.

**4.5.18.** Pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kuchukua hatua za kupunguza riba ya mikopo inayotoa kwa Benki za Biashara (*discount rate*) kutoka asilimia 16 hadi asilimia 12 na kupunguza kiwango cha amana ambacho

benki za biashara hutakiwa kuhifadhi Benki Kuu kama dhamana (*Statutory Minimum Reserve Requirement* – SMR) kutoka 10% hadi 8%. Kamati inaishauri Serikali kuititia Benki Kuu kufanya utafiti wa hatua za ziada za kuchukua ili kuchochea ujazi wa fedha katika mzunguko wa sarafu.

## 5.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkitupatia Wabunge. Namshukuru Mhe. Dkt. Philip I. Mpango, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Mb Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mwongozo kwa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2018/19.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu masuala hayo mawili muhimu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

- |                                       |              |
|---------------------------------------|--------------|
| 1. Mhe. Hawa A. Ghasia, Mb            | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb  | - Mjumbe     |
| 3. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb           | - Mjumbe     |
| 4. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb       | - Mjumbe     |
| 5. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb  | - Mjumbe     |
| 6. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb      | - Mjumbe     |
| 7. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb       | - Mjumbe     |
| 8. Mhe. Augustino Manyanda Masele, Mb | - Mjumbe     |
| 9. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb      | - Mjumbe     |
| 10. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb    | - Mjumbe     |
| 11. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb     | - Mjumbe     |
| 12. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb     | - Mjumbe     |
| 13. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb       | - Mjumbe     |

14. Mhe. Susana Chogisasi Mgonukulima, Mb -Mjumbe
15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb - Mjumbe
18. Mhe. David Ernerst Silinde, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Jitu V. Soni, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Abdallah Bulembo, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Andrew John Chenge, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Dalaly Peter Kafumu, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Mussa A. Zungu, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Hawa A. Ghasia, Mb  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**  
07 Novemba, 2017

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Tunaendelea, sasa namkaribisha Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni aweze kuleta maoni ya kambi hiyo. (*Makofî*)

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee, napenda kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote niseme tu kwamba, hotuba yetu yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo kwa sababu ni ndefu kidogo na ina kurasa 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maoni kuhusu Mapendekezo ya Mpango, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kusema kwamba; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Watanzania wote wanaopenda kuona haki ikitamalaki katika Taifa, tunalaani na kupinga vitendo viovu nya uonevu, ukandamizaji, utekaji na sasa majaribio ya mauaji yanayofanywa dhidi ya wanachama na viongozi wa vyama nya upinzani hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa vitendo hivi vitaachwa viendelee bila kukemewa na kushughulikiwa kwa uzito unaostahilli, kuna hatari ya kundi linalohisi kuonewa likakosa uvumilivu na hivyo kuathiri amani ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miezi miwili sasa tangu Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Tundu Lissu anusurike kifo baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi wakati Mkutano wa Nane wa Bunge ukiwa unaendelea na vikao vyake hapa Dodoma. Mpaka sasa hakuna taarifa rasmi ili yotolewa na Serikali juu ya kukamatwa kwa watu waliohusika na tukio hilo. Ikiwa polisi wameshindwa kufanya uchunguzi na kuwakamata wahalifu hao ndani ya miezi miwili, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni muujiza wowote unaoweza kutendeka ili watu hao wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo nya sheria hata kama polisi wataongezewa miezi miwili mingine. Tafsiri ya ukimya huo wa Serikali ni rahisi tu kwamba hakuna dhamira ya dhati wala utayari wa kushughulikia jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si nia yangu kuorodhesha matukio mabaya wanayofanyiwa viongozi wa upinzani hapa nchini kwa kuwa ni mengi na pia tumeyasemea sana humu bungeni na wakati mwingine kuamriwa kuyafuta katika hotuba zetu, lakini hili la kuanza kutuwinda kwa lengo la kutuuwa, hatuwezi kamwe kulinyamazia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatao wito kwa wananchi wote kupaza sauti zao kipinga uonevu na ukandamizaji wa haki, kipinga matukio ya utekaji, utesaji na umwagaji damu katika nchi. Aidha, tunatoa wito kwa waumini wa dini na madhehebu mbalimbali kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu awaponye wale wote walioathirika na matukio haya, lakini zaidi kuliepusha Taifa na laana kwa damu ya watu wasio na hatia iliyomwagika katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mpango huu wa Maendeleo tunaoujadili leo uweze kufikia malengo yaliyokusudiwa, ni lazima tuutekeleze tukiwa na umoja na mshikamano kama taifa. Kamwe haitawezekana kuyafikia hayo maendeleo tunayotaka kwa kubaguana kwa itikadi za kisiasa au kwa kubezana, kunyanyasana, kuoneana, kuumizana ama kuuana. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa viongozi wote katika ngazi mbalimbali kuitunza na kuilinda amani ya nchi yetu kwa kutenda haki, kuacha mara moja tabia ya ubaguzi, uonevu, ukandamizaji na unyanyasaji dhidi ya watu tunaowaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya hotuba yetu inahusu uwajibikaji mdogo wa Serikali katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa. Hii mnaweza mkaisoma katika hotuba yetu kama ambavyo tumeiandika, sitaisoma kwa sababu ya muda, nahitaji kusoma baadhi tu ya maeneo na sehemu ya tatu, kwa hiyo nakwenda sehemu ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya hoja zilizoibuliwa na Kambi ya Upinzani Katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka wa fedha 2017/2018, mwaka huu ambao tunaendeleanao hivi sasa. Wakati tunajadili Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kambi Rasmi ya Upinzani iliibua baadhi ya changamoto katika maeneo mbalimbali na kuitaka Serikali kufanya kazi baadhi ya maeneo hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza tulioibua; ajira na hali ya uchumi wa wananchi. Kambi Rasmi

ya Upinzani iliipinga Serikali kwa kitendo chake cha kusitisha ajira kwa kigezo kuwa inafanya uhakiki kwa watumishi ili kupambana na tatizo la watumishi hewa. Sababu kubwa ya kuipinga Serikali ni kwamba zoezi hili lilipelekeea kuyumba kwa uchumi kwa baadhi ya familia ambazo zilikuwa na watu wenye sifa ya kuajiriwa katika sekta ya umma kama vile walimu, wauguzi na madaktari. Kusimamishwa huku kwa ajira kulisababisha nguvu kazi iliyokuwa na uwezowa kuzalisha kuishi kama omabaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ajira ni nyenzo muhimu ya kipato na uchumi kwa wananchi; na kwa kuwa fursa za ajira binafsi nazo zimekuwa na changamoto nyingi kutokana na ukosefu wa mitaji unaotokana na hali duni ya uchumi, kwa maana ya umaskini; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua, safari hii Serikali imeweeka mkakati gani katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, msukosuko kwa wafanyabiashara wakubwa. Katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018 Kambi Rasmi ya Upinzani iliipinga kitendo cha Serikali kuwanyanyasa wafanyabiashara wakubwa kwa kukamata mali zao na hata kufunga akaunti zao bila kutoa sababu za msingi hali iliyopelekeea kuyumba kwa uchumi na kupungua kwa mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ilieleza bayana kwamba haipingi kuchukuliwa kwa hatua za kisheria kwa wafanyabiashara wakubwa wanaokiuka sheria za nchi au kuhujumu uchumi, lakini inapinga Serikali kutumia madaraka yake ya kidola kuwanyanyasa wafanyabiashara, kwani kwa kufanya hivyo itawavunja moyo wawekezaji hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kulieleza Bunge hili kwamba safari hii imeweeka mikakati gani katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2018/2019 kuboresha mazingira ya biashara nchini ili kuwavutia wawekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu tulijadili mikopo katika sekta ya kilimo. Kambi ya Upinzani pia ilipinga uamuzi wa Benki Kuu kuzuia baadhi ya benki kukopesha wakulima kwa madai kwamba mikopo katika sekta ya kilimo huwa haina uhakika wa kurudi. Hoja kuu ni kwamba mikopo ya kilimo inahitaji muda mrefu hivyo inatakiwa kubuni utaratibu maalum wa kuziwezesha benki za biashara kuweza kutoa mikopo hiyo na si kusema haina uhakika wa kurudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiishauri Serikali kuweka jicho lake katika sekta ya kilimo kwa kuwa sekta hiyo ndiyo inayotoa ajira kwa Watazania zaidi ya asilimia 70. Tulishauri sekta hiyo iongezewe bajeti hususan bajeti ya maendeleo, tulishauri Serikali itoe ruzuku kwa pembejeo za kilimo na kutafuta masoko kwa mazao ya kilimo ili kukuza sekta hiyo. Hata hivyo, mara zote mapendekezo hayo yamekuwa yakipuuzwa na matokeo yake sekta ya kilimo kuendelea kudorora mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiishauri Serikali kuweka jicho lake katika sekta ya kilimo kwa kuwa sekta hiyo ndiyo inayotoa ajira kwa watazania zaidi ya asilimia 70. Tulishauri sekta hiyo iongezewe bajeti hususan bajeti ya maendeleo, tulishauri Serikali itoe ruzuku kwa pembejeo za kilimo na kutafuta masoko kwa mazao ya kilimo ili kukuza sekta hiyo. Hata hivyo, mara zote mapendekezo hayo yamekuwa yakipuuzwa na matokeo yake sekta ya kilimo kuendelea kudorora mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili juu ya mkakati wake wa kuboresha sekta ya kilimo katika maeneo ya mikopo kwa wakulima ya muda mrefu na riba nafuu, ruzuku ya pembejeo za kilimo na masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ni kuhusu kupungua kwa mapato katika sekta ya utalii. Kambi Rasmi

ya Upinzani ilitoa angalizo la kupungua kwa mapato katika Sekta ya Utalii kutokana na kitendo cha Serikali kuanzisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye huduma zote za kitalii. Tulieleza kuwa kodi hiyo badala ya kuwa kivutio itakuwa kizingiti kwa watalii wanaokuja kuitembelea nchi yetu na hivyo kuathiri hoteli zilizokuwa zinafanya biashara ya utalii pamoja na makampuni yaliyokuwa yakijihuisha na biashara ya utalii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tathmini ya ukuaji wa sekta ya utalii kabla na baada ya kuanzisha *VAT* katika sekta hiyo ili thamini hiyo itoe dira ya namna bora ya kuongeza mapato katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ni kuhusu kodi ya majengo na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Katika mambo ambayo tulipingga Serikali kwa nguvu ni uamuzi wake wa kuziondolea Serikali za Mitaa Mamlaka yake ya kikatiba ya kukusanya kodi za majengo na kupeleka jukumu hilo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Sababu ya kuipinga Serikali ilikuwa wazi, kwamba Serikali za Mitaa zilitegemea sana kodi hiyo kuijendesha na kugharamia miradi ya maendeleo katika Halmashauri husika na kwamba baada ya kuondolewa kodi hiyo, zimeathirika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, *TRA* imeweza kukusanya fedha kiasi gani kutokana na kodi ya majengo, tofauti na zile zilizokusanywa na halmashauri zenyewe. Aidha, katika kiasi kilichokusanywa na *TRA*, ni asilimia ngapi zimepelewa katika halmashauri ili kuzisaidia halmashauri hizo kuijendesha na pia kupunguza gharamia ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita tumejadili kuhusu sera ya elimu bure. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitoa angalizo kwa Serikali kufanya tathmini ya mahitaji kwanza (*assessment of needs*) na kuandaa mpango wa utekelezaji (*implementation plan*) ili kuweka mazingira mazuri

ya kutekeleza sera ya elimu bure. Tulifanya hivyo kwa nia njema kwa kuwa tulijua haukuwa mpango wa CCM kutoa elimu bure na kwa sababu hiyo Serikali haikuwa na mpango au maandalizi yoyote ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utekelezaji ni kitu ambacho hakina mpango wa utekelezaji ni kwamba hali katika shule za umma imekuwa mbaya sana kutokana na Serikali kushindwa kupeleka fedha za kutosha katika uendeshaji wa shule hizo na hivyo kufanya suala zima la elimu ya msingi na sekondari kuwa katika hali mbaya na huenda baada ya muda mfupi ujao shule hizi zikafungwa kutokana na kukosekana kwa fedha za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda sana watoto wa Kitanzania wasomeshwe bure na Serikali, lila inataka kuwe na mpango endelevu wa kufanya hivyo na si kuchangishana kila uchwao kama inavyofanyika kwenye harusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishuhudia watu wakichangishwa kwa ajili ya madawati, ujenzi wa maabara na kadhalika. Hata hivyo hali hiyo haiwezi kuwa endelevu kwa kuwa anaweza akaja kiongozi mwingine ambaye hana karama ya uchangishaji na hivyo kufanya mpango huo kukwama. Kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kulieleza Bunge hili, imeweka mkakati gani wa kutengeneza mpango wa utekelezaji wa sera ya elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu walikuwa 20,183 huku wanafunzi 27,053 wakikosa mikopo ya elimu ya juu katika vuyo vikuu mbalimbali hapa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani ilishangazwa na tukio hilo kwani Rais aliwaahidi Watanzania wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 kuwa hakuna mwanafunzi wa elimu ya juu atakayekosa mkopo na kwamba yeze atakuwa mwarobaini wa tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mikopo ya elimu ya juu halitokani na nani anakalia kiti cha urais ila linatokana na ukosefu wa mpango wa mikopo (*higher learning loan scheme*). Kungekuwa na *higher learning loan scheme* kusingekuwa na matukio ya wanafunzi kuchaguliwa kuijunga vyuo vikuu halafu wakose mikopo kwa sababu *scheme* ingechukua wale ambao inaweza kuwakopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki ya kumchagua mwanafunzi kuijunga chuo kikuu kama inajua haiwezi kumkopesha, vinginevyo utaratibu wa mikopo ufutwe ili kusiwe na ubaguzi (*double standard*) katika kuwashudumia wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza commitment yake katika kuandaa *higher learning loan scheme* katika mpango wa maendeleo wa mwaka 2018/2019 ili kuondokana na tatizo la wanafunzi wa elimu ya juu kukosa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano tulizungumzia hali ya uchumi wa Taifa, ni ndefu kwa sababu sehemu ndogo ya kwanza tumejadili hali ya uchumi wa Taifa na sehemu ya pili tumejadili gharama za maisha na pato la mtu mmoja mmoja. Haya yote yapo katika hotuba yetu, nafikiri yatasomwa kila mmoja kulingana na nafasi na kwa sababu hotuba ni ndefu kidogo, baadhi ya maneno nimeacha. Sehemu ya tatu ni uchumi wa gesi ambayo nitaisoma kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya hivi karibuni Serikali imekuwa ikiwaaminisha Watanzania kwamba ifikapo Mwaka 2025 Tanzania itakuwa ni nchi ya uchumi wa gesi kwa tafsiri pana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia Mwongozo wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2018/2019 haioneshi kwa uwazi mkakati au hatua madhubuti kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa gesi asilia ni lazima maandalizi ya kutufikisha huko yaanza kuanzia sasa kwenye mipango yetu ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelazimika kuhoji, baada ya kupitia taarifa ya Serikali inayohusu uendelezaji wa miradi ya gesi asilia nchini inayoteklezwa kati ya *Pan African Energy Tanzania*, *TPDC*, *Songas* na *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa hiyo ambayo inaonesha ushiriki wa kila kampuni katika mradi huo Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu, hivi kama Serikali inatangaza zabuni za kutekeleza miradi yake, maana yake ni Serikali kupoteza umiliki wa miradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Songas ilikuwa ni kampuni ya ubia ya kutekeleza mradi, *Pan African Energy* ilikuwa ni kampuni ya uendeshaji wa visima vya gesi ambavyo tayari vilikuwepo. Sasa inakuwaje kampuni zinazofanya kazi za uendeshaji mara nazo zinakuwa wamiliki wa gesi hiyo, nazo zinaiuzia *TANESCO* gesi kwa be ya soko wakati *TANESCO* ni mmiliki kwa ubia wa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na Kamati Ndogo iliyoongozwa na Mheshimiwa Selemani Zedi katika Bunge liliopita, kuwa hatuwezi kuingia katika uchumi wa gesi hadi pale mikataba iliyoingiwa kati ya *TPDC* na *TANESCO* kwa niaba ya Serikali, pamoja na makampuni ya *Songas* ambayo ni kampuni ya ubia kati ya *CDC Globaleq* ya Uingereza, Benki ya Maendeleo ya Uhlanzi (*FMO*) na *Tanganyika Development Finance Company Limited (TDFL)* kwa upande mmoja, na upande wa pili mkataba kati ya Serikali, kwa maana ya *TPDC* na *TANESCO* na Kampuni ya *Pan African Energy*; aidha mikataba kati ya *Songas* na *Pan African Energy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema kinyume cha hapo hizi tambo ambazo tuliambiwa humu ndani ya Bunge kuwa sasa gesi imegunduliwa nyangi ya kutosha, jambo ambalo ni sahihi,

Iakini bila kuititia upya mikataba ya uendeshaji ambayo imejigeuza kuwa mikataba ya umiliki kwa Serikali kupoteza haki ya umiliki itakuwa ni shida kwa vizazi vijavyo, na sisi Waheshimiwa Wabunge tutaonekana kuwa ndio tuliuza nchi yetu. Hii ni kwa sababu jukumu letu ni kuvisimamia na kuishauri Serikali pale mambo yanapokuwa si sawa sawa.

Meshimiwa Spika, Kambi Rasmi inapenda kufahamu kuhusu utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati ya Bajeti iliyongozwa na Mheshimiwa Andrew Chenge kuhusu mapato ya gesi kama ilivyowasilishwa Bungeni, mwezi Februari, 2013. Naomba kunukuu; "Serikali ifanye maamuzi ya kutumia gesi hii kama chanzo cha mapato sasa hivi kwa kuweka dhamana kiasi kidogo cha gesi hii."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kiasi kilichogunduliwa sasa hivi katika kina kirefu baharini ni futi za ujazo trilioni 32 ambazo ni sawa na mapipa bilioni sita ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bei ya sasa gesi hii ina thamani ya dola za kimarekani bilioni 660. Iwapo mgao wa Serikali ni angalau 10% na Serikali ikaamua kutumia 10% ya mgao wake kama dhamana au mauzo ya mbele (*collateral or forward sale*), ingesaidia sana katika utekelezaji wa mpango wa miradi ya maendeleo pamoja na bajeti ambayo imekuwa ikisucasua kutokana na kutokuwa na vyanzo vya uhakika kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya sekta binafsi na uchumi wa nchi; sekta binafsi nichini zinapitia katika wakati mgumu sana kutokana na hali ngumu ya uchumi iliyopo sasa, mfumo wa kibiashara usiotabirika, wingi wa kodi na utaratibu usiofaa wa ukusanyaji kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ukusanyaji kodi kuititia *TRA* umekuwa na kero kubwa kwa wafanyabiasha kutokana na mamlaka hiyo kutokuwa na mfumo bora wa ukusanyaji kodi kwani mfanyabiasha mmoja anaweza kutembelewa na timu tofauti tofauti za *TRA* zikiwa na

makadirio ya viwango vya kodi vinavyotofautiana. Jambo hili limekuwa kero kubwa sana kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi pia imekumbwa na tatizo kubwa la kutokukopesheka kutokana na hali mbaya ya kifedha katika mabenki na taasisi nyingine za fedha. Hali hii inajidhihirisha kwani katika kitabu cha Mwongozi wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019 ukurasa 40; unazungumzia kutetereka kwa rasilimali za benki kutokana na kuongezeka kwa mikopo chechelu kutoka asilimia 8.9 Juni, 2016 mpaka 10.6 mwezi Juni, 2017. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 1.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wengi wameuziwa mali zao kutokana na kushindwa kurejesha mikopo na hivyo wengi kujikuta kwenye lindi kubwa la umasikini, fedheha na msongo wa mawazo ambao unaongeza idadi kubwa ya Watanzania wanaokumbwa na matatizo ya akili kwa sasa (*mental distress*).

Pamoja na hilo Serikali hii haioneshi uwezo katika kuziwezesha sekta binafsi kukua ili ziweze kuipunguzia Serikali mzigo mkubwa wa mamilioni ya Watanzania wasio na ajira. Katika kipindi hiki cha Serikali Watanzania wengi wamepoteza ajira Serikalini, viwandani na hata katika biashara za watu binafsi kuliko kipindi kingine chochote kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo zile za waliokaza sifa za kitaaluma, chuki za kisiasa zilizopelekea wengine kuathirika na sakata hili la upotevu wa ajira, wafanyabiashara kufunga biashara zao au kupunguza wafanyakazi kutokana na kushindwa kumudu gharama za uendeshaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kushuka kwa mapato ya kampuni mbalimbali yakiwemo makampuni ya simu, viwanda vya vinywaji, madini, vyombo vya habari, taasisi za kifedha, nyumba za starehe yakiwemo mabaa na hoteli, makampuni ya kitalii, maduka ya biashara ndogo ndogo yaliyokuwa yanaajiri wafanyakazi chini ya watano, lakini k Kutokana na hali ya uchumi idadi hiyo imeshuka zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imepunguza kabisa kufanya biashara na sekta binafsi kama mnunuzi mkuu wa bidhaa na huduma zinazotoka sekta binafsi. Hii ikiwa na maana kwamba kitendo cha Serikali kuwaagiza wakala kuwa taasisi za umma zipewe kipaumbele katika biashara; yaani Serikali kufanya biashara baina ya yenye kwa yenye kwa nia ya kubana matumizi ni mfano wa kuhamisha taasisi zake kutoka kwenye taasisi binafsi za kifedha na kuzirudisha Benki Kuu, biashara ya usafirishaji, huduma za mahoteli na kadhalika. Ni wazi kuwa mfumo huo unakwenda kuangamiza sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kudhani kwamba kusitisha biashara baina ya taasisi zake na sekta binafsi ni kukata mirija ya ubadhirifu au ufujaji wa fedha za umma si dhana yenye uhalisia. Kukwepa kufanya biashara na sekta binafsi maana yake ni kuua sekta binafsi ambayo hutoa ajira kwa maelefu ya watanzania. Pale ambapo Serikali inalemewa na wimbi la watu wasio na ajira sekta binafsi huchukua jukumu hilo. Pamoja na hayo, sekta binafsi inachangia mapato ya Serikali kuitia kodi inayokusanywa kwenye bidhaa (*income tax*) na na kodi ya waajiriwa (*payee*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi iliyowahi kufanikiwa kiuchumi bila kuruhusu ushindani wa kibiashara. Uchumi unakuwa kutokana na kukua kwa soko la kibiashara linalozingatia ushindani ambapo Serikali na sekta binafsi wote ni wadau. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha ili biashara baina ya sekta binafsi na Serikali ifanyike kwa weledi ni kuhakikisha sheria zilizopo zinazingatiwa na kuimarisha mifumo ya kudhibiti rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuchukua wajibu wake wa msingi wa kusaidia na kuziimarisha sekta binafsi ili ziweze kuwa na mchango mkubwa kwenye kuinua uchumi wa nchi. Vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka kuacha tabia ya kuwatishia wafanyabiashara, kufunga makampuni ya wafanyabiashara kiholela kwani kwa kufanya hivyo wanaoumia ni Watanzania maskini wanaotegemea

kuendesha maisha yao kupitia makampuni hayo. Kuna msemo usemao wapiganapo tembo ziumiazo nyasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Serikali haina budi kutatuta changamoto zilizopo kwa wawekezaji na wafanyabiashara wa sekta binafsi badala ya kufanya kazi kwa jazba, kwa kutumia vyombo vyaa dola, kuwaumiza na kuwadhalilisha wawekezaji na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita ni kuhusu uchumi wa viwanda. Uchumi wa viwanda ni maandalizi mtambuka na Wizara ya Viwanda na Biashara ndiyo inayotakiwa kutoa dira au mwongozo wa jinsi gani yakufika huko. Katika hili Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aweke wazi mpango mkakati wake hasa wa jinsi rasilimali watu (*skilled labour*) itakavyopatikana na kutosheleza Tanzania ya viwanda. Kwa mfano, wakati wenzetu Kenya wanajenga reli ya *standard gauge*, Serikali yao ilipeleka Wakenya wasiopungua 30 kwenda kujifunza utaalam mbalimbali kuhusiana na uendeshaji wa treini hizo za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ya viwanda, ndoto au uhalisia? Katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Viwanda na Biashara na hotuba ya bajeti mbadala tulieleza kwa undani mashaka yetu kuhusu ndoto ya Tanzania ya Viwanda pamoja na hatua zinazochukuliwa kutekeleza uchumi wa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulieleza kuwa ili Tanzania ifikie uchumi wa kati ni lazima sekta ya uzalishaji ichangie katika Pato la Taifa kwa asilimia 40 ifikapo mwaka 2020/2025. Katika hali ya kushangaza sekta hiyo inachangia asilimia 5.2 pekee. Ni wazi kuwa kwa takwimu hizi hakuna uhalisia wa kuelekea uchumi wa kati wa viwanda isipokuwa propaganda ambazo zinapigwa kila mara bila kuzingatia uhalisia wa hali tuliyo nayo kwa sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Mapendekizo ya Mpango ukurasa wa 26 hadi 29, hapa ndipo

kuna kitu kinachoitwa kупingana kwa takwimu. Serikali imenorodhesha viwanda 50 ambavyo kati ya hivyo viwanda 32 vimekamilika na kuanza uzalishaji na viwanda 18 bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa sherehe za kitaifa za kuzima mwenge tarehe 14 Oktoba, 2017 Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania alinukuliwa akisema kuwa mwenge umezindua viwanda 148 ambapo viwanda hivyo vimejengwa kwa thamani ya shilingi bilioni 468 ambapo ajira 13,000 zimepatikana, wakati kwenye Mpango ni viwanda 50. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoja juu utofauti wa takwimu ambazo zimetolewa na Mkuu wa Nchi na ambazo zimeoneshwa katika Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019. Je takwimu halisi za viwanda ni zipi? Kwa hiyo, tunahitaji kufahamu hilo jambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Oktoba, 2017 Waziri wa TAMISEMI amenukuliwa na vyombo vy'a habari akielekeza kila Mkoa kujenga viwanda 100 ambapo mpaka Disemba, 2018 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara itatakiwa kuwa na viwanda 2600.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangazwa na maelekezo haya, hii ni kwa sababu kama mikopo kwa sekta binafsi imepungua kama Serikali inavyokiri na kama Serikali haifanyi biashara, hivyo viwanda vinaenda kujengwa na nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haitakaa chini na wafanya biashara na wadau wa sekta binafsi kuhusu namna ya kutekeleza maelekezo haya kutakuwa na matatizo makubwa huko mbele kwa sababu mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi yameshuka, mikopo kwa sekta binafsi iko taabani, soko la ndani limeyumba kutokana na watu kushindwa kununua bidhaa, mzunguko wa fedha umeshuka,

pamoja na mzigo wa kodi kutoka Serikalini. Kwa hiyo hili inatakiwa liangaliwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwemnyekiti, Deni la Taifa. Deni la Taifa ni kati ya nyenzo muhimu katika kurekebisha thamani ya sarafu na hivyo kuimarisha uchumi wa nchi. Katika kufanya hivyo ni muhimu kuwa na sera makini za fedha katika kuhakikisha deni hilo linaleta malengo tarajiwa katika uchumi. Kama deni au mikopo itatumwa vibaya inaweza kuwa balaa kubwa kwa nchi badala ya kuwa baraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia Juni, 2017 Deni la Taifa lilifikia dola za Marekani milioni 26,115.5 sawa na shilingi za Kitanzania trillioni 60.287 kwa kutumia kiwango cha ubadilishaji wa fedha cha sasa. Ukiilinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka 2016 lilikuwa dola za Marekani 22,320.76 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo inayokopwa kwa shughuli za kiuchumi ni ya aina mbili, mikopo ya riba nufuu na mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwneyekiti, katika wasilisho letu Kambi Rasmi ya Upinzani iliuliza ni kwanini Serikali inakopa mikopo ya kibiashara? Kwa kuwa ili nchi ipate mikopo yenye riba nafuu ni lazima kwanza ifanyiwe tathmini (*credit rating*) kuangalia kama inakidhi vigezo. A *credit rating* is an evaluation of the credit risk of a prospective debtor. Kwa hiyo, itasomwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde naomba uhitimishe.

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo naomba hotuba yetu yote ya kurasa 50 iingie kama ilivyo na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofii*)

**HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO  
MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (MB) AKIWASILISHA  
BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU  
MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA  
MWAKA 2018/19 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 94(5) (a) ya Kanuni za Kudumu  
za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

**I. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb) napenda kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2018/19.

**Mheshimiwa Spika**, kabla sijatoa maoni kuhusu mapendekezo ya Mpango, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kusema kwamba; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na watanzania wote wanaopenda kuona haki ikitamalaki katika taifa, tunalaani na tunapinga vitendo viovu vya uonevu, ukandamizaji, utekaji na sasa majoribio ya mauaji yanayofanywa dhidi ya wanachama na viongozi wa vyama vya Upinzani hapa nchini. Ikiwa vitendo hivi vitaachwa viendelee bila kukemewa na kushughulikiwa kwa uzito unaostahili, kuna hatari ya kundi linalohisi kuonewa likakosa uvumilivu na hivyo kuathiri amani ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Ni miezi miwili sasa imepita tangu Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Tundu Lissu anusurike kifo baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi wakati Mkutano wa Nane wa Bunge ukiwa unaendelea na vikao vyake hapa Dodoma na mpaka sasa hakuna taarifa rasmi iliyotolewa na Serikali juu ya kukamatwa kwa watu waliohusika na tukio hilo. Ikiwa polisi wameshindwa

kufanya uchunguzi na kuwakamata wahalifu hao ndani ya miezi miwili, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni muujiza wowote unaoweza kutendeka ili watu hao wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vyaheria hata kama polisi wataongezewa miezi mingine miwili. Tafsiri ya ukimya huo wa Serikali ni rahisi; kwamba hakuna dhamira ya dhati wala utayari wa kushughulikia jambo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, si nia yangu kuorodhesha matukio mabaya wanayofanyiwa viongozi wa upinzani hapa nchini kwa kuwa ni mengi na pia tumeyasema sana humu bungeni; na wakati mwingine kuamriwa kuyafuta katika hotuba zetu, lakini hili la kuanza kutuwinda kwa lengo la kutuuwa, hatuwezi kamwe kulinyamazia. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa wananchi wote kupaza sauti zao kipinga uonevu na ukandamizaji wa haki, kipinga matukio ya utekaji, utesajii na umwagaji damu katika nchi. Aldha, tunatoa wito wa waumini wa dini na madhehebu mbalimbali kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu awaponye wale wote walioathirika na matukio hayo lakini zaidi sana kuliepusha taifa na laana kwa damu ya watu wasio na hatia iliyomwagika katika nchi hii.

**Mheshimiwa Spika**, ili Mpango huu wa Maendeleo tunaoujadili leo uweze kufikia malengo yaliyokusudiwa, ni lazima tuutekeleze tukiwa na umaja na mshikamano kama taifa. Kamwe haitawezekana kuyafikia hayo maendeleo tunayotaka kwa kubaguana kwa itikadi za kisiasa, au kwa kubezana, kunyanyasana, kuoneana, kuumizana na kuuwana. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa viongozi wote katika ngazi mbalimbali kuitunza na kuilinda amani ya nchi yetu kwa kutenda haki, na kuacha mara moja tabia za ubaguzi, uonevu, ukandamizaji na unyanyasaji dhidi ya watu wanaowaongoza.

## **II. UWAJIBIKAJI MDOGO WA SERIKALI KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ndiyo yenyewe wajibu wa kwanza katika kusimamia utekelezaji wa Mpango ya Maendeleo

nchini. Hata hivyo, Serikali imekuwa na tabia ya kukwepa kutimiza wajibu huo kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, misingi ya uwajibikaji katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ipo kikatiba na kisheria. Mathalani, Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inalipa Bunge mamlaka ya kujadili na kuidhinisha Mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo. Lakini, kwa miaka yote, Serikali imekuwa ikigoma kuleta miswada ya sheria ili bunge litekeleze madaraka yake kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(c) ya katiba kutunga sheria ya kusimamia mipango inayoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili tumelipiga kelele sana, lakini Serikali hii ya CCM imeamua kuweka pamba masikioni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatafsiri mgomo huo wa Serikali kuleta miswada ya sheria ya kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo kama kukwepa kuwajibika, lakini mbaya zaidi ni kwamba Serikali inavunja katiba kwa makusudi. Hii ni kwa sababu hitaji la kutunga sheria ya kusimamia mipango inayoidhinishwa na Bunge ni takwa la kikatiba na sio hiari. Kutotekeliza takwa hilo, ni kuvunja Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, uthibitisho mwingine kuwa Serikali inakwepa kuwajibika katika kusimamia kikamilifu mipango ya maendeleo ni kitendo chake cha kuifanyia marekebisho sheria ya bajeti ambayo inatoa mwongozo wa uwajibikaji wa kifedha/kibajeti (financial accountability) katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Serikali ililetä mapendekezo ya kuifanyia marekebisho vifungu vya 41, 53, 56, 57 na 63 vya sheria ya bajeti ya 2017 kwa kuondoa wajibu wa Serikali wa kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Bungeni ripoti ya matumizi ya fedha kwa kila robo mwaka ya mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi mitatu) ambapo sasa ripoti hiyo itakuwa ya nusu

mwaka wa mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi sita).

**Mheshimiwa Spika**, athari za marekebisho hayo ya sheria ya bajeti ni kudumaza ufuatiliaji thabiti (tight follow-up) wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali; na jambo hilo linaweza kupelekea utekelezaji mbovu wa bajeti kutokana na matumizi yasiyofaa au hata ubadhirifu wa fedha za umma. Nasema hivi kwa sababu ikiwa ripoti ya matumizi ya Serikali itatolewa kwa kila nusu mwaka wa utekelezaji wa bajeti, maana yake ni kwamba, ripoti hiyo itatoka wakati mchakato wa maandalizi ya mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata ukiwa umeshaanza. Kwa hiyo, ripoti hiyo inakuwa haisaidii katika kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti katika mwaka wa fedha unaoendelea (current financial year) ili hatimaye kuweza kufanya makisio na maoteo ya bajeti inayofuata.

**Mheshimiwa Spika**, ili mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo yawe na tija, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri na kupendekeza kwamba; Serikali ilete muswada wa marekebisho ya sheria ya bajeti ili kurejesha vile vifungu vilivyokuwa vinaelekeza ripoti za matumizi ya fedha ziwe zinaletwa kila baada ya miezi mitatu (robo mwaka). Kwa kufanya hivyo, kwanza kutakuwa na ufuatiliaji madhubuti wa matumizi ya Serikali, lakini pia ripoti za robo mwaka, zitawezesha kufanya tathmini ya mwenendo wa utekelezaji wa bajeti na hivyo kuisadia Serikali kujipanga vizuri zaidi kwa bajeti zinazofuata.

### **III. MATUMIZI YA SERIKALI NJE YA BAJETI YANAVYOATHIRI UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge hili kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limepewa mamlaka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaaka wa Bajeti kwa madhumuni ya kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Serikali. Na ikumbukwe kwamba Bajeti ya Serikali ndiyo nyenzo muhimu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hivyo, ili

Mpango uweze kutekelezwa ipasavyo, lazima Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge itumike ipasavyo ili kuweza kutekeleza miradi ya Maendeleo ilivyopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ikiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazikutosha kutekeleza majukumu ya Serikali, kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 kinalekeza kwamba: “*Serikali itawasilisha Bungeni kwa idhini, bajeti ya nyongeza ya fedha zilizotumika ambazo zimezidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge au kwa madhumuni ya kugharamia mahitaji ambayo hayakupangwa*”.

**Mheshimiwa Spika** utaratibu huu unatiliwa nguvu na Sheria ya Fedha za Umma wa mwaka 2001(Public Financne Act, 2001)ambapo kifungu cha 18 (3) na (4) kinaitaka Serikali kuleta Bungeni bajeti ya nyongeza (mini-budget) kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha zilizoidhinishwa awali hazikutosha.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu huo wa kisheria umekuwa ukivunjwa na Serikali kwa kufanya matumizi ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge jambo ambalo linaua dhana ya madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, hoja hii ya kufanya matumizi nje na bajeti iliyopitishwa na Bunge si mpya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeipigia sana kelele uvunjaji huu wa sheria katika matumizi ya Serikali. Kwa mfano katika Mwaka wa fedha 2016/17 tulionyesha jinsi ambavyo bajeti ya maendeleo iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/16 ilivyotekeliza nje ya utaratibu. Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka tajwa ilikuwa ni shilingi bilioni 883.8 ambapo kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa ni shilingi bilioni 191.6 Lakini jambo la kushangaza ni kwamba hadi kufikia mwezi Machi 2016 Wizara ilikuwa imeshapokea kutoka hazina shilingi bilioni 607.4 ikiwani fedha za ndani. Kwa takwimu hizo ni

kwamba kulikuwa na ongezeko la fedha zilizotolewa na hazina hadi kufikia mwezi Machi 2016 ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Tangu kuidhinishwa kwa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, hakuna bajeti ya nyongeza iliyoletwa Bungeni na Serikali kwa ajili ya kupata idhini kutokana na matakwa ya Sheria ya Bajeti ya 2015 au sheria ya Fedha ya 2015.

**Mheshimiwa Spika**, hata sasa kuna baadhi ya miradi ya maendeleo inatekelezwa nje ya bajeti na hatujaona Serikali ikiomba bajeti ya nyongeza katika kutekeleza miradi hiyo. Kwa mfano utekelezaji wa mradi wa umeme wa Stigglers Gorge, Ujenzi wa barabara za Juu Dar es Salaam (Interchange), Ujenzi wa mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nk. ni baadhi ya miradi ambayo bajeti zake haziko bayana.

**Mheshimiwa Spika**, kitendo cha Serikali kuamua kufanya re-allocation ya bajeti bila kupata idhini ya Bunge ni dharau kwa bunge lakini mbaya zaidi ni uvunjaji wa Katiba na Sheria. Aidha, kitendo hicho kinaweza kufungua mianya ya ubadhirifu kwa kuwa bunge linakuwa halina taarifa na matumizi hayo.

**Mheshimiwa Spika**, hata kama matumizi yanatakiwa kufanyika kwa jambo la dharura, sheria ya bajeti pia imeweka utaratibu wa kushughulikia jambo la dharura. Kwa mfano kifungu cha 47 (1) kimeweka zuio la kutumia fedha katika mfuko wa dharura (Contingency Fund) isipokuwa kwa sheria au utaratibu utakaowekwa na Bunge. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuainisha matumizi yote yaliyowahi kufanya na Serikali nje ya bajeti, na kueleza sababu za kufanya hivyo kinyume na sheria ya bajeti. Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi Serikali kutumia, lakini hoja ya msingi ni kufuata utaratibu, kanuni na sheria zilizopo. Hapo ndipo utawala wa sheria unapokiukwa, nah ii ni hatari sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

**IV. MAPITIO YA HOJA ZILIZOIBULIWA NA KAMBI YA UPINZANI KATIKA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kujadili Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/18, Kambi Rasmi ya Upinzani iliibua baadhi ya changamoto katika maeneo mbalimbali na kuitaka Serikali kuyafanya kazi. Baadhi ya Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

**i. Ajira na Hali ya Uchumi wa Wananchi**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani iliipinga Serikali kwa kitendo chake cha kusitisha ajira kwa kigezo kuwa inafanya uhakiki wa watumishi ili kupambana na tatizo la watumishi hewa. Sababu kubwa ya kuipinga Serikali ni kwamba zoezi hilo iliypelekea kuyumba kwa uchumi kwa baadhi ya familia ambazo zilikuwa na watu wenye sifa ya kuajiriwa katika sekta ya umma kama vile walimu, manesi na madaktari. Kusimamishwa huku kwa ajira kulisababisha nguvu kazi iliyokuwa na uwezowa kuzalisha kuishi kama omboomba!

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa ajira ni nyenzo muhimu ya kipato na uchumi wa wananchi, na kwa kuwa fursa za ajira binafsi nazo zimekuwa na changamoto nyingi kutokana na ukosefu wa mitaji unaotokana na hali duni ya uchumi (umasikini); Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua, Safari hii Serikali imeweka mkakati gani katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira nchini.

**ii. Msukosuko kwa Wafanyabiashara Wakubwa**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/18; Kambi Rasmi ya Upinzani iliipinga kitendo cha Serikali kuwanyanya wafanyabiashara wakubwa kwa kukamata mali zao na hata kufunga akaunti zao bila kutoa sababu za msingi hali iliyopelekea kuyumba kwa uchumi na kupungua kwa mzunguko wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani ilieleza bayana kwamba haipingi kuchukuliwa kwa hatua za kisheria kwa wafanyabiashara wakubwa wanaokiuwa sheria za nchi au kuhujumu uchumi, lakini inapringa Seriakali kutumia madaraka yake ya Dola kuwanyanya wa wafanyabiashara, kwani kwa kufanya hivyo, itawavunja moyo wawekezaji na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, kwamba; safari hii imeweka mkakati gani katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2018/19 wa kuboresha mazingira ya biashara nchini ili kuwavyutia wawekezaji?

### iii. Mikopo katika Sekta ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani pia ilipringa uamuzi wa Benki Kuu kuzuia baadhi ya benki kukopesha wakulima kwa madai kwamba mikopo katika sekta ya Kilimo huwa haina uhakika wa kurudi. Hoja kuu ni kwamba mikopo ya kilimo inahitaji muda mrefu hivyo inatakiwa kubuni utaratibu maalum wa kuziwezesha benki za biashara kuweza kutoa mikopo hiyo na sio kusema haina uhakika wa kurudishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiishauri Serikali kuweka jicho lake katika Sekta ya Kilimo kwa kuwa sekta hiyo ndiyo inayotoa ajira kwa watazania zaidi ya asilimia 70. Tulishauri Sekta hiyo iongezewe bajeti hususan bajeti ya maendeleo, tulishauri Seriali itoe ruzuku kwa pembejeo za kilimo na kutafuta masoko kwa mazao ya kilimo ili kukuza sekta hiyo. Hata hivyo, mara zote mapendekezo hayo yamekuwa yakipuuzwa na matokeo yake sekta ya kilimo kuendea kudorora mwaka hadi mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili juu ya mkakati wake wa kuboresha sekta ya kilimo katika maeneo ya mikopo kwa wakulima ya muda mrefu na riba nafuu, ruzuku ya pembejeo za kilimo na masoko ya uhakika kwa mazao yakilimo.

**iv. Kupungua kwa Mapato katika Sekta ya Utalii**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitoa angalizo la kupungua kwa mapato katika Sekta ya Utalii kutokana na kitendo cha Serikali kuanzisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye huduma zote za kitalii. Tulieleza kuwa kodi hiyo badala ya kuwa kivutio, itakuwa kizingiti kwa watalii wanaokuja kuitembelea nchi yetu na hivyo kuathiri hoteli zilizokuwa zinafanya biashara ya utalii pamoja na makampuni yaliyokuwa yakijihuisha na biashara ya utalii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tathmini ya ukuaji wa Sekta ya Utalii kabla na baada ya kuanzisha VAT katika Sekta hiyo, ili thamini hiyo itoe dira ya namna bora ya kuongeza mapato katika sekta hiyo.

**v. Kodi ya Majengo na Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

**Mheshimiwa Spika**, katika mambo ambayo tulipingga Serikali kwa nguvu ni uamuzi wake wa kuziondolea Serikali za Mitaa Mamlaka yake ya kikatiba ya kukusanya kodi za majengo na kupeleka jukumu hilo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Na sababu ya kuipinga Serikali ilikuwa wazi kamba; Serikali za Mitaa zilitegemea sana kodi hiyo kujidesha na kugharamia miradi ya maendeleo katika halmashauri husika, na kwamba baada ya kuondolewa kodi hiyo, zimeathirika sana.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, TRA imeweza kukusanya fedha kiasi gani kutokana na kodi ya majengo, tofauti na zile zilizokusanywa na Halmashauri zenyewe. Aidha, katika kiasi kilichokusanywa na TRA, ni asilimia ngapi zimepelewa katika halmashauri ili kuzisaidia halmashauri hizo kujidesha na pia kugharamia miradi ya maendeleo?

vi. Sera ya Elimu Bure

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitaa angalizo kwa Serikali kufanya tathmini ya mahitaji kwanza (assessment of needs) na kuandaa mpango wa utekelezaji (implementation plan) ili kuweka mazingira mazuri ya kutekeleza sera ya elimu bure. Na tulifanya hivyo kwa nia njema kwa kuwa tulijua haukuwa mpango wa CCM kutoa elimu bure, na kwa sababu hiyo, Serikali ya CCM haikuwa na mpango au maandalizi yoyote ya utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya kukurupuka kutekeleza kitu ambacho hakina mpango wa utekelezaji ni kwamba; hali katika shule za umma imekuwa mbaya sana kutokana na serikali kushindwa kupeleka fedha za uendeshaji kwenye shule hizo na hivyo kufanya suala zima la elimu ya msingi na Sekondari kuwa katika hali mbaya na huenda baada ya muda mfupi ujao shule hizi zikafungwa kutokana na kukosekana kwa fedha za uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda sana watoto wa kitanzania wasomeshwe bure na Serikali, ila inataka kuwe na mpango endelevu wa kufanya hivyo, na sio kuchangishana kila uchwao kama inavyofanyika kwenye harusi. *"The Opposition simply needs A Sustainable Implementation Plan"*

**Mhesimiwa Spika**, tulishuhudia watu wakichangishwa kwa ajili ya madawati, ujenzi wa maabara nk. Lakini, hali hiyo haiwezi kuwa endelevu kwa kuwa, anaweza akaja kiongozi mwininge ambaye hana karama ya uchangishaji na hivyo kufanya mpango huo kukwama. Kwa hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kulieleza Bunge hili, imeweeka mkakati gani wa kutengeneza mpango wa utekelezaji wa sera ya elimu bure.

vii. Mikopo ya Elimu ya Juu

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu walikuwa 20,183

tu huku wanafunzi 27,053 wakikosa mikopo ya elimu ya juu katika vyuo vikuu mbalimbali hapa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani ilishangazwa na tukio hilo kwani Rais aliwaahidi watanzania wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu 2015 kuwa hakuna mwanafunzi wa Elimu ya Juu atakayekosa mikopo na kwamba yeze atakuwa mwarobaini wa tatizo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la mikopo ya elimu ya juu halitokani na nani anakalia kiti cha Rais, ila linatokana na ukosefu wa mpango wa mikopo, (*Higher Learning Loan Scheme*). Kungekuwa na *Higher Learning Loan Scheme*, kusingekuwa na matukio ya wanafunzi kuchaguliwa kujunga na vyuo vikuu halafu wakose mikopo kwa sababu scheme ingechukuwa tu wale ambao inaweza kuwakopesha.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki ya kumchangua mwanafunzi kujunga na chuo kikuu kama inajua haiwezi kumkopesha. Vinginevyo utaratibu wa mikopo ufutwe uli kusiwe na ubaguzi (double standard) katika kuwashudumia wanafunzi wa elimu ya juu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza commitment yake katika kuandaa *Higher Learning Loan Scheme* katika Mpango wa Maendeleo wa 2018/19 ili kuondokana na tatizo la wanafunzi wa elimu ya juu kukosa mikopo.

#### **V. HALI YA UCHUMI WA TAIFA**

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanza kuangalia hali ya uchumi wetu, naomba kunukuu kauli ya Waziri Mkuu wa Uingreza, Bibi Thereza May wakati akijibu swali la Kiongozi wa Upinzani katika Bunge la Uingereza (House of Common) kuhusu uchumi wa Uingreza, kwamba; "*Serikali kama Serikali haina fedha, bali inategemea kupata fedha kutoka katika sekta binafsi na kwa wafanyakazi kupitia kodi ya mishahara (PAYE). Hivyo kama sekta binafsi ina-shrink na wafanyakazi wanaachishwa kazi na kipato chao kinakuwa kidogo maana yake ni kuwa Serikali inafilisika*"

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ilikwishatoa ushauri kwamba kwa kuwa Serikali haina fedha na watumishi ndio wahusika wakuu katika ulipaji wa kodi kwa Serikali kuliko kundi lolote la walipa kodi kupitia kodi ya Mshahara (PAYE). Hivyo kuongeza kiwango cha mishahara maana yake ni kuongeza kiwango cha ulipaji wa kodi, na faida pekee ambayo mtumishi ataipata kwa ongezeko la mshahara ni pale atakapo staafu. Hivyo basi, Serikali kuongeza mishahara kwa watumishi wake ni njia mojawapo ya kuongeza mapato yake, lakini kwa Serikali ya awamu ya tano imeshindwa kuliona hilo.

**Mheshimiwa Spika**, hoja hiyo inaonekana kwa uwazi sana kama ukifanya mapitio ya mwelekeo wa uchumi aya ya 16, kwamba makusanyo kwenye kodi ya mapato ya ajira yalikuwa shilingi bilioni 2,278.1 sawa na asilimia 90.5 ya lengo la shillingi bilioni 2,526.7, ikillinganishwa na mapato ya mwaka 2015/16. Kutofikiwa lengo kwenye kodi hiyo ni kutokana na baadhi ya makampuni kupunguza wafanyakazi kufuatia kupungua kwa shughuli za kibashara. Vile vile kupungua kwa Ankara za malipo ya mishahara kulikosababishwa na kuahirishwa kwa ajira mpya za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba hii ni dalili mbaya kwa uchumi wetu, kutokana na ukweli huo uliomo kwenye nyaraka za Serikali pamoja na hali halisi ya maisha ilivyo kwa sasa kwa watanzania.

#### i. Uchumi wa Taifa

**Mheshimiwa Spika**, hali ya *kasi* ya ukuaji wa uchumi kwa sasa ni mbaya. Wakati Serikali imekuwa ikijigamba katika majukwaa ya kisiasa kuwa hali ya uchumi wa nchi imeimarika takwimu za Serikali zinaonyesha kasi ya ukuaji wa uchumi wetu umeshuka tofauti kabisa na maneno ya uongo na hadaa yanayosemwa kwa wananchi kupitia mikutano mbalimbali na ziara za wanasiasa zinazoendelea nchini. Hali hii ni dhahiri kwani katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2018/2019 ukurasa wa 6 unaonyesha wazi kuwa mwaka 2016 kasi ya

ukuaji ilikuwa ni asilimia 7.7 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2017 ambapo ni asilimia 6.8 tu. Hii inaonyesha wazi kwamba kwa nusu mwaka pekee kumekuwa na anguko la asilimia 1 kwenye kasi ya ukuaji wa uchumi wa taifa. Hii ni kutokana na mazingira mabaya yanayotishia wawekezaji, mzunguko mdogo wa fedha, kuwepo kwa sintofahamu katika siasa za sasa za uongozi wa Serikali ya awamu ya tano ambapo matajiri wakubwa na wafanya biashara wamejikuta katika hatari za kafilisiwa kutokana na kauli za vitisho zinazoendelea kutolewa na wanasiwa kuwa wanataka matajiri waishi kama mashetani.

**Mheshimiwa Spika**, katika mapitio ya uchumi wa dunia kasi ya ukuaji wa uchumi dunia inatarajiwa kukua kwa asilimia 3.6 kwa mwaka huu wa 2017 na 3.7 kwa mwaka 2018 huku uchumi wa wa Kikanda ukikadiriwa kukua kutoka asilimia 1.4 mpaka 2.6. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua je, kama nchi tutatumia miujiza gani kufikia kasi hiyo ya ukuaji kwani ni dhahiri kasi ya ukuaji wa uchumi wetu inaporomoka (from ascending to descending)

**Mheshimiwa Spika**, tutakumbuka kuwa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alipochukua nchi kutoka mikononi mwa wakoloni waliokuwa wanaendesha nchi kibepari aliamua kufanya mabadiliko makubwa katika uchumi. Pamoja na makosa makubwa aliyokuwa ameyafanya Mwalimu ya kutaifisha viwanda, mashule na hospitali **kabla** ya kuwaandaa wananchi kuwa na ujuzi bora wa kuendesha na kuendeleza huduma hizo. Mwalimu alifanikiwa sana kupambana na umaskini kwa kuweka bayana maadui watatu wa taifa hili ikiwa ni pamoja na ujinga, maradhi na umaskini wenyewe.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo Mwalimu, alihamasisha ujenzi wa viwanda kwa vitendo ambapo viwanda hivyo vilitoa ajira na kipato kikubwa kwa wananchi hususani wale wa maeneo ya vijijini, alihamasisha ujenzi wa mashule katika mikoa mbalimbali ambayo mpaka leo mashule hayo ni msaada mkubwa kwa wananchi pamoja na hospitali, zahanati, madaraja ya kuunganisha mikoa n.k

**Mheshimiwa Spika**, katika Serikali hii ya CCM inapaswa kujuliza mambo ya msingi yafuatayo:-

1. Ni mambo gani ya msingi ambayo inaweza kujivunia tofauti ya yale aliyoafanya Mwalimu Nyerere? Mfano; Mwalimu alihakikisha ujenzi wa mashule kwenye kila mkoa ambapo elimu iliyotolewa ilikuwa bora, viwanda vilijengwa kwa wingi tena kwenye maeneo yaliyo na malighafi ambapo kwa sasa viwanda vingi vimekufa kabisa. Mwalimu alijenga mahospitali yaliyotoa huduma nafuu kwa wananchi ambapo kwa sasa gharama za matibabu zimekuwa juu sana na wananchi wenye hali duni za maisha ndio wanaopoteza maisha kwa wingi kutokana na hali ngumu ya uchumi. Hali ya kilimo cha mazao ya biashara (traditional cash crops) ni mbaya na maeneo mengi ya nchi hakuna tena kilimo cha mazao hayo kama buni (kahawa), tumbaku, pareto, mkonge, shayiri, pamba na mengine yamepotea kabisa na Serikali ya CCM hajjaweka mkakati madhubuti ya kuhakikisha pamoja na changamoto za kimazingira mazao hayo yanaendelea kuwepo, kuflisika kwa vyama vyaa ushirika vilivyokuwa msaada mkubwa kwa wananchi wa vijijiini yamekwisha kabisa.

2. Je, mpaka sasa Serikali ya CCM ina dira ipi ya maendeleo? Ikiwa mpaka sasa miaka zaidi ya 56 ya uhuru bado tunapambana na maadui wale wale ambao Mwalimu Nyerere aliwatajaa hadharani ikiwa ni pamoja na ujinga, maradhi na umaskini. Mwalimu aliamini dira ya maendeleo inaweza tu kufikiwa endapo tunakuwa wamoja kama taifa. Alihakikisha anapinga ubaguzi wa namna yoyote kwa nguvu zake na akili zake zote. Mwalimu aliamini dira ya maendeleo ya taifa inaweza kufikiwa ikiwa kuna misingi bora ya uwajibikaji na utawala bora. Hivyo, Mwalimu alikuwa mstari wa mbele kushawishi uwepo wa vyama vingi ili Serikali ipate changamoto kwa nia nzuri ya kuboresha utendaji na ufanisi wa shughuli za Serikali. Tofauti na ilivyo sasa kumekuwepo na chembechembe za wazi za chuki za kisiasa, ubaguzi wa kikabila na kikanda, vitisho na matumizi mabaya ya vyombo vyaa dola, kumekuwepo na mambo mengi ya kudhoofisha umoja wetu kama taifa. Huku tukiendelea kukabiliana na

maadui watatu aliowataja Mwalimu Nyerere tumeongeza adui mwingine mkubwa ambae ni utawala mbovu (bad leadership), usiongizatia utawala wa sheria, usiozingatia mgawanyo wa madaraka (separation of power) na usioheshimu utendaji wa mihimili mingine.

3. Je, Serikali ya CCM inawezaje kukuza uchumi wa taifa endapo hali ya amani na usalama wa raia katika maeneo mbalimbali ya nchi sio ya kuridhisha? Katika taarifa ya hali ya uchumi kwa Mwaka 2017 ukurasa wa 5, Serikali imeweka wazi kuwa uwepo wa mivutano ya kisiasa inaleta athari kwenye hali ya amani na usalama wa nchi na hivyo kuathiri kabisa uchumi wa nchi. Kwa hivi sasa kumekuwepo na mivutano mikubwa ya kisiasa nchini ambapo wanasiwa wa Upinzani wamekuwa wakikamatwa na polisi (police harassment), wamekuwa wakitekwa, kupigwa risasi, kunyimwa haki zao za kikatiba za kukusanyika na kuandamana, kufungiwa kwa vyombo vyya habari vinavyoikosoa Serikali n.k Hivi vyote ni viashiria tosha vyya uvunjifu wa amani ambavyo vinalenga kuperomosha kabisa uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo yote Serikali hii imeshindwa kabisa kuchambua vipaumbele vyake kuendana na hali ya uchumi na uhitaji wa wananchi. Kwa hali ilivyoo kwa wananchi hususani wengi wanaoishi vijijini hawanufaiki ipasavyo na mipango ya Serikali na vipaumbele vyake kwa sasa. Hii ikiwa na maana kwamba Serikali hii imeshindwa kupambanua mipango yake ya kimaendeleo ya muda mrefu na muda mfupi (short term and long term development plan).

**Mheshimiwa Spika**, katika miradi mbalimbali inayoendelea nchini kwa sasa ikiwemo ujenzi wa bohari kubwa ya madawa (MSD ), ujenzi wa ofisi kubwa ya TRA na uwanja wa ndege wilayani Chato ambapo eneo hilo sio eneo la kimkakati la kiuchumi yaani (economic strategic area).Katika viashiria vyya maeneo ya kimkakati ya kiuchumi kama vile kiwango cha uzalishaji na shughuli za kibashara, eneo la kijiografia, mzunguko wa fedha na idadi ya watu bado eneo hilo halijaweza kukidhi vigezo jambo ambalo linaonyesha wazi

vile Serikali yetu haiko makini katika kutengeneza mipango yake ya muda mrefu na mfupi na zaidi ya yote haina mipangilio bora katika kupanga vipaumbele.

**Mheshimiwa Spika**, katika kitabu cha Mpango cha Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 ukurasa wa 91 kinaonyesha kuwa Serikali ilianzisha mradi wa ujenzi wa kiwanja kipywa cha ndege Chato kwa ajili ya huduma za usafiri wa anga kwa Mkoa wa Geita na maeneo ya jirani. Katika mpango huo bilioni 2 zilitengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa ujenzi huo. Katika kitabu cha matumizi ya maendeleo (Public Expenditure Estimates Development Votes) 2016 mpaka June 30, 2017 hakikuonyesha kabisa kiwanja hicho kikiwa kimetengewa fedha, hali kadhalika katika kitabu hicho hicho cha matumizi ya maendeleo kuanzia tarehe 1 Julai 2017 mpaka June 30, 2018 hakuna fedha yoyote illyotengwa kwa ujenzi wa uwanja huo. Jambo la kushangaza ni kuwa ujenzi wa mradi huu umekaribia kukamilika huku bilioni 39 zikikusudiwa kukamisha ujenzi huu.

**Mheshimiwa Spika**, mambo haya yakiendelea kufunikwa kimya kimya na kuendelea kuogopa kuikosoa Serikali kwa sababu yoyote ile yatagharimu sana taifa hili. Miradi ya maendeleo ni lazima iwe na tija kwa wananchi na iweze kuwanufaisha walio wengi. Kitendo cha kujenga vitega uchumi hivi Chato na kuacha kuviweka katika maeneo ya kimkakati ya kiuchumi kama vile Geita ambapo ndipo eneo lenye shughuli nyangi za kibiashara, mzunguko mkubwa wa fedha, uwezo mkubwa wa ununuzi wa huduma (high purchasing power) pamoja na mkakati wa kibiashara wa kijigrafia ni kitendo kinachozua maswali mengi na pengine kuendelea kuamsha hisia kubwa za ubaguzi zinazosambaa kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hilo fedha za ujenzi wa miradi hiyo hazionekani katika vitabu vyta matumizi ya maendeleo (Public Expenditure Estimates Development Votes) Ikiwa na maana kwamba fedha hizo za ujenzi wa miradi hazikupitishwa na Bunge lako. Kambi Rambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa hesabu za

Serikali (CAG) kupitia kwa kina miradi hii ili kujuu ni wapi hasa fedha zilipopatikana. Kuendelea kunyamazia matumizi holela ya fedha za walipa kodi wa nchi hii maana yake ni kuruhusu mianya ya ubadhirifu , kuwa na uchumi usio tabirika, kutokea kwa anguko la uchumi kwa kuwa fedha hizo zinatolewa bila kuzingatia sheria ya fedha au sheria ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kufumbia macho tabia ya baadhi ya watumishi wa umma kutumia fedha za umma bila mpangilio kwa kutumia utashi wao wenyewe huku mahitaji muhimu ya wananchi kama vile huduma za afya, huduma bora ya elimu, utoshelevu wa chakula nchini pamoja na huduma muhimu za kibiashara kama unaifuu wa kodi kwa wafanyabiashara wa makundi yote,utafutaji wa masoko kwa wafanyabiashara na wakulima wadogo na upatikanaji wa ajira unaoendana na kasi ya ukuaji wa viwanda . Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupanga mipango yake ya muda mrefu na mfupi kwa kuzingatia ukubwa na umuhimu wa hitaji la huduma kwa wananchi walio wengi.

**ii. Gharama za maisha na pato la mtu mmoja mmoja.**

**Mheshimiwa Spika**, gharama za maisha zimepanda huku kipato cha mtu mmoja mmoja kikishuka sana. Kumekuwepo na taarifa mbalimbali za Serikali zikionyesha kuwa uchumi wa nchi yetu umekuwa. Jambo kubwa la kushangaza ni kuona wafanyabiashara wengi maeneo mbalimbali ya nchi wakifunga biashara zao kutokana na kukosekana kwa wateja na kushindwa kumudu gharama za uendeshaji, wawekezaji wakubwa wakifunga biashara zao na kuondoka nchini, wananchi wengi wakishindwa kumudu kupata milo mitatu kwa siku, hali ya ajira ikizidi kuwa ngumu, taasisi za kifedha zikishindwa kutoa mikopo hasa kwa wafanyabaishara wadogo kutokana na wengi kushindwa kufanya marejesho, dhamana za mali yaani (collateral) kushuka thamani na hivyo kushindwa kufidia thamani ya mikopo.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na ongezeka kubwa la walaji huku uzalishaji ukizidi kushuka, Serikali imekuwa ikiwaumiza wafanyabiashara kwa kodi kubwa na nyingi zisizo na tija zinazosbabisha wafanyabiasha kushindwa kukuza mitaji , matumizi mabaya ya madaraka na kuwa na mikakati iliyokosa ubunifu katika kutatua kero mbalimbali za wananchi ikiwemo bomoa bomoa iliyowaathiri maelfu ya wananchi, kuwekeza katika eneo moja la ujenzi wa miundo mbinu na viwanda pekee na kutelekeza maeneo mengine yanayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja ikiwemo sekta ya kilimo. Serikali kuwatisha na kuwakatisha tamaa wafanyabiashara wakubwa na matajiri walioajiri maelfu ya raia hii ikiwa na maana kwamba Serikali inadhoofisha sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2018/2019 ukurasa wa 7 kimeainisha kuwa pato la taifa kwa mwaka 2016 liliifika milioni 103,744,606 ambapo likigawanya kwa idadi ya watu 48,676,698 wanaokadiriwa kuwepo Tanzania Bara, inaongeza wastani wa Pato la kila mtu kufikia shilingi 2,131,299 ikililinganishwa na shilingi 1,918,897 mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu za namna hii ndizo hasa zinazosababisha wananchi wazidi kuona Serikali kutokuwa makini. Katika takwimu hizi zilizotolewa za Pato la taifa zimejumuisha jumla ya mapato ya bidhaa na huduma za Bara na visiwani. Hivyo, kitendo cha mgawanyo wa kutafuta wastani wa pato la kila mwananchi kwa kutumia takwimu za idadi ya watu kwa Tanzania Bara pekee inaonyesha kuwa Serikali sasa imepoteza mwelekeo na ni mfano dhahiri kuwa uchumi wa nchi umeporomoka.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Tume ya taifa ya takwimu kwa mwaka 2015 pekee Tanzania Bara ilikuwa na idadi ya watu wapatao milioni 48.8 huku Tanzania Zanzibar ikikadiriwa kuwa na jumla ya idadi ya watu wapatao milioni 1.4 na hivyo kufanya idadi ya watu milioni 50.2. Kwa mujibu wa kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 ukurasa wa 3 kilionyesha kuwa Pato Halisi la Taifa ilikuwa

triliuni 44.1. Katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo 2017/18 kimeonyesha katika ripoti yake kuwa Pato la kila mtu lilikuwa shilingi 1,918,897 kwa mwaka huo wa 2015. Hivyo basi, kwa takwimu hizi zinaonyesha wazi kufikia mwaka 2016 pato la kila mwananchi halikuwa kiasi cha shilingi za kitanzania 2,131,299 kama zilivyoonyeshwa katika kitabu cha mpango.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya kigezo cha kukua kwa uchumi wa taifa ni pamoja na kuongezeka kwa uwezo binafsi wa kila mwananchi katika kununua bidhaa au huduma (increasing purchasing power). Katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo ya Taifa ukurasa wa saba *Serikali inakiri kuwa bado tuna safari ndefu ya kuingia katika kundi la uchumi wa kati* ili angalau pato la kila mtu liweze kufikia hadhi ya uchumi wa kati wa dola 1,043.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekwisha kushauri Serikali kwa muda mrefu lakini utekelezaji na utendaji umeendelea kuwa vilevile. Kuna msemo usemao uliosemwa na Louise Hay alisema "*I do not fix problems, I fix my thinking, then problems fix themselves*". Hii kwa tafsiri isiyo rasmi kwamba endapo Serikali na wadau wake wangeruhusu fikra au utashi wao kuwaza na kuchambua mambo basi matatizo tunayokabiliana nayo yangejifutia suluhu yenye.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha wa huu wa hali ngumu ya uchumi tunayokabiliana kama taifa hali hii ingeweza tu kutengemaa na pengine kuwa na uchumi bora zaidi endapo tu Serikali itakubali kukosolewa, kuyafanya kazi yale tunayoyajadili kwa hoja, kukubali ushauri bila kuangalia mrengu wa itikadi za kivyama kwa nia nzuri ya kujenga taifa letu. Ni dhahiri kuwa kwa idadi ya kikatiba ya wabunge 393 tunaweza kubadili kabisa hali ya uchumi wa nchi yetu kwa kuisimamia, kuikosoa na kuishauri Serikali ipasavyo. Nasema haya kwa sababu nchi nyingi dunia zimeweza kufanya vizuri kutokana na kupokea maoni yanayotolewa na Bunge kama chombo chenye nguvu ya uwawakilishi wa sauti za wananchi. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

haitosita kuendelea kusema japo imesema sana kwa muda mrefu bila utekelezaji. Kambi Rasmi inaamini umoja wa sauti zetu ni mkubwa kuliko mgawanyo wa vyama vyetu.

### **iii. UCHUMI WA GESI**

**Mheshimiwa Spika**, miaka ya hivi karibuni Serikali imekuwa ikiwaminisha watanzania kwamba ifikapo mwaka 2025 Tanzania itakuwa ni nchi ya uchumi wa gesi kwa tafsiri pana. Baada ya Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia Mwongozo na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2018/19 haioneshi kwa uwazi mkakati au hatua madhubuti ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa gesi.

**Mheshimiwa Spika**, ilikuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa gesi asilia ni lazima maandalizi ya kutufikisha uko yaanze kuanzia sasa kwenye mipango yetu ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani imelazimika kuhoji baada ya kupitia Taarifa ya Serikali inayohusu uendelezaji wa miradi ya Gesi Asilia nchini inayotekelizwa kati ya Pan African Energy Tanzania (PAET), TPDC, SONGAS na TANESCO.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa hiyo ambayo inaonesha ushiriki wa kila kampuni katika mradi huo.Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu, hivi kama Serikali inatangaza zabuni za kutekeleza mradi maana yake ni Serikali kupoteza umiliki wa mradi husika?

**Mheshimiwa Spika**, ukiangalia SONGAS ilikuwa ni kampuni ya ubia ya kutekeleza mradi, PAET ilikuwa ni Kampuni ya uendeshaji visima vya gesi ambavyo tayari vilikuwepo. Sasa inakuwaje Kampuni zinazofanya kazi ya uendeshaji mara nazo zinakuwa wamiliki wa gesi nazo zinaiuzia TANESCO gesi, kwa bei ya soko wakati TANESCO ni mmiliki kwa niaba ya Serikali?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaungana na Kamati ndogo iliooongozwa na Mheshimiwa Seleman Zedi kuwa hatuwezi kuingia katika uchumi wa gesi hadi pale

mikataba ilioingiwa kati ya TPDC na TANESCO kwa niaba ya Serikali pamoa na makampuni ya SONGAS ambayo ni kampuni ya ubia kati ya CDC Globaleq ya Uingereza, Benki ya Maendeleo ya Uhlanzi-FMO na Tanganyika Development Finance Company Limited (TDFL) kwa upande mmoja na upande wa pili mkataba kati ya Serikali (TPDC &TANESCO) na kampuni ya PAET. Aidha, mkataba kati ya SONGAS na PAET.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kinyume cha hapo hizi tambo ambazo tuliambiwa humu ndani ya Bunge kuwa sasa gesi ni nyingi ya kutosha imegunduliwa, jambo ambalo ni sahihi lakini bila ya kupitia upya mikataba ya uendeshaji, ambayo imejigeuza kuwa mikataba ya umiliki kwa Serikali kupoteza haki za umiliki itakuwa ni shida kwa vizazi vijavyo na tutaonekana sisi wabunge kuwa ndio tuliouza nchi yetu. Kwani jukumu letu ni kuismamia na kuishauri Serikali pale mambo yanakuwa sio sawasawa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi inapenda kufahamu kuhusu utekelezaji wa ushauri uliotolewa na kamati ya bajeti ilioongozwa na Mhe Andrew Chenge kuhusu mapato ya gesi kama ilivyowasilishwa Bunge, February 2013, naomba kunukuu; "Serikali ifanye maamuzi ya kutumia gesi hii kama chanzo cha mapato sasa hivi kwa kuweka dhamana kiasi kidogo cha gesi hii. Kwa mfano kiasi kilichogundulika sasa hivi katika kina kirefu baharini ni futi za ujazo trilioni 32 ambazo ni sawa na mapipa bilioni 6 ya mafuta. Kwa bei ya sasa gesi hii ina thamani ya dola za kimarekani bilioni 660. Iwapo mgao wa Serikali ni angalau 10%, na Serikali ikaamua kutumia 10% ya mgao wake kama dhamana au mauzo ya mbele (collateral or forward sale)",

#### iv. Hali ya Sekta binafsi na uchumi wa nchi kwa sasa

**Mheshimiwa Spika**, sekta binafsi nchini zinapitia katika wakati mgumu sana kutohana na hali ngumu ya uchumi iliyopo sasa, mfumo wa kibashara usiotabirika, wingi wa kodi na utaratibu usiofaa wa ukusanyaji kodi.

**Mheshimiwa Spika**, mfumo wa ukusanyaji kodi kuptitia TRA umekuwa na kero kubwa kwa wafanyabiasha kutokana na mamlaka hiyo kutokuwa na mfumo bora wa kukusanya kodi kwa mafanyabiasha mmoja anaweza kutembelewa na timu tofauti tofauti za TRA zikiwa na makadirio ya viwango nya kodi yanayotofautiana. Jambo hili limekuwa kero kubwa sana kwa wafanyabiashara.

**Mheshimiwa Spika**, sekta binafsi pia imekumbwa na tatizo kubwa la kutokukopesheka kutokana na hali mbaya ya kifedha katika mabenki na taasisi nyingine za fedha. Hali hii inajidhihirisha kwani katika kitabu cha Mwongozi wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2018/19 ukurasa 40 unazungumzia kutetereka kwa rasilimali za benki kutokana na kuongezeka kwa mikopo chechefu kutoka asilimia 8.9 Mwezi June 2016 mpaka 10.6 Mwezi Juni 2017. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 1.7. Wafanyabiashara wengi wameuziwa mali zao kutokana na kushindwa kurejesha mikopo na hivyo wengi kujikuta kwenye lindi kubwa la umaskini, fedheha na msongo wa mawazo ambao unaongeza idadi kubwa ya Watanzania wanaokumbwa na matatizo ya akili kwa sasa (mental distress).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hilo Serikali hii haionyeshi uwezo katika kuziwezesha sekta binafsi kukua ili ziweze kuipunguzia Serikali mzigo mkubwa wa mamillioni ya Watanzania wasio na ajira. Katika kipindi hiki cha Serikali ya awamu ya tano watanzania wengi wamepoteza ajira Serikali, viwandani na hata katika biashara za watu binafsi kuliko kipindi kingine chochote kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo zile za waliokosa sifa za kitaaluma , chuki za kisiasa zilizopelekeaa wengine kuathirika na sakata hili la upotevu wa ajira, wafanyabiashara kufunga biashara zao au kuunguza wafanyakazi kutokana na kushindwa kumudu gharama za uendeshaji , kushuka kwa mapato ya kampuni mbalimbali yakiwemo makampuni ya simu, viwanda nya vinywaji,madini, vyombo nya habari, taasisi za kifedha , nyumba za starehe yakiwemo mabaa na hoteli, makampuni ya kitalii, maduka ya biashara ndogondogo

yaliyokuwa yanaajiri wafanyakazi chini ya watano lakini kutokana na hali ya uchumi idadi hiyo imeshuka zaidi n.k

**Mheshimiwa Spika**, Serikali hii imepunguza kabisa kufanya biashara na sekta binafsi kama mnunuzi mkuu wa bidhaa na huduma zinazotoka sekta binafsi. Hii ikiwa na maana kwamba kitendo cha Serikali kuagiza wakala kuwa taasis za umma zipewe kipaumbele katika biashara yaani Serikali kufanya biashara baina ya yenye kwa yenye kwa nia ya kubana matumizi mfano; kuhamisha taasis zake kutoka kwenye taasis binafsi za kifedha na kuzirudisha Bank Kuu, biashara ya usafirishaji, huduma za mahotelini n.k ni wazi kuwa mfumo huo unakwenda kuangamiza kabisa sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, kitendo cha Serikali kudhani kwamba kusitisha biashara baina ya taasisi zake na sekta binafsi ni kukata mirija ya ubadhiflu au ufujaji wa fedha za umma slo dhana yenye uhalisia. Kukwepa kufanya biashara na sekta maana yake ni kuua sekta binafsi ambayo hutoa ajira kwa maelefu ya Watanzania. Pale ambapo Serikali inalemewa na wimbi la watu wasio na ajira sekta binafsi huchukua jukumu hili. Pamoja na hayo, sekta binafsi inachangia mapato ya Serikali kuititia kodi inayokusanya kwenye bidhaa (income tax) na waajiriwa (payee).

**Mheshimiwa Spika**, hakuna nchi iliyowahi kufanikiwa kiuchumi bila kuruhusu ushindani wa kibiashara. Uchumi unakuwa kutokana na kukua kwa soko la kibiashara linalozingatia ushindani ambapo Serikali na sekta binafsi wote ni wadau. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha ili biashara baina ya sekta binafsi na Serikali ifanyike kwa weledi ni kuhakikisha sheria zilizopo zinazingatiwa na kuimarisha mifumo ya kudhibiti rushwa. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuchukua wajibu wake wa msingi wa kusaidia na kuziimarisha sekta binafsi ili ziweze kuwa na mchango mkubwa kwenye kuinua uchumi wa nchi. Vilevile, Kambi Rasmi inaitaka kuacha tabia ya kuwatishia wafanyakabiashara, kufunga makampuni ya wafanyakabiashara kiholela kwani kwa kufanya hivyo wanaoumia ni watanzania masikini wanaotegemea kuendesha maisha yao kuititia makampuni

hayo. Kuna msemo “usemao wapiganapo tembo ziumiazo nyasi”. Hivyo Serikali haina budi kutatuta changamoto zilizopo kwa wawekezaji na wafanyabiashara wa sekta badala ya kufanya kazi kwa jazba, kwa kutumia vyombo vya dola, kuwaumiza na kuwadhalilisha wawekezaji na wafanyabiashara

## VI. UCHUMI WA VIWANDA

**Mheshimiwa Spika**, uchumi wa viwanda ni maandalizi mtambuka na Wizara ya Viwanda na Biashara ndiyo inayotakiwa kutoa dira au mwongozo wa jinsi gani yakufika huko. Katika hili Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aweke wazi mpango mkakati wake hasa wa jinsi raslimali watu (*skilled labour*) itakavyopatikana na kutosheleza Tanzania ya Viwanda. Kwa mfano, wakati wenzetu Kenya wanajenga Reli ya Standard Gauge, Serikali yao ilipeleka wakenya wasiopungua 30 kwenda chini kujifunza utaalama mbalimbali kuhusiana na uendeshaji wa treini hizo za umeme.

- **Tanzania ya Viwanda, Ndoto au uhalsia?**

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na hotuba ya bajeti mbadala tulieleza kwa undani mashaka yetu kuhusu ndoto ya Tanzania ya Viwanda pamoja na hatua zinazochukuliwa kuelekea uchumi wa kati.

**Mheshimiwa Spika**, tulieleza kuwa ili Tanzania ifikie uchumi wa kati ni lazima sekta ya uzalishaji ichangie katika pato la taifa kwa asilimia 40 ifikapo mwaka 2025. Katika hali ya kushangaza sekta hiyo inachangia asilimia 5.2 pekee. Ni wazi kuwa kwa takwimu hizi hakuna uhalsia wa kuelekea uchumi wa kati wa viwanda isipokuwa propaganda ambazo zinapigwa kila mara bila kuzingatia uhalsia wa hali tuliyo nayo kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kauli mbalimbali ambazo zinatolewa na viongozi wa Serikali kuhusu uchumi wa

viwanda, katika kitabu cha mapendekezo ya mpango ukurasa wa 7 Serikali imeonesha na kukiri kuwa mwenendo wa mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi zilipungua kwa asilimia 29.8 kutoka dola za marekani milioni 1,273 Juni, 2016 hadi dola za marekani milioni 893.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takwimu hizo pamoja na kauli hiyo ya Serikali kuhusu azma ya Serikali ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati, Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana nayo kuwa bado tuna safari ndefu kutokana na ukweli kwamba, Serikali haitaki kuihusisha Sekta binafsi katika kushiriki kujenga uchumi wa nchi na hili linaonekana wazi kutokana na miswada na Sheria(Muswada wa Reli, Muswada wa Uwakala wa meli, muswada wa Shirika la Simu,n.k) zinazoletwa za kupoka ushiriki wa sekta binafsi kwenye sekta mbalimbali za uchumi na kuuweka chini na himaya ya Serikali. Kwa njia hii uwezo wa kufanya manunuzi kwa mwananchi unatoka wapi?

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kukusanya madeni ya miaka mitano hadi kumi ya huko nyuma kwa wafanyabiashara na kujitapa kuwa inakusanya vyema ili kujiveka katika nafasi ya kukopesheka, maana yake ni kuua uchumi wa nchi kwani uchumi unajengwa na sekta binafsi, viwanda haviwezi kujengwa na kuimarisha uchumi kutokana na kuongezeka kwa viwango vya kodi. Na pia kutokana na fedha za wahisani na mikopo, uko ni kujidanyanya kwa ujanja wa Mbuni kuficha kichwa wakati eneo lote la mwili wake liko wazi.

**Mheshimiwa Spika**, Viwanda sio jambo la kufikirika kama ilivyo sasa kwa Serikali ya inavyolifanya jambo hilo lieleweke kwa Watanzania, bali inatakiwa kuwa kitu kinachoonekana kwa macho na bidhaa zake zionekane sokoni, na ajira zinaonekana kwa watanzania. Ili kufikia hapo kuna mazingira wezeshi yanatakiwa yatayarishwe kwa wahusika (wawekezaji), tofauti na viwanda vinavyosemwa na kuaminisha watanzania kuwa sasa ni Tanzania ya viwanda bila ya kuonekana.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa viwanda ni mchakato ambao unahitaji kuangaliwa kwa upana kwa kuzingatia vigezo mahususi ikiwemo miundombinu wezeshi (huduma za kifedha, umeme,maji, barabara) teknolojia, masoko, kodi, mifumo yetu ya ajira, ubora wa bidhaa na namna ya kufanya biashara katika nchi. Kama soko la nje limeyumba kwa takwimu hizo kama ilivyoonesha na Benki Kuu ni dhahiri kuwa mpango wa Tanzania ya viwanda haujaandaliwa kwa kuangalia vigezo ambavyo vinahitajika kama ambavyo tumeainisha.

**Mheshimiwa Spika**, kuna haja ya Serikali kulieleza Bunge na Watanzania kwa ujumla kuhusu dhana ya viwanda na tafsiri yake ili tujue aina na ukubwa wa viwanda ambavyo vinasisitizwa kujengwa hapa nchini. Pamoja na vigezo vyta uanzishwaji wa viwanda kama tulivyoeleza hapo awali ni vema ikazingatiwa kuwa kuna aina kadhaa za viwanda kulingana na uwezo wa uzalishaji, teknolojia pamoja na namna ya usambazaji wa bidhaa zinazotokana na viwanda hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa sherehe za kitaifa za kuzima mwenge tarehe 14 Oktoba, 2017 Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania alinukuliwa akisema kuwa mwenge umezindua viwanda 148 ambapo viwanda hivyo vimejengwa kwa thamani ya shilingi bilioni 468 ambapo ajira 13,370 zinatarajia kuzalishwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kitabu cha mapendekezo ya mpango ukurasa wa 26 hadi 29 Serikali imeorodhesha vinavyoitwa viwanda 50 ambavyo kati ya hivyo viwanda 32 vimeshakamilika na kuanza uzalishaji na viwanda 18 vinaendelea kujengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhaja juu utofauti wa takwimu ambazo zimetolewa na Mkuu wa Nchi na ambazo zimeoneshwa katika kitabu cha mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa mwaka 2018/2019. Je takwimu halisi za viwanda ni zipi?

**Mheshimiwa Spika**, Kitabu cha mwongozo pamoja na kile cha Mapendekazo ya Mpango vinaonesha kuwa mikopo kwa sekta binafsi imepungua kutoka asilimia 19.1 Juni, 2016 hadi asilimia 1.3 Juni, 2017. Serikali imeeleza kuwa anguko hilo linatokana na tahadhari zilizochukuliwa na mabenki kutopteka na mikopo hiyo kushindwa kurejeshwa/kulipwa au kwa maneno ya Waziri "kuongezeka kwa mikopo chechefu"

**Mheshimiwa Spika**, ukichunguza kwa makini ni kuwa kuna anguko kubwa la shughuli za biashara na uwekezaji nchini. Serikali haijaaeleza sababu za msingi zilizopelekea wafanyabiashara pamoja na wawekezaji wengine kushindwa kulipa mikopo katika benki za biashara na kupelekea benki kupunguza mikopo.

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa kuna idadi kubwa ya biashara ambazo zimefungwa kutopteka na hali mbaya ya uchumi, kodi za Serikali zisizotabirika pamoja na kauli na maelekezo ya viongozi ambazo zinafanya wawekezaji na wafanyabiashara kuogopa kuwekeza katika nchi yetu ni kikwazo kuelekea uchumi wa viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Waziri wa Fedha na Mipango ilieleza kuwa pamoja na idadi kubwa ya biashara kufungwa, bado kuna idadi kubwa ya biashara zilizosajiliwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaanini kuwa kusajili biashara ni jambo moja na kuanza kufanya biashara na kuanza kupata faida ni jambo lingine. Kwa hiyo kitendo cha Serikali kujitetea na takwimu za kusajili biashara mpya ni ishara ya udhaiju mkubwa wa namna ya kusimamia mazingira ya uwekezaji na biashara nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Mwezi oktoba mwaka huu Waziri wa TAMISEMI amenukuliwa na vyombo vyahabari akielekeza kila Mkoa kujenga viwanda 100 ambapo mpaka Desemba 2018 katika Mikoa yote ya Tanzania bara itatakiwa kuwa na viwanda 2600. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangazwa na maelekezo haya, hii ni kwa sababu kama mikopo kwa sekta binafsi imepungua kama Serikali inavyokiri

na kama Serikali haifanyi biashara, hivyo viwanda vinaenda kujengwa na nani?

**Mheshimiwa Spika**, Kama Serikali haitakaa chini na wafanya biashara na wadau wa sekta binafsi kuhusu namna ya kutekeleza maelekezo haya kutakuwa na matatizo makubwa huko mbeleni kwa sababu mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi yameshuka, mikopo kwa sekta binafsi iko taabani, soko la ndani limeyumba kutokana na watu kushindwa kununua bidhaa, mzunguko wa fedha umeshuka, pamoja na mzigo wa kodi kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, ieleweke kwamba kuwa na uchumi ambao sekta binafsi inayumba, maana yake ni kukosesha Serikali mapato na hivyo kushindwa kutoa huduma za jamii. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa sasa Serikali inafikiri kwa mfumo wa uchumi wa kijamia ilia inapenda mafanikio ya uchumi wa kibepari au soko huria, jambo ambalo haliwezekani katika karne hizi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekiri kuwa kama Taifa tuna safari ndefu kuelekea uchumi wa kati, hii ni kutokana na pato la kila mtu kuendelea kuwa chini. Naomba kunukuu ukurasa wa saba wa kitabu cha mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019;

*"....wastani wa pato la kila mtu katika Dola za marekani uliongezeka kidogo kutoka dola 967.5 mwaka 2015 hadi dola 979.1 mwaka 2016, hii inamaanisha kuwa bado tuna safari ndefu kuingia katika kundi la uchumi wa kati."*

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeeleza kwenye mapendekezo ya mpango kuhusu kufungamanisha uchumi, jambo hili linaweza kuwa jema lakini kama taifa lina matatizo ya utawala bora, haki za binadamu haziheshimiwi, ukiukwaji wa Katiba na kuyumba kwa uchumi, kufungamanisha uchumi itakuwa ndoto na si la uhalisia. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutetea na kutekeleza Katiba ya nchi na sio kila mara inatoa kauli ambazo zinakiuka misingi ya utawala bora. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa

hakuna ukuaji wa uchumi wala uchumi wa viwanda Serikali inakiuka misingi Katiba na utawala bora.

## VII. DENI LA TAIFA

**Mheshimiwa Spika**, Deni la Taifa ni kati ya nyenzo muhimu katika kurekebisha thamani ya sarafu na hivyo kuimarisha uchumi wa nchi. Katika kufanya hivyo ni muhimu kuwa na sera makini za fedha katika kuhakikisha deni hilo linaleta malengo tarajiwa katika uchumi. Kama deni au mikopo itatumiwa vibaya inaweza kuwa balaa kubwa kwa nchi badala ya kuwa Baraka.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu<sup>1</sup> zinaonesha kuwa hadi kufikia June,2017 Deni la Taifa liliifikia dola za Marekani milioni 26,115.5 sawa na shilingi za kitanzania trillioni 60.287 kwa kutumia kiwango cha ubadilishaji fedha cha dola moja ya Marekani kwa shilingi za Tanzania 2,308.5. Ukilinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka 2016 liliikuwa dola za Marekani milioni 22,320.76 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 17.

**Mheshimiwa Spika**, mikopo inayokopwa kwa shughuli za kiuchumi ni ya aina mbili, mikopo ya riba nufuu na mikopo ya kibiashara. Katika wasilisho letu Kambi Rasmi ya Upinzani iliuliza ni kwanini Serikali inakopa mikopo ya kibiashara? Kwa kuwa nchi ipate mikopo yenye riba nafuu ni lazima kwanza ifanyiwe tathmini yaani "credit Rating" kuangalia kama inakidhi vigezo.

*"A credit rating is an evaluation of the credit risk of a prospective debtor (an individual, a business, company or a government), predicting their ability to pay back the debt, and an implicit forecast of the likelihood of the debtor defaulting."*

Aidha, tuliiata Serikali kulieleza Bunge mara ya mwisho kwa Tanzania kufanyiwa Credit Rating ni lini? Kinyume cha hapo,

---

<sup>1</sup>Mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka 2018/19, aya ya 26

kuendelea kupata mikopo ya kibashara ni kuendelea kuwatwisha zigo la misumali watanzania, na njia hii ya mikopo haiwezi kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati na Tanzania ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Wizara inasema kuwa kuongezeka kwa Deni la Taifa ni matokeo ya mkopo wa kujenga Reli kwa "**standard gauge**". Hapa Kambi Rasmi ya Upinzani na watanzania wengi tunaona kuna utata, kwani Mheshimiwa Rais Magufuli mara kadhaa amesikika akisema kuwa fedha za makusanyo ya ndani ndio yanayojenga Reli, yananaa ndege, yanajenga barabara n.k na hapa taarifa inasema ni fedha za mkopo.

**Mheshimiwa Spika**, katika wasilisho la waziri Kivuli kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano tarehe 27/04/2017 kuhusu ujenzi wa Reli alisema kwamba, nanukuu;

*"Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa reli kati ya Dar es salaam – Morogoro (km 202), ni mkataba na kampuni ya kutoka nchini UTURUKI. Mkataba huo ni wa Tsh trillioni 2.5 ujenzi wa reli ya Dar es salaam – Morogoro zote zikiwa ni fedha za ndani kama Mhe Rais alivyosema, lakini pale pale anasema Waturuki ndio watajenga kwa fedha za mkopo, Kambi Rasmi inataka kufahamu ukweli ni upi katika hilo?"*

**Mheshimiwa Spika**, awali Watanzania tuliaminishwa kuwa Reli hii mpya itajengwa na Wachina kwa kutumia mkopo toka EXIM Bank ya Uchina. Tanzania ilituma timu ya viongozi Uchina akiwemo Rais Mstaafu wa Awamu ya NNE, Waziri wa Ujenzi na timu hiyo iliporudi tuliami biwa China imekubali kutusaidia na hatajenga kipande hiki cha Dar-Moro, ilipotangazwa makampuni mengi ya Kichina yalichukua vitabu lakini hawakuvirudisha.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa zilizochapishwa na gazeti la kila siku la The Citizen katika ukurasa wa mbele zilieleza kuwa benki ya Exim kutoka china ilikubali kutoa mkopo wenye riba nafuu wa Tsh trillion 17.5 au dola za Kimarekani bilioni 7.6 kwa ajili ya kuanza rasmi na kukamilisha ujenzi huo wa reli ya kati

huku Serikali ya Tanzania ikitangaza kutoa Tsh trillion 1, kwa ajili ya hatua za awali za mradi huo. Aidha baadhi ya watanzania pia wanafahamu kuwa Tanzania iliomba mkopo wa fedha kutoka India kiasi cha Tsh Trillion 17.5 ili kufanikisha ujenzi wa reli ya katii.

**Mheshimiwa Spika**, habari ya Benki ya Exim ya China kukubali kutoa mkopo wenye masharti nafuu wa dola za Marekani Bilioni 7.6 sawa na Zaidi ya shillingi trillion 17.6 za kitanzania kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa mradi mkubwa wa reli ya katii kwa kiwango cha kisasa, na taarifa za utiaji saini makubaliano ya awali ya ujenzi wa reli ya katii (standard gauge) ziliripotiwa pia na Serikali kupitia kitengo cha mawasiliano Serikalini, Wizara ya Ujenzi , Uchukuzi na Mawasiliano na shirika la Utangazaji la Uingereza BBC, tarehe 20 julai , 2016 . Aidha kwa mujibu wa taarifa hiyo, mradi wa ujenzi wa reli ya katii utahusisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha kisasa kutoka Dar es salaam - Tabora- Isaka- Mwanza. Tabora - Mpanda - Kalemela. Tabora - Uvinza- Kigoma na Isaka- Keza -Msongati.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kutoa kauli sahihi kuhusu mkanganyiko huu, je, Ni kweli reli ya katii inajengwa kwa fedha za ndani kama ambavyo inasemekana? Ikiwa ni ndiyo je mkopo kutoka benki ya Exim China unahu ujenzi wa reli ipi na nini kilichotokea makampuni ya China ambayo yalikuwa awali yanatajiwa kujenga mradi huu kutojenga na ghafla kampuni ya kutoka nchini UTURUKI ikapewa tenda hiyo? Ni vyema watanzania ambaao wanawajibika kulipa mikopo hii kupitia kodi zao, wakaondolewa sintofahamu iliyopo mionganoni mwao”.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaelewa umuhimu wa kukopa kama mtu mmoja mmoja, taasisi na nchi. Lakini kama ambavyo Bunge hili limekuwa likiitaka Serikali kwamba ni muda mwafaka sasa Serikali iweke wazi mipango yake ya fedha za mikopo. Ni jambo la ajabu na aibu kwa fedha za mikopo au misaada kutumika katika mipango ambayo haimnufaishi mtanzania moja kwa moja.

## VIII. SEKTA YA FEDHA

**Mheshimiwa Spika**, ni ukwelli kwamba uchumi imara katika nchi yoyote ile unajengwa na taasisi imara za fedha katika nchi husika, *"Stable economic growth requires a strong and trustworthy financial sector"*. Taasisi za fedha ndio nguzo kubwa katika kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa Kati na hivyo Tanzania kuwa nchi ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine ili kuwa na taasisi imara za fedha ni lazima awepo mwezeshaji wa hilo ambaye ni Benki Kuu katika kuweka miongozo iliyo sahihi na yenye tija kwa pande zote; kwa maana benki za biashara na wakopaji, pamoja na Serikali yenye. Uchumi wa kati unahitaji uwekezaji mkubwa au mikopo ya muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, ili kilimo cha Tanzania kiwe na tija inayokusudiwa ni lazima mikopo ya kilimo itolewe kwa wakulima wa aina zote, kwa maana ya wakulima wadogo na wakulima wakubwa. Mapinduzi ya kilimo hayawezi kuletwa kwa wakulima wadogo kuwa manamba katika mashamba makubwa ya wawekezaji, hivyo basi sekta imara za fedha pamoja na sera sahihi na wezeshi za benki katika kulfikia hilo. Mkopo wa kilimo kuanza kulipwa chini ya kipindi cha miaka mitano ni jambo ambalo haliwezi kumsaidia mkulima. Aidha, viwanda haviwezi kujengwa kwa kutegemea watu kutoka nje inatakiwa mazingira ya ujenzi wa viwanda yatengenezwe na Serikali yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa jambo hili la kutengeneza mazingira ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda hayapo.

**Mheshimiwa Spika**, msukumo na utaratibu unaotumiwa na Serikali katika suala zima la Kodi unafanywa kwa "personalities" na kukomoana zaidi badala ya kuwa wezeshi ili watanzania wajenge msingi mzuri wa ujenzi wa viwanda. Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona hili kutokana na usemi alioutoa Mheshimiwa Rais kwamba, Watanzania wote tunatakiwa kuishi katika kiwango kimoja cha maisha, eti kuna watu walikuwa wanaishi kama malaika sasa wote tuishi kama mashetani. Jambo hili haliwezekani na linaondoa

ubunifu binafsi katika utendaji wa kazi, hata nchi za kijamaa wananchi wake hawana uchumi unaolingana.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, falsafa hiyo ya watu wote tuishi kama mashetani ambayo inatekelezwa kwa sasa ndiyo inapelekea taasisi za fedha kushindwa kubeba uchumi wetu.

**Mheshimiwa Spika**, ni lazima tukubali kwamba vipawa vyatua fursa mionganini mwa watu vinatofautiana na taasisi za fedha ndio chombo cha kuzifanya fursa na ndoto za watu kuwa na uhalisia.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani yanapewa nguvu na taarifa ya Serikali<sup>2</sup> inayoonesha kuwa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulipungua kutoka asilimia 19.1 Juni 2016 hadi asilimia 1.3 mwezi Juni 2017. Kupungua kwa kasi hiyo kulitokana na tahadhari iliyochukuliwa na benki za Biashara katika kutoa mikopo kwa sekta binafsi kufuatia kuongezeka kwa mikopo chechefu, kupungua kwa mikopo kwa sekta binafsi kunaweza kupunguza fedha za uwekezaji kwa sekta binafsi na biashara na hatimaye kuathiri ukuaji wa uchumi.

**Aidha, Mheshimiwa Spika**, taarifa<sup>3</sup> inaonesha kuwa mzunguko wa sarafu kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni shilingi bilioni 12.4 wakati kwa mwaka 2015/16 ilikuwa ni shilingi bilioni 61.2 na kwa mwaka 2014/15 ilikuwa na shilingi 299.1. Serikali inasema ni kutokana na Sera ya kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo na tija na kupungua kwa kasi ya utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Wakati huo huo Serikali inakusanya kila pahala kwa halali au kwa haramu. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwa kuangalia tofauti ya mzunguko wa sarafu na sababu zinazotolewa na Serikali ni dhahiri tunatatizo mahali fulani na kwa Lugha rahisi ni kwamba

---

<sup>2</sup> Mwongozo wa maandalizi ya Mapango na Bajeti kwa mwaka 2018/19 aya ya 3

<sup>3</sup> Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19 kielelezo 1.8

Serikali inavuna pale isipopanda. Kama benki zinapunguza utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi ni kwa vipi uchumi binafsi wa Watanzania utaimarika?

**Mheshimiwa Spika**, udhaifu wa hoja hiyo ya kupunguza matumizi kwa Serikali ni kuwa Serikali bado inaongeza taasisi mpya na hivyo kuzidisha matumizi na jambo hili linaenda kinyume na azma ya Serikali kujitoa katika uendeshaji wa biashara katika sekta mbalimbali.

a. **Mwenendo wa viwango vya Riba**

**Mheshimiwa Spika**, viwango vya riba vinavyotolewa na mabaenki ni motisha au kikwazo katika ujenzi wa uchumi shirikishi katika nchi. Riba inayoongelewa hapa ni zile zinazotolewa katika ununuzi wa dhamana za Serikali na zile katika mikopo inayotolewa kwa sekta binafsi na taasisi za fedha.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu<sup>4</sup> zinaonesha kuwa riba ya dhamana za Serikali (treasury bills and treasury Bonds) zilishuka kutoka wastani wa asilimia 15.56 kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2016/17 hadi kufikia asilimia 7.64 kwa mwezi Juni 2017. Dhamana za Serikali ndiyo njia maarufu kwa Serikali kukopa katika mabenki ya Biashara au kwa watu binafsi wenye fedha za kutosha. Kambi Rasmi ya Upinzani ilikwisha shauri kwamba ili kuondoa mashindano ya kukopa na kukopesha kwa Taasisi za Fedha, Serikali ilitakiwa kuwe riba za chini ya asilimia 5 kwa dhamana za Serikali ili Taasisi za fedha badala ya kukimbilia kuikopesha Serikali basi, fedha hizo zielekezwe kwenye sekta binafsi. Kuweka Riba hiyo kwa dhamana za Serikali maana yake ni "**clean business**" kwa mabenki kwani hakuna haja ya benki kuomba dhamana kwa maana ya "**corateral**" kwa mkopaji ambaye ni Serikali na hivyo mabenki yatapenda kuikopesha Serikali badala ya sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, mbali na motisha ya riba inayotolewa

---

<sup>4</sup>Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19- Aya 33

na Serikali kwenye dhamana zake bado inailazimu Serikali kukopa kwenye taasisi za fedha kwa riba ambazo zinatolewa kwa wakopaji wa sekta binafsi. Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa riba za amani ni asilimia 9.61 na wastani wa riba za mikopo ni asilimia 16.53 kwa mwaka 2016/17. Kambi Rasmi kwa hili inaona tuna matatizo katika sera zetu za fedha na pia tunarudia wito wetu kuwa kuna umuhimu wa haraka wa nchi yetu kufanyiwa "***credit Rating***" ili kukidhi viwango vyta kuweza kupata mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu. Kwa njia hii Serikali haitakuwa tena inashindana na Sekta binafsi katika kukopa kwenye taasisi zetu za fedha.

**b. Matakwa ya dhamana katika kupata mkopo**

**Mheshimiwa Spika**, sio tu viwango vyta riba vinavyoifanya sekta ya benki kufanya vizuri au vibaya, bali pia kuna matakwa yanayohitajika katika kupatiwa mkopo.

**Mheshimiwa Spika**, Watanzania wengi wenye nia na malengo ya kuwa wajasiriamali wanashindwa kutimiza azma zao kutokana na matakwa yasiyotimilizika yaliyowekwa na taasisi za utoaji fedha na hivyo kuufanya uchumi wetu usikue kwa kuwafanya vijana kuendelea kutegemea kazi za kuajiriwa badala ya wao kujajiri.

**Mheshimiwa Spika**, ukiangalia utafiti uliotolewa na taasisi isiyo ya Serikali lakini inafanyakazi zake kwa kushirikiana na Idara kuu ya Takwimu pamoja na Benki kuu ya Tanzania inayoitwa ***Financial Sector Deepening trust(FSDT)*** katika jarida lake la ***FinScope Tanzania 2017 uk.53*** inaonyesha kuwa kati ya watanzania millioni 27.86 wenye umri zaidi ya 16, ni asilimia 3 tu ndio walipata mikopo toka benki, asilimia 2 kutoka taasisi rasmi za fedha zisizo benki, asilimia 2 kutoka kwenye SACCOS, asilimia 18 vikundi vyta kusaidiana mitaani, asilimia 69 kutoka kwenye familia na marafiki , asilimia 1 kutoka kwa waajiri mbalimbali na asilimia 4 kutoka kwenye mitandao ya simu.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo za ukopaji ni kielelezo kwamba bado asilimia kubwa ya watanzania bado haitumii huduma zinazotolewa na taasisi rasmi za kifedha na hasa

benki na badala yake huduma zinatolewa na taasisi zisizo rasmi katika kutoa mikopo. Fedha zinazotolewa na hizo taasisi haziwezi kuleta tija katika kujenga uimara wa sekta isiyo rasmi na hivyo kujenga uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, masharti na matakwa ya mikopo ni mojawapo ya vigezo vinavyotolewa na Benki Kuu, hivyo kwa kuwa benki hiyo ndiyo msimamizi wa taasisi zote za fedha inalazimika kupitia upya vigezo vyake au maelekezo wanayotoa kwa taasisi za fedha.

## IX. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu kwa sasa inapitia katika kipindi kigumu sana ambacho hata mtu kusema nchi yetu ina amani na usalama ni kujivisha kilemba cha ukoka, naomba kunukuu kauli ya *Pope Paul VI kwamba*;

*"If you want peace, you must work for justice. Justice is our biggest challenge. We need to work for it. But because of lack of functional law enforcement system we need to work even harder for justice and organize ourselves better."*

Je, amani ni kutokuwepo kwa vita? Kama ambavyo tunalazimishwa kuaminishwa? Watanzania wenzetu wamebomolewa nyumba zao ilhali kuna zuio la mahakama kuhusu ubomoaji na sasa wanalala nje kama sungura matope au digidigi na kukimbizana na vibaka, hapo hapo watu wengine biashara zao zimefungwa kwa kudaiwa kodi isiyoendana na uhalisia wa biashara zao ya miaka mitano au sita iliyopita. Hapa amani na utulivu vinatoka wapi?

**Mheshimiwa Spika**, sasa hivi kila mtu anaogopa watu wasiojulikana ambao kwa sasa wamekuwa tishio kubwa kwa uhai wetu, na mali zetu na vyombo vyenye mamlaka ya kulinda maisha yetu na mali zetu haviwafahamu watu hao wasiojulikana. Hivi usalama uko wapi?

**Mheshimiwa Spika**, uchumi imara unategemea pia hali ya kisiaza katika nchi, kama viongozi wa upinzani wanawindwa

kuuawa na wengine wanafunguliwa kesi zisizokuwa na uhakika na mwisho baada ya kupewa adhabu ya kukaa mahabusu wiki nzima wanaachiwa. Haya mambo yanapelekea uchumi wetu kuporomoka.

**Mheshimiwa Spika**, nijukumu la Bunge hili kuhakikisha kuwa wale tunaowawakilisha wanaendelea kuwa na imani na sisi wawakilishi wao katika kusimamia usalama wao kwa kuiambia Serikali maana halisi ya utawala wa Katiba na Sheria na hivyo kupambana na wale wanaoitwa "wasiojulikana".

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
**David Ernest Silinde (Mb)  
K.n.y Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi-  
Wizara ya Fedha na Mipango  
7 Novemba, 2017**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde kwa kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa  
unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na  
Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali  
kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

#### **KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Lubeleje na baadaye Mheshimiwa Maftaha Nachuma ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niunge mkono tu haya yote ambayo yamezungumzwa. Mipango ni mizuri sana, tunapanga vizuri sana lakini tatizo letu kubwa ni utekelezaji na utekelezaji umezorota kwa sababu fedha haziendi Mikoani, fedha haziendi Wilayani. *TRA* wanajitahidi sana kukusanya mapato, wanakusanya sana, lakini fedha haziendi kwenye Halmashauri, haziendi Mikoani; miradi mingi imekwama na tunategemea sana wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani wakati umefika sasa wa kupunguza hii misaada, kwa sababu tukitegemea sana wafadhili ipo siku wafadhili watasema sasa sisi tunajiondoa, Kwa hiyo, tujitahidi sana kutumia fedha zetu za ndani. Miradi mingi imekwama, kwa mfano katika Jimbo langu la Mpwapwa kuna barabara hii ya kutoka Mbande, kwenda Kongwa mpaka Mpwapwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwamba ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umeshaanza tayari, lakini bado wapo kipande cha Mbande hawajafika hata njia panda ya Kongwa.

Kwa hiyo, mimi ni mategemeo yangu kwamba wananchi wa Jimbo la Mpwapwa wategemee kwamba barabara hii itakamilika kwa wakati, kuanzia Mbande - Kongwa mpaka Mpwapwa kwa kiwango cha lami, naisubiri kwa hamu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu misamaha ya kodi. Ni kweli kisheria inaruhusu kwamba baadhi ya wafanyabiashara wasamehewe kodi, lakini hii inatupotazea mapato mengi sana. Ninaishauri Serikali kwamba ipunguze misamaha ili fedha nydingi zikusanywe ziende katika miradi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa kodi ya majengo kwenye Halmashauri zetu. Tulishaishauri Serikali

kwamba utaratibu huu kwa kweli ni mgumu sana. Halmashauri nyingi zilikuwa zinakusanya kodi ya majengo vizuri sana, hii *property tax*.

Kuna Halmashauri ambazo zinaweza zisitegemee hata ruzuku ya Serikali kwa kutegemea mapato yao ya ndani (*own source*). Kwa mfano Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam walikuwa wanajitahidi sana kukusanya *property tax*, lakini baadaye Serikali ikaamua kwamba inakusanya yenyewe. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba taarifa, ni kiasi gani kimeshakusanya na kiasi gani kimesharudishwa kwenye hizi halmashauri zetu. Tulikwishakataa jambo hili; tuachie halmashauri zenyewe zikusanye kwa sababu *property tax* ni chanzo kimoja wapo cha mapato ya ndani kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maghala yetu ya hifadhi ya chakula cha msaada. Kila mwaka tunatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa maghala na Serikali imenunua chakula kingi sana cha akiba, lakini jambo la kushangaza ukame unaendelea katika nchi yetu chakula hawagawi, njaa inaendelea hasa katika Jimbo langu la Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla. Hali ni mbaya sana. Watu hawana chakula, sasa hivi wameanza kuandaa mashamba yao lakini hakuna chakula; kwa nini Serikali isianze kugawa chakula cha msaada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatusemi kwamba kuna njaa maana Serikali inazuia neno la njaa, inasema upungufu wa chakula, lakini mimi nadhani upungufu wa chakula na njaa ni neno lilelile tu. Kwa hiyo, hakuna haja ya kuhifadhi chakula kwenye maghala na chakula kinaharibika. Serikali ianze kugawa chakula maeneo yote ambayo yana upungufu wa chakula au yana njaa, chakula kitaharibika kwenye maghala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Ujenzi wa Vituo vya Afya Jimbo la Mpwapwa. Ninashukuru sana Kituo cha Afya Mima kimepata shilingi milioni mia tano safari hii, lakini bado Kituo cha Afya cha Mbori hakijakamilika. Ninaomba sana

fedha itolewe, vituo vikamilike ili huduma iweze kutolewa kwa maeneo yale. Vituo vya afya vinasaidia sana hasa wale akina mama wajawazito badala ya kupelekwa Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa wanahudumiwa kwenye vituo vya afya kwa sababu pale kuna *Assistant Medical Officer* au *Clinical Officer* ambao wale ni *trained* au wale madaktari wasaidizi wanakuwepo kwenye vituo vya afya kwa ajili ya *operation* ndogo ndogo. Kama akina mama wanashindwa kujifungua basi wanafanyiwa *operation* ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo; nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono asilimia mia moja hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini tukusanye fedha na tutekeleze miradi. Fedha ipelekwe halmashauri na mikoani. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha Nachuma atafuatiwa na Mheshimiwa Japhary Michael ajiandae.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mwelekeo huu wa mpango asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia mwelekeo huu wa mpango, naomba Nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu-Wataala* ambaye ameendelea kunijalia afya njema leo hii, lakini pia niweze kumshukuru Mwenyekiti wa chama changu, Chama cha Wananchi (CUF), *full-bright* Profesa Ibrahim Haruna Lipumba, kwa kuendelea kushirikiana vizuri kutetea maslahi ya Watanzania na hasa katika rasilimali zetu za madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze kuzungumza kidogo kwamba sisi Chama cha Wananchi (CUF) ilani zetu zote za uchaguzi kuanzia mwaka 1995, mwaka 2000, mpaka mwaka 2010 tulikuwa tunazunguka Tanzania nzima kuwaeleza Watanzania ya kwamba rasilimali za madini ya nchi hii zinatumiwa kwa kiasi kikubwa na wageni wa nje na sisi wenyewe kila shilingi 100 tunapata shilingi tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nizungumze katika Bunge lako hili kwa namna ya kipekee kabisa niweze kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu huyu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba anasimamia llani ya Chama cha Wananchi (CUF), anasimamia itikaChama cha Wananchi (CUF), Sera ya Utajirisho kwamba madini yetu yaweze kuwanufaisha Watanzania na sisi lazima tuunge mkono kama chama imara cha siasa, CUF - Chama cha Wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia mwelekeo huu wa mpango kwa kusema ya kwamba viwanda kwa kiasi kikubwa sana, nilikuwa nasikiliza hotuba zote mbili, hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hotuba ya Kamati ambazo zimezungumzia suala zima la viwanda, na tumekuwa tunazungumza sana kwamba sehemu hii ya viwanda ni sehemu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kusema katika Bunge hili wakati nachangia mpango mwaka wa jana na mwaka wa juzi, kwamba nchi nyngi duniani ziliweza kuendelea kupitia sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karne ya 15, ukisoma historia, sisi tuliosoma historia tunaambiwa ya kwamba nchi zote za Ulaya ziliweza kufanya mapinduzi ya viwanda na hatimaye wakaweza kuwa matajiri mpaka leo hii tunasema wao ndio wanaotusaidia sisi nchi za ulimwengu wa tatu. Kwa hiyo, kwa umuhimu wake hili suala ni suala nyeti sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la ajabu, tulikuwa tumezungumza wakati wa bajeti hapa kwamba wapo wawekezaji wengi wanaohitaji kuwekeza Tanzania. Kule Mtwara kuna wawekezaji wa Kijerumani na Kamati hapa imeeleza ambao wanataka kujenga viwanda vyatya mbolea, pale Mtwara Msangamkuu. Kule Kilwa pia kuna mwekezaji ameamua kuwekeza kwa kujenga kiwanda cha mbolea, lakini bado Serikali tunaona inasuasua kuwapa rasilimali ya gesi wale wawekezaji ili waweze kujenga vile viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini viwanda vikijengwa pale Mtwara Msangamkuu wananchi wengi wa Mtwara watapata ajira, wananchi wa Kilwa kule kikiwepo kiwanda watapata ajira na umaskini utaweza kuondoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana katika mwelekeo huu wa mpango kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hotuba yake atueleze kwa nini mpaka leo wale wawekezaji wanaotaka kuwekeza viwanda vyta mbolea pale Msangamkuu, Mtwara Vijiji ambapo ni karibu kabisa yaani ni pua na mdomo katika Jimbo langu la Mtwara Mjini, lakini pia kule Kilwa bado mpaka leo Serikali inasuasua kuwapa wale wawekezaji gesi waweze kujenga viwanda vyta mbolea ili kuweza kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala la umeme *REA*. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, amezungumza hapa kwa kiasi kikubwa kwamba umeme unaotumika mikoa ya kusini unatoka Mtwara Mjini, viwanda vyta kusindika ile mitambo vimejengwa Mtwara Mjini, lakini jambo la ajabu nimekuwa ninazungumza sana, kwenye Mabunge yako yote nimekuwa nazungumza hili; kwamba pale Mtwara Mjini kwenyewe ambapo ndipo mitambo yote ya kusindika umeme ipo, bado kuna maeneo mengi haujapelekwa mtandao wa umeme ikiwemo kule Mbawala Chini, Naulongo, Mkunjanguo na maeneo mengine ambamo pia tulisema kwamba mule mnapita kitu kinachoitwa mkuza wa gesi, lile bomba la gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumelia sana kwa muda mrefu katika Bunge hili na Mheshimiwa Waziri akiwa anaahidi kwamba atapeleka umeme kule kote. Sasa ni jambo la ajabu sana kwamba kila mwaka tuwe tunarudia na kurudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba katika Mpango huu ambao unaandaliwa, hili suala la kuhakikisha ya kwamba umeme wa *REA* unasambazwa basi usambazwe kwenye maeneo yote kwa sababu wananchi wa maeneo

yale ambapo ni vijiji ambavyo viko mjini lakini bado tunaita ni vijiji kwa sababu vinahitaji kupita umeme wa *REA* uweze kwenda kule; Tunaomba Serikali ihakikishe ya kwamba inapeleka na sio kila mwaka kupiga dana dana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vijiji vingi pia kule Mtwaro na Lindi, bado, na wakandarasi wenyewe waliopewa ukiwauliza wanatuambiwa huko sisi hatuna bajeti, bajeti yetu sisi ni kutoka kijiji hiki tunaingia vijiji vya Tandahimba, Newala na wapi, lakini bado tunahitaji wananchi wale waweze kupelekewa umeme. Ili tuweze kuondokana na umaskini lazima kila kijiji, hata kama kipo mjini, basi umeme uweze kufika. Tunaomba sana hili Mheshimiwa Waziri aje atueleze mpango huu wa maendeleo ameliwekaje mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka nilizungumze hapa ni suala la kilimo. Katika Mkutano wa Bunge wa bajeti, wakati tunapitisha Bajeti ya Wizara ya Kilimo nilizungumzia suala zima la korosho. Kulikuwa na suala la mboleo, nilieleza wakati ule na nilimnukuu mtaalam mmoja anaitwa Kunz, mwaka 1988/1989 katika kitabu chake cha *Managerial*, alisema kwamba *failure to plan is planning to fail*, kwamba ukifeli kupanga maana yake unapanga kufeli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza suala la mbolea, kwamba walisema kwamba watagawa mbolea bure kwa wakulima wetu wa korosho lakini halikupangwa lile; na hapa leo kwenye mwelekeo huu wa Mpango bado sijaona pia kama limepangwa. Kilichotokea wakulima wamelanguliwa mbolea badala ya kuuziwa shilingi 20,000 wakanunua mbolea mfuko mmoja shilingi 100,000, 150,000 wengine mpaka shilingi 200,000 baadhi ya maeneo, ni kwa sababu Serikali ilishindwa kupanga sawasawa suala hili la kugawa mbolea bure kwa wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na korosho ndilo zao ambalo linaingiza pesa nyingi Serikalini kuliko zao lolote. Linaanza zao la korosho *then* inakuja tumbaku. Kwa hiyo, ninaomba

kwamba mpango wetu wa safari hii upange sawa sawa, kwamba ni kiasi gani cha mbolea kitapelekwa kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la ajabu katika korosho pia, nilikuwa napitia taarifa za masoko ya dunia; bei ya korosho soko la dunia, kilo moja ni dola 29. Ukijumuisha, ukigawa kwa pesa yetu ya Kitanzania ni sawa sawa na *almost* kama shilingi 49,000; shilingi 50,000 hivi kwa kilo moja, katika soko la dunia. Kama Bandari ya Mtwara itatumika sawa sawa, ukisafirisha korosho kutoka Bandari ya Mtwara mpaka soko la dunia, bei ya korosho haizidi kilo moja shilingi 2,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana, pamoja na kwamba tunajigamba, na tunashukuru kwa kweli kwamba Serikali imejitahidi kuongeza bei ya korosho kwa wakulima, hivi sasa ni shilingi 3,800 mpaka 3,850, lakini bado mkulima angeweza kupata bei kubwa zaidi ya hii kutokana na umuhimu na unyeti wa zao la korosho duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali ihakikishe inatafuta wanunuzi wa korosho ili korosho yetu hii iweze kuingiza pesa nyingi zaidi ya hizi ambazo tunazipata Hazina, lakini kwa wananchi wetu waweze kuondokana na umasikini, hasa maeneo ya Mtwara na Lindi pamoja na Pwani na maeneo mengine wanayolima korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ajabu sana nilikuwa napitia taarifa pia za kimtandao kwamba hata katika zile nchi ambazo zinalima korosho duniani, Tanzania haipo. Afrika kuna *Côte d'Ivoire*, imewekwa Afrika Kusini, imewekwa Thailand na nchi nyingine, Tanzania sisi tunajulikana kwamba hatulimi korosho wakati wanunuzi waliopo Thailand, wanunuzi waliopo India wanakuja kununua korosho Tanzania. Hili linapoteza pia thamani na pato zaidi. Kwa sababu hawa wanunuzi wa kule nchi za nje wanakwenda kununua kule kwenye nchi ambazo zimewekwa kwenye taarifa mbalimbali za kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hili mlizingatie, ni jambo la muhimu sana...

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:**...jambo lingine ambalo ninaomba kuchangia katika huu Mpango ni sekta ya utalii nchini. Ninaomba kuzungumzia suala zima la sekta ya utalii nchini...

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nachuma, subiri kidogo. Taarifa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimrekebishe mzungumzaji. Si kwamba duniani Tanzania hajulikani kwa kuzalisha korosho isipokuwa sisi hatuuzi korosho iliyobanguliwa, kwa hiyo hiyo *list* aliyoinona ni *list* ya mataifa yanayouza korosho ambayo tayari ilishakuwa *processed*. Kwa kuwa sisi hatubangui, kwa hiyo, hatupo kwenye *list* ya *manufactured channels*, sisi ni wauzaji wa korosho ghafi, nilitaka kuweka sawa hiyo taarifa. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nachuma, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa kwa sababu kadandia gari kwa mbele. Nilichozungumza ni kwamba katika orodha ya nchi zinazouza korosho duniani Tanzania haipo, ndiyo taarifa iliyopo pale. Sasa ye ye anazungumza yawezekana kwamba hajasoma sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Analipotosha Bunge bwana! Analipotosha Bunge.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwa sababu kanipotezea muda bure tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba kuchangia katika huu mwelekeo wa mpango ni sekta ya utalii nchini. Sekta hii ya utalii nchini ni sekta muhimu sana na taarifa ambayo tulipewa hapa Bungeni, tulielezwa ya kwamba Tanzania ina vivutio vingi sana, ukiondoa Brazil inayofuata ni Tanzania. Hata hivyo nikapitia mpango wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kuna pesa ambazo wameziweka zinaitwa pesa za *REGROW*, wamekopa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuendeleza sekta ya utalii kule Nyanda za Juu Kusini. Sasa ninaomba sana zile pesa dola millioni moja ambazo zimekopwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuendeleza utalii Nyanda za Juu Kusini basi zifike kule Kusini pia ili sekta hii ya utalii iweze kutangazwa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika hili, pale Mtwara Mjini tuna eneo la Mikindani. Mikindani kuna majengo ya kale sana. Sasa nimeangalia taarifa hapa sijaona mpango uliowekwa sawasawa juu ya sekta ya mambokale katika utalii kwamba Serikali imejipangaje kutangaza mambokale ili iweze kuwaingizia pesa Serikali ya Tanzania, lakini wananchi kwa ujumla kwa kupata ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikindani kuna majengo na vivutio vingine vingi vya kale, lakini vivutio vile vimeachwa kwa wazungu, watu wanaoitwa *Trade Aid* ndio wanaokarabati, ndio wanaotangaza na kukusanya pesa wakati Serikali hii ina shida ya pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha mpango sekta hii ya utalii iangalie sekta ya mambo kale na hasa hasa utalii katika maeneo haya ya Mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumza ni suala hili la miundombinu. Tunaishukuru Serikali kwa kiasi kikubwa imekuwa ikijenga miundombinu, imekuwa ikijenga barabara lakini pia imeweza kuleta pesa za kutosha pale Mtwara Mjini na linajengwa gati linajengwa la mita 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, sambamba na upanuzi wa Bandari uliopo Mtwara Mjini hivi sasa tunaomba swala la reli hili ambalo imekuwa Serikali imekuwa ikizungumza kila mwaka, kila siku, reli ya Kusini, ili *Mtwara corridor*weze kufunguka, iweze kufungua uchumi wa ukanda ule wa Kusini lazima hili suala la kujenga reli kutoka bandari ya Mtwara kwenda Mchuchuma na Liganga kule kwenye makaa ya mawe iweze kuwekwa kwenye bajeti ya mwaka huu, pesa ziweze kutengwa ili sasa uchumi wa Kusini na Watanzania uweze kusheheni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ilikuwepo miaka ya nyuma lakini iliondolewa, sijui iliondolewa kwa sababu gani. Sasa tunaomba sana, kwa sababu kuna mkakati unaitwa *Mtwara corridor* wa kufungua Kusini mwa Tanzania ili Tanzania yetu sasa iweze kweli kuwa ni Tanzania ya uchumi. Bandari yetu inavyojengwa kama reli ikijengwa mizigo ikiletwa pale tunaamini ya kwamba bandari itaingiza pesa nyingi na bajeti yetu itakuwa haisuisui tena kwa sababu ya makusanyo. Tusiangalle sana Bandari ya Dar es Salaam, tutanue Kusini, tutanue *Mtwara corridor* kama tulivyokuwa tunaahaidi siku zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba nizungumze suala zima la ardhi. Wakati tunapitia bajeti hapa, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alizungumzia mipango mikakati, na tunashukuru kwa kweli pale Mtwara Mjini tumezindua mpango kabambe wa ardhi. Hata hivyo kuna mambo ambayo yalizungumzwa na kuahaidiwa katika Bunge lako hili Tukufu, suala la kulipa fidia kwa maeneo ambayo Serikali ilichukua. Kwa mfano, Mtwara Mjini eneo la Mji Mwema, Serikali ilihaidi kwamba mpaka mwezi wa nane mwaka huu itakuwa tayari imelipa fidia. Jambo la ajabu

wanaleta taarifa kwamba Serikali imeshindwa kuwalipa wale watu wa Mji Mwema wakati wale watu wamechukuliwa ardhi tangu mwaka 2013, ni jambo la ajabu sana. Tunazungumza ndani ya Bunge, tunapanga ndani ya Bunge wananchi wanasikia halafu baadaye Serikali inasema haina pesa kuititia *UTT*, *UTT* wameghairi kulipa. Ni jambo la ajabu kwa kuwa tunazungumza, tunapitisha kwenye bajeti lakini utekelezaji wa haya mambo ya msingi unakuwa hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atakavyokuja atueleze kwamba mkakati upoje kuhusiana na sekta hii ya ardhi ambayo bado ina changamoto nyingi; Tanzania pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsanste sana Mheshimiwa Maftaha. Tunamalizia na Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE.RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ya kuchangia. Awali ya yote kwanza niunge mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mpango wa maendeleo, na nishauri kwamba Serikali ijitahidi kuzingatia yale ambayo yatakuwa yanaweza kusaidia kuboresha Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilitaka nizungumzie suala la makusanyo ya Halmashauri, kama ambavyo Mpango unaonesha, kwamba una lengo la kukusanya shilingi bilioni 847.7 kwa mwaka 2018/2019. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napata mashaka sana kuhusu Mpango huu wa Serikali kama kweli unaweza kutekelezeka, kwa sababu mwaka 2017/2018 malengo yetu ni kukusanya shilingi bilioni 687.3, lakini bahati mbaya vyanzo vyote vingi vya Halmashauli vile vikubwa vimechukuliwa. Maeneo ya Halmashauri za Wilaya, ushuru wa mazao

umechukuliwa kwa kiwango kikubwa na kwa bahati mbaya mkuu wetu wa nchi anapopita anawashauri wananchi kwamba kuanzia asubuhi mpaka jioni wasafirishe tani moja moja mpaka jioni, watakuwa wamekwisha kamilisha lengo la kusafirisha tani moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba Halmashauri za Wilaya ukusanyaji wa mapato kupitia kwenye mazao utakuwa mdogo sana, lakini kwenye Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji ukusanyaji wa *proper tax*, ukusanyaji wa kodi za matangazo kwa maana ya *posters* na *billboards* utakuwa umeshuka kwa sababu tayari kodi hizi zinakusanya na *TRA*. Sasa napata mashaka ni namna gani tutaweza kufikia lengo la hii shilingi bilioni 847.7 kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu basi atuoneshe mpango mkakati wa kuhakikisha tunafikia malengo ya kupata hii shilingi bilioni 847.7 katika halmashauli zetu ili tuweze kufikia malengo ya mapato ya ndani ya nchi yetu tunayo tarajia. Vilevile katika eneo hili la halmashauri utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2017/2018 uko katika kiwango cha chini sana katika Halmashauri zetu nyingi. Miradi mingi ya maendeleo fedha hazijaja, sasa nilikuwa naomba wakati Mheshimiwa Waziri atakapojibu atusaidie ni kwa namna gani watazisaidia Halmashauri ili zitekeleze miradi yake ya maendeleo kwa kupeleka fedha za miradi ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Mheshimiwa Waziri akatuambia katika mpango wake, nini malengo yake hasa kuhusu Halmashauri, malengo ya ukweli kabisa kuhusu Halmashauri na dhamira ya Serikali hasa kuhusu Halmashauri. Kwamba dhamira ni kuzifanya Halmashauri ziwepo ama dhamira ni kuziua Halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima haya mambo yawekwe bayana ili tuelewe maana inavyoonekana Serikali ya Awamu ya Tano dhamira yake kubwa ni kuziua

Halmashauri. Unapoondo uwezo wa Halmashauri kukusanya maana yake unazifanya zisiwe na mapato. Na kama unazinyima mapato, maana yake unazinyima uwezo wa kujijendesha. Leo Halmashauri nyingine hazina uwezo wa kulipa hata posho za Madiwani, sasa zitajiendesha namna gani? Ni vizuri Serikali ituoneshe kiukweli kabisa kwamba dhamira yenu hasa nini? Dhamira yenu kwamba Halmashauri ziwepo kama ilivyokuwa mpango wa awamu, dhamira ni kuziuwa Halmashauri? Ili kama ni kuziuwa Halmashauri tuondokane na Halmashauri, tuachane na mzigo wa kuwa na Madiwani ambao hawana kazi, kuwa na Wakurugenzi ambao hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana maana leo katika halmashauri zetu utakuta wanao-*dictate* mipango ya Halmashauri sasa wanakuwa ni Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa kwa sababu *power* ya Halmashauri imeondoka kwa sababu hawana fedha hawana chochote na inaonekana dhamira ya Serikali Kuu ni kuziuwa Halmashauri. Kwa hiyo niombe, kama mpango bado ni kuziboresha Halmashauri basi turudi katika mpango wetu, tuonyeneshe ambavyo tutaziboresha na kuzisitawisha halmashauri zetu ili ziweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo tulikuwa tumejipangia kwamba angalau Halmashauri zetu nchini zijitegemee kuanzia kwa kiwango cha chini asilimia 35 mpaka asilimia 50, ili zimpunguzie Mheshimiwa Raisi na Serikali mzigo wa majukumu madogo madogo, yale ya chini na Serikali ijihushe na majukumu makubwa kama ya reli na ndege, lakini mambo ya vituo vya afya, zahanati, shule za msingi yashughulikiwe na Halmashauri kwa kiwango cha kutosha. Mheshimiwa Waziri naomba sana uonyeshe jinsi ambavyo umepanga kujielekeza katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo ambalo mpango huu unaelekeza kwamba utapunguza umaskini wa wananchi utaendelea na jambo ambalo likizungumzwa mara kwa mara katika mipango yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri atuambie kama kweli mpango wa Serikali ni kupunguza umaskini wa Watanzania, na leo tunapata ujasiri wa kubomoa nyumba za wananchi bila huruma, nyumba ambazo wananchi wamejenga wengine kwa utaratibu, lakini tunazibomoa kwa kisingizio kwamba ziko katika hifadhi ya reli na hifadhi ya reli ni mita 30 kuna nyumba ambazo zipo nje ya mita 30, zimeishi katika maeneo hayo zaidi ya miaka 50, leo tunawabomolea wale wananchi hivi dhamira yetu ya kupunguza umaskini wa hao wananchi iko wapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo wananchi wana vibali vyote vya ujenzi, taratibu za kubadilisha matumizi ya maeneo hayo zimefanyika, lakini leo wananchi wale wanaambiwa walifika maeneo hayo baada ya mpango reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefuatilia mpango wa ramani ya reli, hawana ramani ambayo imepitishwa na Wizara ya Ardhi, wananchi wana eneo ambalo limepitishwa na Wizara ya Ardhi na Serikali ni moja. Wizara ya Ardhi ni moja, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi yote ni Serikali, sasa inakuwaje leo watu waliopewa ruhusa na Wizara ya Ardhi wavunjiwe maeneo yao bila kulipwa fidia wakiambiwa kwamba wamevamia maeneo? Hivi inakuwaje eneo ambalo watu wamepewa kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi hii waambiwe wamevamia hayo maeneo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri kama ana dhamira ya kupunguza umaskini wa Watanzania awasaidie watu wanaovunjiwa nyumba zao wakati wametimiza masharti yote na wana hatimiliki za maeneo ambayo wanayomiliki ili wananchi wawe salama na wawe na miyo yenye furaha yenye amani. Kama ni dhamira kufanya nchi iwe yenye utulivu basi tuwafanye wananchi wetu pia wawe na miyo yenye utulivu na tuwasidie wananchi hawa ambaa ni maskini ambaa wamejenga hizi nyumba kwa hali ngumu sana, leo wanavunjiwa kirahisi kama vile hizo nyumba zimeanguka kutoka mbinguni. Naomba sana Serikali ilione hii kwa uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mikopo ya elimu ya juu. Hotuba ya Kambi ya Upinzani imejaribu kuzungumzia suala la mikopo ya elimu ya juu. Ni vizuri Serikali ibainishe inaweza kukopesha wanafunzi wasome ama haiwezi? Ni vizuri tuweke bayana, kwa sababu kama tunahitaji kuwasaidia wanafunzi na wanafunzi hawa ni watoto wa maskini, maskini tunaowafahamu wana-*qualify* kukopeshwa lakini hawakopeshwi kwa sababu Serikali haina uwezo, inaonekana kuna ubaguzi kwa sababu kuna ambao wanakopeshwa na ambao hawakopeshwi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuondoa hii hali ya ubaguzi ama tuondoe mikopo ama kama tunatoa mikopo tutoe mokopo kwa watu wanaostahili kupewa mikopo kama jukumu la Serikali ya nchi hii. Na kwa sababu ni kweli kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ilijitanabaisha kwamba wananchi wenye kuhitajiwa kukopa watakopeshwa wote bila mmoja kukosekana basi Serikali itimize wajibu wake huo vya kutosha ili wanafunzi wasikose haki yao ya msingi ya elimu ambayo ni haki ya Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana katika Mpango huu Mheshimiwa Waziri atujibu ni wakati gani watamaliza tatizo la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu bila kuonesha aina yoyote ya ubaguzi kama inavyoendelea sasa hivi? (*Makofii*)

Kuhusu suala la utalii, hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni imeonesha jinsi ambavyo VATkuwekwa katika utalii ilivyoathiri utalii katika nchi hii. Malengo yetu ni kuifanya nchi hii ishindane na nchi nyingine katika utalii, bahati nzuri nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii, tunategemea kwamba tungkuwa tuko katika hatua ya juu sana katika utalii. Ni vizuri pia Mheshimiwa Waziri akatueleza ni watalii kiasi gani ambao wameingia kipindi hiki ukilinganisha mwaka uliopita, na ni mpango gani uliopo katika Serikali hii kuingiza watalii zaidi kipindi cha mwaka 2018/2019? Tushindane na nchi ambazo zina vivutio kama vya kwetu, haiwezekani nchi ambazo hazina vivutio kuliko vya kwetu zitushinde katika kuingiza idadi kubwa ya watalii katika nchi hii. Kwa hiyo ni

vizuri tuangalie sana mfumo wa kodi katika eneo la utalii ili itusaidie katika kuongeza idadi ya watalii katika nchi yetu na ukizingatia kwamba Mlima Kilimanjaro ni moja wapo wa vitega uchumi muhimu sana katika nchi yetu, ni vizuri tuone jinsi ambavyo tunaweza kuutumia ule mlima kutuingizia mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka pia niongelee suala la mfumo wa kodi. Mheshimiwa Waziri kwenye mpango wake ameonyesha kwamba angalau wananchi wameonesha *ku-comply* kulipa kodi, ameonesha kuwa wananchi wengi wameingia kwenye mfumo wa *EFD machine*. Ni kweli, sasa ni wakati wa mpango wetu Mheshimiwa Waziri uoneshe namna gani tunaangalia upya sera ya kodi na mfumo wa kodi ili sera hii ya kodi na mfumo wa kodi ifanye kodi ilipike kwa wafanyabiashara vizuri zaidi. Kwa sababu kodi ikilipika vizuri maana yake ni kwamba watu wengi watakuwa wanafanya biashara na uchumi wetu utapanuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi tulionayo sasa hivi hailipiki ndio maana watu wengi inabidi waingie kwenye mfumo wa rushwa ili wakwepe kulipa kodi. Kwa hiyo, watu wengi wanakwepa kodi kwa sababu ya viwango vya kodi kuwa vikubwa pamoja na mfumo wa kodi kuwa mgumu. Kwa hiyo tuangalie kwa kiwango cha kutosha mfumo wetu wa kodi ili kodi yetu ya nchi hii ilipike na wafanyabiashara wapate nafuu katika kufanya biashara zao. Ili wasifunge biashara zao kama ambavyo wanafunga sasa, ili wasigombane na *TRA* kama wanavyogombana na *TRA* sasa, tuwafanye watu wa-*comply* kulipa kodi wenyewe na Mheshimiwa Waziri unafahamu kodi nzuri ni ile inayolipika. Sasa kama kodi hailipiki maana yeke hiyo kodi inapoteza ule uzuri wake, naomba Mheshimiwa Waziri hilo lifanyiwe kazi kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la viwanda. Suala la viwanda katika nchi hii tunalolizungumza ni jambo bora; ni jambo la msingi kuifanya nchi hii kuwa ya viwanda. Hata hivyo tunazungumzia viwanda vya vyerehani vitatu, vinne, vitano ndivyo tunavyovipigia kelele, lakini kuna

viwanda vimebinafishwa katika nchi hii, tumeendelea kusema viwanda vile virudishwe kwa watu ambao wana uwezo wa kuiyidesha, lakini havirejeshwi mpaka sasa hivi. Watu wamekalia viwanda vimekuwa magofu halafu tunaendelea kupiga kelele viwanda vidodo vidogo. Sawa, hata hivyo ni viwanda, lakini hivi viwanda vikubwa lazima vifanyiwe kazi, virejeshwe katika uendeshaji. Viwanda havifanyi kazi, vimekufa na vilikuwa viwanda vyetu nya kodi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama waliopewa wameshindwa kuiyidesha wavirejeshe kwa wanaoweza kuiyidesha. Kilimanjaro viwanda vingi vimelala kwa sababu tu watu wamevichukua na haviyendeshwi. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri utusaidie katika mpango wako, nini mpango wa Serikali katika kuhakikisha kwamba viwanda viliivyobinafishwa vinarejeshwa kwa watu wanye uweza kuiyidesha kama wale waliokuwa wamepewa wameshindwa kuiyidesha ili vifanyi kazi viongeze ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho nataka kuongea katika siku ya leo ni suala la sekta binafsi. Serikali inakuwa kama inajinadi kwamba ina dhamira ya kusaidia sekta binafsi lakini katika uhalisia tunaonekana hatuna dhamira ya kusidia sekta binafsi. Leo tunavyozungumza sekta binafsi haikopesheki, benki haziwezi kukopesha sekta binafsi, na watu wengi wa sekta binafsi wanafunga biashara zao kama hotuba ya Kambi ya Upinzani ilivyosema. Hatujafanya tathimini ya kutosha ni kwa nini watu binafsi wafunge biashara zao? Hatujafanya utafiti wa kutosha ni kwa nini leo benki haziwezi kukopesha sekta binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujafanya utafiti wa kutosha ni kwanini benki zishindwe kukopesha. Mheshimiwa Waziri ni lazima mpango wako utuoneshe ni namna gani mmejipanga kuhakikisha kwamba mnasaidia sekta binafsi na mnazisaidia benki zikopeshe sekta binafsi. Hatuna sababu ya kujenga ugomvi na benki zetu, hatuna sababu ya kujenga ugomvi na sekta binafsi kwa sababu sekta abinafsi ndiyo

chachu muhimu sana yakuinua uchumi wetu. Huko nyuma Serikali ilishajitoa kufanya biashara, leo Serikali mnakuja sana katika kufanya biashara. Sasa wakati mnakuja kwa kasi isaidieni sekta binafsi kwa sababu ndiyo inayoinua uchumi katika dunia hii. Mheshimiwa Waziri mpango wa Serikali utusaidie sekta binafsi ili sekta hizo binafsi zisaidie malengo ya Serikali ya kufikia uchumi wa viwanda, malengo ya Serikali ya kuinua uchumi wa nchi hii, malengo ya Serikali ya kuondoa umaskini wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Michael, huyo ni msemaji wetu wa mwisho kwa asubuhi hii. Naomba niwataje wachangiaji ambao wataanza jioni, kwanza Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Hassan King, Mheshimiwa Masoud Salim na Mheshimiwa Peter Msigwa. Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imemaliza muda wake kwa sasa.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge nina tangazo moja kutoka kwa Mwenyekiti wa Ibada Mheshimiwa Anna Lupembe anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa imani ya kikristo kuhudhuria ibada katika ukumbi wa Pius Msekwa, ghorofa ya pili leo siku ya Jumanne saa saba mchana, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge mchana huu.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa  
unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na  
Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali  
kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

### **KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Mipango tunaendelea na wachangiaji wetu, jioni hii tunaanza na Mheshimiwa Janet Mbene na baadae Mheshimiwa Hassan King ajiandae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia suala hili ambalo liko mbele yetu la mwongozo wa maandalizi ya mpango wa bajeti kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hizi, nataka kushukuru sana na kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakiendesha shughuli za kimaendeleo kiasi kwamba Tanzania sasa hivi, imekuwa ikiendelea kwa kasi na kwa kweli hata takwimu tunazopata kutoka *IMF* na Mashariki mengine ya Kimataifa, Tanzania tunafanya vizuri sana kiuchumi, hata kwa Afrika Mashariki inasemekana sisi tunakuwa mara nydingi zaidi kuliko hata wanavyokua jirani zetu Kenya, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiongoza katika ukuaji wa uchumi kwa Afrika Mashariki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa juhudi za kufanya yote haya na vilevile kwa kusimamia

mfumuko wa bei na kuweka katika hali ambayo ni nzuri na inayowezesha sasa biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mheshimiwa Rais Magufuli kwa juhudzi zake anazofanya katika kuhakikisha kuwa mapato yote yanayotakiwa kupatikana yanapatikana na juhudzi hizo zinafanywa pamoja na Wizara ya Fedha. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wake kwa jinsi ambavyo wamepanga mpango huu kwa njia ambayo kwa kweli inatoa matumaini na mwelekeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi niiombe Serikali kuwa kwa jinsi ambavyo tumepanga mipango yetu na jinsi ambavyo tumeweka vipaumbele vyetu, basi tuhakikishe kuwa tunasimamia vipaumbele hivi na tunasimamia utekelezaji wa miradi ambayo tumejiwekea ya kipaumbele ili Taifa letu likue. Tumekuwa kwa muda mrefu tukiona miradi ya kielelezo ikiletwa Bungeni na kuoneshwa katika mipango, tunaomba sasa tuoneshwe inaanza kufanyiwa kazi. Miradi ya Mchuchuma na Liganga, miradi ya maeneo maalum ya uwekezaji, miradi ya kupanua bandari kwa sababu tunajua bila bandari kuwa imara na yenye kuwezesha usafirishaji wa mizigo na kupokea mizigo tutakuwa hatuwezi kuendelea na tutashindwa kupata mapato tunayoyategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebarikiwa kuwa na madini, vito vya thamani sana, vito hivi namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kuanza kuona jinsi gani ambavyo Tanzania na yenye sasa inufaike na vito ambavyo viko nchini kwetu kama Almasi, *Tanzanite*, Dhahabu na madini mengine ambayo ni muhimu sana katika kutuletea uchumi na kutuletea maendeleo ya haraka. Sasa haya yote yafanyike katika utaratibu ambao umewekwa katika mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupongeza vilevile Serikali kwa suala zima la bomba la mafuta la kutoka Uganda kuja Tanzania, huu nao ni uwekezaji muhimu kwetu lakini yote tunataka kusema tuhakikishe kuwa tunazingatia

masuala yanayohitajika kifedha au kitaalam yafanyike kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi ambayo ingekuwa imeshaanza sasa hivi tungekuwa tuko mbali. Tunasisitiza sana kilimo, kilimo ndiyo uti wa mgongo na kweli ni kilimo ndiyo kitakachotuwezesha kufikia maendeleo tunayoyahitaji kwa sababu kinaajiri watu wengi, kilimo kinasaidia vijjini, kinasaidia nchi nzima kwa chakula, lakini vilevile kwenye viwanda vyetu hatuwezi kwenda bila kilimo.

Kwa hiyo, tunataka kusisitiza suala la kilimo lipewe kipaumbele kama vile ambavyo miundombinu na miradi mingine inapewa kipaumbele, umwagiliaji kwa kutumia maji, tuhakikishe kuwa yale mambo yote muhimu ambayo yanawagusa wananchi moja kwa moja yanafanyiwa kazi na yanapewa kipaumbele. Kwa hiyo, kilimo, mbolea, maji, utaalam, mitaji ni vitu ambavyo lazima vishuke kwa wananchi wengi kwa ujumla vijjini ili tuweze kuhakikisha kuwa na wao wanafaidi hili suala zima la maendeleo ya haraka tunayoyapata hapa Tanzania. Maana maendeleo yako huku juu lakini bado hayajashuka chini kwa kuonesha jinsi ambavyo umaskini unapungua lakini watu wanaendelea kuwa na kipato, wanajajiri na mwisho wa yote ufanisi unakuwa mkubwa kwa nchi nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la utekelezaji wa sera ya viwanda. Tumekuwa tukizungumza sana kwa sasa hivi tunataka kujikita kwenye uchumi wa viwanda lakini tuna maeneo ambayo yalitengwa, ambayo kama yangetumika vizuri tungekuwa na maendeleo ya haraka zaidi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia masuala ya maeneo maalum kwa ajili ya uchumi yaani *SEZ* au *Export Processing Zones* ambazo zilishatambuliwa na zimeshawekwa nchi nzima, tungehakikisha kuwa tunaanza japo na mbili kila mwaka au moja kila mwaka tuhakikishe kuwa sasa tunaeneza viwanda nchi nzima ili kuwe na uwiano wa maendeleo katika Taifa zima.

Kwa hiyo, ningependa sasa kusisitiza kuwa hilo suala la viwanda tuanze kwa kutumia yale maeneo ambayo tulikuwa tumeshyaweka na kwa kiasi kikubwa sana tutumie sekta binafsi.

Mheshimiwa wenyekiti, tumekuwa tuna tatizo la Deni la Taifa limekuwa likiongezeka sana kwa kipindi cha miaka miwili, mitatu. Linaongezeka kwasababu tunataka kufanya kila kitu sisi wenyewe. Hebu tuangalie uwezekano wa kushirikisha sekta binafsi. Wao wachukue ile miradi ambayo ni mikubwa inayohitaji hela nyingi, vilevile ambayo inataka ufanisi mkubwa kuiendesha basi tuingie ubia na sekta binafsi au tuwaachie wao waiendeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia mashirika ambayo hayafanyi kazi vizuri na yanakuwa mzigoto kwa Taifa, hebu tuangalie sasa uwezekano wa kuziachia sekta binafsi wayaendeshe yale mashirika ambayo hayafanyi kazi vizuri ili Serikali isiwe na mzigoto wa kuendelea kuyalisha na kuyahudumia wakati yenye hayarudishi kitu chochote kwa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie suala zima la Tanzania sasa hivi tunajulikana kuwa tumepiga hatua kubwa sana na pengine tunaongoza kwenye *financial inclusion* (matumizi ya mitandao kwa ajili ya miamala ya fedha). Hebu tutumie fursa hiyo sasa kuhakikisha kuwa hiyo teknolojia hiyo inatumika katika kuwasaidia wakulima, wanawake, vijana vijijini kwetu ili na wao sasa waanze kunufaika. Kwa mfano, kupata mitaji, kupata taarifa pamoja na masuala mazima ya miundombinu muhimu ya umeme itakayowekwa katika maeneo yetu ya vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la sekta binafsi kwa kweli nalionia kama ni suala ambalo lingetukomboa sana, sijui kwa nini bado Serikali yetu haijapenda sana kutumia *PPP* katika kuendesha shughuli zake. Jamani tuangalie mifano, tujifunze mifano ya wenzetu nchi nyingine. Ukienda Malaysia sasa hivi kila kitu kinafanywa kwa kutumia *PPP*, hebu tuanze japo kidogo eneo moja tuanze kusema hapa tuachie *private*

sector waendeshe na tutaona jinsi ambavyo inatupunguzia mzigو wa madeni, kwa sababu inabidi sasa mitaji itoke kwenye *private sector.*(*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kodi napongeza sana masuala ya ukusanyaji wa mapato, lakini bado kuna sehemu kubwa sana ya wananchi ambaao wako kwenye sekta isyo rasmi ambaao bado hatuwatambui katika kutozwa kodi. Sasa hivi nimeona katika mpango kuna suala la urasimishaji wa wananchi katika masuala ya ujasiriamali na hivi. Ningependa vilevile kupongeza hilo likafanywe na Halmashauri zetu. *TRA* sidhani kama wataweza kwa sababu hawawatambui hawa watu, hawajui walipo lakini ikifanywa kwenye Halmashauri zetu wanawajua kabisa vijana gani wanazalisha nini, wako wapi, wafanyabiashara wadogo wako wapi, vikundi gani viko wapi, hiyo itarahisisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa rai Serikali itumie Halmashauri zetu ili kwanza na wao pia wapate mapato lakini vilevile itarahisisha hili zoezi zima la kuwarasimisha watu hawa ambaao tunataka kuwaingiza katika mfumo usiokuwa rasmi.(*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yalikuwa ni haya masuala ya bajeti yetu izingatie yale maeneo ambayo yanawagusa wanawake na vijana. Huko nyuma tuliwahi kuzungumzia masuala ya *gender budgeting*, sasa sijui yaliishia wapi. Najua nitajibowi kuwa unavyozungumzia hivi na wenyewe wamo, lakini hili suala bila kutambua moja kwa moja na kuiwekea mikakati na fedha itakuwa vigumu. Tuangalie maeneo ambayo yanawaathiri sana akina mama na vijana au na watoto. Masuala ya vifo vyaa kina mama wanapoifungua, masuala ya vifo vyaa watoto wa mwaka mmoja mpaka miaka mitano, yote ni masuala yanayogusa wanawake sasa kama Serikali ikijielekeza kuweka miundombinu inayofaa kwa hospitali, vituo vyaa afya kwa ajili ya hawa akina mama tutajikuta watoto wetu na akina mama wanaponaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukija kwenye suala

la maji, najua Serikali imefanya makubwa sana juu ya maji na bado inaendelea kufanya. Maji ni suala ambalo ni la *gender* moja kwa moja. Wanaohangalka na maji ni akina mama na watoto wao. Watoto wa shule wanabebeshwa ndoo za maji asubuhi kabla hawajaenda shule hii ni kwasababu hatuna miundombinu mizuri ya maji na maeneo mengine yana maji mengi yanachohitaji ni miundombinu tu. Kwa hiyo, nafikiri Serikali iangalie zaidi suala la *gender budgeting* siyo kwa sababu ya wanawake *per se*, lakini kwa sababu ndio kitu sahihi kukifanya na kitaturahisishia maendeleo yetu katika vijiji vyetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala la elimu vilevile tuangalie hayo, watoto wa kike wengi pamoja na kuwa wanakwenda shule lakini hawamalizi kwa sababu ya miundombinu isiyofaa, ambayo haizingatii mazingira yao. Tunaiomba Serikali ijielekeze katika mabweni ya watoto wa kike, iangalie kuwa shulenii kuna maji ya kutosha, kuna vyoo vya kutosha kwa ajili ya watoto wa kike na huduma nyingine ambazo watoto wa kike wanazihitaji kwa sababu ya maumbile yao.

Kwa hiyo, hivi ni vitu ambavyo huwezi kuviepuka ukasema haya mambo ya wanawake, hapana! Bila kuyazingatia na kuyaweka kwenye bajeti utajikuta bado kila siku yale maeneo ambayo yanahuusu wanawake na watoto yako nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niishie hapo kwa rai ambazo nimezitoa kwa Serikali nikiamini watachukua maoni haya na kuyaingiza katika mipango yao ili kila kitu ambacho tumekizungumza hapa kikafanyiwe kazi kama ambavyo mpango ulivyoonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na naendelea kupongeza Serikali kwa juhudii zote ambazo inazifanya. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbene. Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan King, hajafika eeh? Basi

tunaendelea na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali na baadae Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha kuhusu Mpango wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na suala zima la kilimo na ningegusia moja kwa moja mlinganisho uliopo kwenye kilimo na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na uchumi wa kati, hatuwezi kuwa na uchumi wa viwanda kama hatutawekeza ipasavyo kwenye kilimo. Viwanda vyote ambavyo tunavikusudia vinahitaji malighafi kutoka kwa wakulima, wakulima hawa lazima tuwawezeshe ili waweze kuzalisha kisasa na waweze kuzalisha kwa tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozalisha ili uchumi uweze kukua hautakua kwa maneno mazuri tutakayokuwa tunayazungumza, wala hautakua kwa kauli mbiu nzuri, kama hivi sasa tunasema uchumi wa viwanda. Tuzungumze Watanzania wote uchumi wa viwanda, havitapatikana viwanda kama hakuna mikakati kwa sababu kauli mbiu nzuri za namna hii zilishawahidi kupatikana huko nyuma kwamba kilimo uti wa mgongo na kauli mbiu nyingine, kulikuwa na kauli mbiu nyingi sana katika kilimo, lakini mwisho wa siku bado kilimo chetu kimeendelea kubaki kuwa kilimo cha kutumia jembe la mkono na kilimo kile cha kizamani *primitive way*. Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea kwa kutumia kaulimbiu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri nakushukuru unanisikiliza kwa makini nataka niseme jambo moja, katika suala la korosho ambalo ni zao ambalo kwa sasa linatuingizia kama Taifa kipato kizuri, tunahitaji tuwekeze kwenye viwanda ili korosho zetu tuweze kuzibangua hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia takwimu ambazo yuko mzungumzaji alikuwa anasema hapa na nilijaribu kum-

*crush* kwamba siyo takwimu sahihi. Tanzania kwa kusaidia tu na kuweka sawa, Tanzania mwaka jana tulizalisha tani 250,000 za korosho na ni nchi mionganoni mwa wazalishaji wakubwa tu wa korosho na kwa bahati nzuri korosho ya Tanzania ni moja ya korosho bora duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye mitandao wameandika kabisa *best cashewnuts producers* ni Tanzania na Mozambique. Ni korosho tamu, zenye mafuta na ni korosho ambazo zinapendwa sana. Kwenye soko la dunia zikifika korosho za Tanzania na Msumbiji zingine zinasubiri ili ziweze kuuzwa. Sasa nini ninachokusudia kusema? Ninachokusudia kusema ni kwamba, hii thamani ya korosho ya sasa shilingi 3,900 mpaka shilingi 4,000 bado haikidhi haja wala haifikii kiwango ambacho wakulima wanapaswa kukipata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nimejaribu kuangalia leo soko la dunia bei ya korosho ghafi ni shilingi ngapi, ni kuanzia dola tano mpaka dola 13 lakini korosho iliyobanguliwa yaani zile *cashewnuts canals* nilizokuwa nazisema mara ya kwanza, leo zinacheza kwenye dola 25 mpaka dola 29. Ni korosho ambazo tayari zimeshakuwa *processed*, maana yake ni zaidi ya shilingi milioni 50 lakini huko mbali. Katika soko la ndani pekee hivi sasa korosho iliyobanguliwa ukifika pale Mtwara inauzwa kati ya shilingi 25,000 na shilingi 30,000 maana yake ni zaidi ya dola 12 mpaka dola 15. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokusudia kusema ni kwamba kama tuna mipango iliyokuwa madhubuti, tunaweza tukabangua korosho zetu, tukategemea soko la ndani na soko la nje, tukapata kipato kikubwa zaidi. Ndiyo maana wasioelewa ukiingia leo kwenye mtandao ukatafuta kujua wauzaji wa korosho kwenye soko la dunia hautaiona Tanzania, *you will never see it!* Utaona tu pale Brazil, utaiona India, utaiona Vietnam, utaiona Ivory Coast, utaiona Canada, kwa sababu wao siyo kwamba wana mikorosho mingi bali wao wana viwanda ambavyo wana-*process* korosho zao na wanawenza kuzipeleka kwenye soko la dunia,

bali Tanzania ni wazalishaji lakini hatupeleki korosho zetu kwenye soko la dunia, *we are not recorded anywhere kwamba tunauza korosho kwenye soko la dunia.* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninaomba sana hivi ni viwanda ambavyo tunavipoteza, tungeweza kuwekeza kwenye korosho kwa kuweka vile viwanda, kuvifufua vilivyopo, tungeweza kupata kipato kikubwa. Wanatushinda Msumbiji ambao wamepigana vita miaka mingi, leo Msumbiji wanabangua *more than 80 percent* ya korosho zao, sisi hatujafikia hata asilimia 20, maana yake bado tuko chini kwenye suala la ubanguaji wa korosho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Mheshimiwa Waziri naomba sana mpango tunapopanga kwamba tunataka kwenda kwenye uchumi wa kati na uchumi wa viwanda basi tuhakikishe kwamba tunakuwa na mipango madhubuti lakini siyo maneno matamu yanayoweza kusikika na kufurahisha wasikilizaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninataka nilichangie ni suala la miradi mikubwa ambayo ilizungumzwa kwenye mpango wa mwaka jana. Mheshimiwa Waziri tunakumbuka kwamba mwaka jana kwenye hotuba yako ya mpango ulizungumzia suala la mradi wa gesi wa Lindi (*Liquidfied Natural Gas*) nataka kujua umefikia wapi? Taarifa zilizopo mpaka sasa ambazo wananchi wa Lindi, Wabunge na wawakilishi wa wananchi tunajua kwamba ule mradi ndiyo umekufa kifo cha mende, sasa tunataka tujue kwamba mradi ule umekufa au umeendelea na kama unaendelea umefikia wapi, kwa sababu taarifa tulizonazo ambazo inawezekana isiwe rasmi ni kwamba wale jamaa *Wentworth Resources* na wenzao wameshafunga hata ofisi zao pale London, kwamba shughuli za kuendelea ku-negotiate na ile miradi imeishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama siyo hiyo njoo ututoe hofu, kwa sababu wale wananchi walifanyiwa

tathmini ya kutaka kulipwa fedha zao, watu wameacha kuendeleza mashamba yao, watu wameacha kuendeleza nyumba zao, basi njoo tuambie watalipwa lini na mradi ni lini utaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kwenye hotuba ya mpango kwa sababu mradi huu ni moja ya miradi mikubwa inawezekana Watanzania hawajui, Mheshimiwa waziri uje utueleze, mradi huu ni mkubwa kama unavyoonekana mradi wa *standard gauge*, ni mradi mkubwa sana ambao utatumia *trillions of shillings*, kama tutaupata utatusaidia sana katika kukuza kipato na pato letu la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka niseme ni suala la kuwekeza kwenye uvuvi. Mheshimiwa Waziri katika hotuba hii nimejaribu kuangalla uvuvi namna ulivyouzungumza *it is just like a minor issue*. Kuna nchi ambazo zinaendesha bajeti zao kwa kutegemea uvuvi tu, na sisi Mwenyezi Mungu ametujalia tuna bahari kuanzia Tanga mpaka unafika Mtwara, bahari ambayo ina samaki wengi na sasa Watanzania wameacha kupiga mabomu, kuua samaki kwa kutumia mabomu na samaki leo wako wengi sana. Mimi mlezi miwili hapa niliyokuwa Jimboni pale Mchinga tumekula samaki wengine kama ingekuwa ni binadamu tungeona mpaka mvi, samaki waliozeeka tayari. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kiashiria kwamba samaki wako wengi lakini uwezo wa wavuvi wetu kwenda kuvua kwenye Bahari Kuu imekuwa ni changamoto. Leo Mheshimiwa Waziri anatambua kwamba mapato pekee tunayoyapata kutoka kwenye uvuvi wa Bahari Kuu ni kutegemea leseni tu, kama tunategemea leseni wakati meli moja ya uvuvi na ninamuona hapa Naibu Waziri wa Uvuvi anajua ni mtaalam, meli moja ya uvuvi ikienda pale Bahari Kuu wana uwezo wa kuvua samaki kwa siku mbili wenye thamani zaidi ya shilingi bilioni moja, bilioni mbili. Lakini sisi tunachukua ushuru wa shilingi milioni 30, milioni 40 na tunafikiria kwamba ndiyo inatosha kabisa!

Mheshimiwa Waziri kama kuna jambo ambalo tunapaswa tuliwekee msingi na msisitizo ni kuwekeza katika bandari ya uvuvi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwekeza katika bandari ya uvuvi tutapata mapato makubwa, kwanza wale wavuaji wataleta samaki wao bandarini tutawa-*charge* ile kodi, lakini pia kutakuwa na viwanda vya uchakataji ambavyo vitaajiri vijana wengi. Jambo hili liendane sambamba na kuwawezesha wavuvi wetu wa ndani waweze kuwa na *capacity*ya kwenda kuvua kwenye Bahari Kuu, kwenye kina kirefu cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Mheshimiwa Waziri suala la uvuvi halipaswi kuwa ni suala ambalo linazungumzwa kana kwamba ni suala la utani au kama suala dogo. Uvuvi ni sawa na madini, uvuvi ni sawa na kilimo na uvuvi ni sawa na kitu kingine kama tutawekeza vizuri tunaweza tukapata pesa nzuri na itakayotosheleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la kilimo. Suala la uhakika wa bei ya mazao ya wakulima. Mwaka jana tulisisitiza sana na tuliona Waziri Mkuu wa India alikuja hapa akasaini mkataba na Serikali ya Tanzania juu ya suala la zao la mbaazi, lakini jambo hili linakwenda sambamba na uzalishaji wa zao la ufuta. Nimesikia hapa kwenye taarifa kwamba ufuta sasa umepanda kutoka tani 2,000 na mpaka kufika tani 8,000, lakini wakulima wa ufuta wenyewe hawajui uhakika wa soko la mazao yao. Tunaendelea pale pale kwamba kwenye vichwa vyetu tumejjenga na *mentality* kwamba mazao ya kuyasafirisha na kupeleka nje ya nchi, kuwatafuta Wahindi wako wapi ili tuwasafirishie, kuwatafuta Wavietnam wako wapi tukawauzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiwe na mipango mikakati kwamba huu ufuta uwe *processed* ndani ya nchi, tukawa tunakula mafuta ya ufuta, na imethibitishwa na madaktari kwamba mafuta ya ufuta ni mionganoni mwa mafuta mafuta mazuri ambayo hayana lehemu nyingi.

Tunaweza tukaondoa magonjwa ya *pressure at the same time* tutakuwa tunaongeza kipato cha wakulima na pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri ni kuhusu suala la uwekezaji kwenye sekta ya afya. Hatuwezi kuwa na rasilimali watu ambao watakuwa *more productive* kwenye nchi kama afya zao zitakuwa ni zenye utata. Hivi sasa nilikuwa nasoma hapa ripoti ya ongezeko la ugonjwa wa saratani nchini (*cancer*), taarifa kutoka Hospitali yetu ya *Ocean Road* ni kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika ambayo kiwango kikubwa cha wagonjwa wa kansa wamekuwa wakiongezeko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jirani zetu wa Uganda walikuwa wametuzidi miaka fulani hapa, wameweka mikakati mambo yamekuwa mazuri tumewazidi sisi sasa, Kenya na wenyewe mambo wameweka vizuri kidogo tumewazidi. Katika huu Ukanda wa Afrika Mashariki Tanzania ndio tuna orodha kubwa, tuna *percentage* kubwa ya watu kuugua saratani kuliko nchi yoyote nyingine. Sasa Mheshimiwa Waziri jambo hili ni baya, kwa sababu ugonjwa huu kwanza unatisha jamii lakini pia ni ugonjwa ambao matibabu yake ni *very expensive*. Kwa hiyo, tunahitaji kuwekeza kama Taifa kuhakikisha kwamba tunatengeneza *mechanism* nzuri za kufanya *prevention* ya ugonjwa ama kutoa elimu, ama kuhamasisha jamii kuachana na baadhi ya vyakula au na vitu vingine ili tuwe na jamii ambayo itakuwa na afya njema iweze kuwa *productive* kwenye nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala la afya lisiwe tu suala la kulipigia ngonjera kuja kusema tumewekeza dawa kiasi gani, linahitaji kuwekewa mikakati kuhakikisha kwamba tunapambana madhubuti kabisa na huu ugonjwa wa saratani ambao kwa sasa unatishia kwa kiwango kikubwa sana maisha ya Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa fursa hii. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bobali. Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Msigwa baadae Mheshimiwa Flatei Massay na Mheshimiwa Selemani Kakoso ajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturudisha tena Bungeni salama na ninaamini maneno ya Mheshimiwa Spika kwamba ulinzi utakuwa salama katika maeneo yetu ya Dodoma.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango nadhani kama Wabunge tumekushauri kuhusiana na jinsi ambavyo mliamua kutoa vyanzo vya mapato (*own source*) kwenye Halmashauri zetu ambavyo kimsingi vimeathiri sana maeneo mbalimbali. Kwa mfano, miltoa ile *property tax* Manispaa yangu ya Iringa tulikuwa tukijiwekea bajeti ya kukusanya shilingi milioni 700 lakini hela iliyorudi kutoka *TRA* ni shilingi milioni 182 na hatujapata maelezo, *TRA* hawana hiyo *capacity*, hawana *manpowerya* kukusanya hiyo hela wakati sisi tulikuwa tunakusanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mmechukua hela ya mabango ambayo tulikuwa tumejipangia kwenye bajeti kukusanya karibuni shilingi milioni 357, hiyo hela bado hajijapatikana na kwa kukosekana kwa hela hii, tumeshindwa kutengeneza chumba cha uchunguzi katika Hospitali yetu ya Wilaya ya Frelimo, tumeshindwa kujenga wodi ya wagonjwa katika eneo linaitwa Itamba katika Manispaa yangu, na hizi ni athari ambazo tulizisema toka mwanzo kwamba tulikuwa na uwezo wa kukusanya baada ya nyinyi kutoa hivi vyanzo mme-*cripple* maendeleo yetu kama Manispaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mifano inawezekana na wenzangu kwenye maeneo yao kuna matatizo kama hayo, ningombaa kama inawezekana katika mpango huu mngerudisha hivi vyanzo vya mapato vibaki katika maeneo yetu. Ninavyozungumza Manispaa yangu ya Iringa ni moja ya Manispaa bora kabisa mpaka maeneo mengine wanakuja

kujifunza namna ya usafi, namna ya kupanga Mji, lakini mkiendelea kutu-*cripple* namna hii mtaturudisha nyuma, nadhani hata Naibu Waziri alikuwa *DC* pale anajua jinsi Manispaa ya Iringa ilivyo nzuri, ikiongozwa na CHADEMA katika Mkoa wetu wa Iringa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite katika eneo moja kubwa, katika kitabu chako ulichotuletea ukurasa wa 35 umezungumzia kuhusu utawala bora. Kwangu hayo uliyoyazungumza kwenye utawala bora naweza kusema hii ni *hardware* hujazungumza *software*. Utawala bora niliotaka uzungumzie wewe umezungumzia kuhusu mahakama ambazo zitajengwa ambazo zinataka kujengwa, kwangu mimi hiyo ni *hardware*. Mimi nataka tuzungumzie *component, characteristics* za utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yetu iweze ku-*flourish* lazima utawala bora uonekane kwa vitendo. Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani ukisoma ukurasa wa tatu tumezungumza vizuri sana, naomba minukuu: "Misingi ya uwajibikaji katika kutekeleza mipango ya maendeleo ipo kikatiba na kisheria. Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 inalipa Bunge mamlaka ya kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutungia sheria."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na mipango mizuri kama Serikali yenyewe haiko *accountable*, inakwepa *accountability*. Kipindi cha nyuma Serikali ilikuwa inapaswa iwe inaleta namna inavyotekeleza bajeti kila baada ya miezi mitatu, juzi hapa tumepitisha sheria ambayo asubuhi leo tumeambiwa kwamba imeshapitishwa kwamba tutakuwa tunaletewa utekelezaji wa Serikali kila baada ya miezi sita, na sasa hivi tumeshaanza mpango wa mwaka unaokuja wakati utekelezaji wa Serikali muda uliopita hatujaupata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa hatuna uwezo wa kusema tunaisimamia Serikali kama Serikali yenyewe

inakwepa *accountability*. Nasema hivyo kwa nini, mfano mzuri kama tunapanga vizuri matumizi yetu ya fedha Waziri wa Maliasili ambayo amebadilishwa juzi alikuja Iringa kule tulikuwa tunahamasisha mambo ya utalii huku *Southern Circuit* na mojawapo ya mambo ambayo tulyajadili ilikuwa ni pamoja na kuuboresha uwanja wa Nduli kwa sababu Iringa imekaa ki- *strategy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mbuga ya wanyama ambayo tuna-*attract* watalii na maeneo mengine, tukazungumzia kuhusu barabara, lakini kwa sababu Serikali haitaki kuwa *accountable*, imechukua hela ambazo hazikuonekana popote kwenye vitabu vyako ulivyotuletea hapa ikaenda kupeleka Chato shilingi bilioni 39 mnajenga uwanja wa ndege Chato, mnaacha mahali kama Iringa ambapo pamekaa kimkakati na Wizara ya Maliasili wamesema pale pamekaa kimpango. (*Makofii*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inaonekana ni ya ubinafsi mkubwa sana, Mwalimu Nyerere angekuwa mbinafsi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa naomba usubiri taarifa Mheshimiwa Musukuma.

## T A R I F A

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mchangiaji, anasema kwamba Serikali imechukua shilingi bilioni 39 kwenda kujenga uwanja wa Chato na kwamba hazikuonekana popote. Nadhani huwa hasomi vizuri au neno Chato ndiyo linalomuumiza kwenye kifua chake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita kuna pesa ziliainishwa katika kujenga viwanja vya ndege kwenye Mikoa ikiwemo Mkoa wa Geita. Suala la kujengwa uwanja

wa ndege Chato naomba lisimumize kifua, hiyo ni mipango ya Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake naipuuza na kama ninavyompuuza mwenyewe, siichukui. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia Chato, nimezungumza mipango kama tuna-*synchronize*, Iringa imekaa kimkakati kwamba tukijenga kiwanja cha ndege kuna tija tutakayoipata kutokana na kiwanja cha ndege. Kujenga kiwanja cha ndege Chato tunataka tupate nini? Tulikuhoji muda uliopita hatukupata majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inaonesha ubinafsi wa hali ya juu, kama Mwalimu Nyerere angefanya hivyo Musoma ingekuwa Ulaya, lakini Mwalimu alikuwa anafanya mambo kimkakati, hatuwezi kusema tunataka tujenge, tupanue uchumi wa viwanja kwa upendeleo wa namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hili la Serikali inatakiwa ilete matumizi ndiyo dhana nzima ya Wabunge kuwepo hapa, tukiuia dhana nzima ya Bunge kuisimamia Serikali, Bunge linakuwa halina maana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimezungumza kwenye *briefing* nimesema ukisoma historia kwa wale wanaosoma historia, nenda Ufaransa, nenda Uingereza, kwa mini waliwaua wale wafalme? Ni kwa sababu kodi yao walikuwa wanaitumia pasipo kusimamiwa, Bunge likaanzishwa ili liwe ni mlinzi wa Serikali. Sasa vifungu vyote hapa tumenyofoa kwa maana ya kwamba tunali-*cripple* Bunge, Serikali inaanza kujifanyia kama inavyotaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hazina ya nchi hii siyo mali

ya mtu mmoja. Hazina ya nchi hii ni mali ya Watanzania na sisi ni *tax payer representative*, tukiacha kuisimamia Serikali ifanye inavyotaka tuna *deceit the whole purpose* ya kuwa na Bunge. Bunge siyo kuja kuvalaa suti hapa, Bunge ni kuisimamia Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia *good governance* kuniambia kumejengwa mahakama, nimezungumza hiyo ni *hardware, components* za *good governance* kuna *accountability*. Serikali ya Awamu ya Tano inakataa *accountability*, haitaki kufuatiliwa, hamtaki tujue mmetumia kiasi gani na kuwepo kwa Bunge ni kutaka kujua Serikali imetumia kiasi gani na imetumia kama tulivyopanga kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, hauwezi kuniambia *good governance* hapa kama hatuwezi kufuata sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu hii ili tuzijue *characteristics of good governance* unaweza uka-google tusaidiane haya ninayoyasema, hii ni *UNDP*ilitoa mwaka 1997, inasema lazima kuwe na *participation*. Mme-cripple Halmashauri ambazo ndio hela zikienda kule chini wanashiriki watu kuanzia chini, sasa hakuna hela, wamekuwa *crippled*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima kuwe na *rule of law, good governance, human rights, democracy*. Katika nchi hii hakuna *democracy*, watu wakitaka kuzungumza, wakitaka kuhoji wanakataliwa, tunawezaje kuutekeleza Mpango huu kama haya mambo hayapo? Ili Mpango uweze kutekelezwa ni lazima haya mambo yawepo nazungumzia *good governance*. Hii *good governance it is not about* Upinzani tu, *good governance* ni kwa wote, kwenye maeneo ya Manispaa zetu wote, haya mambo hayapo, ukienda mbele inasema hakuna upendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi Naibu Waziri anajibu hapa maeneo mengine wanaambiwa kwamba ninyi kwa sababu mlinipa kura hamtabomolewa, maeneo mengine ma- *bulldozer* yanaenda yanabomolea watu, kutakuwa na *good governance* hapo? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

### KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68 vilevile nitakwenda Kanuni ya 64(1)(a).

Mheshimiwa Mbunge anasema asubuhi wakati Serikali ikitoa majibu humu ndani Naibu Waziri amejibu hapa kwamba maeneo yanayobomolewa ni maeneo ambayo hayakutoa kura. Amesema hivyo na *Hansard* lko hapa na tunaweza tukaipata sasa hivi, kwa hiyo, ninaomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge jambo hili analolisema siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijawahi kuvunja eneo mahali popote kwa sababu eneo hilo halikutoa kura kwa Serikali yetu. Naibu Waziri alijibu hapa ndani asubuhi kwamba uvunjaji wa majengo utazingatia sheria na taratibu zilizowekwa ambazo zinajulikana katika nchi nzima. Kwa hiyo, ninamuomba tu sana Mheshimiwa Mbunge asitumie Bunge hili kuvunja huu utaratibu wa kupandikiza maneno ambayo siyo kauli za Serikali ndani ya Bunge letu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa naomba ujielekeze kwenye hoja ambayo unazungumza.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma *good governance*, kuna utawala bora kwenye hiki kitabu, kwa hiyo nimejikita hapo na haya maneno ninayozungumza Waziri alisema hivyo, mimi nayanukuu maneno aliyosema Rais alipokuwa Kanda ya Ziwa alisema ninyi hamtabomolewa kwa sababu mlinipa kura. Nimesema kwenye *characteristics za good governance* lazima kusiweipo

na upendeleo. Ukienda Kimara, ukienda Tabora huko *bulldozer* yanapita yanabomoa nyumba kwa nini tunajitoa ufahamu? (*Makofî*)

Kwa hiyo Mheshimiwa Mhagama anaongea kitu kingine mimi nazungumzia nukuu za Mheshimiwa Rais alizosema, jamani hamkusikia haya mambo?

**MBUNGE FULANI:** Tulisikia.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ndiyo ninayoyazungumza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufanye kazi ndani ya Bunge kwa kufuata utaratibu. Nimetoka kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwa Kanuni hiyo ya 68(1) Kanuni aliyovunja mara ya kwanza illikuwa ni ile ya 64(1), lakini anakwenda sasa kuvunja Kanuni ya 64(1)(d) anataka sasa kutumia jina la Rais humu ndani katika kushawishi Bunge hili kutoa maana ya tafsiri ya kazi ambazo ni za kitaasisi ambazo siyo *part* ya mjadala huu na hazina uhakika wa jambo hilo analolisema kama maana yake ni hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mjadala huu ndani ya Bunge uende kwa kufuata utaratibu, yapo mambo yanakatazwa ya kikanuni, hasa pia hili ambalo anaendelea nalo mchangiaji wa hoja hii, utaratibu ufuatwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, naomba usitafsiri kauli anazozungumza Mheshimiwa Rais, naomba urudi kwenye Mpango wa Maendeleo ambao umeletwa na Serikali.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *tusilinajisi Bunge*. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mimi ni *tax payer representative*, nimekuja hapa kuwawakilisha walipa kodi wangu, nipo hapa kuhakikisha kodi ya walipa kodi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa tafadhali lugha ya kunajisi Bunge siyo sahihi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Nimenajisi wapi Mwenyekiti?

**MWENYEKITI:** Umesema hivyo naomba uifute hiyo kauli.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ina maana Rais hatuwezi kumnukuu.

**MWENYEKITI:** Hapana, umesema lugha ya kunajisi, umezungumza sasa hivi habari kuhusu kunajisi Bunge naomba hiyo lugha uifute.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA.** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la kunajisi Bunge nalitoa, lakini mtuambie kama hatuwezi kumnukuu Rais, Rais hatuwezi kumnukuu?

Mheshimiwa Rais alisema waliojenga kwenye mito wasiondolewe wakati Mwenyekiti wetu hapa mmebomoa kwake, sasa tusiseme haya maneno? Haya ndiyo nayasema *good governance*, hii hela tunayoitoa hapa ni pamoja na kuhakikisha Polisi wanafanya kazi vizuri, Usalama wa Taifa wanafanya kazi vizuri. (*Makof!*)

**MHE. STANSILAS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, tafsiri anayoitumia ya maneno ya Mheshimiwa Rais siyo sawa. Kwa sababu ukweli ni kwamba Mwanza kwenyewe barabara inayojengwa sasa imebomolewa nyumba ya ghorofa nne na nyumba ya Chama cha Mapinduzi ikiwemo. Kwa hiyo tafsiri ya maneno yale siyo sahihi kama anavyoisema naomba ieleweke hivyo na mimi ndiyo Mbunge wa Nyamagana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unitunzie muda wangu, maana si kila mtu anachangia anavyotaka? Si mtulie basi na mimi niseme jamani?

**MWENYEKITI:** Lakini si umeipokea hiyo taarifa?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Hiyo taarifa naikataa! Ninachosema, tulipata taarifa kwenye vyombo vyahabari kwamba wale waliompa kura watasamehewa na wengine watabomolewa. Huo ndiyo msimamo wangu, hiyo haikataliwi. (*Makofi*)

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kuna Taarifa tena?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Msigwa kwamba Mheshimiwa Rais yuko Kyaka leo na amesema wale watu ambao wanalima pembezeno wasibugudhiwe kabisa, wasisumbuliwe, waendelee kulima kwenye mito pembezoni. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa naipokea kwa mikono miwili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo naipokea kwa mikono miwili.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, kama kweli tunataka mipango hii itekelezwe lazima tuwe na *good governance*. Tuko kwenye nyakati ambazo usalama wa raia hauko vizuri, tuko kwenye nyakati ambazo watu hawana uhakika na maisha yao, kwa hiyo, tunapozungumzia kupanga mipango mwenzangu Mheshimiwa Bobali amezungumza hapa kwamba tusije na kauli tu kwamba sasa hivi tunasema viwanda. Utawala uliopita wa Awamu ya Nne ilikuwa *Big Results Now* ambayo imevunjwa juzi juzi na niliwahi kusema nilikuwa hapa hapa, nikasema *Big Results* haitatokea kwa sababu tu ya kubandika vibao kwamba *Big Results*, milango yote ya Halmashauri iliandikwa *Big Results*, lakini hiyo *Big Results* haikuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuonekana! Mbona ninyi wenyewe mnaiponda Serikali iliyopita! Leo tumekuja na kelele za viwanda, kuwa na viwanda ni jambo jema hakuna mtu anayekataa. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Bobali, hivi viwanda lazima tuwe na mipango mkakati, lazima tuwe na maeneo ambayo tunaamini yatatusaidia kuleta mipango mikakati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumlinda Mbunge mwenzetu ambaye alipata mateso makubwa sana kwa hawa watu wanaoitwa wasiojulikana. Kwa masikitiko makubwa wale wahalifu, wale ambao walikuwa wapo tayari kutoa uhai wa mwenzao kwa matakwa yao ambao hawajulikani mpaka leo ambao siyo mhimili huu, siyo Serikali, siyo Mahakama siaona zimepiga kelele za kutosha kwa kitendo kibaya alichofanyiwa mwenzetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningombwa Wabunge wote kwa umoja wetu tusikubali mateso aliyoypata mwenzetu mionganoni mwetu ye yote aje ayapate kwa sababu ni kitu ambacho Mungu hapendi. Sisi sote hapa ni ndugu, mwisho wa siku tunaijenga Tanzania, tusimame wote kwa pamoja

kulaani. Waasisi wa nchi hii hawakutufundisha mambo yanatokea sasa hivi katika nchi hii. Kuona maiti kwenye viroba, kupigana, kuchukizana, kununiana, haya mambo hatukujifunza, tunayaona katika Awamu ya Tano haya mambo yanachipua, tuyakatae wote kwa pamoja kama Bunge ili kwa pamoja tushirikiane, tuhakikishe nchi ya viwanda tunayoitaka, tuweke mikakati ambayo tutakubaliana wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Flatei Massay na baadae Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa Rhoda Kunchela ujiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na nimshukuru sana Mungu kwa kunijaalia afya njema ya kuongea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijielekeze haraka katika mchango wangu kwenye taarifa hii au na hotuba hii iliyolekwa mbele yetu ya Waziri wa Fedha na Mpango. Nijielekeze moja kwa moja kwenye ukurasa wake huu wa 29.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kukuza uchumi wa viwanda ni lazima kabisa ujielekeze katika mpango huu moja kwa moja. Kwa bahati nzuri sana Mheshimiwa Mpango ameandika vizuri sana hapa kwamba kuna miradi ya vielelezo na miradi ambayo itatausaidia Tanzania kwenda kwenye uchumi wa viwanda. Sasa basi ninaomba kutokana na mpango huu ambao ameandika hapa kwenye suala hili la gesi na naomba nijielekeze kabisa katika suala la gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gesi; ameandika vizuri hapa kwamba Serikali inataka kujielekeza katika kujenga mtambo wa kusindika gesi ya kimiminika. Sasa basi ni kweli kwamba miradi hii iko mingi na nimetaja huu mmoja ili walau Waziri Mpango anieleewe. Leo hii gesi *Mnazi Bay* imezalishwa vyaa kutosha. Lakini ukiangalia wataalam

wanatuambia gesi pale inazalishwa na inaweza kutumika kwa kipindi cha miaka 70. Ukiangalia matumizi ya gesi pale hayafiki asilimia 25 mpaka 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji aliyewekeza gesi pale amewekeza kwa bilioni za pesa za kutosha. Sasa ukiangalia gesi inayotumika sio ya kutosha na kwa kuwa sisi tuna gesi na tunataka sasa kutengeneza na kuisadia Tanzania kwenda kwenye uchumi huu na Mwenyezi Mungu ametujaalia kupata gesi, naomba mpango huu basi kadri ulivyoandikwa hapa ujielekeze kutumia gesi ili walau gesi hii ambayo Mungu ametupatia isaidie basi kwenda kwenye viwanda hivi vilivyoanzishwa sasa katika eneo lote la viwanda na Serikali iweke basi mazingira wezeshi ya kujengwa kwa viwanda maeneo yale ambayo bomba la gesi linapita, kwa kufanya hivi tutasaidia uchumi upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi utapanda kwa sababu ukiangalia katika bajeti ya Serikali ya mwaka uliopita, Serikali inaagiza mafuta kwenye bajeti yake zaidi ya robo inatumia kwa kuagiza mafuta nje. Kwa kuwa nishati ya mafuta inaagizwa kwa kutumia fedha za walipa kodi, nimshauri Mheshimiwa Mpango na wachumi wengine waone namna gani ya kufanya kitaalam ili walau gesi hii iweze kuendesha mitambo, tukaachana au tukapunguza kiwango cha matumizi ya mafuta, tukatumia gesi kwa sababu gesi imechimbwa pale na gesi hii ni bure tunaweza kutumia tunavyopenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ikitokea leo Serikali inaanua hata wenywew tu kwa magari ya Serikali ikaondoa mfumo wa kutumia petroli kwenye magari tukatumia gesi ambayo imo imezalishwa pale, Tanzania tutasogea sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Serikali nayo ikiamua kutumia wachumi wetu kushauri na wataalam tulionao nchini wakajenga sheli za kutumia gesi, magari yetu na magari mengine ya Serikali yakabadilisha huo mfumo ikawekwa sheli nyingine Dar es Salaam, ikawekwa sheli

nyingine Arusha, tukawekewa sheli nyingine huko Kigoma, mtandao wa gesi ukaundwa katika nchi yetu, hii nchi ya Tanzania hii itasonga mbele kwa sababu tuna gesi asilia na wataalam wametuambia gesi yetu ni *pure* yaani haihitaji zaidi kubadilishwa na kitu chochote. Tunapata, tunaweka kwenye matumizi na tunaweza kujengewa uwezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ukiangalia leo hii *TPDC* uwezo wao wa kuuza gesi ni mdogo sana, ni mdogo kwa sababu tunaona kabisa wale wawekezaji walioko kule wanaidai Serikali pesa kubwa sana na kwa sababu pesa hii ni nyingi zaidi ya dola milioni 20 na ukiangalia uwezo wao wa kutumia siyo mkubwa na *TANESCO* ni shirika letu la Kitanzania linalojindesha kwa hasara. Kama Serikali itaamua kuweka mpango huu vizuri, na mimi leo nimeamua kuelekeza mchango wangu katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuisaidia sana Tanzania kwenye sekta ile ya madini, nimuombe tena kupitia Bunge hili achungulie tena hili eneo la gesi kwa sababu eneo la gesi mimi siamini kama gesi hii inashindwa kutusaidia Watanzania. Nina wasiwasi na gesi hii ambayo kimsingi haitumiki ipasavyo. Kwa nini nasema haitumiki ipasavyo? Ni kwa sababu gesi tunayo, haitumiki ipasavyo na haiuziki. Kwa bahati nzuri sisi Kamati tumepata bahati ya kutembelea kule na tunaona jinsi ambayo rasilimali hii ya gesi haitumiki vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kujielekeza katika eneo hili la gesi ili walau gesi basi isaidie mitambo mingi ambayo inasubiriwa saa hizi. Ukiangalia Mheshimiwa Rais siku moja nimemsikia katika vyombo vya habari ametembelea maeneo ya Lindi na Mtwara, kuna kiwanda kikubwa pale cha Dangote, hebu angalia kwa nini mpaka sasa hivi hakijapelekewa gesi ili gesi itumike basi, maana kiwanda kile kikifanya kazi ya kuzalisha saruji bei ya saruji inashuka Mikoani na uchumi wa Tanzania unapanda kwa sababu saruji kule imeshafanyika kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona mchango wangu

niuelekeze hapo kwa sababu ninafahamu vizuri matumizi ya gesi ambayo kwa kweli kwa sasa hayatumiwi inavyotakiwa. Pamoja na haya nataka nielezee jambo llingine dogo tu. Katika mpango huu, umeeleza jinsi ambavyo mikopo na jinsi ambayo mikopo chechefu inavyoleta shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana, sasa hivi kuna shida katika maeneo ya mikopo yetu katika mabenki, Mheshimiwa Mpango elekeza sasa namna rahisi ya kusaidia wananchi ili wasiende kupigwa huko katika suala la mikopo, wanapata uchungu kupewa riba ya juu sana. Sasa naomba Mpango huu basi tunapoenda mwaka huu wa 2018/2019 usaidie eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliamua kuyasema haya na huu ndio mchango wangu kwa leo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Flatei Massay. Tunaendekea na Mheshimiwa Sulemani Kakoso na baadae Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Yahaya Massare wajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nipate nafasi ya kuchangia Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali kwa kuleta mpango mzuri na nishukuru sana Serikali kwa miradi ambayo imeanza kutekelezwa kwenye maeneo ya Jimbo langu na Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie na suala la kilimo. Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Iringa, Rukwa, Katavi na Songwe ni mikoa ambayo inategemea sana kilimo cha mazao ya mahindi na mpunga, kwa ujumla ni wazalishaji wa nafaka ambaao wanalisha sehemu ya nchi yetu kwa ujumla. Kwa bahati mbaya sana mikoa hii imepata balaa kwa sababu ya kuzalisha hizo nafaka ambazo kimsingi zinasaidia maeneo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo tunaona kwa mikoa hii tuna balaa ni kwamba Serikali ilipiga marufuku kuza mazao ya aina ya nafaka kwa maana ya mahindi na mpunga kuza nje ya nchi jambo ambalo kwa sasa linawatesa sana Watanzania wa mikoa hiyo. Ninaiomba sana Serikali ifike mahali sasa waangalie kwamba kuchagua zao la mahindi kulima si sehemu ya adhabu kwa wananchi wa mikoa hiyo, kwa sababu wananchi wanajitegemea, wanafanya shughuli za kilimo kwa kujituma sana, wamezalisha kwa kiwango cha juu mpaka wamepata ziada na matokeo yake eneo hilo mkulima hanufaiki na kitu chochote na inaonekana kwamba mkulima wa zao la mahindi hana thamani kubwa kwa sababu zao hilo halina soko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Serikali wasipochukua umuhimu wa aina yake wa kuangalia kutatua tatizo la ukosefu wa soko la mazao hayo wananchi hawatafanya shughuli za uzalishaji na mwakani kunaweza kukajitokeza njaa kubwa sana kwa sababu wanaona watalima kilimo cha kujikimu wao na familia zao tu. Ni vema Serikali lile katazo ambalo waliliweka wakaliondoa ili liweze kuwasaidia wananchi waweze kufanya shughuli zao. Sasa hivi wakulima watoto wao hawaendi shule, hawana uwezo wa kufanya shughuli za maendeleo kwa sababu mazao yako ndani, Serikali hakuna ilichowasaidia na ukizingatia mkulima huyu katumia nguvu zake zote kwake ye ye binafsi na wala Serikali haikumsaidia kitu chochote. Kwa hiyo, naomba mliangalie hili na muone ni jinsi gani mnawasaidia wakulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie zao la tumbaku. Mkoani kwangu wakulima wanazalisha zao la tumbaku, lakini si mkoa wa Katavi tu na mikoa jirani ya Tabora, Mbeya, Kigoma, Kahama kwa maana ya mkoa wa Shinyanga wanalima zao la tumbaku na Mikoa mingineyo. Wakulima walizalisha zao la tumbaku wakajituma, wamefanya shughuli njema wamezalisha lakini zao lile halina soko mpaka sasa na tumbaku yao iko ndani. Niombe sana Serikali wasiliangalie jambo hili kama ni jambo ambalo ni

dogo, ifike mahali Serikali waangalie umuhimu wa kusimamia mazao mengine kama walivyosimamia korosho, walivyosimamia kahawa na mazao mengine kama pamba, walipe kipaumbele zao hili, kwa sababu ndiyo zao liliokuwa linaongoza kwa uzalishaji mkubwa na kuingiza kipato kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao hili limesaidia sehemu za Halmashauri ambazo wanazalisha ziliokuwa na kipato kizuri kuliko ilivyo sasa, ni vema sasa Serikali ikaona umuhimu wa kulisimamia zao hili ili na wao waweze kunufaika kama mazao mengine yalivyosimamiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie jitihada za Serikali zilizofanywa hasa kupeleka umeme vijiji. Niipongeze Serikali kwa juhudhi ambazo zimefanyika lakini niombe sasa Serikali ielegeze nguvu sana kuhakikisha ile miradi ya umeme *Phase III* inafanyiwa kazi na inasambazwa kwenye maeneo husika. Jimboni kwangu nina vijiji 32 ambavyo viro kwenye mpango. Mpaka sasa bado hata kijiji kimoja hakijafanyiwa kazi kwa sababu umeme ulikuwa umepangwa kuanza *Phase III* bado. Ulionanza kufanyiwa kazi ni ule ambaulikuwa wa mpango wa *Orion* ambauliji vitano wamepata, tunaishukuru na kuipongeza Serikali. Pia tunaomba maeneo mengine ambayo yilibaki yaweze kufanyiwa haraka na kuweza kufanya shughuli za maendeleo yatakayowasaidia sana wananchi kwenye eneo la Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo tetesi kuwa mradi huu umekwama kwa ajili ya kushindwa kuelewana kati ya wakandarasi, ninaiomba Serikali iingilie zoezi zima la kukamilisha utaratibu ambauliji ni wa kisheria ili waweze kuwaruhusu wakandarasi waweze kufanya kazi yao kwenye mikoa ambayo walikuwa wameelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la elimu. Niipongeze Serikali kwa jitihada ambazo zimefanywa kwa kupata idadi kubwa ya watoto ambauliji wanafauli. Inaonesha Serikali imeangalia mfumo mzima na kuuthamini nzima hasa ya sekta ya elimu. Tunalo tatizo kubwa sana,

tuna idadi ya wanafunzi ambao wamefaulu na wamekosa vyuo nya kwenda kusoma. Niombe sana Serikali iweke mazingira ya haraka kuhakikisha wale wanafunzi ambao wamefaulu wapewe nafasi kwenye vyuo ili waweze kuanza masomo ya kwao katika vyuo ambavyo wameomba. Na tuiombe Serikali, zile tofauti zinazojitokeza, zinazowafanya watoto washindwe kufika kwenye maeneo husika ya vyuo wazitoe ili waweze kuratibu haraka, watoto waanze kupata masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna maeneo kwenye suala hili la elimu hasa maeneo ya jumboni kwangu. Tunayo majengo mengi ambayo yameanzishwa, tunaomba sana Serikali ielegeze nguvu kusaidia yale majengo ambayo yameanzishwa na Halmashauri na Halmashauri zikawa hazina uwezo hasa yale yaliyoanzishwa na wananchi wenyewe kwa kujitolea. Serikali ielegeze nguvu kusaidia maeneo hayo ili kuweza kumudu ufaulu wa wanafunzi walio wengi kwenye maeneo husika ambayo ni kwenye eneo la shule za msingi, eneo la shule za sekondari, kote huko kunahitaji kukamilisha yale majengo ambayo yameanzishwa na wananchi kwa jitihada zao binafsi, lakini uwezo wa Halmashauri wa kuweza kuhudumia nguvu za wananchi ukweli bado hazijakuwa kubwa za kutosha. Kwa hiyo, tunaomba na maeneo haya Serikali ielegeze nguvu kuhakikisha miradi hii inasimamiwa na inafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye eneo la afya. Tunaipongeza Serikali kwamba huduma za dawa kwa sasa zinapatikana, lakini bado tuna changamoto kubwa sana hasa pale sera ya Serikali ilipokuwa imezungumza kwamba kila kijiji kiwe na zahanati. Vijiji vingi vimejitokeza, wananchi wameweza kujenga majengo mengi na wameandaa utaratibu wa kuanzisha majengo ya zahanati lakini majengo yale bado hayajakamilika.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali itenye fedha za kutosha kuhakikisha nguvu za wananchi ambazo wamejitolea waweze kupewa nafasi ya kukamilisha yale majengo. Naamini tukifanya hivyo tutakuwa tumewasaidia sana

Watanzania hasa wa maeneo ya vijiji, ambako bado huduma za afya zinahitajika kwa karibu sana ili kuweza kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni sekta ya maji. Kwenye eneo la sekta ya maji Serikali inajitahidi kufanya kazi yake vizuri, lakini kwa ukubwa wa nchi yetu bado tunahitaji miradi ya maji kwa kiwango kikubwa sana. Niombe sana Mkoa wa Katavi ambaao upo unategemea sana kupata maji kutoka kwenye chanzo cha Bwawa la Milala bado hautoshelezi. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba maji yapelekwe, hasa tunahitaji mradi mkubwa wa kutoka Ziwa Tanganyika ambaao utapeleka maji kwenye Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi, lakini utasaidia kwenye maeneo mengine ya maeneo husika ya Jimbo la Mpanda Vijiji. Kwa hiyo, niiombe Serikali iharakishe kuweka mpango mkubwa wa maji ambaao utasaidia kutoa kero ya maji ndani ya Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naiomba sana Serikali, Mkoa wa Katavi hauna hospitali ya Mkoa. Tunaomba Serikali iweze kutenga fedha za kutosha kujenga hospitali ya Mkoa sambamba na hospitali ya Wilaya mpya ya Tanganyika ambayo bado haijaanza kujengwa. Tunategemea sana Serikali itafanya hayo, ili kuweza kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ahsante.  
*(Makof)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Kakoso. Tunaendela na Mheshimiwa Rhoda Kunchela, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2018/2019 pamoja na Mwongozo wake wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza juhudini kubwa zinazofanywa na Serikali yangu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika jitihada zake za kuhakikisha rasilimali za nchi hii zinanufaisha wananchi wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niipongeze Serikali kwa jitihada za kusogeza huduma karibu na wananchi ikiwemo hili kubwa la Serikali kuhamia Dodoma ambapo ni katikati na Makao Makuu ya nchi hii. Kuna kazi nydingi zinazofanywa na Serikali ni njema kabisa, lakini pia kuna changamoto kadhaa. Sasa mimi nijielekeze sasa hivi katika changamoto, lakini pia katika kupongeza yale ambayo yamefanywa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais na Serikali yake na Mawaziri wake ambao tuko nao hapa wamejitalidi na wameonesha dhamira ya kweli katika ujenzi wa reli katika kiwango cha *standard gauge* ambacho leo mkandarasi wa pili ameshasaini mkataba, reli hii itasogea hadi karibu na Mkoa wa Singida, kule Makutupora. Mimi nikiwa Mbunge wa Mkoa wa Singida, mikoa ya katikati ni mikoa ambayo inanufaika sana na itanufaika na ujenzi wa reli hii ya kati kwa kiwango ambacho ni cha *standard gauge*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunazo changamoto pamoja na jitihada kubwa sana za Serikali kutaka kuunganisha mikoa yake ifikike kwa njia ya barabara. Mkoa wa Singida ukiwa mmojawapo kuunganishwa na Mkoa wa Mbeya, lakini pia na Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango nimeona jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha miundombinu hii inafanyika, lakini niombe jicho la tatu katika barabara za Mkoa wa Singida kuunganishwa na Mkoa wa Mbeya. Barabara inayotokea Mkoa wa Singida kuunganishwa na Mkoa wa Simiyu kuititia Daraja la Sibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia kuu na uti wa mgongo

wa uchumi wa nchi yoyote duniani miundombinu ikiwa rafiki ni rahisi mwananchi kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine, itarahisisha ulipaji wa kodi na hata kuirahisishia Serikali kukusanya maduhuli na kodi mbalimbali kuititia wananchi hawa wanapowezeshwa katika kuhakikisha wanasafiri na kupeleka mazao yao katika masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kufanya Makao Makuu Dodoma ningeomba sana Serikali iangalie barabara inayotoka Mkiwa kwenda Rungwa hadi Makongolosi. Kuna ahadi ya Serikali ya kujenga barabara ile katika kipindi hiki, lakini kumekuwa na ukimya ambao hatuelewi. Sisi Wabunge ambao tulienda kuwaambia wananchi kule kwamba Serikali yenu sikivu ya Chama cha Mapinduzi, mimi nikiwa Mbunge wake, tumeiomba na imekubali kujenga barabara na hata Mheshimiwa Rais alipokuja pale aliendelea kutoa ahadi hii, lakini kumekuwa na ukimya ambacho tunapata kidogo mashaka, tunaomba basi mje mtuambie mmeifikia wapi katika kujenga barabara ile kutoka Mkiwa kuelekea Rungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kipande pekee ambacho kimebaki kikubwa chenye urefu mkubwa, barabara hii ambayo leo bado ni kilometra 413. Ni barabara pekee ambayo ni ndefu, lakini barabara ya zamani, barabara ambayo ina uchumi mkubwa sana katikati yake kuna *reserve* za wanyama na maeneo mbalimbali, lakini na wakulima wengi wazuri wako maeneo haya ambayo tunatarajia kuleta na kuza mazao hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo tunahitaji tuiombe Serikali yetu ilifanyie kazi kwa bidii sana ni suala la umeme vijijini. Kuna maeneo mengine kazi imefanyika vizuri na nipongeze jitihada za Mawaziri husika kwa kazi wanazozifanya, hasa Mheshimiwa Kalemani, lakini na Naibu ambaye ameteuliwa hivi karibuni, naona jitihada zake zinaweza zikatupeleka pazuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme vijijini Mkoa wa Singida, mkandarasi alitangazwa, lakini baadaye

akapotea. Tulipofuatilia tukaambiwa kwamba, yule mkandarasi kuna sifa zilipungua, walishindwana naye, kwa lugha ya sasa tunasema alitumbuliwa. Sasa alipotumbuliwa ndiyo wamepata mkandarasi mwingine, leo wananchi wa Mkoa wa Singida hatujafika popote, hakuna hata kijiji kimoja ambacho unaweza ukasema *REA Awamu* ya *Tatu* nayo imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe basi Serikali yangu ya chama changu basi iwaangalie wananchi waaminifu wa Mkoa wa Singida katika umeme vijijini. Ni eneo pekee ambalo lina tatizo sana vijiji, vingi havijafikiwa na umeme na mimi naamini mkifanya hivi itatusababisha sasa na wananchi wa Singida, maeneo yote ya Mkoa wa Singida na hata Mkoa wa Dodoma bado wakandarasi hawa wanaonekana hawajafanya kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ahadi zetu kwa wananchi wetu kuhakikisha tunaboresha huduma za afya katika vijiji vyetu kwamba tujenge zahanati kila kijiji. Wananchi wameanza kujenga kwa juhudhi, Serikali zao za vijiji na wakati mwingine tunaiomba Halmashauri au Serikali itsaidie kufunika yale maboma, lakini tuliahidi kila kata kujenga kituo cha afya. Hili naomba sana katika mipango tunayokwendanayo nalo tulizingatie, ni mionganini mwa mambo ambayo ninaamini yatatufanya tuwe na jambo zuri la kufanya huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji vijijini ni changamoto kubwa sana. Vijiji vyetu vingi na hasa mikoa kame hii ya Dodoma na Singida hatuna mabwawa, basi tufanye juhudhi za makusudi angalao basi malambo madogo madogo katika maeneo mbalimbali. Tumekuwa tukisema hapa Wabunge tunaotoka katika mikoa hii kwamba, kungekuwa na mito basi angalau, hatuna mito, mito ile ni ya msimu mvua ikinyesha baadae jioni imekauka, njia rahisi ya kusaidia wananchi ni kuchimba visima. Halmashauri zetu tunajitahidi, Serikali basi ituunge mkono katika hili ili wananchi wetu wengi nao wapate huduma hii. Ninaiomba Serikali mlitolee jicho la tatu kuona vijiji vyetu vingi vinapata huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu katika kuona kwamba, sasa gesi hii ambayo ipo kwenye Mikoa ya Kusini imefika Dar es Salaam. Ni wakati sasa wa kuona na kujipanga na kuona tunafanyaje ili gesi hii ipite mikoani ikiwezekana ifike hadi Mwanza kwa kupita Dodoma, ikija Morogoro – Dodoma – Singida pengine Simiyu au Shinyanga ikafika mikoa ya Kanda ya Ziwa ambapo kuna viwanda vingi. Naamini watu wanashindwa kujenga viwanda maeneo mengine kwa sababu tu pengine ya miundombinu, likipita bomba la gesi tukawekeza katika gesi, nchi hii ninaamini kule mbele hatutakuwa na changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wawekezaji wako wengi wana nia ya kuwekeza, lakini changamoto hizi za miundombinu ikiwemo matatizo ya umeme, kukatika-katika kwa umeme kunasababisha watu wapate uwoga wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango basi muangalie mipango madhubuti ya kuhakikisha bomba la gesi linakwenda hadi Mwanza pengine na Mikoa ya Kaskazini na hata Mikoa ya Kusini kama Mbeya na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilikuwa na haya machache yanatosha. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahaya Massare. Tunaendelea na Mheshimiwa Mendrad Kigola na baadae Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha na Mheshimiwa Augustino Masele ajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata nafasi, ili niweze kuchangia Mapendelekezo ya Mpango wa Taifa wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuipongeza Serikali, katika miaka miwili Serikali imefanya mambo

makubwa sana na Wabunge kwa macho yetu kwa masikio yetu, tumesikia na tumeona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopanga mpango wa miaka ya mbele lazima uangalie miaka ya nyuma umefanya nini. Serikali miaka ya nyuma tukichukua *reference* kwa kweli, imefanya kazi nzito sana na mambo yanaonekena. Nikianza kutoa mifano, Serikali ilipanga kununua ndege na kweli ndege imenunua. Serikali ilipanga kutoa elimu bure na kweli kazi hiyo imeanza kutoa elimu bure kwa watoto wetu. Serikali ilipanga kupanua Bandari ya Dar es Salaam na kweli Serikali inapanua Bandari ya Dar es Salaam. Serikali ilipanga kujenga bomba la mafuta kutoka Tanga mpaka Uganda, Serikali inafanya na tunaona na tunasikia. Serikali ilipanga kununua meli kule Bukoba na Mheshimiwa Rais tumeona hata juzi akisema pale, tunaona Serikali inafanya. Serikali tunaona kila inachopanga na inasema, tulipanga hiki tumefanya moja, mbili, tatu, ndiyo utekelezaji tunaoutaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kweli, anasimamia vizuri. Ndiyo maana nataka tuende kwa *data*, ameahidi nini amefanya nini na anasema kila mmoja tunaona kitu kinachofanyika. Leo, sasa Serikali imeleta mapendekezo ya mpango, yaani Wabunge tutoe mapendekezo, sio tulaumu, tutoe mapendekezo tunataka nini. Sasa na mimi nataka nitoe mapendekezo yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nimesoma vizuri mwongozo, nimesoma vizuri mapendekezo ya Serikali ambayo imeleta kwa Wabunge tutoe mapendekezo. Kuna maeneo ambayo lazima tupendekeze ili Serikali ikae vizuri na Serikali ili ifanye kazi vizuri lazima iwe na fedha. Bahati nzuri Serikali imesema kuna mapungufu kidogo katika ukusanyaji wa kodi, hiyo na mimi nakubaliana kabisa, sasa tunafanyaje? Naomba niishauri Serikali, kwenye eneo hili lazima tuhakikishe kwanza tunatoa elimu ya kutosha kwa walipa kodi wetu ili mtu anapolipa kodi asione kama adhabu, aone kama ni hiyari yake kutoa kodi bila matatizo yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kinachotakiwa ni kutoa elimu ya kutosha kwa wafanyabiashara, hilo la kwanza. Pili, vitendea kazi lazima viwepo. Kwa mfano, sasa hivi wafanyabiashara wengi zile mashine ambazo tunatumia kwa ajili ya kukata risiti mashine zile hazipo, bado ziko chache wengine hawana, nyingine wanasema mbovu. Kwa hiyo, hatuwezi kukusanya mapato kama vitendea kazi bado havieleweki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, sasa hivi ukusanyaji kodi sio lazima uende *TRA*, naomba Serikali itafute mfumo mzuri, wewe unaweza hata ukawa barabarani unatembea ukatumia hata M-Pesa ukalipa kodi. Kwa mfano, kama wewe ni mfanyabiashara au kama wewe mtu una magari yako kwa mfano hata *insurance*, kama mtu anataka kulipa *insurance* siyo lazima aende *TRA* au aende wapi, analipa kwa njia ya M-Pesa tu. Kwa hiyo, nataka niseme hivi tuhakishe kwamba tunaweka vitendea kazi vimekaa vizuri kwa walipa kodi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la msingi sana, nimeona kwenye taarifa ni uvujaji wa mapato. Hii ni njia ambayo Serikali inaweza kuidhibiti na bahati nzuri mnajitahidi sana kudhibiti mianya, zile njia za panya, njia za nini sasa hivi hazipo zimepungua sana naipongeza. Na mimi naiomba Serikali iendelee kutafuta mbinu kuhakikisha kwamba, kile kiasi ambacho kinakusanywa kinatumika vizuri, hakivuji, hakuna mianya ile ya uvujaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naipongeza Serikali kwenye Wizara ya Afya. Wizara ya Afya hata Mheshimiwa Ummy leo amejibu swali hapa vizuri sana kwamba Wizara ya Afya zamani ilikuwa na uwezo wa kupewa shilingi bilioni 29, lakini sasa hivi tuna uwezo wa kuipatia Wizara ya Afya shilingi bilioni 296 kama sijakosea, ni kiwango kikubwa sana. Katika hiyo, tumekwenda vizuri, katika fedha hiyo bahati nzuri Serikali imeangalia kwamba umuhimu wa watu lazima tuwe na afya nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe msisitizo,

Serikali ihakikishe kwamba vituo vya afya vijijini vinamaliziwa kujengwa, kuna maboma mengi sana, bado hatujamaliza vituo vya afya. Kuna zahanati, tuna maboma ya zahanati bado hayajaisha nchi nzima, lazima tujitahidi tuhakikishe kwamba kwenye sekta ya afya tunapeleka fedha za kutosha na bahati nzuri kwenye mpango umeongea, lakini bajeti inayokuja kwa sababu tunaongelea mpango halafu tunakuja kuupangia bajeti. Naomba kwenye sekta ya afya tuangalie tumeipatia fedha ya kutosha kwenye bajeti inayokuja na mpango ueleze vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya maji. Sekta ya maji vijijini naiomba Serikali, bado iongeze nguvu kubwa sana. Kwa sababu hata kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini wananchi wanapata taabu sana ya maji, lakini katika mpango, bahati nzuri Waziri wa Fedha ameeleza vizuri kwamba, ataiangalia sekta ya maji, naomba aiweke kipaumbele zaidi. Tuhakikishe kwamba miundombinu yote ya maji, kama kuna matenki, kama kuna visima, tuhakikishe kwamba wananchi wana uwezo wa kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya leo hii mwananchi hawezi kutembea kilometra 10, kilometra 20. Kuna sehemu nydingine nimeona watu wanachota na punda kilometra ngapi, hayo ni mambo ya zamani sana, naiomba Serikali ihakikishe kwamba sekta ya maji imekaa vizuri, wananchi wetu wapate maji ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye sekta ya umeme, bahati nzuri umeme vijijini Serikali imekaa vizuri na wameshafanya surveytayari kwenye vijiji vingi. Hata kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini wamekuja, tumeona wamefanya surveyna Serikali imeahidi, imesema kila kitongoji kitapata umeme na kila kaya itapata umeme. Tumeona hatua zimeanza kufanyika, lakini nataka niiombe Serikali, tuhakikishe kila tulichopanga tunatengeneza *time frame*, tusije tukaahidi halafu tukachukua muda mrefu sana, kwa sababu sasa hivi tunaweka na muda, ukiahidi kitu lazima kuwe kuna *progress* ya kazi, lakini bahati nzuri kwenye vijiji vyetu mmenza tayari, *survey* imeshafanyika, sasa

tunategemea Serikali ianze kupeleka nguzo katika vijiji vyetu na katika mitaa yote ambayo imeshapimwa tayari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee tena suala lingine ambalo ni la muhimu sana. Wenzangu wameshaongea, hasa Wabunge wanaotoka Rukwa ambalo ni suala la kilimo hasa kilimo cha mahindi inaonekana bado kuna tatizo na tatizo tunaongelea ni soko. Nafikiri kuna kilimo cha matumizi ya chakula, kuna kilimo cha biashara. Kwa mfano, nataka nikwambie Tanzania bahati nzuri kila mikoa imepata neema, ukienda Kaskazini wenzetu utakuta wanaongelea labda karafuu, ukienda Magharibi huku utakuta wanaongelea masuala ya pamba, ukienda Kusini wanaongelea masuala ya korosho, ukienda mikoa ya Rukwa Kusini tena wanaongelea masuala ya mahindi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kwenye korosho Serikali inaweza ikatafutia soko korosho na ika-*subsidise* fedha. Kama kwenye pamba Serikali inaweza ikapeleka fedha kwenye pamba, basi ipeleke fedha hata kwenye kilimo cha mahindi ili watu wa mahindi waweze kuhakikisha kwamba kilimo kinaenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuambie kitu kimoja, Tanzania ni nchi ambayo inategemea zaidi kilimo cha mahindi kuliko kilimo kingine. Nitoe ushauri kwamba kama Serikali itashindwa kununua mahindi ya wakulima, mahindi yakaozea kwenye maghala basi iruhusu ifanye *open market*, kama kuna uwezekano wa watu kuuza nje, wauze nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nataka nikumbuke Mheshimiwa Rais alisema vizuri sana, kwamba tusiwigandamize wakulima wa mahindi. Kama debe litauzwa hata shilingi 100,000 basi liuzwe laki moja ili mkulima apate. Wewe kama unaona unashindwa kununua basi lima. Na sasa hivi bahati nzuri mvua zinanyesha sehemu kubwa sana, lakini isionekane kwamba wakulima wa mahindi hatuwa-*support*, tuwape uhuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba inaweza ikatokea njaa, tuwafundishe jinsi ya kuhifadhi mahindi, lakini tuisiwafundishe kuuza kwa bei ndogo ili wapate hasara, wakulima wanalamika. Tuseme wahifadhi mahindi, lakini wawe wanaweza kulima zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona, hili naipongeza Serikali kwa upande wa mbolea, Serikali imetoa bei elekezi kwa wafanyabiashara, imesimamia vizuri na imefanya vizuri sana. Sasa hivi wakulima wana uwezo wa kununua ile mbolea lakini ukienda kwenye Mjimbo yetu mbolea bado haijafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Jimbo la Mufindi Kusini hata Wilaya ya Mufindi sasa hivi ndio tunalima lakini mbolea ya kupandia haipo. Naomba Waziri wa Kilimo atusaidie kwenye hilli, mbolea ya kupandia ifike miezi hii; miezi hii Mufindi kule ndio tunalima sasa hivi. Mbolea ya kupandia ukileta mwezi wa 12 hatuwezi kuoandia mahindi, tutakuwa tumeshachelewa, tunaenda na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali kwa upande wa kilimo ihakikishe kwamba mbolea inafika kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu gesi; hili suala la gesi kwanza ni neema. Tumepata neema kubwa sana kwamba uchumi wa nchi ili upande tumefanikiwa kupewa gesi na gesi inatoka Mtwara lakini ili gesi ipate soko ni lazima tupanue wigo. Kama kuna viwanda vinatakiwa kutumia gesi basi tuwaruhusu watumie gesi ili Serikali iweze kukusanya hela nyingi sana na fedha nyingi sana tunaweza tukapata kutoka kwenye masuala ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vingi kwa mfano mikoa ya Pwani hiyo nimeona wamejenga viwanda vingi sana. Sasa vile viwanda kama havitatumia gesi, tutazalisha gesi nyingi halafu tunasema soko tunashindwa kumbe viwanda vile havitumii gesi. Naiomba Serikali basi ihakikishe kwamba viwanda vyote vinatumia gesi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hata Mufindi tuna viwanda vingi sana, kama kweli mtatuletea gesi na viwanda vya Mufindi, kwa mfano tuna Kiwanda cha Chai kikubwa sana, katika Afrika nadhani ni kiwanda cha kwanza, tuna Kiwanda cha Karatasi, katika Afrika nadhani ni cha kwanza na tuna viwanda vya mbao. Vile viwanda vyote vikitumia gesi, nadhani gesi itapata soko kubwa sana na Serikali itakusanya mapato makubwa na bajeti tuliyopanga ya mwaka 2018/2019 tumesema Serikali itakusanya shilingi trillioni 32.47. Sasa hizi shilingi trillioni 32 kama hatutapata *revenue* kutoka kwenye gesi, tutapata wapi? Tukitaka kufanikiwa makusanyo makubwa lazima tuhakikishe tunafanya makusanyo makubwa kwenye gesi, tunaweza kufikisha hilo lengo la shilingi trillioni 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe tunakusanya mapato kutoka kwenye madini, tutapata hizo shilingi trillioni 32, tunapata mapato kutoka kwenye maliasili na utalii tunaweza kufanikiwa. Kama hatutakusanya kwenye vyanzo vikubwa tukategemea kwamba tutakusanya kutoka kwenye sigara, vinywaji maana kwenye vinywaji ndiyo tunapandisha hata bei, hii hatuwezi kufikia lengo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuhakikishe kwamba kwenye vyanzo vikubwa kwanza vile tunakusanya mapato ya kukamilika halafu tunakuja kwenye vyanzo vidogo. Ukitsema kwamba labda utategemea minada ya kuuza haya masoko ya pembeni ya wakulima wadogo wadogo hii haitasaidia. Tuhakikishe kwamba tunakusanya kutoka kwenye vyanzo vikubwa ili tufikie lengo tulilojiwekea la shilingi trillioni 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa wafugaji na wenyewe lazima waheshimiwe sana. Kuna sehemu nyingine nataka nimshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani, sasa hivi ule ugomvi wa wafugaji na wakulima umepungua sana, naipongeza sana Serikali, ni jambo zuri sana hilo, sasa hivi hatujasikia malalamiko makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali isimamie

vizuri kuhakikisha kwamba wafugaji wanalindwa kwa sababu na wafugaji lazima tuwaheshimu, wanafuga ng'ombe na tunapata nyama, bila nyama hatuwezi kuishi. Ukiangalia katika Afrika nchi ya kwanza kwa ufugaji nadhani ni Ethiopia kama sikosei na ya pili ni Tanzania, kwa hiyo lazima tuwaenzi. Lazima kuwe kuna mpangilio mzuri ili isitokee kugombana kati ya wafugaji na wakulima. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali naona kwenye hilo imefanikiwa na sasa hivi inakwenda vizuri na huo mpango wa kudhibiti wafugaji na wakulima ili waende vizuri. Wafugaji wafuge mifugo hatuwakatalii, wakulima na wenyewe walime kama inavyowezekana, hii itakuwa ni vizuri sana na watu watakuwa na maisha mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigola kwa kujikita kwenye mpango. Tunaendelea na Mheshimiwa Ryoba Chacha na baadae Mheshimiwa Augustino Masele ajiandae.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Naomba na mimi nichangie kwenye mpango huu mambo machache, lakini ya msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Wabunge huwa hawailewi hii Serikali, mmojawapo ni mimi huwa siielewi, ninazo sababu za msingi mnisikilize wote mkae kimya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni ya wakulima na wafugaji, unapokuja kwenye mikoa iliyopo Kanda ya Ziwa, wafugaji waliopo kandokando mwa hifadhi na mapori ya akiba na misitu wana kilio kikubwa sana. Ng'ombe wa wafugaji wa mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza mpaka huko Kagera inataifishwa na Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi maskini ambao tegemeo lao ni mifugo, leo unapiga mifugo mnada, unamuacha mfugaji akiwa maskini akiwa ana watoto

wanamtegemea yeye, akiwa na rundo la familia nyuma wanamtegemea yeye awalipie ada za chuo kikuu na shule za sekondari, leo mmepeiga minada, watu wetu wamebaki maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Serengeti ng'ombe wameuzwa, watu wanalia. Mama mmoja ng'ombe wameuzwa wote, mama akapigwa miaka mitatu jela na kulipa faini ya shilingi 800,000, ameacha familia haina chochote, mnatupeleka wapi ninyi Serikali ya CCM? Mnasema ninyi ni Serikali ya wanyonge, mnatesa wafugaji. Mimi nawaambia wafugaji wa Kanda ya Ziwa wale wa Mikoa ya Simiyu, Biharumulo, Serengeti na Mkoa wa Mara hii Serikali ya CCM 2020 ishughulikieni kweli. Haiwezekani wafugaji wetu waendelee kuteswa na Serikali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kuwaelewa, njoo kwenye viwanda. Nchi hii tuna viwanda vyta kuchakata mazao ya mifugo vingapi, kiwanda kipo kimoja tu, tena cha mjasiriamali mmoja Mtanzania yupo pale Mwanza, ndiye mwenye kiwanda kikubwa ambacho angalau. Tembea kokote huko hakuna wana bucha tu wanaita viwanda, hakuna kiwanda ni *butchery*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri Mheshimiwa Mpango, tuambie mna mpango gani kuhusu viwanda vyta kuchakata mazao ya mifugo, mtuambie hapa. Ukienda hata kwa yule ambaye ana kiwanda pale Mwanza analalamika kweli, kodi kibao, hakuna namna ya kumsaidia yule mjasiriamali, tumsaidie kwa ajili ya kusaidia wafugaji wetu wa Kanda ya Ziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Mpango uniambie, mifugo ya nchi hii ambayo kimsingi tuna mifugo mingi, mna mpango gani maana kiwanda ni hicho cha huyo na kiwanda kingine kipo huku Rukwa yule Mbunge mstaafu yule Mzee Mzindakaya, kinakaribia kufa kile. Tumeshindwa kuwasaidia watu wetu ili wawe na viwanda vyta kwao wenye. Kwa hiyo, nikisema siwaelewi, siwaelewi kweli na wananchi hawawaelewi kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye fedha za maendeleo, mwaka wa fedha uliopita zilitengwa shilingi trilioni 11.8 kwa ajili ya maendeleo, zikatoka shilingi trilioni 6.5 sawa na asilimia 55, fedha za maendeleo hizo. Kwenye bajeti ya mwaka huu, fedha zilizotengwa za bajeti ni kama shilingi trilioni 12 kwenye robo ya kwanza zimetoka shilingi trilioni 1.3 sasa piga zipo robo nne. 1.3 trilioni mara nne ni ngapi, utaona ni kama asilimia 44, hapo wanasesma hapa kazi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Serengeti, Mkoa wa Mara barabara ya lami inayounganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha, tangu Mheshimiwa Kikwete aliondoka mzee mpaka leo na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi wa barabara ni Mheshimiwa Magufuli, tangu hapo barabara ya kuunganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha imekuwa ni ndoto. Kibaya zaidi allyepewa *tender* kujenga barabara ile ni rafiki yake na Magufuli na ndio huyu amempa kujenga uwanja wa Chato sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mpango unapokuja tuambie yule mkandarasi mliyemba kilomita 50 miaka zaidi ya mitano ameshindwa kumaliza kilomita 50, bado mnaendelea nae? Barabara ya kuunganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha “*baakerwa*” wameshindwa! Barabara hiyo kipande cha Mugumu - Nata mwaka wa fedha 2016/2017 kilitengewa shilingi bilioni 12, mwezi wa 12 2016 wakatangaza *tender* mpaka leo wanatafuta mzabuni, sema hamna hela bwana msitudanganye hapa! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maji nako ni aibu. Mwaka jana zimetengwa zaidi ya shilingi bilioni 600 kwenye maji, zimetoka asilimia 18. Kwenye nchi hii shida kubwa ya watu wetu ni maji, ukienda vijiji ni maji na ukienda mijini ni maji, unatoa asilimia 18 tu halafu unasema hapa kazi tu, hapa kazi kwa kitu gani...*mura nu tune ng'ana [unatafuta jambo].* (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya sana, barabara sasa hivi wameanzisha kitu kinaitwa *TARURA*.

*TARURA* sijui iko chini ya nani? Ukija kimsingi Madiwani na Mkurugenzi ndio wasimamizi ambao wapo karibu na wananchi, barabara zimeondolewa kwa wala barabara hazipo chini ya Mkurugenzi tena, hazipo chini ya Baraza la Madiwani wala Mbunge, zipo chini ya kitu kinaitwa *TARURA*. *TARURA* ina mapembe, wao wenyewe ndio wanajua walime barabara ipi na waache ipi, mimi sielewi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekomba *engineers* waliokuwa kwenye Halmashauri za Wilaya na Manispaa wamekwenda *TARURA*, Halmashauri za Wilaya hazina wahandisi sasa hivi. Mheshimiwa Mpango unapokuja utuambie mpango wenu ni kuua Halmashauri au mna mpango gani? Kwa sababu kwenye mapato mimi sijawahi kuona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zilikuwa zinakusanya mapato vizuri sana, *property tax*, ushuru wa mabango na ushuru mwininge mwangi walikuwa wanakusanya. Leo Serikali hii inayojiita Serikali makini imechukua mapato ya Halmashauri hata ushuru, ushuru unakusanywa unapelekwa Serikali Kuu halafu ushuru wenyewe umeshindwa kukusanya, Halmashauri zinakaa hata kuendesha vikao imeshhindikana. Mtuambie mna mpango gani hizi Halmashauri, mna mpango wa kuziua Halmashauri kwa kuzinyng'anya vyanzo vya mapato? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia Madiwani nchi nzima, wawe wa CCM ama CHADEMA wote muungane pamoa, ninyi ndiyo mnatafuta kura za Wabunge na Rais. Madiwani wote wa CCM na CHADEMA unganeni muishughulikie hii Serikali ijue kwamba ninyi ndiyo wasimamizi wakubwa wa miradi ya maendeleo. Haiwezekani Baraza la Madiwani, haiwezekani Halmashauri zinyang'anywe mapato, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Serikali inaitwa Serikali ya bomoa bomoa. Mmewakuta wananchi, enzi hizo mlikuwa hamuwapimii viwanja, walijenga kwenye *squatters* ndiyo utaratibu uliokuwepo, leo mnabomoa hovyo hovyo. Serikali

makini, Serikali ya wanyonge! Mimi naangalia kilio, eti Rais anabomolea watu wa Dar es Salaam halafu anakimbilia Mwanza anasema, eti Mwanza ndiyo walimpa kura, hivi Mwanza ndiyo walimpa kura nchi hii nzima! Sasa kwa kuwa Mwanza ndiyo walimpa kura, aache mwaka 2020 uone maeneo mengine watamshughulikia kama hana akili. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira. Viwanda hakuna, ukija kwenye nchi hii, hivi wamemaliza wanafunzi wangapi vyuo vikuu, wapo wapi, ajira ziko wapi? Mnasema Serikali ya viwanda, hamjajenga vyuo vya kati vya ufundi, vyuo vya VETA, unakuja Mkoa mzima unaweza kukuta Chuo cha VETA kimoja au mikoa mingine haina. Mimi hata pale Serengeti nataka kufungua kiwanda, lakini ukitafuta hata fundi tu wa kuongoza ile mitambo hayupo, mkoa mzima hayupo! Hata nchi hii wa kuhesabu ni wachache, sasa tunaenda wapi? Elimu ya ufundi iko wapi tuambieni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango unapokuja hapa sema mpango unasema nini kuhusu VETA kila Wilaya, tungelikuwa na VETA kila Wilaya tungekuwa na vijana mafundi wazuri tu ambao wangekuwa wanachakata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nendeni hata Kenya hapo msiende mbali, msiende Ulaya, nenda hapo Kenya uone vijana wanavyofanya kazi, wana mafunzo mazuri na wanajajiri. Leo unasema, kwa mfano hivi mwalimu ambaye amemaliza chuo kikuu ana *Bachelor of Arts* atajajiri kwenye nini maana kazi yake ni kufundisha, anaenda kujajiri wapi, akajenge shule, umempa mtaji? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya. Ninyi Serikali ya CCM nisikilizeni. Sera yenu ya afya inasema kila kijiji kiwe na zahanati na kila kata iwe na kituo cha afya. Njoo Serengeti tuna vituo vya afya viwili tu, Kituo cha Nata na Ilamba, hata hivyo vituo viwili bado havijakamilika vizuri vina mapungufu kibao, lakini sera yao inasema kila kata iwe na kituo cha afya, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtuambie pesa mnayojidai mnasema mnakusanya zipo wapi? Mimi nataka waniambie wanasema wanakusanya matrillioni, tunataka kuona huko mtaani ukienda hakuna pesa wananchi wanalamika, hata Wabunge wanalia. Wananchi wanalia kweli, sasa mtuambie hizo pesa mnakusanya mnalalia au mnafanya nini! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuanenda kwa Mheshimiwa Masele.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kujadili na kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusiana na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Wasaidizi wake kwa kuja kwa wakati na mpango mzuri wa mapendekezo haya. Mimi katika kuchangia niseme tu kwamba vipaumbele ambavyo vimewekwa na Serikali katika miradi ambayo itapewa kipaumbele, nami nipendekeze kwamba suala zima la ujenzi wa Mji Mkuu wa nchi yetu wa Dodoma liwekwe katika mipango ya Serikali, jambo hili liwe la kudumu, ili kwamba kwa sababu huko mbele hatuna mpango mwingine tena wa kuja kuhamisha Makao Makuu ya nchi yetu kutoka hapa tulipo Dodoma kwenda sehemu nydingine, basi maandalizi yawepo ya Serikali ya muda mrefu ya kuhakikisha kwamba Mji huu unapangwa vizuri. Mji huu uje uakisi Tanzania mpya ambayo tunaitarajia kuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ninaiomba sana Serikali ije na mpango mkakati kabambe kabisa wa kuhakikisha kwamba Mji huu unapimwa, unawekewa miundombinu yake halisi ambayo *ita-reflect uwepo* wa

Dodoma mpya, Dodoma ambayo itakuwa na miundombinu mizuri ya zile gari ambazo zinaendeshwa kwa umeme hapa Dodoma, *flyovers* ambazo tunaziona kwenye nchi za wenzetu zijengwe Dodoma, Dodoma hii iwe na uwanja wa ndege ambao ni wa kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo niombe Serikali iliangalie eneo la uwanja wa ndege la Msalato kama eneo lenyewe linaweza lisiwe kubwa sana basi Serikali ione uwezekano wa kupanua eneo hilo ili kusudi tuepukane na uwezekano wa baadae kuja kuanza kubomolea watu, kufidia watu na kuwahamisha katika miaka mingine ijayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya nikjua kabisa kwamba nchi hii ni yetu wote na kwa maana hiyo tufikiri sana, niombe sana kwamba yale maeneo ambayo yanatengwa kwa ajili ya ujengaji wa viwanda katika maeneo mbalimbali ya nchi hii, hata maeneo Maalum kama *strategic cities* au *satellite cities* kama kule Kigamboni inavyofanyika kule Dar es Salaam, na hapa Dodoma mipango hiyo iwepo, tusije tukachelewa tukaja tukafika mahali sasa tukajikuta kwamba sasa tunapotaka kujaribu kufanya *master plan* nyininge mpya tunaanza kujikuta tupo kwenye *crisis*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali yangu iwe makini kabisa katika kuhakikisha kwamba tunapokwenda na mipango hii mizuri, ujenzi wa miundombinu ya umeme, kwa mfano hiyo *Stiegler's Gorge* kwa maana hiyo tuna uhakika wa kuja kupata umeme wa kutosha na Tanzania ya viwanda inaelekeea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kusema ni kuhusiana na kuiomba Serikali ijandae kuweka taratibu nzuri kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya mpya, kuna maeneo mengi watu wanakaa kwenye majumba ambayo kwa kweli hayastahili. Kwa mfano, katika Halmashauri yangu ya Mbogwe, Ofisi ya Halmashauri ni jengo ambalo lilikuwa *guest house* zamani, sasa ukiangalia kwa kweli haikubaliki. Niombe kwa kweli

Serikali ifanye utaratibu iweke katika mipango yake kuhakikisha kwamba maeneo kama haya mapya yanapata ofisi na nyumba za wafanyakazi ambazo zinalingana na hadhi yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa pia kuishauri Serikali ni kuhusiana na viwanda vya mbolea. Nchi hii ni nchi inayotegemea kilimo kwa kiasi kikubwa na bahati nzuri Serikali yetu na nchi yetu imejaliwa kupata gesi ambayo ni malighafi nzuri ya kuweza kutumika katika ujenzi wa viwanda vya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali jambo hili iliangalie na ilione kwamba ni jambo la msingi, *i-w-encourage* watu wanaoweza kuja kuwekeza katika sekta hii ya viwanda vya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea inatumika katika mazao yote; mazao ya chakula na mazao ya biashara yanategemea sana mbolea, Sasa mbolea ikipatikana kwa bei rahisi maana yake uzalishaji utakuwa ni wa hali ya juu na uzalishaji ukishakuwa mzuri maana yake sasa hata hiyo Tanzania ya viwanda ambayo itakuwa inahitaji malighafi kutoka kwa wakulima itashamiri kwa wepesi zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ninaunga mkono hoja zote ambazo zimeletwa na Serikali za kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa viwanda hivyo vya makaa ya mawe, kufua chuma kule Liganga na ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge*, ni ukombozi na zaidi niiombe Serikali iendelee na upanuzi wa bandari zote zilizopo kule Tanga, Bagamoyo, Dar es Salaam pamoja na kule Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara kuna bandari moja nzuri sana, Kamati yetu ilitembelea kule, ile bandari nadhani Mungu aliumba pamoja na ile Dar es Salaam kwa sababu namna ambavyo Bandari ya Mtwara ilivyokaa imekaa sawa sawa na Bandari ya Dar es Salaam, hiyo ni ishara kwamba Mungu anaendelea kutupenda na hivi ni vitu ambavyo

anatujaalia tuvitumie katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inaanza kuwa ni *center* ya maendeleo kwa nchi nyingine za jirani zinazotutegemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mungu aibariki Serikali yetu na Mungu awabariki wote mlionisikiliza. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Amina. Waheshimiwa Wabunge huyo ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho leo. Katibu tuendelee.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imemaliza kazi yake kwa leo.

*(Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana shughuli zetu za leo zimefikia mwisho, kabla sijaahirisha kuna miwani naomba mwenyewe aweze kuifuata.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.46 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 8 Novemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*